Kutoka Katika Bustani Ya Moyo

TABIA ZA MFANO ZA MARAFIKI WA ALLAH

Othman Nuri TOPBASH

AIC
As Salaam Islamic Center



Dar Es Salaam

As-Salaam Islamic Center

Plot 354 Mbezi Beach, Makonde, Dar Es Salaam - Tanzania

Cell: +255 254 734 362,

Email: aic2013@gmail.com

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kutolesha sehemu yoyote ya toleo hili, kuitunza katika mfumo utakaowezesha kunakiliwa au kukisambaza katika aina au namna yoyote ile, iwe elektroniki, kuchapa, kunakilisha, kurekodi au vinginevyo bila kupata ruhusa kutoka kwa mwenye haki miliki.

ISBN: 978-9944-83-710-1

Mwandishi:	Othman Nuri Topbash
Msimamizi Mkuu:	Abdi Mohamed Adam
Mfasiri:	Ibrahimu H. Kabuga
Mhariri:	Dkt. Abbas Gurbanov
Msanifu jalada:	Altinoluk Graphics
Kupangiliwa vizuri na:	Nijat Garibov

Kutoka Katika Bustani Ya Moyo

TABIA ZA MFANO ZA MARAFIKI WA ALLAH

-1-

Othman Nuri TOPBASH

YALIYOMO

Dıbajı 13

Kumjua Mtume Muhammad ﷺ Kwa Moyo 31

Uwezo Wa Kıroho Usıokuwa Na Kıkomo 32

Kama Walıı Wake Yuko Hıvı 34

Anapımwa Kwa Uwezo Wa Alıyemtuma..... 34

Njıa Bora Ya Kumjua Mtume ﷺ 36

Kumpenda Muhammad ﷺ..... 38

Kwa Sababu Alıkuwa Akıfanya
Hıvı Na Vıle 39

Kuzıpa Umuhımu Sunnah (Ada Na Desturı
Za Mtume Muhammad ﷺ) 44

Staha 49

Marafıkı Wa Mwenyezı Mungu 49

Kıwango Cha Halı Ya Juu Cha
Kujınyenyekeza: Staha 52

Upanga Nı Kwa Wale Wenye Shıngo
(Ndefu Zenye Jeurı Na Kıburı) 56

Unyenyekevu Wa Mtume WeTu ﷺ 58

Staha Ya Maswahaba 59

Uwastanı Katıka Staha 61

Nafası Ya Staha Katıka
Mafunzo Ya Kıroho 63

Kuwa Na Subıra Na Uvumılıvu Mbele Ya Wajınga Na Wenye Tabıa Mbaya 71

Subıra Na Uvumılıvu Wa
Mtume Muhammad ﷺ 72

Subıra Na Uvumılıvu Wa Marafıkı Wa
Mwenyezı Mungu 76

Kuukabılı Ubaya Kwa Wema 89

Leo Hapana Lawama Juu Yenu... 90

Sıkutumwa Kuwa Mchochezı Wa Laana 92

Ponyo Ya Kuondoa Mateso 94

Kusamehe Katıka Wakatı Sahıhı 96

Je Hampendı Mwenyezı Mungu
Akusamehenı? 98

Kıası Ganı Cha Wema Kınachotakıwa Kuonyeshwa
Katıka Kukabiliana Na Uovu? 99

Bınadamu Nı Watumwa Wa Fadhıla 100

Macho Yanayoweza Kuwalılıa Maaduı..... 100

Watu Huuza Walıcho Nacho..... 102

Kutabasamu..... 107

Tabasamu La Muumını Huwa Usonı
Mwake; Huzunı Zake Huwa Moyonı Mwake..... 112

Tabasamu La Mtume ﷺ 114

Tabasamu La Marafıkı Wa
Mwenyezı Mungu 116

Adabu Na Tabıa Njema 125

Kuwa Na Tabıa Njema Mbele Ya
Mwenyezı Mungu Mtukufu 127

Kuwa Na Adabu Mbele Ya Mtume
Wa Mwenyezı Mungu ﷻ..... 133

Kuwa Na Adabu Mbele Ya Marafıkı
Wa Mwenyezı Mungu 136

Adabu Za Kuongea Kwa Mujıbu
Wa Qur'an Tukufu..... 143

Kuwa Na Mazoea Ya Kutumıa Lugha
Ya Huruma Ya Qur'an Tukufu 146

Qur'an Inataka Tutumıe Lugha
Ya Aına Ganı?..... 151

Aına Ganı Ya Lugha Inayokatazwa
Na Qur'an Tukufu? 154

Ukarimu Na Kutoa Sadaka 163

Shındanenı Katıka Ukarımu 163

Tabıa Na Sıfa Yenye Kumpandısha Mtu:
Ukarımu 166

Maradhı Makubwa Mawılı:
Ubadhırıfu Na Ubakhılı 167

Tıba Ya Ugumu Wa Moyo:
Ukarımu Na Kutoa Sadaka 170

Toa Kılıcho Nje Ya Mahıtajı Yako 174

Juhudı Za Kuongeza Ukarımu 175

Upofu Wa Ubakhılı 177

Toa Msaada Ilı Nawe Upate
Kusaıdıwa Pındı Utakapouhıtajıa 179

Adabu Za Kutoa 183

Usıpoteze Sadaka Yako 185

Kutoa Sadaka Pamoja Na Hısıa
Ya Shukranı 189

Njıa Ya Kufıkıa Wema 192

Saıdıanenı Katıka Wema
Na Uchamungu 193

Mwenye Kujulısha Kherı Nı
Kama Alıyeıfanya 195

Usafı Wa Moyo Katıka Kutoa 201

Alama Ya Ikhlas:
Kumtafuta Mhıtajı Wa Kwelı 203

Kama Una Nıa Ya Dhatı, Mwenyezı
Mungu Atakujaalıa Baraka Zake 209

Mkono Wa Kushoto USıjue
Kınachotolewa Na Mkono Wako Wa Kulıa 212

Ithaar - Kuwatangulıza Wengıne 219

Kutoa Katıka Kıla Aına Ya Baraka 221

Ithaar Ya Mtume Wa Mwenyezı
Mungu Na Maswahaba Wake 222

Ithaar Ya Marafıkı Wa
Mwenyezı Mungu 226

Kılele Cha Ithaar: Kujıtolea Maısha 229

Baraka Kubwa Ya Ithaar 233

Kuharakısha Kutenda Wema 239

Umuhımu Wa Kuharakısha
Mambo Mema 241

Mandharı Yenye Mfano Wakatı
Wa Pumzı Ya Mwısho 243

Kıla Mtu Hujuta 247

Malı Halısı Ya Mtu Nı Ile
Anayoıandaa Kwa Ajılı Ya Akhera 249

Jiokoeni Na Maradhı Ya Ubakhılı 250

Udugu 257

Udugu Katıka Uıslamu
Nı Bora Kulıko Udugu Wote 260

Udugu Wa Muhajırın (Wahamıajı)
Na Ansaar (Wasaıdızı) 262

Uwe Rafıkı, Usıwe Mzıgo 263

Kuhuısha Udugu 275

Kuhamasısha Amanı Baına Ya Waumını 275

Kuchukıa Dhambı; Kuwahurumıa Wakosajı 278

Msıngı Wa Awalı Wa Umoja:
Udugu Wa Kııslamu 281

Kuhısı Maumıvu Ya Ndugu
Yako Muıslamu 283

Swahaba Alıyeacha Ibada Ya
Itıkafu Kwenda Kumsaıdıa Muumını 287

Baraka Kutoka Kwa Mwenyezı
Mungu: MWezı Wa Ramadhan 288

**Kupenda Na Kuchukıa Kwa Ajılı Ya
Mwenyezı Mungu** 293

Matunda Ya Mtı Wa Utume 294

Majarıbu Na Vıshawıshı Vya Dunıa 296

Kuwapenda Wale Wanaostahıkı Kupendwa
Na Kuwachukıa Wale Wanaostahiki Kuchukıwa 298

Dalılı Za Upendo Wa Kwelı 302

Kupenda Na Kuchukıa Kwa Ajılı
Ya Mwenyezı Mungu 305

Ikhlas Katıka Kupenda Na Kuchukıa..... 311

Hısıa Ya Imanı Inapopotea 312

Eneo Dhaıfu La Waıslamu:
Kurıdhıa Maovu 313

Radıamalı Ya Imanı 317

Maradhı Ya Kuıga 319

Mazungumzo Na Wasıo-Waıslamu 321

Kanunı Za Msıngı Za Mazungumzo
Na Majadılıano Na Wasıo Waıslamu..... 324

Tusısahau Kufa..... 329

Halı Mbılı Tofautı Kuhusu Kıfo 330

Msımlılıe Marehemu Zılılıenı Nafsı Zenu... 332

Jambo Muhımu Lısılojulıkana:
Pumzı Ya Mwısho 335

Nını Itakuwa Hatıma Yako? 339

Kuıpendelea Akhera Zaıdı Ya Dunıa 345

Alama Ya Moyo Safı 346

Hatubadılı Mema Ya Akhera
Kwa Thamanı Ya Dunıa Nzıma..... 348

Nı Nanı Mwenye Akılı Ya Kwelı? 351

Tıba Ya Ugumu Wa Moyo..... 356

Kosa Sıyo La Dunıa Balı Nı La Wale
Wanaodanganyıka Nayo..... 357

DIBAJI

Yule aliyeumba kutokana na bure viumbe wasıohesabıka ambao rasilimali yao ni ***"hali ya kutokuwepo;"***

Yule aliyetufanya kuwa bora juu ya viumbe wengine wote kwa kutuumba kama "wanadamu" japokuwa hatukulipa fidia yoyote kwa hilo;

Yule anayetuongoza kwenye unyoofu na wema kwa vitabu na Mitume aliowatuma;

Yule ambaye ni mwema mno kwa kuuendeleza muongozo huu wa kiroho kwa njia ya wanazuoni na wenye maarifa ambao ni warithi wa Mitume;

Himidi na shukrani za milele ni za Allah Mtukufu aliyetujaalia, sisi waja wake wanyenyekevu, furaha na utuvu wa imani!

Yule ambaye amekuwa njia ya kuwaokoa wanadamu kutoka kwenye giza la ukafiri na ujahiliya na kuwajazia nuru ya furaha ya milele;

Yeye ambaye alieneza huruma, upendo, na baraka za roho yake ambayo ni rehema kwa walimwengu.

Yeye aliyepambwa kwa tabia njema za kipekee, mwalimu, mkufunzi na muongozo wetu mkuu; Yeye ambaye atakuwa muombezi wetu huko akhera,

Amani na baraka zisizokuwa na kikomo ziwe juu ya fakhri ya ulimwengu, Muhammad Mustafa ﷺ, familia (ahl al-bayt) yake na maswahaba!

Wasomaji wetu wapendwa:

Makala zinazochapishwa kila mwezi katika jarida la ALTINOLUK chini ya kichwa cha habari "Kutoka katika bustani ya moyo" zimehaririwa, zikakusanywa hatua kwa hatua kwenye kitabu na kuchapishwa kwa manufaa ya wasomaji waheshimiwa.

Kwa baraka za Mola wetu tulipata fursa ya kuongeza duara mpya katika mnyororo wa vitabu vyetu mbalimbali kama vile ***"Siri katika kumpenda Mwenyezi Mungu," "Pumzi ya Mwisho," "Machozi ya moyo kutoka katika bustani ya Mathnawi," na "Wakfu, sadaka na kutoa huduma katika Uislamu,"*** na vinginevyo.

Kuna hitajio la vitabu katika kila uwanja wa sayansi ya Kiislamu, vitakavyopeleka uzuri, utamu na umaridadi wa Uislamu katika nyoyo za wanadamu. Jambo hili ni muhimu sana hasa katika uwanja wa muongozo wa kiroho… sababu ya hili ni kwamba katika zama hizi tupo kwenye kilele cha njaa ya kiroho na hitajio la kimaadili. Kwa hivyo, mahitaji ya huduma za kidini ni dharura iliyo dhairi katika jamii yetu, na tunatakiwa tuwe tayari kujitolea kwa ajili ya huduma hiyo.

Katika jambo hili, yatupasa kutumia baraka za Mwenyezi Mungu kama vile utaalamu wa kielimu na maarifa ya kiroho, maisha yetu, mali na muda wetu katika namna anayoiridhia.

Hivyo basi, yatupasa kutumia kikamilifu baraka zote tulizojaaliwa, kama vile utaalamu wa kielimu na maarifa ya kiroho, muda wetu katika ardhi, mali zetu, kwa ajili ya kumridhisha Mwenyezi Mungu.

Mojawapo ya huduma muhimu tunazoweza kuzitoa kwa ajili ya Uislamu ni kujaribu kuuelewa na kuishi na Uislamu kama Maswahaba wa Mtume ﷺ na Marafaiki wa Allah walivyofanya, na kuutumia katika maisha yetu kwa kila namna inayowezekana, kwa kujumuisha imani, ibada, tabia, na ukamilifu wa kiroho.

Ili kufanya hivyo, tunatakiwa tuwe na uwezo wa kuonyesha hali kamili ya utambulisho wa Kiislamu na moyo wa muumini. Naam, ili kuuonyesha utambulisho huo wa Kiislamu na kiwango cha moyo, tunatakiwa kwanza tuzijue tabia, sifa, uzuri na mafundisho ya Uislamu.

Katika jitihada za kufikia lengo hili, tumefanya juhudi ya kuelezea kiwango cha ubora, uzuhali, umaridadi, huruma, bashasha, na umakini ambao Uislamu unataka tuufikie, katika mfululizo wa makala yaitwayo *"Tabia njema za mfano kutoka kwa Marafiki wa Mwenyezi Mungu,"* pamoja na mifano kutoka katika maisha ya watu maarufu katika historia ya Kiislamu.

Kitabu kilichopo mkononi mwamko ni juzuu ya kwanza ya kazi hii. Makala zitakazotengeneza kitabu cha pili cha mfululizo huu zinachapishwa na gazeti la ALTINOLUK.Makala haya, Inshallah, yatawasilishwa kwa manufaa yako kama kitabu cha pili cha mfululizo wa *"Tabia njema za mfano kutoka kwa marafiki wa Mwenyezi Mungu."*

Isisahaulike kuwa mtu anaweza kuwa **"Binadamu"** kupitia tabia yake njema. Kanuni ya tabia ndiyo inayomhusu binadamu miongoni mwa viumbe wote. Kwa sababu hiyo, hata kama mtu ambaye hana tabia njema anaonekana kama bina-

damu kwa nje, katika hali halisi, mtu huyo ni duni kuliko viumbe wengine wengi. Mwishowe hupoteza heshima na hadhi. Hivyo, siri inayomfanya mtu kuwa mwanadamu, humtambulisha kwenye hazina yake halisi, na mwisho humuwezesha kufikia sifa iliyoelezwa ya kuwa "kiumbe aliye mtukufu zaidi kati ya viumbe wote," kuwa na **"tabia njema / tukufu"** kwa msingi wa imani ambayo hutekelezwa kwa upendo.

Msingi wa maadili mema unaambatana na **"tabia kamilifu"** katika kila nyanja ya maisha. Maadili ni ushahidi wa ubinadamu wetu; kama harufu ya mawaridi inayoziburudisha nyoyo zetu. Harufu hii lazima ipenye ndani ya moyo wa muumini na kutakiwa kuonekana katika kila nyanja ya maisha yake. Wakati huo huo, hii pia ni ishara ya ukamilifu katika imani.Kutokana na ukweli huo, Jalal al-Din Rumi anasema:

"Akili yangu iliuuliza moyo wangu 'Imani ni nini?' Moyo wangu ukaliinamia sikio la akili yangu: 'Imani ni ukamilifu wa tabia!'"

Kila kanuni ya Uislamu ni kama ishara ya uzuri wake wa maadili, ambayo yanaakisi imani katika maisha.

Mtume r anasema:

"Hakika Mimi nimetumwa kukamilisha tabia njema." (Muwatta, Husnul khulq, 8)

Hivyo kila tabia na matendo ya wanazuoni na wanamaarifa ambao ni warithi wa Mitume ni kama somo la maadili kwetu. Aidha, majina mengi maarufu katika Uislamu yaliuchukulia Usufi kama **"Muundo wa tabia njema na maadili."** Walibainisha kuwa somo la kwanza la Usufi ni "Usimuumize yeyote" na somo la mwisho ni "Usiumizwe na yeyote."

Marafiki wa Mwenyezi Mungu ni mifano bora kwa wale ambao hawakuweza kupata heshima ya kukutana na Mtume

Muhammad ﷺ na maswahaba wake. Mwongozo na ushauri wao huzihuisha nyoyo za waumini kwa Lugha ya huruma na kuzirutubisha roho kwa hali ya kiroho inayotokana na chemchem ya utume.

Hawa ni wale wenye elimu, wajuzi, wanyoofu, na marafiki wakubwa wa Mwenyezi Mungu waliofikia ubora wa hali ya juu katika uchamungu, na hatua kwa hatua wakapiga hatua za hali ya juu kuelekea kwenye daraja za kiroho kwa uchamngu wao na kumjua Mwenyezi Mungu. Wamepanua uelewa na ufahamu wao katika anga za ulimwengu huu na ule wa Akhera. Jitihada zao za pekee ni kuwakomboa binadamu dhidi ya tabia, mwenendo mbaya na matamanio ya nafsi, na kuwainua kuelekea kwenye ukomavu wa kiroho na vilele vya ubora.

Wale ambao ni marafiki wa Mwenyezi Mungu hawajasahaulika baada ya miili yao ya muda kuondoka katika dunia hii, badala yake wameendelea kuishi ndani ya nyoyo za wapendwa wao na kuendelea kuwaongoza. Mwenyezi Mungu anawapenda na ameujaalia upendo wao juu ya wale wenye kufuata nyayo zao. Hili limeashiriwa ndani ya **Qur'an** kama ifuatavyo:

"Hakika walioamini na wakatenda mema Arrahmani Mwingi wa Rehema atawajaalia mapenzi." (19:96)

Upendo ...

Upendo mkubwa ... upendo wa dhati ambao huzivutia nyoyo nyingi kama sumaku ...

Je idadi ya wale wenye kutembelea makaburi ya Shah-i Naqshiband, Jalal al-Din Rumi, Yunus Emre, au Hudayi (Mwenyezi Mungu azirehemu nafsi zao) kila siku haitoshi kuthibitisha ukweli huu?

Kisa kifuatacho ni ushahidi mzuri wa ukweli huu:

Khalifa wa kibani-Abbas, Harun Al-Rashid alikuwa akiishi katika utukufu na anasa mjini Raqqa. Siku moja Abdullah bin Mubarak alikuja Raqqa. Watu wote wa mji wakatoka nje ya mji na kwenda kumkaribisha. Khalifa kwa kawaida aliachwa peke yake katika mji. Mmoja wa masuria wa Khalifa akishangazwa na hali hiyo akauliza:

"Ni nini hii? Nini kinatokea?" akaambiwa:

"Mwanazuoni kutoka Horasan ameingia mjini. Jina lake ni Abdullah bin Mubarak. Watu wamekwenda kumkaribisha." Kisha huyo suria akasema:

"Usultani wa kweli ni huo, siyo wa Harun Al-Rashid; kwa sababu, bila nguvu za polisi (Harun) hawezi hata kuwakusanya wafanyakazi wake."

Huu ndiyo Usultani wa kweli; kwa sababu, siku moja, wafalme wote wa ulimwengu huu watafikia mwisho. Lakini, Usulatni wa kiroho utaendelea kuheshimiwa hata baada ya kifo.

Daima watu wanahitajia masultani wa nyoyo. Wanawatafuta na kufuata nyayo zao. Hii ndio sababu kwamba marafiki wa Mwenyezi Mungu, kama vile Abdul Qadir Jailani, Bahauddin Naqshabandi, Yunus Emre, Rumi, na wengineo, wameendelea kutamaniwa kwa karne nyingi.

Ashqi na upendo wa kiroho wa marafiki wa Mwenyezi Mungu ndiyo siri iliyo nyuma ya usulatni wao wa kiroho. Sifa zao za kipekee nazo pia ni miongoni mwa sababu za kuheshimiwa kwao.

Marafiki wa Mwenyezi Mungu ambao wametopea moja kwa moja katika kumpenda Mtume wa Allah (fana fi al –Rasul) hawazungumzi kwa matamanio ya nafsi zao. Ni kama filimbi ya mwanzi ambayo imeondolewa kila kitu kinachoiweka mbali na Mwenyezi Mungu. Mazungumzo na matendo yao yote kwa

hakika hutokana na desturi na maneno ya Mitume ﷺ. Nyoyo zao ni kama vioo visafi ambavyo juu yake nuru na ukweli wa Mwenyezi Mungu hupata kuonekana. Ukweli huu umeelezwa ndani ya maneno yafuatayo ya Mtume ﷺ:

"... na kitu bora ambacho mja wangu hujikurubisha nacho kwangu, ni kile nilichomuamrisha; na mja wangu huendelea kujikurubisha kwangu kwa kutekeleza matendo ya sunnah mpaka ninampenda, na kwa hivyo Mimi huwa ndiyo sikio lake analotumia kusikia, na macho yake anayotumia kuona, na mkono wake anaoshikia, na miguu yake anayotembelea; na akiniomba humjibu, akiniomba ulinzi humlinda (yaani humpa kimbilio) na sijapata kusita kufanya jambo kama ninavyosita kuchukua roho ya muumini, kwa maana yeye hakipendi kifo, nami sipendi kumhuzunisha." (Bukhari, Kitabu al-Riqaq, 38)

Ulimwengu wao wa kiroho ni mahala pa kipekee ambapo sifa nzuri za Mwenyezi Mungu Mtukufu hujidhihirisha. Sifa za Mwenyezi Mungu zinazorudiwa mara kwa mara ndani ya Qur'an, "Rahman" (Mwingi wa rehema) na "Rahim" (Mwenye kurehemu), huonekana ndani ya nyoyo za marafiki wa Mwenyezi Mungu kama rehema kwa viumbe wote. Kuwatazama viumbe kupitia dirisha la huruma na upendo wa Muumba yamekuwa ndiyo mafundisho ya maisha yao.Hallaj Mansur alipopigwa mawe alisema:

"Ewe Mola wangu! Wasamehe wale wanaonipiga mawe kabla hujanisamehe mimi."

Marafiki wa Mwenyezi Mungu hujitahidi kujipamba kwa sifa ya Mwenyezi Mungu ya "Mwingi wa kusamehe", ambapo huionyesha sifa hii katika vipengele vyote vya maisha yao.

Siku moja, mgeni mmoja alipiga kelele kwa bahati mbaya mbele ya Hatam As'am, na Hatamaa akajifanya hakuisikia, ili aisije akamsumbua mgeni wake. Hivyo, kwa miaka mingi

Hatam aliendelea kujifanya kana kwamba hasikii vizuri. Kwa sababu hii, alikumbukwa kwa jina la “As’am”, yaani kiziwi au mtu ambaye hasikii vizuri. Huu ni mfano mzuri wa ishara ya sifa ya Mwenyezi Mungu ya “Sattar al-uyuub”, yaani mwenye kusitiri aibu na kasoro za watu.

Jalal al-Din Rumi ni mfano mwingine mkubwa wa namna muumini na rafiki wa kweli wa Mwenyezi Mungu anavyotakiwa kuwa. Alikuwa miongoni mwa viongozi wa kipekee wa kiroho katika historia ya Kiislamu na miongoni mwa Masultani wa nyoyo.

Kwa karne saba, kitabu chake adhimu cha Mathnawi, kilichojaa siri na hekima, kimeendelea kulinda hadhi yake ya kuwa muongozo wa kiroho na kimaadili kwa waumini. Tukio lifuatalo ni mfano stahili wa hali ya kiroho ya Rumi:

Siku moja, kwa mshangao wa kila mtu, Rumi alipita katika bwawa ambalo wagonjwa wa ukoma walikuwa wakitibiwa. Waliwatibu kiroho na kuwafariji wagonjwa kwa kuwaonyesha huruma na upendo. Kwa kweli, ulimwengu wa kiroho wa rafiki huyu wa Mwenyezi Mungu, anayewatazama viumbe kwa mtazamo wa jicho lenye huruma la Muumba wao, ulikuwa kama kituo cha ukarabati ambapo watu walipata amani na ponyo.

Katika kipindi cha miaka saba ya kwanza ya utumishi wake, Bahauddin Naqshabandi, aliishi maisha ya kutoa hudumа adhimu kuanzia kwenye kuwahudumia wagonjwa, masikini, watu wasio na makazi na wanyama waliojeruhiwa, mpaka kwenye kusafisha barabara zinazotumiwa na watu. Alielezea hisia yake ya “kutokuwa chochote” iliyojikita katika moyo wake ndani ya tungo zifuatazo:

Dunia ni ngano, mimi ni nyasi,
Dunia ni nzuri, mimi ni mbaya...

Yeye pia alieleza kuwa alipata maongozi makubwa ya kimungu katika kipindi cha huduma zake hizi.

Kwa sababu ya kukataa kutoa fatwa ya kisheria kuhusu matamanio binafsi ya Khalifa, Abu Hanifa alichagua kukaa gerezani badala ya kuwa Kadhi Mkuu wa Baghdad. Kwa hatua yake hiyo, alionyesha mfano mkubwa wa haki na unyoofu kwa gharama ya maisha yake binafsi.

Ahmad bin Hanbal alichagua kupata mateso gerezani kwa sababu ya mtazamo wake katika kadhia maarufu ya iwapo Qur'an iliumbwa au la, kuliko kuuacha mtazamo wake na kile alichokiamini kuwa ni kweli.

Kwa muhtasari, mifano yote hii ya ujasiri na nguvu ya imani ni mifano michache tu katika mifano lukuki inayoakisi tabia bora za marafiki wa Mwenyezi Mungu. Ni wale walio karibu na Mwenyezi Mungu Mtukufu na hivyo wakaokolewa dhidi ya hofu na huzuni za Moto wa Jahannam.

Kama kweli tunawapenda mawalii (marafiki wa Mwenyezi Mungu), waja waliopendwa na Mwenyezi Mungu, na tukawa tunataka kufufuliwa pamoja nao siku ya mwisho, lazima tufuate tabia zao njema.Kwa kuzilinganisha tabia zetu na zao, kuyafanya matendo yao kama kielelezo chetu, na kujaribu kuendana kikamilifu na hali yao ya kirorho, tutaweza kufika kwenye furaha ya milele.

Haya ni mambo ambayo tunajaribu kuyaelezea katika kitabu hiki kidogo kilichopo mikononi mwako.Mada zifuatazo zimeelezewa kwa muhtasari:

Mtume wetu Muhammad ﷺ ni kilele cha tabia njema, upole na umaridadi miongoni mwa wanadamu. Ubora na uzuri huu wote unapatikana katika tabia zake bora na za mfano. Ulimwengu wake wa kiroho ni kama bustani ya pepo, iliyojaa maua ya thamani, mazuri na maridadi yenye harufu maridhawa.

Marafiki wa Mwenyezi Mungu na wafuasi wa Mtume ﷺ ni wenye thamani ya juu kama upepo wa Sheba unaovuma kutoka katika bustani ya pepo.Kitu cha muhimu zaidi kwetu katika ulimwengu huu ni kutafuta njia iliyonyooka inayopita katika bustani hii ya pepo. Kwa sababu hiyo, ni jambo la dharura "kumjua Mtume ﷺ kwa moyo" kama marafiki wa Mwenyezi Mungu walivyofanya.

Kwa kweli haiwezekani kuyaelewa maisha yake ya kiroho kwa kujifunza tu maandishi (chronology) ya vitabu vya historia ya maisha yake.

Uzuri wote wa kimaadili katika ulimwengu huu uliochanua kwa misingi ya imani ni sehemu ndogo tu ya maadili ya Mtume ﷺ yaliyotolewa kwa wanadamu. Kwa sababu hii, haiwezekani kuishi maisha ya utiifu yanayokubalika bila kupata sehemu ya moyo wa Mtume Muhammad ﷺ na bila kumsoma kwa macho ya roho zetu.

Ulimwengu huu ni shule ya imani. Tumekuja hapa kupata mafunzo ya kiroho. Jukumu tulilokabidhiwa ni kukamilisha kitabu cha maisha yetu kwa kumridhisha Mwenyezi Mungu kwa kupata ukomavu wa kiroho.

Somo la kwanza tunalotakiwa kujifunza katika mafunzo haya ni "unyenyekevu," ili tuweze kuwa waja wa kweli wa Mwenyezi Mungu Mwenye kurehemu. Aina yoyote ya ibada inayotekelezwa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu haiwezi kukubalika bila kufanywa kwa moyo mnyenyekevu, jambo ambalo linachukuliwa kuwa msingi wa kuwa mja wa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Ni pale tu mja anapokuwa mnyenyekevu, ndipo Mola humkirimu rehema na kumnyanyua.

Kwa sababu hii, sharti la kwanza la kupita kwenye mlango wa urafiki na Mwenyezi Mungu ni kuwa na unyenyekevu na kuacha ubinafsi. Baraka zote za kimaada na kiroho ni zawadi

kutoka kwa Muumba. Ubinafsi, kwa upande mwingine, ni aina ya maradhi ya moyo.

Tena, majaribio ya Dunia katika mfumo wa “subira na kuwavumilia wajinga na wenye tabia mbaya” kamwe haichi kuibuka katika safari ya wale walio kwenye njia ya Mwenyezi Mungu. Utii, kujisalimisha na nia zao hupata kujaribiwa. Waja wenye maarifa hukamilisha mafunzo yao ya kiroho kwa mafanikio kwa “kukabiliana na ubaya kwa wema.”

Inaeleweka kuwa imani kamili ni uwezo wa kuacha malalamiko yote, na kuzika huzuni zote ndani ya moyo, kwa nia ya dhati, huku ukidumisha mwenendo mwema. Uso wenye tabasamu ni sifa ya waumini wote, na kwa kweli Uislamu unaakisi “tabia na adabu njema.” Muislamu hapaswi kudai kuwa yeye ni mtu wa dini wakati huohuo akawa fidhuli, mgomvi na asiye muungwana.

Kila kitendo na mwenendo wa Muumini kamili, kuanzia kwenye namna anavyoketi mpaka anavyosimama, na kuanzia kwenye kutembea mpaka kwenye kutabasamu, anaongozwa na Qur’an na Sunnah. Adabu za kuongea zinakuwa ndiyo kichwa cha matendo yote, ambayo huongozwa na misingi ya Qur’an na Sunnah. Maneno ni kama kioo kinachoakisi akili, kiwango cha kiroho, imani na hali ya kimaadili ya muongeaji. Ndiyo maana, ili kujilinda kutokana na matokeo ya maneno yetu, tunatakiwa kuzijua “adabu za kuongea zilizoelezwa na Qur’an Tukufu”.

Kwa upande mwingine, matunda ya kwanza ya imani ni huruma na upendo. Ukiwa na moyo uliokosa huruma na upendo, huwezi kupata huruma ya Mwenyezi Mungu.

“Ukarimu na kutoa sadaka” ni matokeo ya asili ya kuonyesha huruma na upendo kwa viumbe kwa ajili ya Muumba wao. Muumini anatakiwa kuwa na upole kama upepo mwa-

nana wa asubuhi na awe mkarimu kama mvua. Anatakiwa kutafuta radhi za Mwenyezi Mungu kwa kuwa mtu wa amani, mwenye huruma na upendo kwa viumbe wengine wote. Kwa maneno mengine, muumini anatakiwa kuishi na wengine kwa heshima na ukarimu kwa kufuata "adabu za kutoa." Mtoaji anatakiwa kumshukuru mpokeaji. Muumini anatakiwa kuwa makini asimbughudhi masikini. Anatakiwa kujizuia na unafiki, riya, ubadhirifu, na uchoyo. La sivyo, matendo yake mema yatakwenda bure kwa kutofuata msingi wa "ikhlasi katika kutoa sadaka."

Ithaar (kutanguliza shida ya mwingine juu ya shida yako) ni kilele cha kiwango cha kutekeleza wema wa kuwasaidia wengine.

Ithaar, ambayo ni sifa ya kipekee ya waja wema wa Mwenyezi Mungu, ni kuwa na uwezo wa kumpa mtu mwingine kitu fulani ambacho wewe mwenyewe unakihitajia. Ni kuweza kumtanguliza mtu mwingine badala yako, kwa jili ya Mwenyezi Mungu na kwa ajili ya amani na furaha ya ndugu zako katika Uislamu.

Thamani ya matendo mema hupatikana kwa kuyatekeleza kwa wakati bila kuchelewa. Tendo jema lisitekelezwe pindi linapohitajika halina maana yoyote. Vilevile muumini huwajibika kama hatomsaidia Muislamu mwenzake aliye na shida, hasahasa kama akichelewesha kufanya mambo mema kwa ajili ya Allah kwa sababu ya uzembe wake tu. Hatujui kitakachotokea baadaye. Kwa sababu hii, ni muhimu tusikose fursa pale zinapofika. Tunatakiwa "kufanya haraka kutekeleza mambo ya kheri."

Kwa upande mwingine, Uislamu ulileta "udugu " ambao haukuwahi kushuhudiwa hapo kabla katika historia ya binadamu.

Uislamu ulitamka kuwa wafuasi wake ni ndugu, na kuwaunganisha mmoja na mwingine. Mwenyezi Mungu aliwaamrisha kufaana katika majanga.

Wakati wote muumini anatakiwa kuwa rafiki wa dhati na mwenye kujali, akiwa mwenye furaha au mwenye huzuni. Kwa muhtasari, utekelezaji sahihi wa jukumu hili, ambalo tunaweza kuliita "uhuishaji wa udugu," humfurahisha Mwenyezi Mungu na Mtume wake Muhammad ﷺ; ambapo kuwadhuru na kuwaumiza ndugu katika Uislamu kwa visingizio binafsi na vya kiovu inachukuliwa kuwa dhambi kubwa katika Uislamu. Kumbeza au kutukana ndugu yako Muislamu ni sawa na kumwaga sumu kwenye maisha ya kiroho.

Kwa upande mwingine, upendo wetu ni rasilimali kubwa ya kuwa mja wa Mwenyezi Mungu katika ulimwengu huu.

Kuuelekeza upendo kwa wale wanaostahiki zaidi kupendwa ni njia kuu ya kuboresha hali ya kiroho; na kuupoteza katika njia isiyostahili kutasababisha maafa milele.

Kuvipenda mno vitu visivyostahili kupendwa ni hasara kubwa katika hii dunia. Upendo wenye kupelekwa kwenye maslahi rahisi na yasiyo na maana ya dunia hii ni kama maua yaliyoota kwenye lami, ambapo muda mfupi hukanyagwa na kuharibiwa. Bahati mbaya iliyoje kwa almasi kutupwa mtaani! Hasara iliyoje iwapo almasi hiyo itachukuliwa na mtu asiyestahili!

Katika dunia hii, kila kitu kina kinyume chake. Kwa kuwa kinyume cha upendo ni chuki, kuvichukia vitu vinavyochukiwa sana na Mwenyezi Mungu ni matokeo asili ya upendo wa Mwenyezi Mungu. Wale wanaopenda imani huuchukia ukafiri; wanaopenda matendo mema pamoja na wema huzichukia dhambi na matendo maovu. Kwa sababu hiyo, ni lazima "kukipenda na kukichukia kitu kwa ajili ya Mwenyezi Mungu." Msin-

gi wa imani yetu unapaswa kuwa “kuwapenda wale wanaostahili kupendwa na kuwachukia wanaostahili kuchukiwa.”

Kukipenda kitu bila kukichukia kile kilicho kinyume chake ni upendo pungufu na usiokuwa na ukweli na ikhlasi ndani yake. “Ikhlasi katika kupendwa na kuchukia” inatakiwa iendane na vile Mwenyezi Mungu anavyopenda na kuchukia vile vinavyomchukiza, na hata kuonyesha radiamali kwa ajili ya Mwenyezi Mungu pindi inapobidi.

Muumini anayejua kwamba ulimwengu huu ni mahali pa mitihani, majaribio na mateso, na akaishi kwa “kutousahau ulimwengu wa milele”, habadilishi uelekeo wake kwa ajili ya matamaanio ya kimaada au ya kibinafsi kwa hali yoyote ile. Hatoipoteza furaha yake ya milele kwa ajili ya vishawishi vya kupita vya ulimwengu huu. Hadanganywi na alinacha. Hauweki moyo wake kwenye vishawishi vya mpito vya dunia hii. Habadilishi manufaa ya Akhera kwa manufaa ya dunia na mara zote “huipendelea Akhera kuliko dunia.” Hujaribu kutumia suhula na fursa za kimaada kama njia ya kupata mtaji wa furaha yake ya milele.

Kwa muhtasari, muumini ambaye daima huishi maisha ya unyoofu hufanywa kuwa rafiki wa Mwenyezi Mungu.

WASOMAJI WETU WATUKUFU:

Maisha mema yaliyojaa uzuri na siri mbalimbali yanajionyesha katika maisha ya mawalii. Wao ni watu wa mfano kwetu katika kuwa marafiki wa Mwenyezi Mungu. Hasa, katika utiifu wao, ni mifano ya kipekee.

Furaha kubwa iliyoje kwetu kama tukiweza kufaidika kikamilifu na mifano hii!

Kadri tunavyoishi kwa ikhlas na moyo wa dhati katika vipengele na nyakati zote za maisha yetu, Mwenyezi Mungu atazijaalia nyoyo zetu elimu na maarifa yatakayotuwezesha kutofautisha baina ya mema na maovu na haki na batili.

Ukweli huu umeelezwa katika aya ifuatayo:

"... Basi mcheni Mwenyezi Mungu. Kwa maana ni Mwenyezi Mungu anayekuelimisheni ... " (Qur'an, 2: 282)

Ni kweli pia kwamba, kama ilivyo kwa vitabu vyote, kitabu hiki kidogo kilichopo mikononi mwako kitafikia lengo lake kwa kadri yale yaliyomo ndani yake yatakavyotumika katika maisha ya wasomaji. Kwa hali hii, tunakimbilia kwenye baraka na msaada wa Mola wetu.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu azijaalie nyoyo zetu neema na baraka zitokanazo na hali ya kiroho ya maswahaba wa Mtume ﷺ na marafiki wa Mwenyezi Mungu ambao ni muongozo wetu kwenye njia iliyonyooka. Tunamuomba azijaalie roho zetu neema zitokanazo na ulimwengu wao wa kiroho.

Amin...

Osman Nuri TOPBAS

Julai 2009

Uskudar

KUMJUA MTUME MUHAMMAD ﷺ KWA MOYO

Waridi ni alama ya Mtume Muhammad ﷺ na mafunzo muhimu katika dunia hii ni:

Kuwa na habari za Mfalme wa mawaridi ﷺ, Kunufaika kutokana na harufu takatifu ya hili waridi na ulimwengu wake wa kiroho, na Kuwa umande juu ya majani ya waridi hili ﷺ

Muumini anapoanza kuhisi upendo wa Mtume ndani ya kina cha nafsi yake, na akaanza kupata fungu lake kutokana na hali ya kiroho ya Mtume, basi hakika yu katika njia ya kuwa sawa na yeye na kupata raha kutokana na Upendo wake.

KUMJUA MTUME MUHAMMAD ﷺ KWA MOYO

Darwesh mmoja alimuuliza mwana-maarifa fulani:

“Ni nani aliye maarufu zaidi, Junayd al-Baghdadi au Bayazid al-Bistami?”

Mwana-maarifa akajibu:

“Ili mtu aweze kuamua tofauti baina ya daraja zao za ubora, anapaswa kuwa Walii mkubwa kuliko wao...”[1]

Kwa maneno mengine, si kila mtu anaweza kuuelewa upeo wa ubora walionao marafiki wa Mwenyezi Mungu. Pindi akili ya mwanadamu inaposhindwa hata kuelewa daraja ya mawalii, itawezaje kuelewa tunu na thamani ya kipenzi cha Mwenyezi Mungu (Mtume Muhammad)?

Mara nyingi mtu hushangaa, kwa ufinyu wa lugha na maneno ya mwanadamu, ni kiasi gani cha hakika ya maisha ya Mtume Muhammad ﷺ imeelezewa katika vitabu vyote ambavyo vimeandikwa kumhusu.

1.Ahmed Eflaki, Manakibul - Arifin, II, 225.

UWEZO WA KIROHO USIOKUWA NA KIKOMO

Siku moja Jalal al- Din Rumi alipokuwa akizungumza na wanafunzi wake, shams-i Tabrizi akauliza swali lifuatalo ili kumpima:

“Nani mwenye kuchomoza zaidi? Bayazid-i Bistami au Muhammad ﷺ?”

Rumi akashtuka na akasema kwa hasira:

“Swali gani hili?! Unawezaje kumlinganisha Mtume aliyetumwa kama rehema kwa walimwengu na walii ambaye kazi yake kubwa ni kumfuata Mtume ﷺ na kupata maarifa kutoka kwake?!”

Shams-i Tabrizi kwa upole kabisa akalifafanua swali lake kama ifuatavyo:

“Kama Bayazid angemuomba Mwenyezi Mungu amuingize Jahannamu na kuufanya mwili wake kuwa mkubwa sana kiasi kwamba hakuna mtu mwingine anaweza kuenea, lakini wakati huo huo akikutana na baadhi ya ishara na Mungu, atasema ‘Heshima na utukufu ulioje niliopewa mimi! ninajisifu!”, basi kwa nini Mtume Muhammad ﷺ, licha ya ufunuo mwingi, afanye kwa unyenyekevu kama alivyofanya, huku akimshukuru na kumsifu Mwenyezi Mungu, na kuomba Ishara zaidi ?...”

Maelezo haya ya Rumi na ukingoni mwa elimu, ambayo iliweza kupatikana kwa akili. Ilikuwa vigumu kujibu swali kwa hali hii. Hivyo, Shams alimuongoza mbali zaidi. Aidha, nje ya ulimwengu unaoonekana kuna ulimwengu wa kiroho usiokuwa na mwisho.

Kutokana na athari ya hali ya ghafla ambayo haikutarajiwa, Rumi alitoa jibu lifuatalo kana kwamba alikuwa amelihifadhi kabla kama mojawapo ya maelezo ya sayansi chanya:

"Maneno ya Bayazid "Heshima na utukufu ulioje niliopewa mimi! Ninaisifu nafsi yangu!" ni maelezo ya kukifiwa kiroho. Kwa maneno mengine, kiu yake ya kiroho imetoshelezwa na tone moja la ishara ya Mwenyezi Mungu. Ukubwa wa bahari ni wa milele (hauna mwisho) lakini uwezo wa moyo wake (Bayazid) ni mdogo. Kwa sababu hii, kwa ishara ndogo tu kutoka kwa Mwenyezi Mungu, roho yake siyo tu kwamba itatosheka, bali itakifiwa sana kiasi kwamba hatoweza kustahimili zaidi. Hivyo, atatoka katika ulimwengu wa akili.

Kwa upande mwingine, Mtume ﷺ alipata siri ya **" Hatukukunjulia kifua chako?"**[2] Pamoja na ufunuo na ishara mbalimbali za Mwenyezi Mungu zilizomfunika kutoka kila upande, moyo wake, ambao ni mkubwa kama ulimwengu haukutosheka na ishara hizo. Kama ambavyo umbali baina ya moyo wa mja na muumba wake haupimiki, uwezo wake wa kubeba haupimiki. Kwa sababu hii, hata ufunuo na ishara zisizokuwa na kikomo hazikukata kiu ya upendo wake wa kumpenda Mwenyezi Mungu, badala yake, kila alivyozidi kunywa ndivyo kiu yake ilivyoongezeka. Alitaka kuwa karibu na Muumba wake zaidi na zaidi. Aliendelea kupandishwa kutoka kwenye daraja moja kwenda nyingine na katika kila hatua alikuwa akiomba maghfira na kuomba dua akisema: *"Mola wangu! Sijaweza kukujua kama ninavyotakiwa na kama unavyostahiki ... sijaweza kukutumikia kama unavyostahiki..."* [3]

Rumi alivuka mipaka ya maarifa kwa kukomaza aina hii ya mambo ya siri na hekima. Akawa mmoja wa marafiki wakubwa wa Mwenyezi Mungu na ambaye watu wamaenufaika na moyo wake kwa karne nyingi.

2.Quran, 94: 1
3.Munawi, Fayz al Kadir, II,520

KAMA WALII WAKE YUKO HIVI ...

Gurhu Hatun (mwanamke kutoka Gergia), binti wa Sultan wa Kiseljuk na mwanafunzi wa Rumi, alimuagiza ayn al-Dawlah, mchoraji maarufu wa Ikulu, kwenda kwa Rumi akachore picha yake (Rumi) kwa siri na amletee. Mchoraji huyo kwa kiasi fulani na bila kudhamiria akamueleza Rumi hali husika. Rumi akamwambia huku tabasamu likichomoza usoni mwake:

"Ukiweza, fanya ulivyoambiwa!"

Akaanza kuchora. Lakini, mwishoni akagundua kuwa picha aliyokuwa akichora haiendani na mtu aliye mbele yake na hivyo akaanza upya kuchora. Hivyo, wakati akijaribu kuchora picha ya Rumi, alipoteza (aliharibu) vipande ishirini vya karatasi. Hatimaye aligundua kuwa asingeweza kuchora na hivyo akaacha.[4]

Tukio hili liliuamsha moyo wa mchoraji. Alizama katika fikra nene za mshangao, haiba, na kutetemeka na kumfanya asafiri katika ulimwengu wake mwenyewe. Mwishoni, mchoraji huyo, ambaye alimuona Mtume wa Mwenyezi Mungu kupitia dirisha lililofunguliwa katika moyo wake, akatamka maneno yafuatayo:

"Kama walii wa dini yuko hivi, Mtume wake atakuwaje!"

ANAPIMWA KWA UWEZO WA ALIYEMTUMA

Khalid bin Walid ﷺ, katik moja ya safari zake, alitumia usiku mmoja pamoja na kabila moja la Waislamu. Kiongozi wa kabila hilo akamuuliza:

4.Picha hizo zinapatikana katika makumbusho ya Mawlana

"Unaweza kutuelezea kuhusu Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷻ?"

Khalid ؓ akasema:

"Liko nje ya uwezo wangu kuelezea mazuri yasiyo na kikomo ya Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ. Sasa, kama wataka nikuambieni kwa undani, haiwezekani kabisa!"

Kiongozi wa kabila alipomwambia:

"Tuelezee unachojua! Tuelezee kwa ufupi!"

Khalid akajibu:

"Yule aliyetumwa anaangaliwa kwa uwezo wa yule aliyemtuma!..." [5]

Kwa maneno mengine, kwa kuwa aliyemtuma ni Mola wa walimwengu, unaweza kuvuta picha ya utukufu wa huyo aliyetumwa!..

Kwa muhtasari, mwanadamu hana uwezo wa kutosha kuuelewa kikamilifu ukuu wa Mtume wa Mwenyezi Mungu, Muhammad ﷺ. Hatuwezi kuupima ukuu wake kwa akili zetu zenye kikomo. Kwa sababu ya ufahamu mdogo wa mwanadamu, Mola wetu anamtambulisha na kumsifu kama ifuatavyo:

" Hakika Mwenyezi Mungu na Malaika wake wanamsalia Nabii. Enyi mlioamini! Msalieni na mumsalimu kwa salamu." (33: 56) Mola wetu Mtukufu Yeye mwenyewe anaitangazia akili ya mwanadamu kuwa Mtume Muhammad ﷺ ndiye kiumbe mkamilifu zaidi.

Katika hali hii, kumjua Mtume Muhammad ﷺ ni hatua muhimu mno katika kuwa mja wa Mwenyezi Mungu. Bila kumjua,

5.Munawi, V, 92/6478; Kastalani, Tafsiri ya Mawahib Laduniyyah, Istanbul 1984, uk. 417

kumuelewa vizuri, kumfuata, na kupata fungu letu kutoka katika hali yake ya kiroho, imani yetu haiwi kamili, hatuwezi kuielewa Qur'an Tukufu na wala hatuwezi kuwa waja wa kweli.

Qur'an Tukufu inasema:

" Ameuteremsha Roho muaminifu, Juu ya moyo wako, ili uwe katika Waonyaji, Kwa ulimi wa Kiarabu ulio wazi." (26: 193-195)

Miaka yake ishirini na tatu ya utume ilikuwa kama tafsiri ya Qur'an Tukufu. Siri na hekima za Qur'an zinaweza kujulikana tu kwa kuchukua mafunzo kutoka katika ulimwengu wa kiroho wa Mtume wa Mwenyezi Mungu.

NJIA BORA YA KUMJUA MTUME ﷺ

Mtume wa Mwenyezi Mungu anaweza kujulikana vizuri kwa kumsoma kwa moyo badala ya kumsoma kupitia vitabu. Kwa maneno mengine hakuna budi kumuelewa kwa kupata muongozo na hali ya kiroho kutoka katika ulimwengu wa kiroho wa wanazuoni na wana-maarifa ambao ni wachamungu na wanafuata kanuni za maadili ya Mtume katika kila kipengele cha maisha yao. Tunaweza kumjua kwa ukamilifu kwa hisia za dhati za waumini wema. Tunaweza kumjua kulingana na kiwango cha uchamungu wetu.

Imeamriwa katika aya ifuatayo:

"...basi mcheni Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu ndiye anayekufundisheni..." (2:282)

Hivyo, kusoma maisha ya Mtume ﷺ hakuwezi kukamilika kwa kujishughulisha tu katika kusoma maandishi. Wale wanaoyajua vizuri maisha ya Mtume ﷺ ni wale ambao maisha yao

yanafafanana na maisha ya Mtukufu Mtume ﷺ. Wanaomjua vyema ni marafiki wema wa Mwenyezi Mungu, ambao huishi katika sunnah za Mtume ﷺ kwa hisia ya hali ya juu, na ambao hulifuata jua hilo la rehema kwa upendo na mahaba. Hayo ni kwa sababu wanafuata njia yenye nuru ya Mtume wa Mwenyezi Mungu kwa utiifu kamili na kuungana na kivuli chake.

Kama ilivyothibitishwa na aya ya Qur'an Tukufu, Mtume ﷺ hakuzungumza kwa matamanio yake mwenyewe. Alikuwa ni mfasiri, mtekelezaji, mfafanuzi, mtangazaji, na mwakilishaji wa kile kinachofunuliwa kwake.

Wale marafiki wa Mwenyezi Mungu waliofikia daraja ya *fana fi al-Rasul*, yaani wale waliotopea na kuyeyuka ndani ya upendo wa Mtume wa Mwenyezi Mungu, nao pia hawazungumzi kwa tamaa na matamanio yao. Wameondosha katika ulimwengu wao wa ndani kila kitu isipokuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, kama filimbi ya matete, sauti zote za uongofu zinazotoka kwao ni sehemu ya pumzi ya Mtume ﷺ ambaye maadili yake wameyafuata. Nyoyo zao ni vioo vyenye kung'aa ambavyo huakisi nuru na ukweli wa Mwenyezi Mungu. Kama ilivyosemwa katika maneno ya Mtume ﷺ: *"...Mwenyezi Mungu huwa ndiyo sikio lake analotumia kusikia, na macho yake anayotumia kuona, na mkono wake anaoshikia, na miguu yake anayotembelea..."* (Bukhari, Kitab al-Riqaq, 38)

Mtume ﷺ ni jua linalotawanya msisimko wa furaha ya milele na kuuangazia ulimwengu wote. Marafiki wa Mwenyezi Mungu, ambao ndiyo warithi wa Mitume, ni mwezi ambao ni sawa na kioo. Uwepo wa mwezi unategemea uwepo wa jua. Hayo ni kwa sababu mwezi huakisi mwanga, nuru, uzuri na ukuu unaotoka juani.

Sheikh Saadi anahadithia kisa kifuatacho kwa namna ya istiari kutoka kwenye kitabu chake kiitwacho *Gulistan ("ardhi*

ya waridi"). Anaelezea jinsi marafiki wa Mwenyezi Mungu wanavyopata uzuri wao kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu na jinsi hali zao zote za kiroho zinavyotokana na hali ya kiroho ya Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ.

"Siku moja mtu mmoja alikwenda katika bafu ya umma. Katika bafu hiyo ya umma mmoja wa rafiki zake akampa udongo wenye kunukia (udongo msafi) ili ajisafishe. Harufu maridhawa iliyokuwa ikitoka kwenye udongo ule ikaugusa moyo. Mtu yule akauuliza udongo:

"Ewe mpendwa! Je wewe ni miski au kahawia? Nina furaha kutokana na harufu yako nzuri ambayo inazivutia nyoyo..."

Udongo ukamjibu kama ifuatavyo: "Mimi siyo miski wala kahawaia. Mimi ni udongo wa kawaida. Lakini, nilikuwa chini ya jani la waridi na kila alfajiri nilikuwa nikidondokewa na umande unaotoka kwenye jani la waridi. Hivyo, harufu nzuri unayoisikia na kuziburudisha nyoyo ni harufu ya mawaridi hayo..."

Waridi ni alama ya Mtume Muhammad ﷺ. Dunia hii ni kama darasa na katika darasa hili kuna mafunzo muhimu: Kuwa na habari za Mfalme wa mawaridi ﷺ,Kunufaika kutokana na harufu takatifu ya hili waridi na ulimwengu wake wa kiroho, na Kuwa umande juu ya majani ya waridi hili ﷺ.

Muumini anapoanza kuhisi upendo wa Mtume ndani ya kina cha nafsi yake, na akaanza kupata fungu lake kutokana na hali ya kiroho ya Mtume, basi hakika yu katika njia ya kuwa sawa na yeye na kupata raha kutokana na Upendo wake.

KUMPENDA MUHAMMAD ﷺ

Maarifa yetu kuhusu Mtume wa Uislamu yanategemea kiwango cha upendo tulionao kwake.Mtume ﷺ anasema:

"Mtu atakuwa pamoja na wale awapendao." (Bukhari, Adab, 96)

Kwa maneno mengine, upendo ni kitu chenye athari sana ambacho huleta hali ya kuwa pamoja kiroho. Upendo huziunganisha nyoyo kama mtandao wa umeme. Hali hii huwa kama vyombo vya mawasiliano, maadamu mawasiliano yao kwa njia ya upendo yanadumu basi hali zao pia huwa zenye kufanana. Kuonja, kuchukia, hisia, na hata mtazamo huelekea kuwa kitu kimoja.

Watu wawili wanaopendana kwa dhati hubadilisha zawadi kwa kupeana kile ambacho wote kwa pamoja wanakipenda. Ataleta maua yanayopendwa na mwenzake; na anafanya kinachopendwa na mwenzake. Hayo ni kwa sababu yule anayependa hupenda pia kile kinachopendwa na mpendwa wake na huchukia kile kinachochukiwa na mpendwa wake; kamwe hasahau na daima humzungumzia mpendwa wake.

KWA SABABU ALIKUWA AKIFANYA HIVI NA VILE

Tangu akiwa mtoto, Abdullah bin Omar رضي الله عنه alikuwa amejitolea kwa dhati kumfuata kwa karibu Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ, na maisha yake yote aliyatumia katika kujaribu kufanya kila kitu kilichofanywa na Mtume ﷺ- iwe anajua hekima yake au la.

Kwa mfano, siku moja alimuona Mtume ﷺ akinywa maji kutoka katika kisima fulani, naye mara kwa mara akawa anakwenda kunywa katika kisima hicho; akimuona Mtume akiwa amepumzika chini ya kivuli cha mti fulani naye pia huanza kwenda kupumzika katika mti huo; tena akimuona Mtume ﷺ amekaa kwa muda fulani akiwa ameegemea jiwe, naye pia hufanya hivyo.

Siku moja Abdullah bin Omar ﵁ alikaa kwenye jiwe ubavuni mwa jabal al-Rahma (Mlima wa rehema) wakati wa Hijja. Alipoulizwa sababu ya kufanya hivyo, akajibu:

"Bwana wetu Mtume ﷺ alikaa kwenye jiwe hili kwa muda baada ya hotuba yake ya mwisho."

Mara nyingine, alipokuwa safarini pamoja na msafara, aliusimamisha msafara kwenye eneo fulani akaenda kwenye mti mmoja uliokuwa jirani na mlima na kisha akarudi. Alipoulizwa akajibu kuwa:

"Siku moja tulipokuwa tukipita hapa Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikwenda kwenye mti ule na kurudi."

Hali ya swahaba huyu mwaminifu katika umauti wake nayo pia inatupa mafunzo muhimu:

Siku moja Ibn Omar ﵁ ghafla aliumwa. Kwa mujibu wa msimulizi, alipewa sumu na Hajjaj, mtawala wa enzi hizo. Alikuwa katika maumivu makali. Watu wakamchukua mzee huyu na kumpeleka hemani. Wakati huo hakuwa na uwezo wa kuongea wala kuhamisha mikono au miguu yake. Alijaribu kuwaambia kitu watu waliokuwa hapo lakini wakashindwa kujua alichokuwa akiomba. Wakati wakisubiri hapo bila msaada, mara mtu mmoja aliyekuwa akimjua vizuri Ibn Omar ﵁ akaingia. Wakamwambia kwamba Ibn Omar alikuwa akijaribu kuwaambia kitu lakini wameshindwa kumuelewa. Mtu huyo akawauliza:

"Mlifanya nini dakika moja iliyopita?" Wakasema:

"Tulimsaidia kuchukua udhu."

Yule mtu akauliza tena:

"Sawa, wakati wa kuchukua udhu, mlifikicha masikio yake?" Wakasema:

"Hapana, tulisahau!" Kisha yule mtu akasema:

"Hamumjui huyu mtu? Katika maisha yake yote amejaribu kufanya kila kitu

kilichofanywa na Mtume ﷺ na kujitenga na kila kitu ambacho Mtume ﷺ alijitenga nacho.

Baada ya kusikia hivyo, wakafikicha nyuma ya masikio yake. Baada ya kufanya hivyo, wasiwasi wa Abdullah bin Omar ukatoweka, akatulia na kutabasamu na baadaye akaikabidhi roho yake kwa amani.

Kwa hakika, maswahaba waaminifu ambao nyoyo zao zilijaa upendo wa kumpenda Mtume ﷺ walikuwa makini sana siyo tu kutekeleza maagizo ambayo aliwaambia waziwazi, lakini pia hata ujumbe usiokuwa wa bayana.

Walikuwa makini sana kiasi kwamba ilitosha tu kumuona akifanya jambo jema mara moja tu. Haikuhitajika Mtume ﷺ kuliamrisha tena, bali wangelitekeleza mara tu wanapoliona na kuendelea kulitekeleza katika maisha yao yote.

Anas ؓ anasema:

"Siku moja nilimuona Mtume ﷺ akiswali swala ya Dhuha raka sita. Baada ya siku hiyo sikuicha kamwe swala hiyo."

Mtu ambaye anasimulia hadith hii, Hasan al-Basri (q.s), ambaye alikuwa na umakini kama huo, anasema:

"Baada ya maneno haya ya Anas ؓ, nami pia sikuacha kuswali swala ya Dhuha." (Tabarani, Awsat, II, 68/1276)

Jabir ؓ alisimulia tukio lifuatalo:

"Siku moja, Mtume ﷺ alinishika mkono na kunichukua mpaka nyumbani kwake. Alichukua kipande cha mkate na kuuliza familia yake:

"Kuna chochote kinachoenda pamoja na hii?"

Wakasema:

"Hakuna kitu nyumbani isipokuwa siki."

Mtume ﷺ akasema:

"Usuhuba mzuri ulioje wa mkate na siki!"

"Tangu niliposikia hivyo kutoka kwa Mtume ﷺ nami nikapenda kutumia siki." (Muslim, Ashribah, 167 - 169)

Kwa hakika walibadilisha hata ladha na vile wanavyovipenda kwa sababu ya mapenzi yao kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ. Mfano mwingine wa hali hii ya akili ni ile inayomhusu mwanachuoni mkubwa wa dini, Imam Nawawi. Alijaribu kumfuata Mtume ﷺ kwa umakini mkubwa kiasi kwamba kwa kuwa hakujua namna Mtume alivyokula tikiti, alikataa kulionja, akaacha kabisa kulila, katika maisha yake yote kwa hofu ya kwenda kinyume na mwanendo wa Mtume ﷺ.

Mtu mwingine ni Ahmad Yasawi (q.s), rafiki mkubwa wa Mwenyezi Mungu ambaye alikuwa akiipenda Nuru hiyo ya Uongofu, aliacha kuzunguka ardhini katika umri wa miaka 63 kwa kuwa Mtume ﷺ alifariki dunia akiwa na umri wa miaka 63. kwa muda wa miaka kumi mpaka mauti yalipomfika, aliendeleza maisha yake ya kuwaongoza watu akiwa katika maeneo yanayofanana na kaburi.

Muadhini wa Mtume ﷺ, Bilal ؓ hakuweza kukaa Madina baada ya kifo cha Mtume ﷺ. Swahaba huyu mwaminifu wa Mtume wa Allah, ambaye aliishi maisha yake yaliyobaki akii-

subiri kwa hamu siku atakayokutana tena na Mtume, alifariki dunia katika umri wa miaka sitini mjini Damascus. Akiwa katika kitanda chake cha mauti, alisema:

"Kesho, Mwenyezi Mungu akipenda, nitakutana na marafiki zangu wapendwa, Muhammad ﷺ na maswahaba Wake." Wakati mke wake akilia kwa huzuni na kusema:

"- Tazama kitu kilichonisibu!" Bilal ؓ, ambaye moyo wake ulikuwa amejaa mapenzi ya kumpenda Mtume ﷺ alikuwa akifurahia na kusema, "Oh, uzuri ulioje!" Zahabi, Siyar, I, 359)

Naam, uhai ukitumika kama uhai na maisha ya Bilal ؓ, basi kifo huwa ni kama harusi ambapo furaha ya muungano hushuhudiwa.

Uzuri ulioje wa maneno ya Rumi anaposema:

"Njoo ee moyo! Karamu ya kweli ni karamu ya kuungana na Muhammad. Hayo ni kwa sababu mwanga wa ulimwengu unatokana na nuru ya wajihi wa kiumbe huyu mtukufu."

Kwa hakika, kwa zile nyoyo zenye kupendwa ambazo ni kama vipepeo wanaovutwa na mwanga huu, kifo huwa ni kama usiku wa harusi na wakati wenye furaha ya kuungana.

Kwa hakika, hali ifuatayo ya Aisha ؓ, ambaye alikuwa ni swahaba wa maisha wa Mtume ﷺ na mama wa waumini, inatupa somo kubwa:

Mtume ﷺ aliungana na Rafiki wa Juu (Mwenyezi Mungu) ndani ya chumba cha mama yetu Aisha na akazikwa hapo. Mama yetu Aisha, ambaye alipata baraka ya kuwa mke wa Mtume wa Mwenyezi Mungu, hakukiacha chumba hicho baada ya kifo cha Mtume. Aliendela kuishi humo kama mlinzi wa kaburi la mfalme jirani kabisa na kaburi la furaha.

Baada ya miaka miwili na miezi mitatu, baba yake, Abu Bakr ﷺ pia akafariki dunia. Naye alizikwa karibu na miguu ya Bwana wetu. Katika chumba ilibaki nafasi ya kaburi moja tu. Aisha ﷺ alikuwa akiichukulia nafasi hiyo kuwa yake. Lakini, pindi Umar ﷺ alipokuwa katika kitanda cha umauti alimuomba ruhusu azikwe hapo. Aisha akaonyesha tabia ya hali ya juu ya ithaar na akamuachia Umar.

Kwa mujibu wa simulizi hiyo, kabla ya Umar kuzikwa katika chumba hicho, mama yetu Aisha ﷺ alikuwa akitembea hapo kwa uhuru. Lakini baada ya Umar kuzikwa, aliweka pazia ili kukigawa chumba hicho katika sehemu mbili kutokana na hisia kali ya staha aliyokuwa nayo.

Wosia ufuatao aliuandika alipokaribia kufariki dunia. Wosia huu ni ishara ya kipekee inayooonyesha msisimko wa mtu unapokaribia wakati wa kuungana na Mtume ﷺ:

1. Nitakapokufa, baada ya maandalizi yote nizikeni bila kunicheleweshа hata kama itakuwa usiku.

2. Wakati wa kuubeba mwili wangu kwenda makaburini, washeni matawi makavu ya mtende pembezoni mwa jeneza yangu.”

Kwa mujibu wa desturi za Arabia ya kale, walikuwa wakiwasha matawi makavu ya mitende wakati wa kumpeleka bibi harusi nyumbani kwa bwana harusi katika usiku wa harusi. Kwa hakika, inaonekana wosia huu wa mama yetu Aisha ﷺ ndiyo iliyoipa nguvu nadharia ya Rumi ya “Shab-i Arus” (Usiku wa harusi).

KUZIPA UMUHIMU SUNNAH (ADA NA DESTURI ZA MTUME MUHAMMAD ﷺ)

Ushahidi mkubwa unaothibitisha kuwa mtu anamjua Mtume ﷺ na kumpenda ni uwezo wake wa kutekeleza sunnah zake kikamilifu. Kutekeleza sunnah zake bila kumpenda moyoni ni kumfuata kwa nje tu na kwa kujilazimisha na utekelezaji huo hauna nguvu, hali ya kiroho na wala thawabu.

Abdullah bin. Daylami anaelezea umuhimu wa utiifu pamoja na mapenzi ya kuzipenda sunnah za Mtume ﷺ kama ifuatavyo:

"Kulingana na nilivyosikia, mwanzo wa uharibifu wa dini utaanza na kujitenga na sunnah. Kama ambavyo kamba huanza kupoteza uzi mmoja mmoja, na kisha ikakatika, hatimaye dini itaharibika kwa kuziacha sunnah za Mtume ﷺ moja baada ya nyingine." (Darimi, Muqaddimah, 16)

Kwa maneno mengine, kuziondosha sunnah katika maisha yetu - Mungu aepushie mbali - kutaifanya furaha yetu ya milele itegemee kamba moja nyembamba ya pamba.

Kwa sababu ya jambo hili, muujiza mkubwa wa marafiki wa Mwenyezi Mungu na wana-maarifa wanaomjua vyema Mtume ﷺ ni kufuata na kuishi kwa mujibu wa sunnah za Mtume ﷺ kwa hisia kubwa.

Bila shaka, Mtume wa Mwenyezi Mungu ndiye mtu mwenye kustahiki mno kupendwa, shakhsia ya hali ya juu ambayo Mwenyezi Mungu Mtukufu ametubariki kwayo, na muujiza mkuu uliotokea kwa wanadamu. Ulimwengu wa ndani wa moyo wake ni makazi ya uzuri ambao ni zaidi ya bustani ya pepo, uliopambwa kwa maua ya nadra na mzuri na mawaridi yenye miski na harufu nzuri.

Tunapofika hapa tunatakiwa kujiuliza maswali kadhaa:

Tupo katika hali gani linapokuja suala la kufaidika na upepo mwanana wa hali ya kiroho kutoka katika bustani hiyo ya pepo?

Ni kwa kiwango gani maisha yetu yanafanana na maisha yake?

Maisha yetu ya utafutaji yanakaribiana kwa kiwango gani na mtindo ambao anaukubali?

Ni kwa kiwango gani maisha yetu ya kijamii yapo ndani ya mipaka aliyoianzisha?

Wakati moyo wake ukipiga kwa huruma ya kuuhurumia umma wake, tuna hisia kwa kiwango gani juu ya masikini, wanyonge, mafukara, waliodhulumiwa, mayatima, na wale wanaosubiri kuongozwa kwenye njia iliyonyooka?

Katika kuendana na tabia zake njema, ni kwa uzuri kiasi gani tunautangaza umma wake na wajihi wenye tabasamu wa Uislamu, jengo lake la kiroho, muundo wake wa kiroho, uzuri, wema na unyoofu?

Tunamuomba Mwenyezi Mungu atujaalie kuwa waja wake wenye ikhlasi na watu wenye kustahiki kuwa katika umma wa Mtume ﷺ! Tunamuomba atupe fursa ya kumsoma Mtume ﷺ kwa jicho la kiroho, ambaye amemleta kwetu kama shakhsia ya kipekee mpaka siku ya hukumu. Tunamuomba atupe nafasi ya kupata sehemu katika moyo wake na kuishi kwa kufuata sunnah zake! Atujaalie fursa ya kukutana na Mtume wetu ﷺ chini ya bendera ya himidi na kunywa katika chemchem adhimu ya Kawthar na kupata uombezi wake mkuu.

Amin...

STAHA

Utumwa huanza na kuijua nafasi ya mtu. Pindi mtu anapoitambua kikamilifu nafasi ya mtu, hakuna nguvu atakayokuwa nayo ya kumfanya awe na kiburi, ubinafsi na hata uwepo wake mwenyewe.

Kama ilivyo kwa matawi yenye matunda yaliyoiva, Waislamu wenye maarifa, hekima na ukomavu wa kiroho ni wenye staha na ukarimu. Huyageuza maisha yao yote kuwa hazina, ambayo kila mtu anaweza kunufaika nayo.

STAHA

Kinachomfanya mtu kuwa mwanadamu, kikamtambulisha kwenye asili yake ya msingi, kikampeleka kwenye lengo lake la awali, na hatimaye kumgeuza kuwa mwanadamu kamili ni tabia njema zilizotengenezwa kwa imani.

Thamani halisi, sifa, heshima, ukomavu, na utukufu wa mtu hutokana na kiwango chake cha maadili. Kuwa mja unayependwa na kuridhiwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu kunahitaji ukomavu wa kiroho, na njia ya kuelekea kwenye ukomavu huu inapitia kwenye **"mafunzo ya kiroho".**

MARAFIKI WA MWENYEZI MUNGU

Kama ambavyo ujuzi na vipawa huhitaji muongozo wa mshauri, marafiki wa Mwenyezi Mungu ndiyo wanaoonyesha njia bora na inayofaa zaidi kwa ajili ya shakhsia na tabia ya mtu. Kwa sababu wao ni waumini wenye busara, wema na wakamilifu

- ambao wamekusanya vipengele vya ndani na vya nje vya dini katika shakhsia zao,

- ambao wamefikia ukamilifu wa kimwenendo kwa kufikia hali na daraja za kiroho kwenye njia ya uchamungu na unyoofu,

- ambao wamepata raha ya imani na undani wa hisia kwa kupanua upeo na kuielewa hii dunia na Akhera

- ambao kazi yao kubwa ni kumuokoa mwanadamu kutoka kwenye mashimo ya nafsi na giza la maadili mabaya na kuwainua kwenye maadili mema, ukomavu wa kiroho na kutaalamika.

Kwa sababu ulimwengu wao wa kiroho daima uko pamoja na Mwenyezi Mungu Mtukufu, huendelea kuwakumbusha watu kuhusu Mwenyezi Mungu. Wale wenye kufuata nyayo zao hufikia kwenye hekima na maarifa ya kuyaangalia maisha na matukio kupitia dirisha la Akhera.

Tabia na matendo ya marafiki wa Mwenyezi Mungu daima yanaambatana na radhi za Mwenyezi Mungu; kwa sababu, Mtume wa Mwenyezi Mungu anatuhabarisha kuwa Mwenyezi Mungu anasema:

"Mja wangu huendelea kunikurubia kwa uchamungu zaidi ya kiwango kinachotakiwa, mpaka humpenda; Nami huonyesha upendo wangu kwa kuwa jicho lake analotazamia, sikio analosikia, mkono anaoshikia..." (Bukhari, Riqaq, 38; Majma' al-Zawaid, II, 248)

Maadili ya marafiki wa Mwenyezi Mungu hubeba ishara zitokazo katika ulimwengu wa kiroho wa Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ, ambao ulikuwa ufafanuzi wa kivitendo wa Qur'an Tukufu. Marafiki wa Mwenyezi Mungu, wanaojitahidi kutumia mtindo wa maisha ya Mtume wa Mwenyezi Mungu katika maisha yao, ni kama vioo vinavyoakisi uzuri wote wa maadili ya Mtume ﷺ. Hii ndiyo sababu kwamba wale wanaofuata na

kuchunga kikamilifu matendo na mwenendo wa marafiki wa Mwenyezi Mungu hushuhudia ishara nzuri za tabia na maadili ya Mtume ﷺ.

Malipo ya ikhlasi na usafi wao wa moyo, Mola Mtukufu amewajaalia watumishi wake wema uwezo wa kuzisimamia nyoyo. Kwa sababu huanza wao kuzitekeleza kanuni za Uislamu katika maisha yao wenyewe, hivyo huwakilisha na kuhubiri neema ya Uislamu kwa ulimwengu wote unaowazunguka. Hii ndiyo sababu kwamba wamejaaliwa neema ya kipekee ya kuwashawishi na kuwaathiri watu.

Maneno yasiyofaa katika maisha na tabia zisizokuwa na ikhlasi ndani yake ni kama matendo matupu. Husahaulika kirahisi chini ya upepo mkali wa maisha na kutoacha athari yoyote; wakati ambapo sababu ya marafki wa Mwenyezi Mungu kuacha athari zisizofutika katika nyoyo ni ikhlasi yao na upendo katika matendo yao.

Katika suala hili, Usufi, kama unavyoelezewa na Yunus Emre, hauna maana ya kuacha mambo ya kidunia na kuridhika tu kutaja majina ya Mwenyezi Mungu katika nyumba ya mafunzo ya Kisufi. Kinyume chake, Usufi kwa asili yake ni kuwa na uwezo wa kusonga mbele kwenye njia ya hali ya kiroho na kuungana na Mwenyezi Mungu kwa njia ya ishara zisizokuwa na kikomo za maisha na ulimwengu. Hili linategemea mtu kutambua hali yake ya kutokuwa chochote ikilinganishwa na ishara na uwezo na Nguvu za Mwenyezi Mungu na kutumia kila pumzi moja kwa kuelewa kuwa anahitajia msaada wa Mwenyezi Mungu.

Marafiki wa Mwenyezi Mungu ni njia za baraka na rehema kwa majirani zao. Wao ni mikono ya huruma inayoyakumbatia makundi yote ya jamii. Wao pia ni kama sumaku inayowavu-

ta waumini, kwa kuwa Mwenyezi Mungu amewapenda watu hawa wema na watu nao pia wanalazimika kuwapenda.

Qur'an Tukufu inasema:

"Hakika walioamini na wakatenda mema Arrahmani Mwingi wa Rehema atawajaalia mapenzi." (19: 96)

Hii ndiyo sababu kwamba marafiki wa Mwenyezi Mungu hawasauliki baada ya kufa kwao na huendelea kuishi katika nyoyo za wale wanaowapenda. Upendo huu wa kuwapenda marafiki wa Mwenyezi Mungu ni neema kubwa kwa nyoyo zenye bahati; kwa sababu Mtume ﷺ ameahidi kuwa siku ya Kiyama kila mtu atakuwa pamoja na wale aliowapenda. Kujaribu kuwapenda na kuwa karibu na waja hawa wa kipekee wa Mwenyezi Mungu humfanya mja awe karibu zaidi na Mola wake.

Tukiwapenda marafiki wa Mwenyezi Mungu na kutaka kufufuliwa pamoja nao siku ya Kiyama, tunatakiwa kufanya juhudi ya kuzijua tabia zao njema; kwa sababu alama ya upendo wa mtu kwa mtu ni kujaribu kuwa kama mpendwa wake.

Katika suala hili, ili kuzijua tabia njema za Marafiki wa Mwenyezi Mungu, inatakiwa kuzielewa ishara na sifa hizi kwao. Ifuatayo ni mojawapo ya tabia na sifa adhimu za marafiki wa Mwenyezi Mungu:

KIWANGO CHA HALI YA JUU CHA KUJINYENYEKEZA: STAHA

Kujinyenyekeza kwetu kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, kwanza, ni kitendo cha utambuzi. Ni msingi wa kujinyenyekeza kwetu kutambua hali yetu ya kutokuwa chochote mbele ya Uwezo na Nguvu za Mwenyezi mungu, na kuelewa kwamba

tumetoka katika hali ya kutokuwepo kwenda kwenye hali ya kuwepo kwa Utashi Wake na kujua kwamba tunaendelea kuwepo kutokana na baraka Zake na kujua ukweli kwamba tunamhitajia katika kila pumzi moja tunayovuta na kila sekunde ya uhai wetu.

Kwa maneno mengine, kujinyeyekeza kuna maana ya kuwa na uwezo wa kuona hali yetu dhaifu mbele ya Ufalme wa Mungu na kuijua nafasi yetu. Pindi mtu anapoitambua kikamilifu nafasi yake, hukosa nguvu ya kudai kuwa na kiburi, ubinafsi na hata uhai wake mwenyewe. Kisha huonyesha shukrani, kuridhika na kutii kwa unyenyekevu kama asemavyo Aziz Mahmud Hudayi:

"Wewe Ndiwe unayetwaa; Wewe ndiwe Mwenye kutoa; Wewe ndiwe Mwenye kutenda! Tuna kitu gani mbali na kile ulichokitoa?"

Wale wasiokuwa na sehemu katika staha ni wale wasiotambua Ukuu wa Mola wao.

Staha ya kweli humfanya mja akiri kuwa yeye si chochote mbele ya Ukuu wa Mwenyezi Mungu na kukiinamisha kichwa chake, kama inavyojionyesha katika dua ifuatayo ya Mawlana jalal al-Din Rumi:

"Nimekuwa mja, nimekuwa mja, nimekuwa mja. Mimi, mja mnyenyekevu, nimeona aibu ya kutotekeleza utumwa wangu kikamilifu na nimekiinamisha kichwa changu (kwa aibu). Kila mtumwa hufurahi pale anapokombolewa. Mola wangu! Nimekuwa mwenye furaha kwa kuwa mtumwa wako."

Kutokana na ukweli huu, dua ya mjukuu wa Mtume ﷺ, Hassan رضي الله عنه baada ya kuizunguka Kaaba na kuswali rakaa mbili kwenye *maqaam Ibrahim*, ni mojawapo ya mifano bora ya tabia za utumwa:

"Mola wangu! Mja wako mdogo na dhaifu amekuja mlangoni kwako. Ewe Allah! Mja wake mnyonge amekuja mlangoni kwako! Mola wangu! Muombaji wako amekuja mlangoni kwako, Masikini wako amekuja mlangoni kwako..."

Baada ya dua hii yenye hisia, Hassan ﷺ alikutana na masikini njiani ambao walikuwa wakila mkate mkavu. Aliwatolea salamu, wakamuita kwenye chakula chao cha staha. Mjukuu wa Mtume ﷺ, Hassan ﷺ akakaa nao na kusema:

" Mkate huu usingekuwa umetokana na sadaka ningekula pamoja nanyi." Kisha akasema:

"Twendeni nyumbani kwangu." Baada ya kuwapa chakula kizuri, aliwapa masikini hao nguo nzuri na kuwapa kiasi kikubwa cha pesa na kisha akawarejesha wakiwa na furaha sana." (Absshihi, al-Mustatraf, Beirut,1986, I, 31)

Hii ndiyo hali ya staha ya kweli na tabia tukufu ya kujinyenyekeza, inayomfanya muumini aishi katika hisia ya ndani mbele ya Mola wake na mbele ya viumbe wengine. Wale wanazipamba roho zao kwa tabia hii ya kipekee huwa na busara katika matendo na mwenendo wao. Tabia hii hujionyesha katika kukaa, kusimama, kutembea, kuchagua nguo, kuongea, na, kwa ufupi katika matendo yao yote.

Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

"Na waja wa Arrahman Mwingi wa Rehema ni wale wanaotembea ulimwenguni kwa staha, na wajinga wakiwasemeza hujibu: Salama!" (25: 63)

"Wala usitembee katika ardhi kwa maringo. Hakika wewe huwezi kuipasua ardhi wala kufikia urefu wa milima." (17: 37)

“Wala usiwabeuwe watu, wala usitembee katika nchi kwa maringo. Hakika Mwenyezi Mungu hampendi kila anayejivuna na kujifakhirisha.” (31: 18)

Katika aya hizi, kutembea kwa maringo na matambo kumekatazwa kabisa. Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ daima alikuwa akitembea kwa haraka hali ya kuwa macho yake kayainamisha chini kana kwamba anashuka mlimani. Hii ilikuwa ishara ya unyenyekevu wake. Kwa hakika, tabia hii imekuwa miongoni mwa kanuni za Masufi, ambapo wanaiita kama **“nadhar bilqadam - kutazama miguuni.”**

Kuna ubora mwingi katika kutazama miguuni wakati wa kutembea kama vile staha, tabia njema, kujua nafasi yako, kuyalinda macho yasitazame mambo ya haramu, kutii maamrisho ya Mwenyezi Mungu na Mtume Wake.

Unyenyekevu siyo tu katika kutembea bali katika vipengele vyote vya maisha; kwa kufanya hivyo inakuwa sababu ya kupata upendo na radhi za Mwenyezi Mungu. Ukweli huu umeelezwa katika hadith ifuatayo:

“...Mwenyezi Mungu huzinyanyua daraja za wale wanaoishi kwa staha kwa ajili ya Mwenyezi Mungu; na huzishusha daraja za wale wafanyao maringo.” (Haythami, x, 325)

Mwalimu mkubwa wa Usufi, Mawlana Jalal al-Din Rumi anaashiria unyenyekevu wa ardhi, na anawalingania watu kuwa kama ardhi kwa staha katika tungo zifuatazo:

“Mwenyezi Mungu Mtukufu alisema, “Enyi watu! Tazameni vizuri namna nilivyopandikiza mbegu itokanayo na roho yangu ndani ya mwili wenu ulioumbwa kutokana na ardhi, kisha nikakuinueni; nyinyi ni vumbi la ardhi, na nimewainua juu. Nimekujalieni akili na upendo. Hivi mnatenda matendo

yatokanayo na ardhi (staha), ili niwafanye kuwa wakuu juu ya viumbe wote." [6]

Sheikh Sadi Shirazi anaashiria nafasi ya staha katika mafanikio ya kiroho na anaitafsiri hekima ya maji kama ifuatavyo:

"Mafuriko hutambaa chini kwa sababu ya kiburi chake. Kwa upande mwingine, tone la umande kwa sababu ya udogo na unyonge wake, jua lililinyanyua juu mawinguni."

Staha ni sababu ya kupata thawabu kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Imeelezwa katika aya ifuatayo kuwa:

"Na kila umma tumewafanyia mahala pa kuchinjia mihanga ya ibada ili walitaje jina la Mwenyezi Mungu juu ya vile walivyoruzukiwa katika wanyama wa mifugo. Basi Mungu wenu ni Mungu Mmoja tu. Jisalimishieni kwake tu, na wabashirie wanyenyekevu, ambao, anapo tajwa Mwenyezi Mungu nyoyo zao hutetemeka, na wanaovumilia kwa yanaowasibu, na wanaoshika Sala, na wanatoa katika tulivyowaruzuku." (22: 34-35)

Kwa hiyo, unyenyekevu na ikhlasi vina umuhimu mkubwa katika utekelezaji wa wajibu wetu kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu.

UPANGA NI KWA WALE WENYE SHINGO (NDEFU ZENYE JEURI NA KIBURI)

Watu wenye staha na wanaojitenga na umimi wanalindwa na aina nyingi za hatari za kiroho. Rumi (q.s) anauelezea ukweli huu katika istiari ifuatayo:

6.Mathnawi, juzuu III, 455 -456.

"Upanga ni kwa yule mwenye shingo (ndefu yenye kiburi); hakuna pigo linalokidondokea kivuli kilichotupwa (kimelala chini)" [7]

Kwa upande mwingine, unyenyekevu wa kweli unaompandisha mtu kiroho pia husababisha kuongozeka kwa hekima na maarifa ya mtu husika. Suala hili linaashiriwa ndani ya Mathnawi:

"Kwa sababu ya unyenyekevu unaweza kuonekana kama unapoteza heshima yako, lakini Mwenyezi Mungu atayajaalia macho yako uwezo wa uoni wa kweli. Kisha utaelewa maana ya maneno ya Mtume Mustafa ﷺ"Mola wangu! Tuonyeshe ukweli wa mambo kama uyaonavyo wewe". [8]

Staha hubeba huruma, kuwahudumia wengine, na ukarimu. Mtu mwenye staha ni mtu wa huduma – mwenye huruma, na mwenye upendo. Kinyume cha hayo, wale wasiokuwa na chembe ya staha ni wenye kiburi, wabakhili na wako mbali na baraka za Mwenyezi Mungu.

Imam Sharani anaeleza katika kitabu chake cha *Bahr al-Mawrud* kuwa:

"Wale wanaofaidika zaidi na mikusanyiko ya kiroho ni wale waliojazwa unyenyekevu na wenye staha kuliko watu wote; kwa sababu rehema ya Mwenyezi Mungu huteremka katika nyoyo za waja wenye staha na wanyenyekevu. Je hatuoni ya kwamba maji ya mvua huingia katika mashimo na mabonde na kuingia katika mito?"

7.Mathnawi, Juzuu IV, 2759
8.Mathnawi, Juzuu iv, 3565-3569

UNYENYEKEVU WA MTUME WETU ﷺ

Mtume wa Mwenyezi Mungu anasema:

*"Mwenyezi Mungu alinifunulia ya kwamba "**kuweni wanyenyekevu mno nyinyi kwa nyinyi kwamba asiwepo mingoni mwenu atakayevuka mipaka yake na kuonea wengine. Tena asiwepo miongoni mwenu atakayejivuna na kujifanya mkuu dhidi ya wengine."*** (Muslim, Janna, 64)

Mtume wetu ﷺ, ambaye alitumwa kuja kukamilisha tabia njema, alikuwa akikubali mwaliko wa kila mtu, awe mtu huru au mtumwa. Vile vile alikuwa akipokea zawadi anazoletwa na watu hata kama ikiwa ni zawadi ndogo kama kikombe cha maziwa na kuwakirimu kwa kuwapa zawadi mbalimbali. Aliyapa uzito mkubwa matakwa ya watu waliobezwa katika jamii kama vile watumwa na masikini.

Mtume ﷺ na maswahaba zake walipokuwa safarini kuelekea Badr, hapakuwepo na Ngamia za kutosheleza kila mtu. Hivyo, walikuwa wakifanya zamu kupanda. Mtume ﷺ alikuwa akifanya zamu na Sayyidna Ali ؓ na Abu Lubabah ؓ. ilipofika zamu ya Mtume kutembea, maswahaba wakamwambia:

"Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Tafadhali panda juu ya ngamia. Tunaweza kutembea badala yako."

Mtume ﷺ akajibu:

"Nyinyi siyo imara kunishinda mimi katika kutembea nami nahitaji thawabu nyingi kama nyinyi." (Ibn Sa'd, II, 21)

Ufunguzi wa Makka ulikuwa ushindi mkubwa ambao Mwenyezi Mungu aliwajaalia Waislamu baada ya miaka ishirini ya huzuni, taabu, na mateso; lakini Mtume ﷺ aliingia Makka bila kuonyesha alama za ushindi, bali akimshukuru Mwenyezi Mungu; alikuwa amekiinamisha kichwa chake juu ya ngamia.

Vile vile alikuwa akimuomba Mwenyezi Mungu amlinde na hisia za nafsi zinazoweza kuwa zimejitokeza kutokana na ushindi, pale aliposema:

"Ewe Allah! Hakuna maisha yenye hadhi kama maisha ya Akhera." (Waqidi, II, 824; Bukhari, Riqaq, 1)

Siku ya ufunguzi wa Makka, mtu mmoja, alimjia Mtume ﷺ huku akiwa anatetemeka na kumtaka amfundishe Uislamu. Mtume ﷺ akamtuliza bwana huyo kwa kumpa mfano utokanao na zama alipokuwa mnyonge sana:

"Usitetemeke ewe ndugu yangu! Mimi siyo mfalme au mtawala. Mimi ni mtoto wa jirani yako wa zamani wa Kiquraish, ambaye alikuwa akila nyama kavu." [9]

Tena siku hiyo hiyo, alimwambia Abu Bakr ؓ ambaye alimleta baba yake na kumuomba Mtume wa Mwenyezi Mungu amfundishe Uislamu:

"Ewe Abu Bakr! Kwa nini umempa tabu mzee wako kwa kumleta hapa? Je tusingeweza kwenda kwake?" [10]

Aliwaonya wale waliomuheshimu kupita kiasi kuwa:

"Msiniweke sehemu ambayo sistahili; kwa maana, Mwenyezi Mungu Mtukufu alinifanya kuwa mja kabla ya kunifanya kuwa Mtume." *(Haythami, ix,21)*

STAHA YA MASWAHABA

Kizazi cha maswahaba ambao walilelewa chini ya muongozo wa Mtume ﷺ, walipata fungu kutoka katika maisha yake ya mfano.

9. Tazama Ibn Majah, At'imah, 30; Tbarani, al-mu'jam al-awsat, II, 64.
10. Ibn Sad, v 451

Kwa mfano, Abu Bakr ﷺ, pamoja na kwamba alisifiwa na Mtume ﷺ kuwa "*wa pili katika marafiki wawili, ambaye watatu wake ni Mwenyezi Mungu"*[11] na *Abu Bakr anatokana na mimi, nami ninatokana naye..",*[12] alikuwa na staha sana kiasi kwamba alisema katika hotuba yake baada ya kuchaguliwa kuwa Khalifa:

"Enyi watu!Ingawa nimechaguliwa kuwa khalifa wenu, mimi si bora kwenu."

Hivyo, ingawa alikuwa na uwezo mkubwa wa kutekeleza jukumu hilo, alionyesha staha akitarajia baraka za Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Salman ﷺ alipokuwa gavana wa Madain, mfanyabishara mmoja alikuja kutoka Damascus. Mfanyabishara huyo, akiwa anamtafuta mbebaji wa kumbebea mzigo wake, alikutana na Salman ﷺ ambaye alikuwa amevaa nguo kuukuu. Kwa kuwa mfanyabishara huyo hakuwa akimjua, alimwambia Salman ﷺ:

"Njoo ubebe huu mzigo."

Salman ﷺ aliuchukua mzigo na kuubeba mgongoni mwake. Watu walipomuona gavana kabeba mzigo, wakamwambia mfanyabiashara kuwa alikuwa amembebesha mzigo gavana. Mara mfanyabishara huyo wa Kidemiski akaomba radhi na kujaribu kuutoa mzigo mgongoni mwa gavana; lakini Salman ﷺ akajibu:

"Siutui mzigo huu mpaka tufike nyumbani kwako." (Ibn Sa'd, iv,88)

Muadhini wa Mtume ﷺ, Bilal ﷺ alikuwa mtu mweusi. Siku moja, Abu Dharr ﷺ alipomkasirikia Bilal, akamuita "Ewe mwa-

11.Tazama Bukhari, Tafsir, 9/9.
12.Tirmidhi, Manaqib, 20.

na wa mwanamke mweusi.” Mtume ﷺ alipopata habari kuhusu maneno ya Abu Dharr, alisikitika sana.

Ma’rur bin Suwayd anasimulia ripoti ifuatayo kuhusu hali ya Abu Dharr baada ya tukio hilo:

“Nilikutana na Abu Dharr ambapo alikuwa amevaa joho, na mtumwa wake naye alikuwa amevaa joho kama sawa na lake. Nikamuuliza sababu yake. Akajibu, “Nilimtendea mtu vibaya kwa kumuita mama yake kwa majina mabaya.” Mtume ﷺ akaniambia, “Ewe Abu Dharr! Umemtukana kwa kumuita mama yake majina mabaya. Bado una tabia za kijahiliyyah. Watumwa wenu ni ndugu zenu na Mwenyezi Mungu amewaweka chini yenu. Hivyo, yeyote mwenye ndugu ambaye yuko chini yake anatakiwa kumlisha kile anachokula yeye na kumvika kile anachovaa yeye. Msiwaambie kufanya mambo yaliyo nje ya uwezo wao, na kama mkifanya hivyo, basi wasaidieni.”
(Bukhari, Iman, 22; Itq, 15; Muslim, Ayman, 40)

UWASTANI KATIKA STAHA

Kujionyesha na kuonyesha staha nyingi humfanya mtu kuwa na kiburi kwa namna isiyokuwa ya moja kwa moja. Unyenyekevu wa kweli ni sifa ya wale waliofikia ukamilifu wa kiroho; lakini, kujifanya kuwa kama wale ambao tayari wamefikia ukamilifu wa kiroho ni sawa na kiburi na unafiki. Uzuri ulioje wa maneno ya Sheikh Sa’di akielezea ukweli huu:

“Wale wanadhani kuwa wana kitu ndani mwao kama njugu dama huja kuonekana kuwa ni maganda kama ya vitunguu.”

Kwa maneno mengine, ni katika unafiki mtu asiyekuwa na sifa fulani kujifanya kuwa anazo na kuzungumzia jinsi alivyo na staha, akiwa amejipamba na sifa hizo.

Watu wenye busara na maarifa ni kama miti yenye matunda yaliyoiva. Hutoa matunda yao kwa watu wote. Kwa hiyo, badala ya kujaribu kujitangaza na kuwa maarufu, watu wanatakiwa kuubadilisha ulimwengu wao wa kiroho kuwa hazina ambayo kila mtu atafaidika nayo.

Wengine wanaweza kujifanya kuwa wana staha kwa msukumo wa nafsi ili wapate kujulikana kuwa ni **"wenye staha."** Kiukweli hali hii ya unafiki ni aina ya majivuno ya ndani yaitwayo **"majivuno ya unyenyekevu",** ambayo ni kiburi katika namna ya staha. Kwa mfano, kusema maneno kama vile"Mimi, mja mnyenyekevu na faqiri, niliweza tu kutoa kiasi kile na kile cha pesa" au "nimefanya ibada ile na ile" ni majivuno yaliyojificha nyuma ya pazia ya unyenyekevu.

Hassan al-Basri anasema:

"Wale wenye kujitia aibu miongoni mwa watu kiukweli wanajisifu. Na hizi ni alama za unafiki."

Kwa hiyo kuzidisha staha kupita kiasi nalo ni jambo hatari mno; kwa sababu majivuno na kiburi huiua roho huku vikiihuisha nafsi. Rumi anatuonya kuhusu hatari hii kama ifuatavyo:

"Kuwa mpole kama mtumwa na usijaribu kujiweka juu kama jeneza juu ya mabega ya watu. Nafsi iligeuzwa kuwa Fir'aun kwa wingi wa majisifu: kuwa duni wa moyo kwa unyenyekevu, usifanye jeuri. Kwa kadiri uwezavyo, kuwa mtumwa, usiwe mfalme. Teseka kwa makofi: kuwa kama mpira, usiwe kama popo." [13]

13.Mathnawi, I, 1866 - 1868.

Unyenyekevu wa kweli ni kuiweka nafsi katika hali ya kujinyenyekeza mbele ya Mwenyezi Mungu na kuwahurumia viumbe. Kwa maneno mengine, ni kukiri una dhaifu na unyonge wako, kuyatii maamrisho ya Mwenyezi Mungu kwa moyo wa dhati, kukubali maneno sahihi ya watu wengine, na kuacha kukaidi ukweli.

Fudayl b. I'yad (q.s) anasema kuwa:

"Unyenyekevu nikuukubali ukweli hata kama aliyeusema ni mjinga au mtoto."

NAFASI YA STAHA KATIKA MAFUNZO YA KIROHO

Imeelezwa katika methali moja kwamba "staha ni kama mwindaji anayewinda majivuno." Kwa kweli hakuna njia bora kuliko staha katika kupata hali na daraja ya kiroho; wakati ambapo, majivuno na kiburi ni miongoni mwa sifa mbaya sana, ambazo humchukiza Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Kuhusu suala hili, Sayyidna Abu Bakr ﷺ anasema kuwa:

"Pindi mja anapopata kiburi kwa sababu ya neema fulani, Mwenyezi Mungu Mtukufu humchukia mpaka anapoipoteza neema hiyo."

Katika mafunzo ya kiroho, awali kabisa huanza na kuitakasa nafasi. Majivuno na ubinafsi ni tabia mbaya na ngumu kuondokana nazo.

Abu Hashim al- Sufi, mmoja katika Masufi wa mwanzo, anasema:

"Ni vigumu sana kuyakwangua majivuno kutoka moyoni kuliko kuchimba milima kwa sindano."

Hata hivyo, hakuna njia ya kupata daraja za kiroho na kuwa mwanadamu kamili mpaka suala hili linapofanikiwa. Rumi anasema:

"Pindi fana' (hali ya kutokuwepo) inapomtunuku mtu kupitia ufukara (wa kiroho), (mtu huyo)huwa hana kivuli kama Muhammad ﷺ. Kwa maneno mengine atajikomboa na uwepo wake wa kufikirika na wa kivuli."[14]

Masikitiko yaliyoje kwa mwanadamu ambaye asili yake ni kutokuwepo, kudai uwepo na kujiona! Tamaa zote za kidunia na raha za kinafsi ni mitego ya mtihani, ambayo humuandalia mja sababu za kuangukia katika hali mbaya. Wale wanaoangukia katika mitego hii ni kama samaki, ambaye hujiangamiza kwa furaha ya muda mfupi ya chambo kilichopo kwenye ndoana. Uzuri ulioje wa maneno ya Rumi katika kulielezea hili:

"Kwa sababu uwepo kamili huzalisha sumu kali: huondosha akili kutoka kichwani na unyenyekevu kutoka moyoni. Kutokana na shambulizi hili sumu hii hii ya uwepo kamili Azazil alifanywa kuwa Ibilisi, akasema, "Kwa nini Adam awe bwana juu yangu? Mimi pia ni huru na nimezaliwa huru: ninaweza kupata na niko tayari kwa ajili ya(kupata) uwezo wa hali ya juu. Kwa ubora wa hali ya juu, mimi siwezi kuwa duni mbele ya yeyote kwa kusimama mbele ya adui yangu na kumtumikia." Hivyo akalaaniwa." [15]

Ndiyo maana ni wajibu kwa muumini ausafishe moyo wake kutokana na maradhi ya kiburi.

Hasan al- Basri anasema kuwa:

"Staha ni kumkubali kila uliyekutana naye kuwa ni bora kuliko wewe."

14.Mathnawi, juzuu v, 672
15.Mathnawi, juzuu, 1920 - 1924

Sultan wa watu wana-maarifa, Bahauddin Naqshiband, katika siku zake za mwanzo wa kufuata Usufi. alikuwa akisafisha barabara, kuwahudumia wagonjwa na wanyonge, na hata kuwahudumia wanyama waliojeruhiwa. Kwa kufanya hivyo, alijipamba na unyenyekevu na hali ya kutokuwa chochote, na baadaye alieleza kuwa alikuwa amepata mabadiliko mengi ya kiroho kwa sababu ya neema ya huduma hizi. Maneno yake yafuatayo kuhusu ishara na kiroho alizozifikia ni ya maana sana:

Watu ni ngano, mimi ni nyasi

Kila mtu ni mkamilifu, mimi ni mbaya

Mtu huanza safari yake ya kiroho baada ya kufikia hali hiyo ya kiroho. Rumi anawaambia wale waliofikia hali hii ya kiroho:

"Ukianza safari, watakupisha njia. Ukiwa katika hali ya kutokuwepo, watakupeleka kwenye hali ya kuwepo. Ni kipi kioo cha uwepo? Kutokuwepo. Ewe Rafiki wa Ukweli! Ilete hali yako ya kutokuwepo kama zawadi mbele ya Ukweli, kama wewe sio mpumbavu." [16]

Ni vigumu kufikia daraja za kiroho ukiwa na mzigo na hali ya kughafilika kama vile kiburi na majivuno; kwa sababu kama ilivyoelezwa na Haji Bayram al- Walii:

"Kiburi ni kama jiwe lililofungwa kiunoni mwako. Huwezi kuruka wala kuogelea nalo."

Ndiyo maana Masufi hujivua mavazi ya uwepo na kiburi na kuvaa kwa moyo wa dhati mavazi ya hali ya kutokuwepo na hali ya kutokuwa chochote ili wapate kuzitakasa nafsi zao.

16.Mathnawi, I, 3201

Ni baada ya hapo tu ndipo wanapofikia usultani wa ulimwengu wa kiroho.

Pindi Aziz Mahmud Hudayi (q.s) alipoingia kwa Uftadah (q.s), kitu cha kwanza alichoambiwa ni kuacha nyuma starehe zote za kidunia na kinafsi. Kwa hiyo alitakiwa kuuza katika masoko ya Bursa, ambapo alifanya kazi kama hakimu; kisha akapewa kazi ya kusafisha vyoo vya nyumba ya kulala wageni.

Mfano mwingine ni rafiki mkubwa wa Mwenyezi Mungu, Halid al-Baghdadi (q.s). Alikaa mbele ya Dahlawi (q.s) alipokuwa kama jua la duara za kitaaluma; na kwa uangalifu akatekeleza jukumu la kusafisha vyoo. Kwa kufanya hivyo alipata taji la hali ya kutokuwa chochote na hali ya kutokuwepo na matokeo yake akapata sifa na pongezi za mwalimu wake.

Kwa Muhtasari, ili kufikia ukomavu wa kiroho hatupaswi hata kidogo kulivua vazi letu la staha. Utii bila unyenyekevu ni utii usiokuwa kamili na usiokuwa na siha; wakati ambapo kiburi na kujiona ni maradhi hatari sana yanayoweza hata kumfanya mtu amkufuru Mwenyezi Mungu kama ilivyotokea kwa Ibilisi.

Kwa sababu ya Masufi kuchagua staha kama kanuni ya maisha yao, wamepata neema na baraka nyingi za Mwenyezi Mungu Mtukufu na wamekuwa nyota katika ulimwengu wa kiroho. Siyo tu kwamba wametumia uhai wao wote katika kuwaongoza watu, bali pia hata baada ya kufa kwao wameendelea kuwaonyesha watu njia iliyonyooka.

Tunamuomba Mola wetu atupe baraka ya staha ya marafiki zake. Atupatie fungu katika ulimwengu wao wa kiroho, ambao umekuzwa na hali ya kutokuwa chochote

na staha. Tunamuomba aturahisishie kuujua na kuutekeleza wajibu na majukumu yetu kwa tabia kamilifu.

Amin...

KUWA NA SUBIRA NA UVUMILIVU MBELE YA WAJINGA NA WENYE TABIA MBAYA

Ni ukweli unaojulikana vyema kuwa watu waliostaarabika na wenye vipaji daima hukabiliwa na ukosaji wenye wivu na tabia mbaya. Wanatarajiwa kuwa tayari kwa matatizo yanayoweza kusababishwa na watu waovu. Vivyo hivyo, wale waliokomaa kiimani wanatakiwa kuwa tayari kukabiliana na maumivu yanayotokana na wajinga na wakorofi; kwani kufanya subira kwa ajili ya Mwenyezi Mungu ni daraja ya hali ya juu na umadhubuti wa imani ya kidini.

Uzuri ulioje wa maneno ya Rumi katika kuelezea maana hii kwa tungo zifuatazo za shairi:

"Kwa kufanya subira dhidi ya giza la usiku mwezi huwa na mwanga; kwa kufanya subira dhidi ya miba, mawaridi hujipatia harufu maridhawa na rangi nzuri." [1]

1.Mathnawi, V, 1408

KUWA NA SUBIRA NA UVUMILIVU MBELE YA WAJINGA NA WENYE TABIA MBAYA

Kila kitu, mema na mabaya, ukweli na uongo, na haki na makosa huwa wazi kwa mifano inayopatikana katika mtazamo wetu wa kibinaadamu.

Wakiongozwa na Qur'an Takatifu na Sunnah ya Mtume Muhammad ﷺ, marafiki wa Mwenyezi Mungu wanawakilisha vigezo halisi na mifano hai kwa ajili yetu. Tunapaswa kuchukua masomo kutokana na tabia zao adhimu, kulinganisha matendo yetu na yao, na kujaribu kuwa na moyo uliojaa baraka na huruma, kama nyoyo zao.

Kwa kuwa marafiki wa Mwenyezi Mungu ni warithi wa Mitume, wanaendelea kutekeleza uongozi wa mitume na ukamilifu wa kimaadili kwa ajili ya wanadamu wengine. Kwa maneno mengine, marafiki wa Mwenyezi Mungu ni watu wenye kuheshimiwa sana na wale ambao hawakuwaona maswahaba wa Mtume Muhammad ﷺ, kwa maana ya kujifunza kutokana na matendo yao mema. Muongozo na ushauri unaotoka katika ndimi za marafiki wa Mwenyezi Mungu hutoa uhai mpya kwa nyoyo za watu wengine kupitia lugha ya huruma na matokeo yake ushauri huu hutokana na maelekezo ya mitume.

SUBIRA NA UVUMILIVU WA MTUME MUHAMMAD ﷺ

Moja ya sifa zinazowabainisha marafiki wa Mwenyezi Mungu ni kwamba katika kukabiliana na ukatili na uchungu unaosababishwa na watu wasiojua na wenye tabia mbaya, radiamali yao huwa ni subira na uvumilivu. Marafiki wa Mwenyezi Mungu wanahitaji kuishi katika jamii ili kuwafundisha watu njia iliyo sahihi. Kama ilivyo katika mambo mengine mema, mifano bora ya tabia hizi inapatikana katika shakhsia adhimu ya Mtume Muhammad ﷺ. Subira na uvumilivu wa Mtume ﷺ vinawakilisha ukamilifu wa dhana hizi mbili, kwani alikabiliana na ukatili na mateso katika kipindi cha uhai wake. Kuhusu jambo hili Mtukufu Mtume ﷺ anasema: *"Hakuna aliyeudhiwa katika njia ya Mwenyezi Mungu kama nilivyoudhiwa mimi."* (Tirmidhi, Qiyāma, 34/2472)

Hata hivyo, hakuwahi kufikiria kuwa mateso hayo hayavumiliki, na wala hakuacha kutoa ujumbe wake kwa wanadamu. Pamoja na hayo yote, alijua kwamba alikuwa akitafuta radhi za Mola wake, na madamu alikuwa akimridhisha Mola wake, hakujali sana ukatili aliokuwa akitendewa na watu katika ulimwengu huu wenye mwisho. Katika muktadha huu Qur'an Tukufu inasema:

"Wala usiwatii makafiri na wanafiki, na usijali udhia wao. Nawe mtegemee Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu anatosha kuwa Mtegemewa."(33:48)

Vitabu vya Mwenyezi Mungu vilivyokuja kabla ya Uislamu viliandika sifa za Mtume wa mwisho na kutaja kuwa atakuwa na uvumilivu usio kifani dhidi ya mateso ya watu wake. Zaid bin Sa'na, Myahudi mwenye ujuzi wa utamaduni wake wa kidini ambaye aliishi wakati wa zama za Mtume Muhammad ﷺ,

alijua kutokana na maandiko ya Wayahudi kwamba mtume aliyekuwa akisubiriwa sana atakuwa na sifa fulani.

Kila mara Zaid alipokuwa akimtazama Mtume ﷺ alikuwa akichunguza alama hizo kwa Mtume ﷺ. Kama ya kufanya uamuzi wake wa mwisho kuhusu kuingia katika Uislamu, Zayd alikuwa na swali moja akilini mwake na kujiambia, “Nitashangaa kama Muhammad atawasamehe wale wanaomtendea vibaya, na iwapo subira na uvumilivu wake utaongezeka kadiri ya mateso yatakavyoongezeka.” Hivyo basi, Zayd alimuweka Mtume ﷺ katika namna ya kumjaribu na alipoona kwa ukaribu tabia za kipekee za Mtume ﷺ Zayd akafikia hitimisho kuwa hakika alikuwa mbele ya Mtume ﷺ, na hivyo akaingia katika Uislamu kwa moyo wote. (Hakim, III, 700 / 6547)

Siyo tu kwamba Mtume Muhammad ﷺ alivumilia ukatili wa makafiri na wanafiki, bali pia radiamali yake ilikuwa ni subira na uvumilivu dhidi ya tabia mbaya zilizofanywa na Waislamu wapya, ambao walikuwa bado hawajaweza kutenda kwa mujibu wa mafundisho.

Walikuwa wakitumia tabia zisizokuwa za kistaarabu katika kuzungumza na Mtume ﷺ. Kwa mfano, walikuwa wakimuita mara kwa mara, “Ewe Muhammad, Ewe Muhammad!” kwa sauti ya juu isiyokuwa na upole ndani yake. Lakini Mtume ﷺ alikuwa akiwajibu kwa namna ya upole. Hakuwa akiwavunjia heshima, licha ya inda yao. (Muslim, Nudhur, 8, Abu Dawud, Ayman 21/3316, Tirmidhi, Zuhd 50, Ahmad, IV, 239)

Katika tukio moja, Bedui mmoja alikojoa katika msikiti wa Mtume ﷺ. Maswahaba wakamkamata na kuanza kumtukana, lakini Mtume ﷺ aliwakataza akisema, “Muacheni. Mwageni ndoo ya maji mahali alipokojoa. Mmeagizwa kufanya mambo

yawe rahisi na si kufanya yawe magumu." (Bukhari, Wudū, 58, Adab, 80).

Radiamali hiyo yenye umaizi ya Mtume ﷺ iliwafanya watu wengi kuingia katika Uislamu, na kuboresha kiwango cha kuielewa dini hii mpya. Qur'an Tukufu inaeleza ukweli huu ikisema:

"Basi ni kwa sababu ya rehema itokayo kwa Mwenyezi Mungu ndiyo umekuwa laini kwao. Na lau ungelikuwa mkali, mwenye moyo mgumu, bila ya shaka wangelikukimbia. Basi wasamehe, na waombee maghfira... "(3:159)

Hata wakati wa uhai wake katika mji wa Madina wakati wa Waislamu walipofikia kiwango cha kuridhisha cha mafanikio na nguvu Mtume ﷺ hakutarajia maisha rahisi. Alivumilia aina zote za tabu katika njia ya Mwenyezi Mungu na hakutaka kutumia fursa yoyote ya kuyaacha majukumu yake. Siku moja Bedui mmoja alipomuona Mtume ﷺ pamoja na maswahaba wake akiwa amekaa kwa unyenyekevu na kula kwa staha ya hali ya juu, Bedui akaona kuwa hali hii siyo ya kawaida na yenye kustaajabisha. Hakuacha kumuuliza Mtume ﷺ kuhusu mandhari hayo naye Mtume ﷺ akajibu:

"Mwenyezi Mungu ameniumba kama mja mwenye heshima, si dhalimu mkaidi." (Abu Dawud, At'ima, 17/3773)

Kama Mtu wa wema na huruma, Mtume ﷺ aliashiria kuwa tabia na sifa mbaya za binadamu, kama ukaidi na uonevu, kamwe haviwezi kukaa pamoja na nafsi ya muumini. Ami wa Mtume ﷺ, 'Abbas (Mungu awe radhi naye) hakufurahia jinsi watu wanavyoamiliana na mpwa wake na kupendekeza kuwa Mtume ﷺ awe na kiti maalum na kukaa mbali kidogo na watu na kupunguza tabu walizokuwa wakimfanyia. Mtume ﷺ hakulipendelea pendekezo hilo la Abbas na kusema:

"Nitaendelea kukaa nao mpaka Mwenyezi Mungu atakaponichukua na kunipa furaha ya milele. Hivyo waache wanipe mateso" (Ibn Şa'd, II, 193; Haythamī, IX, 21)

Vilevile, Mtume aliwaonya waumini akisema," Muislamu ambaye anaishi kati ya watu na kutaabika kwa ukatili wao ni bora kuliko Muislamu ambaye hawezi kuishi pamoja nao na kuvumilia matatizo yao". (Tirmidhi, Qiyāma, 55/2507)

Rumi analielezea kwa uzuri wazo hili katika mistari yake ya mashairi yafuatayo:

"Kwa sababu ya kulivumilia giza la usiku mwezi hupata kutoa mwanga; Kwa kuivumilia miiba, uaridi hupata harufu mwanana na rangi nzuri.

Kwa sababu ya kuvumilia aina zote za mateso kutoka kwa makafiri na wajinga, mitume wote wakapata waja wateule wa Mwenyezi Mungu na hata kuwa watawala washindi.

Ukiweza kushikamana na subira kwa amani, subira hiyo huwa ni bawa kwa ajili yako, na unaweza kupaa juu mbinguni. Mtazame Mustafa [Mtume Muhammad ﷺ]! Subira iligeuka kuwa Buraq[17] ya kumpeleka Miraji[18] na Sidrat al- Muntaha[19] na kumfikisha mbinguni."[20]

huruma na upendo wa Mtume ﷺ kwa wafuasi wake katika dini vilifanya shida zote kuwa rahisi. Kamwe hakuchoka kukabiliana na matatizo yaliyosababishwa na jamii yake, na wala hakuwahi kuyalalamikia, bali daima alikuwa akiwaombea kwa upendo akisema, "umma wangu, umma wangu." Vivyo hivyo, aliweka kando faraja yake binafsi kwa ajili ya wafuasi wake.

17.Jina la farasi au kipandwa kilichombeba Mtume Muhammad ﷺ katika safari yake ya mbinguni.

18.Safari ya kimiujiza ya Mtume Muhammad ﷺ kwenda mbinguni.

19.Mti wa mkunazi katika mbingu ya saba.

20.Mathnawi, V, 1408 - 1417

SUBIRA NA UVUMILIVU WA MARAFIKI WA MWENYEZI MUNGU

Kwa kufuata mkondo wa matendo ya Mitume, marafiki wa Mwenyezi Mungu hawajali sana mateso, tabia za ukaidi, na makosa kutoka kwa watu wanaoishi nao. Marafiki wa Mwenyezi Mungu huvumilia kila aina ya dhulma zinazofanywa na wanajamii wenzao ili kuwafikia na kuzirekebisha tabia zao mbaya, kwa sababu mkakati huo hutokana na elimu na maarifa ya kweli. Ibrahimu Hakki wa Erzurum anaelezea sifa na tabia za marafiki wa Mwenyezi Mungu kuhusu jambo hili kwa kusema,

"Kati ya matendo ya marafiki wa Mungu ni kuwa madhubuti dhidi ya majanga, subira dhidi ya kuvunjiwa heshima, na kusimama imara dhidi ya misukosuko yenye kushangaza. Mwanzo wa elimu ni uvumilivu, mwanzo wa hekima ni kuishi vizuri na watu."

Hivyo, kutokuwa na subira na uvumilivu dhidi ya matatizo yanayosababishwa na mafedhuli kunatokana na ukosefu wa hekima na maarifa. Watu wenye ujuzi na utambuzi hutenda kwa wema na kwa kufikiri, wakati watu wajinga hutenda kwa ufedhuli na bila kufikiri. Miongoni mwa aina mbaya kabisa za ujinga ni kutojua ukarimu na wema wa dini ya Kiislamu; kwa maana adabu inawakilisha sifa na tabia ya dini. Rumi analielezea hili kwa uzuri anaposema:

"Akili yangu iliuuliza moyo, 'imani ni kitu gani?' Moyo wangu ukalinong'oneza sikio la akili na kuliambia, 'Imani yote ni tabia njema (adabu)'"

Kuhusiana na jambo hili kuna ufafanuzi mzuri uliotolewa na Ibn Abbas ﵁ kuhusu aya ya Qur'an ifutayo:

"Mema na maovu hayalingani. Pinga uovu kwa lilio jema zaidi. Hapo yule ambaye baina yako naye pana uadui atakuwa kama rafiki jamaa wa kukuonea uchungu." (41:34)

Ibn Abbas anasema: "Neno **'lililo jema zaidi(ahsan)**' katika aya hii lina maana ya kuwa na subira unapokuwa na hasira na kusamehe unapokabiliana na uonevu. Wanadamu wakiishi kulingana na msingi huu, Mwenyezi Mungu huwalinda na maadui wao huwa wanyonge mbele yao, kana kwamba maadui hao wamekuwa marafiki wao waaminifu." (Bukhari, Tafsir 41 / 1)

Vilevile, Anas bin Malik anaelezea neno "rafiki mwaminifu (walii hamīm)" katika sehemu ya mwisho ya aya hii kama ifuatavyo:

"Ni mtu mwema na mwenye kutafakari ambaye anapoambiwa na mtu maneno mabaya yeye hujibu, "Kama uyasemayo ni kweli, basi Mwenyezi Mungu anisamehe, na kama siyo kweli, basi Mwenyezi Mungu akusamehe."

Katika muktadha huu, Qur'an pia yasema:

"Na waja wa Arrahman Mwingi wa Rehema ni wale wanaotembea ulimwenguni kwa staha, na wajinga wakiwasemeza hujibu: Amani!" (25:63)

Marafiki wa Mwenyezi Mungu hawawapi kipaumbele wajinga, na wala hawajibishani nao; kwa sababu Marafiki hao wa Mwenyezi Mungu wanajua kuwa wakibishana nao, hao wajinga, kutokana na mielekeo yao ya ubinafsi, watazidi kuwa wajinga. Lakini marafiki wa Mwenyezi Mungu hawapeleki wajinga kwenye uelekeo huu. Ali bin. Abi Talib ﷺ anatuzindua na hali hii na kusema:

"Kamwe usijibu neno lililosemwa kwa ufidhuli (matusi), kwa sababu mtu anayetamka neno hilo ana maneno mengine mengi ya kifedhuli kama hayo na atayatumia pindi utakapoji-

bu. Kamwe usifanye utani na mjinga, kwani atauumiza moyo wako, kwa sababu ulimi wake una sumu."

Vilevile, Rumi anasema:

"Unapokuwa mbele ya wajinga kaa kimya, kama kitabu. Mtu mzuri ni yule anayestahimili masengenyano na kuyatazama makosa ya kutoka kwa watu kana kwamba ni kipofu na kiziwi." [21]

Mtume Muhammad ﷺ anaonyesha mfano wa sifa nzuri za marafiki wa Mungu katika namna yenye kuvutia sana. Siku moja aliwauliza maswahaba wake, "Je, mtu yeyote kati yenu hawezi kuwa kama Abu Damdam?" Maswahaba wakasema, "ni nani huyo Abu Damdam?" Mtume ﷺ akasema, "Alikuwa ni mtu wa kabila moja lililokuwa kabla yenu na alikuwa akisema, 'Nimewasamehe wale wote walionitusi na kunisengenya.'"(Abu Dawud, Adab 36/4887) Muamala ulioje wenye busara wa Abu Damdam kwa binadamu wenzake! Kumpenda Mwenyezi Mungu Mtukufu bila kikomo huleta huruma kwa viumbe Wake wote. Abu Damdam hataki wale waliompa machungu wakumbwe na kuona matokeo ya makosa yao kwake Siku ya Malipo. Kinyume chake, anataka kuwapa faraja na matumaini ili wapate kuwa na nafasi ndani ya huruma ya Kimungu.

Abu Hamid al-Ghazālī anasimulia kisa kifuatacho kuhusu kuwa mvumilivu mbele ya mizigo inayosababishwa na watu.

"Mtu mmoja mwenye hekima aliandika vitabu mia tatu na sitini kuhusu hekima (hikmah) na akadhani kuwa, kutokana na vitabu vyake hivyo, amekuwa karibu na Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu Mtukufu akamteremshia wahyi Nabii wa zama hizo kuwa, 'Mwambie mtu huyo kwamba ameijaza ardhi

21.Mathnawi, IV, 774

kwa unafiki. Sikubali chochote katika unafiki wake.' Aliposikia hivyo, mtu huyo akajitenga ndani ya pango na kuanza kufanya ibada muda wote. Akajiwa na fikra akilini mwake kuwa atakuwa amepata radhi ya Mwenyezi Mungu. Kwa mara nyingine Mwenyezi Mungu akamfunulia Nabii (wa zama hizo) akisema, "Mwambie kwamba kamwe hatoweza kupata radhi zangu madamu haishi pamoja na watu na kuteseka na mateso yao.' Alipoambiwa kuhusu jambo hilo, mara hii alikwenda eneo la sokoni na akachanganyika na watu kwa kutembea, kula, na kunywa pamoja nao. Hapo Mwenyezi Mungu akateremsha ufunuo kwa Mtume wake na kusema: "Mwambie kuwa sasa amepata radhi za Mwenyezi Mungu'". (Ihyā ', II, 610-611)

Kukaa katika faragha kwa kipindi cha muda fulani ni sehemu ya mafunzo ya Usufi na Sufi anatarajiwa kujitenga na jamii yake na kujitenga na mambo ya dunia hii ili kuboresha na kuukamilisha uwezo wake wa kiroho. Hata hivyo, Usufi, hauenezi maisha ya kitawa; badala yake unaona kuwa ni jambo lisiloruhusiwa. Sufi anatarajiwa kuishi miongoni mwa watu na kumtumikia Mola wake akiwa katika jamii, msingi unaoitwa kama "kujitenga hali ukiwa ndani ya jamii (*halvet der-encumen*)". Kwa maneno mengine, "umoja ndani ya wingi (*kesrette vahdet*)", ikiwa na maana ya kuwa pamoja na Mwenyezi Mungu Mtukufu hata kama upo katika umma, ikiwa ni ishara ya ukomavu wa hali ya kiroho ya muumini. Sufi anatakiwa kuungana na jamii yake kimwili, japokuwa moyo wake daima unatakiwa kushughulishwa na Mola wake. Kwa muktadha huu, Rumi anasema:

"Hakuna kona hata moja katika huu ulimwengu isiyokuwa na taabu na mitego.

Hakuna wokovu, furaha, na faraja katika mahali popote pale zaidi ya kumtafuta Mola katika moyo,kutafuta kimbilio

kwake, na kuishi katika uwepo wake.Ninaapa kwa Mwenyezi Mungu, yule asiyekuwa na uvumilivu kikamilifu hatoweza kupata mahali popote salama katika dunia hii." [22]

Vile vile, katika kisa kifuatacho, Muhammad Iqbal anaonyesha mfano wa ubora wa kuishi kati ya watu na kuvumilia taabu inayotokana na watu:

"Paa asiyekuwa mzoefu na mjinga alikuwa akimwagia matatizo yake paa mzoefu na mwenye hekima,

'Kuanzia sasa nitaishi katika Kaaba, Haram (eneo takatifu ambalo ni haramu kuwinda ndani yake. Kwa sababu wawindaji wameweka mitego katika kila eneo la malisho na kututafuta siku hadi siku. Ninataka kuwa salama dhidi ya mitego yao na kupata amani ya akili.'

Aliposikia haya paa mwenye uzoefu na mwenye hekima alijibu:

'Ewe rafiki yangu mwenye akili! Kama unataka kuwa hai, unatakiwa kuishi katika hatari. Unapaswa kuwa tayari kwa kila kitu. Daraja ya imani huwa wazi pale tu unapokabiliana na matatizo. Hatari huijaribu nguvu yako na kutufanya tujue uwezo wa mwili na roho yako.'"

Sifa nyingie ya marafiki wa Mwenyezi Mungu kwamba wanapowekwa katika hali ya wao kuchagua kati ya kuwa waonevu au wanaoonewa, kwa hiari kabisa huchagua kuwa wanaoonewa. Siku moja Sa'd bin Abi Waqqas ﵁ alimuuliza Mtume ﷺ: "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, kama mtu ataingia nyumbani mwangu (wakati wa machafuko) na akanitishia kuniua, unanishauri nifanyeje?" Mtume ﷺ akajibu: "Fanya kama alivyofanya mtoto wa Adam [Habil]!" (Tirmidhi, Fitan 29/2194)

22.Mathnawi, II, 591, 593.

Tunaweza kujumlisha sifa ya msingi ya marafiki wa Mungu katika suala hili kama ifuatavyo, “Kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, mtu anapaswa kuwa na uwezo wa kufanya subira mbele ya taabu zinazotendwa na watu.”

Moja ya mifano hai ya jambo hili ulitolewa na Ma’rūf Karkhī. Katika nyumba yake alikuwa na mgeni ambaye alikuwa mahututi kwenye kitanda cha mauti ambapo alikuwa akimtunza vizuri sana. Lakini, kutokana na maumivu aliyokuwa nayo, mgonjwa huyo alikuwa akilalamikia hali yake na kumkoromea kila mtu katika nyumba.

Siku baada ya siku, mgonjwa aliongeza malalamiko na mayowe na kufanya maisha ya wenyeji wake katika nyumba kuwa magumu. Mwishowe, hawakuweza kuvumilia tena na wakaanza kuondoka katika nyumba mmoja baada ya mwingine. Hakuna aliyebaki zaidi ya Ma’ruf na mkewe. Ma’ruf aliendelea kumuhudumia usiku na mchana bila kulala hata kidogo. Lakini siku moja alishindwa kuuzuia usingizi na akasinzia kidogo sana. Mgonjwa alipomuuona Ma’ruf amepitiwa na usingizi, alianza kumfokea, bila kujali hata kidogo fadhila anazofanyiwa na Ma’ruf. Mgonjwa alisema, “Darwesh gani wewe! Kwa kweli watu kama wewe wana majina na sifa tu, ingawa kiuhalisia ni wanafiki. Wanawaamrisha watu kumcha Mwenyezi Mungu, lakini wao wenyewe hawaifanyii kazi. Wewe ni mmoja wao; unakula na kulala bila kujali hali yangu.” Ma’ruf hakujibu lolote bali alifanya subira mbele ya maneno ya mgonjwa, lakini mkewe alishindwa kujizuia kumwambia Ma’ruf kuwa anatakiwa kumtoa mgonjwa yule nyumbani, kwa sababu hana shukrani hata kidogo. Lakini Ma’ruf alimjibu mkewe kwa uso wenye bashasha: “Ewe mpendwa! Kwa nini uumizwe na maneno yake? Yote hayo aliyosema alikuwa akiniambia mimi. Kwangu mimi maneno yake mabaya yanayomtoka daima yanaonekana kuwa mazuri. Wamuona kuwa anaendelea

kuteseka. Hawezi kulala hata kidogo. Unatakiwa ufahamu pia kwamba ustadi, upendo na huruma ya kweli inafanya kazi pamoja na uvumilivu na kuwaelewa watu wa aina hii..."

Sheikh Şa'dī anasimulia kisa hicho *Bostān* yake na anatoa ushauri ufuatao:

"Moyo wenye upendo unakuwa wenye kusamehe.

Kama wewe ni mwili tu, utakapokufa, jina lako litatoweka pale mwili wako utakapotoweka.

Lakini kama wewe ni mtu mwema na mkarimu, utaendelea kuishi ndani ya nyoyo za watu hata baada ya mwili wako kuondoka katika ulimwengu huu.

Je huoni kuwa kuna makaburi mengi yaliyojengewa katika mji wa Karkh, lakini hakuna lililo kama la Ma'ruf kwa kuhudumiwa na linalojaa wageni."

Vivyo hivyo, Yunus Emre anabainisha kwa uzuri kabisa:

"Darwesh anatakiwa kutovutwa [na chochote];

Anatakiwa kuendelea kukaa kimya dhidi ya yule anayemtusi;

Hatakiwi kutumia nguvu dhidi ya yule anayempiga;

Anatakiwa kutenda tofauti kabisa na watu wengine."

Kwa maneno mengine, anatakiwa kushikamana na tabia ya unyenyekevu mbele ya taabu zitokanazo na watu; anatakiwa kuwa na subira na kuzivumilia; daima anatakiwa kuzingatia kuwa kheri na shari vyote hutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, na hivyo basi awatazame viumbe kwa mtazamo wa Muumba. Sufi akitenda kama watu wa kawaida, ambao huwa na radiamali ya hasira na kulipiza kisasi wanapokabiliana na ufedhuli, anaweza kuonekana kana kwamba anatetea haki binafsi. Lakini kwa mtazamo wa Usufi anakuwa amekosa usa-

mehevu, subira na uvumilivu ambavyo ni shuruti za msingi katika desturi ya kidini.

Daima Sufi anatakiwa kukumbuka kuwa kila kitu anachokumbana nacho ni mtihani anaopewa na Mwenyezi Mungu na hivyo anapaswa kufahamu siri na hekima ya Mwenyezi Mungu katika kila kitu anachokumbana nacho. Kiukweli, sifa nzuri za msingi za kibinadamu, kama vile usamehevu, uvumilivu, subira, na stahmala ni mambo yaliyo muhimu sana kwa mtu kupata huruma, radhi na upendo wa Mwenyezi Mungu. Kutokana na mtazamo huu, sifa hizi ni nyeti mno katika maadili ya Usufi, kama asemavyo Rumi:

"Kuwa na subira dhidi ya muovu ni njia ya kukinyanyua kiwango cha hali ya kiroho ya mtu; Popote penye moyo wenye hamu na Mola, subira huujaza neema."[23]

Aidha, mara nyingi maadili hayo huwa ni njia ya kuzirekebisha tabia mbaya za watu wenye ufedhuli. Kama watu wenye ufedhuli wasipohisi masikitiko kuhusu uovu wao na kuzirekebisha tabia zao, basi watajipeleka kwenye kujiangamiza, kwa sababu mara hii Mwenyezi Mungu.Yeye Mwenyewe atahakikisha watu wema wanapata haki zao. Hatua hii ya kuhakikisha wanapata haki zao kutoka kwa waonevu inaweza kuwa maangamizi makubwa kwa waonevu hao; maana wakati mwingine hutokea kwa njia ya ishara ya sifa ya Mwenyezi Mungu ya ukuu (Jalal), matokeo machungu mno huwakumba waonevu husika.

Kisa kifuatacho kinaelezea hekima hii vizuri:

Katika kipindi cha ujana wake, Ibrahimu Hakki alikuwa akimhudumia Mwalimu wake, Ismail Fakirullah na kumhudumia mahitaji yake. Siku moja, Ibrahimu Hakki alikwenda kisi-

23.Mathnawi, IV, 2041

mani kuchukua maji. Wakati huo huo, mwendesha farasi naye akaja kisimani na kumwambia: “Ondoka!”

Mpanda farasi huyo akamfokea Ibrahimu Hakki na kumpeleka farasi wake kwenye kisima. Ibrahimu Hakki alipotaka kuchukua chombo chake na kurudi nyuma, Mpanda farasi alimuelekeza farasi wake upande wa Ibrahimu Hakki na kumsukumia pembeni. Ibrahimu Hakki aliweza kujiokoa kwa tabu, lakini chombo chake kilikanyagwa na farasi na kupasuka vipande vipande.

Ibrahimu Hakki alirudi kwa mwalimu wake na kumsimulia yaliyomkuta huku yakiwa yametanda machoni pake. Mwalimu akamuuliza: “Je ulimtamkia chochote mtu huyo?” Ibrahimu Hakki akajibu: “Hapana! Sikumtamkia hata neno moja.” Mwalimu akamuamuru akisema, “Basi nenda haraka na umwambie maneno machache!”

Ibrahimu Hakki akaenda kisimani na kumkuta mtu yule akiwa anashughulika na farasi wake, lakini alikuwa amepewa malezi mazuri sana kiasi kwamba alishindwa kumwambia kitu kama radiamali ya yale aliyokuwa amemtendea.

Aliporudi kwa mwalimu wake, Fakirullah alimuuliza kama aliweza kumwambia Mpanda farasi chochote. Lakini jibu la Ibrahimu Hakki lilikuwa la hapana. Kwa mara mwingine, mwalimu aliinyanyua sauti yake akimuamrisha, “Ninakwambia ewe mwanangu, nenda na umwambie maneno machache mtu huyu; vinginevyo atakumbana na balaa kubwa!” Mara hii, akiwa imara zaidi, Ibrahimu Hakki alikwenda kisimani, lakini akamkuta mtu yule akiwa amelala chini akiwa maiti; alikuwa amepigwa sana na farasi wake na kumuua. Ibrahimu Hakki alikwenda mbio mpaka kwa mwalimu wake na kumhadithia aliyoyaona. Mwalimu alihuzunika na kusema, “Huruma iliyoje, mtu kukabiliana na mtungi!” Watu waliokuwa pamoja na

mwalimu wakati huo hawakuelewa chochote katika maneno yake na kuomba ufafanuzi zaidi. Basi mwalimu akatoa maelezo yafuatayo:

"Mpanda farasi alimuonea Ibrahimu Hakki. Lakini yule aliyeonewa hakumjibu hata kwa neno moja, bali alimuachia Mungu jambo hilo. Hali hii ilimkasirisha Mwenyezi Mungu na kumuadhibu yule Mpanda farasi. Kama Ibrahimu Hakki angelipa kisasi na kumwambia mtu yule maneno machache, suala hilo lingekuwa limetatuliwa hapo hapo. Lakini, Ibrahimu Hakki alipendelea kuwa mwenye kuonewa, japokuwa nilijaribu kulitatua tatizo hili kwa kumlazimisha Ibrahimu Hakki amfanyie jambo lolote Mpanda farasi, lakini kwa bahati mbaya, sikufanikiwa."

Kwa hivyo, marafiki wa Mwenyezi Mungu wanaoifahamu siri hii kwa kuielewa wanaweza kuujibu kidogo ukatili unaofanywa na waonevu, kwa sababu hujaribu kuwaokoa watu hao wasikumbane na ghadhabu ya Mwenyezi Mungu. Marafiki wa Mwenyezi Mungu hawataki mtu yeyote, hata muonevu, aadhibiwe kwa sababu ya jambo ambalo wao ni sehemu yake.

Kwa muhtasari, waumini waliokomaa kwa nje huujibu uonevu unaotoka kwa watu kwa kufanya subira, uvumilivu na kustahmili. Wanafahamu kwamba kwa ndani masaibu yote hayo yanatoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, kama ishara ya majaaliwa, ambayo ni mtihani kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Rumi analiweka wazi jambo hili kama ifuatavyo:

"Mlima wenye hazina kidogo za ulimwengu huu hugeuka kuwa vipande vipande kwa kushambuliwa na wachimbaji." [24]

Ni ukweli unaojulikana vyema kuwa watu waliostaarabika na wenye vipaji daima hukabiliwa na ukosaji wenye wivu

24.Mathnawi, IV, 2758

na tabia mbaya. Wanatarajiwa kuwa tayari kwa matatizo yanayoweza kusababishwa na watu waovu. Vivyo hivyo, wale waliokomaa kiimani wanatakiwa kuwa tayari kukabiliana na maumivu yanayotokana na wajinga na wakorofi; kwani kufanya subira kwa ajili ya Mwenyezi Mungu ni daraja ya hali ya juu na umadhubuti wa imani ya kidini.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu atujaalie sehemu ya ufahamu, ujuzi, maarifa na hekima aliyowajaalia wana hekima! Atulinde na shari za mafedhuli na kero za wajinga na watu wenye tabia mbaya! Atuweke pamoja na wale wanaoishi kulingana na maarifa ya kawaida yanayowafaa wale wenye ukomavu wa imani na tufike mbele yake tukiwa na moyo salama!

Amin...

KUUKABILI UBAYA KWA WEMA

Muumini aliyekomaa anapaswa kuwa na moyo mkubwa na wenye utajiri kama bahari. Daima anatakiwa kuonyesha sura ya amani na utulivu wa Uislamu kwa adabu, uzuri na wema.

Kutoa msamaha na upatanisho siku za sherehe za kidini (Eid) pekee, haina manufaa kwa waumini wenye ukomavu; kwa sababu kuwasamehe wengine ni sifa ya msingi ya waumini waliokomaa ili wapate kustahili msamaha wa Mwenyezi Mungu Mtukufu.

KUUKABILI UBAYA KWA WEMA

Kila kanuni ya Uislamu inaundwa na tabia njema, ambayo ni ishara ya imani katika maisha. Mtume ﷺ anasema:

"Nimetumwa kuja kukamilisha tabia njema." (Muwattā, Husn Al-Khuluq, 8)

Ili kuwa Waislamu wliokomaa tunahitaji kuchukua tabia za maadili ya Uislamu na kuzitumia katika kila hatua ya maisha yetu. Vinginevyo tutapoteza utu wetu na kuuharibu wokovu wetu wa milele.

Mtume Wetu ﷺ aliupa ubinaadamu ustaarabu wa tabia njema kwa sifa zake za maadili ya hali ya juu. Marafiki wa Mwenyezi Mungu, ambao ni warithi wa Mitume, wanaendeleza desturi na sifa njema za Mitume. Miongoni mwa sifa muhimu sana za Mitume na Marafiki (Mawalii) wa Mwenyezi Mungu ni kuwa wao husamehe mateso na maonevu wanayofanyiwa na watu kwa jili ya Mwenyezi Mungu na kuyakabili kwa wema. Na kwa hivyo hupata kuwakumbatia waja wa Mwenyezi Mungu kwa huruma na upendo na kuzihuisha nyoyo zao zilizoharibiwa. Sifa hii ya ubora pia ni bishara yenye kufurahisha ya mwisho mwema. Qur'an Tukufu inasema:

"Na ambao husubiri kwa kutaka radhi ya Mola wao Mlezi, na wakashika Sala, na wakatoa, kwa siri na kwa

uwazi, katika tulivyowapa; na wakayaondoa maovu kwa wema. Hao ndio watakao pata malipo ya Nyumba ya Akhera." (13:22)

Wale wanaotaka kupata rehema na msamaha wa Mwenyezi Mungu wanapaswa kusamehe makosa ya watu na kushikamana na tabia ya kukabiliana na ubaya kwa wema kama sifa yao ya kimaadili. Kwa sababu Mitume, Masufi, Wana maarifa na wanazuoni wote walioletwa na Mola wetu kuja kuwaongoza wanadamu, walionyesha sifa hii katika maisha yao.

LEO HAPANA LAWAMA JUU YENU...

Mojawapo ya mifano bora kuhusu umuhimu wa kusamehe iliyotajwa ndani ya Qur'an Tukufu ni unaopatikana katika kisa cha Yusufu عليه السلام na ndugu zake.

Baada ya Yaqub عليه السلام kuiona hali yake mwenyewe ya kiroho kwa Yusufu عليه السلام, alimpenda Yusufu sana miongoni mwa watoto wake kumi na mbili.

Jambo hili liliwafanya nduguze Yusufu kumuonea wivu. Hatimaye walipanga kumuua Yusufu kwa kumtumbukiza kisimani.

Yusufu aliokolewa kisimani na msafara uliokuwa ukipita; hata hivyo aliuzwa kama mtumwa pindi msafara huo ulipofika Misri. Baada ya miaka mingi ya taabu, mitihani ya kiroho na mateso, hatimaye Yusufu aliteuliwa kuwa mkhazini wa Misri. Alipewa jukumu la ugawaji wa chakula wakati wa miaka ya njaa katika nchi ya Misri. Ndugu zake nao pia walikuja kuomba chakula kutoka kwake. Yusufu aliuficha utambulisho wake ndugu zake wasipate kumtambua. Ingawa ingekuwa rahisi sana kwake kulipiza kisasi kwa aliyofanyiwa na ndugu zake,

Yusufu hakuwaadhibu wala kuwatukana. Badala yake, aliwaongezea zawadi nyingi.

Kutokana na ukarimu na usamehevu wake, ndugu zake walilazimika kukubali makosa yao kwa kusema:

"Kumbe wewe ndiye Yusuf? Wallahi! Mwenyezi Mungu amekufadhilisha wewe kuliko sisi, na hakika sisi tulikuwa wenye kukosa." Jibu na msamaha wa Yusufu kwa ndugu zake umeelezwa katika Qur'an Tukufu kama ifuatavyo:

"Akasema: Leo hapana lawama juu yenu. Mwenyezi Mungu atakusameheni, naye ni Mwingi wa kurehemu kuliko wote wanao rehemu." (12: 92)

Kisha, ili kuwaondolea aibu ndugu zake, akasema kwamba: "Wakati huo, Shetani aliweka uchochezi baina yenu na mimi."

Kwa hiyo, sifa bora ya kweli ni kuwa na uwezo wa kuwasamehe waja wa Mwenyezi Mungu ili kupata malipo ya Akhera, pale unapokuwa na uwezo wa kuwaadhibu.

Kukasirika na kulipiza kisasi, kutokana tu na sababu binafsi, ni njia ya kuyaridhisha matamanio ya nafsi na kuonyesha uwezo wa mtu. Mja kuidhibiti hasira yake na kumsamehe yule aliyemuonea katika mazingira kama hayo ni matokeo ya kipekee ya imani yake; kwa sababu, pindi hasira inapokuwa imepanda, ni vigumu sana kuidhibiti nguvu ya utashi na kuirudisha isilipize kisasi.

Hasira ni janga katika maisha yetu. Kwa namna moja, ni aina ya uwenda wazimu, ambao huizuia akili isifanye kazi. Njia bora ya kuidhibiti hasira ni kujipamba kwa tabia njema, kama vile kusamehe na hali ya amani. Mola wetu Mtukufu anatupa habari njema zinazowasubiri waumini wanaoweza kuidhibiti hasira yao:

"Yakimbilieni maghfira ya Mola wenu Mlezi, na Pepo ambayo upana wake ni mbingu na ardhi, iliyowekwa tayari kwa wachamungu, ambao hutoa wanapokuwa na wasaa na wanapokuwa na dhiki, na wanajizuia ghadhabu, na wasamehevu kwa watu; na Mwenyezi Mungu huwapenda wafanyao wema." (3: 133-134)

Kwa maneno mengine, muumini anatakiwa kuyazuia maovu yanayoelekezwa kwake kwa kutumia misingi ya kimaadili ya Uislamu. Kwanza anatakiwa kuidhibiti ghadhabu yake. Kisha linakuja suala la kuwasamehe waonevu, na kisha kukabiliana na ubaya kwa wema na ukarimu.

SIKUTUMWA KUWA MCHOCHEZI WA LAANA ...

Maisha ya Mtume ﷺ yamejaa ishara na kuukabili uovu kwa wema. Kwa kuwa alitumwa kuwa rehema kwa ulimwengu, huruma, wema na upendo wake uliwaenea wanadamu wote.

Siku moja aliombwa kumlaani kafiri aliyekuwa akimtesa. Aliposikia ombi hili akasema:

"Sikutumwa kuwa mchochezi wa laana, bali nimetumwa kuwa rehema." (Muslim, Kitab Al-Bir, 87)

Kwa kuwa roho yake ilikuwa ni hazina kubwa ya huruma na upendo, lengo lake kuu ilikuwa ni kuwaokoa wanadamu wote. Alipokwenda katika mji wa Taif kwa lengo la kufikisha ujumbe wa Uislamu, watu wajinga na washirikina wa Taif walimtupia mawe. Mtume ﷺ aliporudi Makka akiwa katika hali ya kusikitisha, Mwenyezi Mungu alimtuma Malaika Jibril عليه السلام na malaika wa milima kwa ajili ya kumfariji. Malaika wa milima

alikuja na kumsalimia, na kisha akasema: “Ewe Muhammad! Agiza unachotaka. Ukipenda, nitaidondosha milima ya al-akh-shabain (milima miwili) juu yao.” Mtume ﷺ akasema:

“Hapana, bali ninataraji kuwa Mwenyezi Mungu atawaacha wapate vizazi ambavyo vitamuabudu Yeye pekee yake pasipo kumshirikisha na chochote.” (Bukhari, bad’ul Khalq, 7; Muslim, Jihad, 111)

Watu wa Taif waliendelea kuukataa wongofu wa Uislamu, mpaka mwaka wa tisa wa Hijrah na kusababisha hasara nzito kwa majeshi ya Kiislamu. Hatimaye, Waislamu hawakuweza kustahmili tena wakamwambia Mtume ﷺ:

“Ewe Mtume wa Allah! Mikuki na mishale ya Bani Thaqif (yaani kabila kuu katika mji wa Taif) inatuteketeza, tafadhali waombee adhabu na uwalaani.” Lakini Mtume ﷺ aliomba kama ifuatavyo:

“Ewe Mola wangu! Wajaalie muongozo wako na uwafanye waipate njia iliyonyooka ya Uislamu. Ewe Mola wangu! Wafanye waungane nasi.” Baada ya muda mfupi wakazi wa Taif walikuja Madina na kuukubali ujumbe wa Uislamu. (Ibn Hisham, al-Sīrah Al-Nabawiyah, IV, 134; Tirmidhi, Manāqib, 73/3942)

Mfano mwingine wa huruma yake ilikuwa Siku ya ushindi wa Makkah. Siku hiyo, washirikina wa Makkah, ambao hapo kabla waliwahi kuwatesa Waislamu kwa miaka mingi, walikuwa mikononi mwa Waislamu. Neno moja tu kutoka kwa Mtume ﷺ lingetosha kuwa adhabu yao. Mtume ﷺ aliwauliza watu hao wa Makkah: “Enyi Maquraishi! Mnafikiri nitawafanyia nini leo?” Wakajibu: “Tukitumaini wema na muamala wako wa haki, tunasema kuwa utatutendea wema. Wewe ni mkarimu na ndugu mwema, mwana wa mkarimu na ndugu mwema.”

Mtume ﷺ akasema:

"Ninawaambia yale ambayo Nabii Yusufu aliwaambia ndugu zake, "*Hapana lawama juu yenu leo; Mwenyezi Mungu atakusameheni, hakika yeye ni Mwingi wa rehma na mwenye kurehemu.*" [25] Nendeni, mko huru.[26]

Huruma ya Mtume isiyokuwa na ukomo iliwaathiri sana watu wa Makkah ambapo chuki na uadui wao ulibadilika kuwa upendo, urafiki na ikhlasi. Wengi wao waliingia katika Uislamu. Siku hiyo ukweli wa aya hii ulijionyesha wazi wazi kwa washirikina wa Makkah:

"Mema na maovu hayalingani. Pinga uovu kwa lilio jema zaidi. Hapo yule ambaye baina yako naye pana uadui atakuwa kama rafiki jamaa wa kukuonea uchungu." (41: 34)

Kwa kweli binadamu daima amekuwa akishindwa kwa ukaribu na wema. Wema na ukarimu daima vimekuwa nyenzo tosha ya kumrekebisha adui mbaya.

PONYO YA KUONDOA MATESO

Siyo ubora kuukabili wema kwa wema na uovu kwa uovu. Ubora wa kweli si tu kuukabili wema kwa wema bali pia kuukabili ubaya kwa wema. Kwa sababu ya ukarimu wetu, kama mtu anayetendewa wema ni adui yetu, atabadilika na kuwa rafiki; kama mtu huyo si rafiki wala adui yetu, basi huzidi kuwa karibu nasi; na kama ni rafiki, urafiki na mapenzi yake yataongezeka. Na kuupinga uovu kwa wema huwa ni uzio kati yetu na mtenda shari.

Jalal al-Din Rumi anaielezea tabia hii ya kitume kama ifuatavyo:

25.Qur'an 12: 92

26.Tazama Ibn Hisham, *al-sirah al-Nabawiyah*, IV,32; Waqidi, II, 835; Ibn Sa'd, II, 142.

"Rehema Yake (Mungu) inashinda kisasi chake: hiyo ndiyo sababu kwamba kila Mtume alimshinda adui yake; kwa maana (mtume) ni matokeo ya rehema (ya Mwenyezi Mungu) na kinyume chake ni (shetani): huyo aliyekosa rehema ni matokeo ya ghadhabu (ya Mwenyezi Mungu."[27]

"Vurugu siyo njia ya kuzuia balaa: njia (ya kuzuia balaa) ni ukarimu, kusamehe na wema. Onyo lifuatalo kutoka kwa Mtume ﷺ likuamshe:

(Mtume) anasema, ***'Sadaka ni njia ya kuzuia balaa: waponye wagonjwa wako kwa (kutoa) sadaka****.' Sasa ielewe vyema njia ya kuponya magonjwa na mateso."*[28]

Katika matukio mengi, Mtume ﷺ alipokuwa na nafasi ya kuwaadhibu wahalifu, alionyesha ubora wa kusamehe ili kuwarekebisha na kuwafanya wapate wokovu wa milele. Kwa sababu ubora na ushujaa wa kweli ni mtu kuwa na uwezo wa kuidhibiti nafsi yake na kusamehe pindi anapokuwa na nafasi na uwezo wa kulipa kisasi. Kwa hakika, jambo hili limeelezwa na Mtume ﷺ akatika maneno yake yafauatyo:

"Shujaa siyo yule awashindaye watu kwa nguvu zake, bali shujaa wa kweli ni yule anayeidhibiti nafsi yake pale anapokuwa na hasira." (Bukhari, Adab, 76)

Aya ifuatayo inatoa habari njema kwa wale wenye tabia hii:

"Na malipo ya uovu ni uovu mfano wa huo. Lakini mwenye kusamehe, na akasuluhisha, basi huyo malipo yake yapo kwa Mwenyezi Mungu. Hakika Yeye hawapendi wenye kudhulumu." (42: 40)

Kusamehe makosa na kulipa uovu kwa wema ili kuweka amani na urafiki ni tabia ya kipekee ya Mtume ﷺ. Na sisi kama

27.Mathnawi, V, 515 - 516
28.Mathnawi, VI, 2590 -2591

wafuasi wake, tunapaswa kujipamba kwa sifa hizo hizo. Kusamehe siku za sikukuu pekee na kulipuuza siku za kawaida siyo sifa na tabia muafaka ya muumini wa kweli. Kuzifanya tabia hizi kama sifa zetu za kimaumbile ni alama na ishara muhimu ya ukomavu wa imani zetu.Maneno yafuatayo ya Mtume ﷺ yanatakiwa kuwa kipimo cha mfano kwa kila muumini:

"Yeyote miongoni mwenu asiwe katika wale wanaosema "Niko pamoja na watu, wakinitendea mema nitawatendea mema; na wakinitendea mabaya, nitawatendea mabaya." Kinyume chake, mnatakiwa kuzifundisha nafsi zenu kulipa wema kwa wema na kutowatendea mabaya wale wanaowatendea mabaya." (Tirmidhi, Kitab al-Birr, 63)

"Usikate uhusiano wako na wale wanaokata uhusiano wao nawe. Wape msaada wale wasiokupa msaada. Wasamehe wale wanaokutendea mabaya." (Ahmad b. Hanbal, IV, 148,158)

"Muogope Mwenyezi Mungu popote utakapokuwa. Fuatisha ovu kwa jema ili ulifute lile ovu. Amiliana na watu kwa tabia njema." (Ibrahim Canan, kütüb-i sitte, V, uk. 304)

Niliona majumba katika mabustani ya peponi nikamuuliza Jibril عليه السلام:

"*Majumba haya ni ya nani?"* Akasema:

"Ni makao ya waumini wanaozidhibiti hasira zao, wanazifukia chuki zao katika nyoyo zao na wanasamehe makosa ya watu." ('Ali Al-Muttaqī, 7,016; Awārif, uk. 253)

KUSAMEHE KATIKA WAKATI SAHIHI

Tunapaswa kukumbuka kwamba kusamehe kila aina ya makosa haipaswi kuchukuliwa kuwa ni jambo sahihi. Msama-

ha unahusika tu pale ambapo kosa limetendwa katika mambo binafsi. Kuna makosa na uhalifu unaotendwa dhidi ya jamii, dini na mambo matukufu, ambao hauwezi kuvumiliwa. Katika hali kama hiyo, adhabu inatakiwa ili kuwarekebisha wahalifu, kutenda haki na kubainisha baina ya haki na batili. Vinginevyo, kusamehe matendo haya ya kihalifu itakuwa ni dhulma kubwa kwa jamii.

Bibi Aisha ﵂, mke wa Mtume ﷺ, anaelezea yafuatayo kuhusu utoaji msamaha wa Mtume ﷺ:

"Alipotakiwa kuchagua kati ya mambo mawili alichukua lililo jepesi zaidi, kama jambo husika likiwa siyo dhambi, lakini kama ni dhambi yoyote alikuwa akijiweka mbali nayo zaidi kuliko watu wote; na Mtume ﷺ kamwe hakulipa kisasi kwa yeyote kwa maumivu yake binafsi, labda kwa lile ambalo Mwenyezi Mungu Mtukufu alitaka lisikiukwe kisha likakiukwa." (Muslim, Fadāil, 79, Abu Dawud, Kitab al-Adab, 4).

Kama ambavyo kukasirika katika mahali ambapo hapastahili kukasirika husababisha uovu na machafuko kati ya watu, kutokasirika wakati inapobidi ni udhaifu wa kimaadili wenye matokeo yale yale. Kukasirika kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, pindi inapobidi kufanya hivyo, ni sharti la imani. Kwa mfano kuwa na hasira dhidi ya adui katika medani ya vita ni alama ya msisimko wa imani ndani ya moyo na ni dalili ya uchamungu na uzalendo. Kuonyesha hasira dhidi ya uhalifu unaotendwa kuhusu mambo ya haki za jamii, dini na tunu za umma ni ishara ya ubora wa imani ya mtu.

Maisha ya Mtume wa Allah yamejaa ishara na mambo hayo. Hakuwasamehe tu wakosaji katika mambo binafsi bali pia aliwatendea wema.

JE HAMPENDI MWENYEZI MUNGU AKUSAMEHENI?

Abu Bakr ﵁, ambaye alizama ndani ya upendo wa Mtume ﷺ, naye pia alionyesha mifano ya kipekee ya kusamehe. Kwa mfano, palikuwa na masikini mmoja aitwaye Mistah, ambaye ilikuwa ni kawaida kwa Abu Bakr kumsaidia. Abu Bakr alipogundua kuwa Mistah alikuwa miongoni mwa wale waliomzushia uongo Aisha ﵂, aliapa kuwa asingetoa tena msaada kwa Mistah na familia yake. Kutokana na kukosa msaada wa kifedha wa Abu Bakr, Mistah na familia yake walianza kuteseka. Kutokana na jambo hili aya zifuatazo zikateremka:

"Na wale katika nyinyi wenye fadhila na wasaa wasiape kutowapa jamaa zao na masikini na waliohama kwa Njia ya Mwenyezi Mungu. Na wasamehe, na waachilie mbali. Je! Nyinyi hampendi Mwenyezi Mungu akusameheni? Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe Mwenye kurehemu." (24: 22)

"Wala msifanye jina la Mwenyezi Mungu katika viapo vyenu kuwa ni kisingizio cha kuacha kufanya wema na kumchamungu na kupatanisha baina ya watu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia na Mwenye kujua." (2: 224)

Abu Bakr As-Siddiq akasema, "Ndiyo, naapa kwa Mwenyezi Mungu, ninapenda Mwenyezi Mungu anisamehe." Akatoa fidia ya kuvunja kiapo na akaendelea kumpa Mistah pesa aliyokuwa akimpatia hapo kabla. Akaongeza kusema, "Ninaapa kwa Mwenyezi Mungu, kamwe sitomnyima msaada huu hata kidogo." (Bukhari, Maghazī, 34, Muslim, Tawbah, 56; Tabari, Tafsir, II, 546)

Kwa sababu kuendelea kuwasamehe waja wa Mwenyezi Mungu na kustahili kusamehewa na Mwenyezi Mungu ni sifa ya lazima ya marafiki wa Mwenyezi Mungu.

KIASI GANI CHA WEMA KINACHOTAKIWA KUONYESHWA KATIKA KUKABİLİANA NA UOVU?

Siku moja maswahaba walimuuliza Mtume ﷺ kwa nini anampenda sana Ali رضي الله عنه. Mtume ﷺ akaagiza kuwa Ali رضي الله عنه aitwe. Sahaba mmoja akaenda kumuita. Kabla hajawasili, Mtume ﷺ akawauliza maswahaba:

"Rafiki zangu wapendwa! Mtafanya nini iwapo utamtendea mtu wema, lakini yeye akakulipa ubaya?"

Maswahaba wakajibu kuwa wataamiliana naye kwa wema. Mtume ﷺ akauliza: *"Mtafanya nini iwapo ataendelea kukutendea vibaya?"* Kwa mara nyingine wakatoa jibu hilo hilo. Mtume ﷺ alipouliza swali hilo kwa mara ya tatu, waliinamisha vichwa vyao na wakawa hawakujibu.

Baadaye Ali عليه السلام alifika. Ingawa Mtume ﷺ alimuuliza swali hilo hilo mara saba, kila mara Ali رضي الله عنه alijibu:

"Nitamtendea uzuri." Kisha akaongeza kusema:

"Hata kama akiendelea kulipa fadhila zangu kwa kunitendea vibaya, nitaendelea kuamiliana naye vizuri." Kwa hakika Ali alisema:

"Mtu mbaya kabisa kati ya watu ni yule anayelipa wema kwa ubaya na mbora wao ni yule anayeukabili ubaya kwa wema."

"Wafanyie watu mema bila kutarajia radiamali mbaya kwa wema wako."

BINADAMU NI WATUMWA WA FADHILA

Kwa mujibu wa simulizi moja, mtu mmoja alimuita majina mabaya mjukuu wa Ali ﷺ aitwaye Ali. Katika kujibu lugha ya matusi ya mtu huyo, Ali ﷺ alimpa kanzu yake na kuwaamuru wasaidizi wake wampatie mtu huyo dirhamu elfu moja. Inaelezwa kuwa kwa kitendo chake hicho alionyesha sifa na tabia tano kwa wakati mmoja:

Mosi, upole kwa sababu hakupata hasira;Pili, aliondosha uovu;Tatu, alimlinda mtu huyo asiende mbali na njia ya Mwenyezi Mungu Mtukufu; Nne, alimuongoza mtu huyo kwenye toba na kujuta;

Na tano, aliisimamisha lugha chafu ya mtu huyo na kumfanya mtu huyo aanze kumsifia badala ya kumtukana.

Katika tukio jingine, mtu mmoja alitumia lugha chafu dhidi ya Ibn Abbas ﷺ. Lakini Ibn Abbas hakujibu chochote na kisha akamgeukia Ikrimah na kusema:

"Angalia kama mtu huyu anahitaji chochote na umpatie." Kwa jambo hili mtu huyo aliona aibu na kuinamisha kichwa chake.

MACHO YANAYOWEZA KUWALILIA MAADUI

Tabia ifuatayo ya Fudayl bin 'Iyad ni mfano mzuri kwetu. Watu walimuona akilia wakamuuliza kwa nini analia. Akasema:

"Ninalia kwa sababu ninawasikitikia Waislamu walionikosea. Huzuni yangu yote ni kwa sababu ya adhabu ya kutisha itakayowakuta huko Akhera."

Katika tukio jingine, Fudayl bin. 'Iyad aliambiwa kuwa:

"Mtu fulani anasema maneno mabaya dhidi yako," akasema:

"Ninaapa kwa Mwenyezi Mungu, simkasirikii mtu anayenikashifu, lakini ninamkasirikia Ibilisi aliyemdanganya". Kisha akaomba akisema:

"Ewe Mola wangu! Nisamehe kama ayasemayo ni kweli, na msamehe kama ayasemayo ni uwongo."

Siku moja Hassan Al- Basri alimtumia zawadi mtu aliyekuwa akimsengenya badala ya kumghadhibikia. Kwa sababu alijua vyema kuwa msengenyaji huyo alikuwa aidha akipunguza thawabu zake kumpa yule anayemsengenya au anachukua dhambi za mtu yule.

Hallaj Mansur alipokuwa akipigwa mawe alikuwa akiomba dua akisema:

"Mola wangu! Wasamehe wale wanaonipiga mawe kabla hujanisamehe mimi."

Siku moja Rab'i b. Haytham alikuwa akiswali, farasi wake mwenye thamani ya dirhamu elfu ishirini aliibiwa mbele ya macho yake. Laini, aliendelea kuswali kwa amani badala ya kumkamata mwizi. Marafiki zake waliposikia habari hizi, walikwenda kumfariji. Akawaambia;

"Nilimuona mwizi akimchukua farasi wangu, lakini wakati huo nilikuwa nashughulika na jambo ambalo ni muhimu zaidi na linapendeza zaidi kwangu. Hii ndiyo sababu iliyonifanya nisimkimbilie mwizi."

Baada ya jibu hili, marafiki zake wakaaza kumlaani mwizi, lakini Rab'i b. Haytham akawakatisha na kusema:

"Tulieni, hakuna aliyenidhulumu. Mtu yule ameidhulumu nafsi yake mwenyewe. Hatutakiwi kumdhulumu kwa yale aliyonitendea.

Uzuri ulioje wa maneno ya Rumi:

WATU HUUZA WALICHO NACHO

Siku moja Nabii Issa عليه السلام alikwenda kwa Wayahudi fulani kufikisha ujumbe wake. Ingawa walianza kumkashifu, yeye alizungumza nao kwa uzuri. Watu walipomwambia kuwa:

"Wanakwambia mambo hayo ya kutisha na bado unaendelea kuzungumza nao kwa upole." Akasema kuwa:

"Watu huuza walicho nacho."

Kwa maneno mengine, tabia, mwenendo na mazungumzo ya mtu yeyote ni vioo vinavyoonyesha ulimwengu wake wa ndani. Kama ambavyo hatuwezi kuchora msitari ulionyyoka kwa kutumia rula iliyopinda, tusitarajie matendo mazuri kutoka kwa mtu aliyeghafilika ambaye anaishi katika ulimwengu wa kiroho uliojaa mawingu. Wale wenye dhamiri (nia) nyeusi hawawezi kuwa na njia nyeupe yenye mwanga mbele yao. Kila birika huvujisha kile kilicho ndani yake.

Kwa hiyo basi kuukabili uovu kwa kutumia uovu ni tabia ya watu wasiokomaa. Kuwa na uwezo wa kufanya mema katika hali na mazingira ya aina yoyote ile, kwa upande mwingine, huonyesha daraja ya juu ya hali ya kiroho ya mtu husika. Kuna daraja tatu za kuwatendea watu wema:

Mosi, kulipa wema kwa wema. Ni jambo la asili na ni maumbile ya mtu kuhisi kuwa anatakiwa kushukuru kwa wema aliotendewa. Litakuwa jambo jema iwapo wema utalipwa kwa wema mkubwa zaidi.

Pili, kutenda wema bila kutarajia kulipwa wema. Watu hawa ni bora kuliko wale wa kundi la kwanza.

Aina ya mwisho ni kulipa ubaya kwa wema. Hili ndilo kundi bora kabisa kwa sababu thamani ya tendo hutegemea ugumu wake. Ni jambo gumu sana kutarajia wema katika kuukabili ubaya. Ndiyo maana kuna methali ya Kituruki isemayo kuwa: "Kila mtu anaweza kufanya wema katika kuulipa wema, lakini mtu mkomavu ndiye pekee anayeweza kulipa wema kwa ubaya aliotendewa."

Rumi analielezea jambo hili kwa uzuri kabisa katika tungo zifuatazo;

"Ndani ya maji kuna baraka na marhamu nyingi mno; yanakubali udhalili na kusafisha uchafu." [29]

Muumini aliyekomaa anapaswa kuwa na moyo mkubwa na wenye utajiri kama bahari. Daima anatakiwa kuonyesha wajihi wa amani na utulivu wa Uislamu kwa fadhila, uzuri na wema.

Tena Rumi anasema kuwa kama ardhi. Ardhi hutoa mazao yake bila uchoyo na kuwapa watu wanaoikanyaga. Vile vile husafisha takataka za viumbe na kuwarudishia mazao mazuri, safi na yenye afya.

Mwenyezi Mungu Mtukufu anatupatia mifano ya ajabu kama maji na ardhi ili tujifunze kutokana na vitu hivyo. Kwa mwanadamu ambaye asili yake ni ardhi na maji, linapaswa

29.Mathnawi, V, 200 -236

kuwa jambo la kiroho kutafakari juu ya hekima yake na kufikia sifa na tabia mfano wa vitu hivyo.

Mola wetu tujaalie ladha tamu ya kiroho! Tupe baraka ya kuwa miongoni mwa waumini wema wanaopata msamaha wa Mwenyezi Mungu kwa sababu ya kuwasamehe watu wengine! Ifanye furaha ya kupata mafunzo kutokana na maisha ya Mawalii wake kuwa hazina isiyokauka ya maisha yetu ya kiroho!

Amin....

KUTABASAMU

Lengo la dini ni kulea watu wenye adabu, wema na wenye kujitambua. Waumini kamili daima huwa katika hali ya kuwapa salamu viumbe wote kwa nyuso zenye tabasamu. Dirisha la ulimwengu wao wa kiroho hufunguka kwa ajili ya viumbe wengine; kwa sababu, waumini kamili ni watu wenye heshima na utambuzi kama maua na wakarimu kama matunda ya miti.

KUTABASAMU

MAISHA katika dunia hii yanaendelea pamoja na milima na mabonde yake. Roho ya mwanadanu ni kama nyumba ya wageni. Siyo huzuni na mateso pekee bali pia furaha na mazuri ya ulimwengu huu ni kama wageni wake. Hakuna kati ya hivyo chenye kudumu. Ndiyo maana muumini hatakiwi kuvuruga mpangilio na utulivu unaopatikana katika ulimwengu huu kwa kujisikia furaha au huzuni kupita kiasi anapokabiliwa na matukio mbalimbali ya uliwengu huu wenye kuchosha.

Maisha yenye ukamilifu ya Mtume ﷺ yamejaa alama za huzuni na mateso. Aidha, analielezea hili katika maneno yafuatayo:

"Hakuna aliyeteseka katika njia ya Mwenyezi Mungu kama nilivyoteseka." (Tirmidhi, Qiyama, 34/2472)

Lakini, hakuna taabu yoyote iliyozuia nia na azma yake. Alikabiliana nayo yote kwa uthabiti na ridhaa. Ingawa moyo wake ulikuwa umejaa huzuni, kamwe uso wake haukuondokana na tabasamu. Hakuna mtu aliyewahi kumuona akiwa na uso chukivu au wenye kununa; kwa sababu, daima alikuwa akitabasamu kwa amani na utulifu kwa kuwa mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu na kuonyesha uso wenye tabasamu wa Uislamu katika mazingira ya aina yoyote ile.

Wema wa uzuri wa ndani wa maswahaba wa Mtume ﷺ na marafiki wa Mwenyezi Mungu, ambao waliziyeyusha nafsi zao ndani ya Mtume ﷺ *(fanaa fi rasuulillah)*, unajionyesha katika nyuso zao. Ummu al - Darda ﵂ anasimulia kuwa:

"Abu Darda alipokuwa akizungumza, daima alitabasamu. Siku moja nikamwambia: "Mimi nina wasiwasi kuhusu watu kufikiri kuwa tabasamu lako siyo la kawaida wakakuogopa" naye akajibu:

"Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ hakika alitabasamu pale anapozungumzia jambo fulani." (Ahmad, V, 198, 199)

Tabasamu la mara kwa mara la Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ ni alama bora ya furaha anayohisi kuwa pamoja na Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Kila mwanadamu huhisi raha kutokana na kuwa na furaha; hata hivyo, kama ilivyo katika kila kitu, lazima kuwa na kiwango cha wastani na sahihi cha kufurahi. Kama ambavyo ni vibaya mtu kuiharibu nafsi ya mtu kwa sababu ya mateso yanayomkabili katika dunia hii, vivyo hivyo ni vibaya kuonyesha furaha kupita kiwango mbele ya matukio ya kufurahisha ya ulimwengu huu. Hizi hali zote mbili huharibu utu na shakhsia ya mwanadanu.

Muumini daima anapaswa kuwa na moyo sikivu na maridadi. Daima anatakiwa kuwa na tabasamu usoni mwake. Tabasamu ndiyo utu wa muumini kwa kulinganisha na utovu wa ustaha wa kucheka. Kwa upande mwingine, huleta haiba na mvuto kwa muumini kinyume na uchushi wa uso wenye kujikunja.

Jalal al-Din Rumi anatoa onyo kuhusu hilo kwamba hata tendo la kawaida kama kutabasamu linaweza kuonyesha tabia ya mtu na kusema kuwa:

"Kutokana na anavyotabasamu, hupata kujua ubora wa tabia zake; na kutokana na kile anchotabasamu ninapata kujua kiwango cha akili yake."

Kucheka kupita kiasi wakati mwingine humsukuma mtu kwenye hali ya kughafilika na kusahau kwamba anatahiniwa hapa duniani. Kusahau kwamba furaha ya kweli inapatikana Akhera matokeo yake ni kuitia nafsi katika utumwa wa furaha za kidunia. Vicheko virefu na vyenye kuendelea huipa sumu roho, huufifiza moyo, na kuufanya upoteze hisia zake.

Omar ﷺ anatoa tahadhari ifuatayo kuhusu hatari ya kucheka kupita kiasi:

"Wale wanaocheka kupita kiasi hupoteza heshima yao. Wale wanaofanya mzaha mno huudhiwa. Watu hujulikana kwa mambo wanayoyafanya. Wale wanaongea sana hufanya makosa mengi sana. Wale wanaofanya makosa sana hupoteza aibu. Wale wanaopoteza aibu ni mara chache kuepuka vitu vya haramu. Nyoyo za wale wanaoepuka mambo ya wajabu hupoteza uhai." (Ghazālī, Ihyā, III, 288)

Hali ya kughafilika ambayo ni maradhi makubwa ya kiroho, humdanganya mwanadamu kwa kumuonyesha kuwa maisha yake katika hii dunia ni ya milele. Hali ya kughafilika huyavuruga mawazo yake na kumfanya ayasahau matatizo makuu ya mwanadamu katika dunia hii kama vile kifo, kufufuliwa, siku ya hukumu, na akhera. Tabia hii ya mwanadamu imeelezwa katika aya ifuatayo:

"Na mnacheka, wala hamlii? Nanyi mmeghafilika?" (53: 60 -61)

Kuhusiana na jambo hili, Mtume wa Mwenyezi Mungu anasema kuwa:

"Laiti mngejua ninayojua mngecheka kidogo na kulia sana." (Bukhari, tafsir, 5 / 12) Jalal-al-Din Rumi pia anaelezea ukweli huu kama ifuatavyo:

"Watu wenye busara, kwa hakika, hufanya maombolezo kwanza na kutabasamu baadaye; wajinga, kwa upande mwingine, hutabasamu kwanza na kupiga vichwa vyao mwisho. Enyi watu! Tangu mwanzo wa mambo utambueni mwisho (wake), ili msije mkawa mnatubu Siku ya hukumu." [30]

Katika suala hili Imam Ghazālī anasimulia kisa kifuatacho.

Mtu mmoja alimuuliza ndugu yake ambaye alikuwa akicheka sana:

"Kuna nini? Umepata taarifa kuwa umeokolewa na moto wa Jahannamu?" Ndugu yake akasema: "Hapana." Mtu huyo akamuuliza tena: "Sasa inakuwaje unacheka sana?" (Ghazālī, Ihyā, III, 288)

Hakuna mja hata mmoja katika waja wa Mwenyezi Mungu, tofauti na mitume, ambaye ana uhakika wa kuingia peponi.

Wahb bin Ward ﷺ alitoa ushauri ufuatao kwa watu aliowaona wakicheka siku ya sikukuu:

"Kama mmesamehewa dhambi zenu, hii siyo tabia ya watu wanaoshukuru. Kama hamjasamehewa dhambi zenu, basi hii siyo hali ya wale wanaoogopa adhabu ya Mwenyezi Mungu." (Ghazālī, Ihyā, III, 288)

Muhammad bin Waşi (Mwenyezi Mungu aihurumie nafsi yake) anasema kwamba:

"Vicheko vya wale wasiojua kama ni watu wa peponi au motoni ni vya ajabu kama kilio cha mtu ambaye tayari amepokelewa mbinguni." (Ghazālī, Ihyā, III, 289)

30. Mathnawi, III,1623 - 1624

Kitendo hiki kina kipengele ambacho, maadili ya Kiislamu yanawasaidia wafuasi wake kukipata. Hivyo, hata kama muumini ana volkano kubwa zinazochemka moyoni mwake, uso wake unatakiwa kutawanya utulivu kama vile bandari salama. Hatakiwi kulewa raha mno wala kuelemewa na huzuni kupita kiasi.

Muumini anatakiwa kustawisha hali ya kati kwa kati ndani ya moyo wake baina ya *hawf* na *raja'. Hawf* ina maana ya kutoharibiwa na matendo mema na kuwa katika hali zote mbili za kuendeleza maombi na kuhofu adhabu ya Mwenyezi Mungu.

Raja', kwa upande mwingine, ina maana ya kutumaini rehema Yake na kutokata tamaa.

Khalid al-Baghdādī anaelezea hali hii ya moyo kumwambia mmoja wa wanafunzi wake katika barua:

"Naapa kwa Mwenyezi Mungu kwamba mimi siamini kwamba nimetekeleza amali hata moja ambayo ni yenye kukubaliwa na Mwenyezi Mungu na ambayo sitoulizwa mbele yake tangu siku nilipozaliwa ... (Ninatumaini tu rehma ya Mola wangu)

... Tafadhali usisahau kuomba kwa ajili ya mafanikio ya mja huyu masikini na ili awe na mwisho mwema. "

Uso wenye tabasamu, ambalo ni sifa muhimu ya muumini, unaonyesha pia daraja ya hali ya kati kwa kati. Hata hivyo, hata tabia nzuri, kama vile kutabasamu, ina balaa lake na balaa la kutabasamu ni kulifanya kwa nia mbaya. Kutabasamu kwa nia mbaya kama vile kujiona, kuwadhihaki, kuwakejeli ndugu zako katika Uislamu litakuwa na matokeo mabaya siku ya Kiyama.

Ibn Abbas akitafsiri neno "**dogo au kubwa**" katika aya isemayo: **"Watasema**: **Ole wetu! Kitabu hichi kina nini! Hakiachi dogo wala kubwa ila huliandika?..."** (18: 49) anasema: "dogo linalokusudiwa ni kutabasamu wakati wa kumdhihaki muumini, na dhambi kubwa, kwa upande mwingine, ni kucheka wakati huo huo." (Ghazālī, Ihyā, III, 294)

TABASAMU LA MUUMINI HUWA USONI MWAKE; HUZUNI ZAKE HUWA MOYONI MWAKE

Kulingana na yote yaliyoelezwa hapo juu, moyo wa muumini pia unahitaji kuwa na kiasi fulani cha huzuni na hofu. Lakini, hata katika nyakati za huzuni na wasiwasi, uso wake unatakiwa ung'arishwe kwa tabasamu.

Sayyidna Ali ﷺ anasema kwamba:

"Tabasamu la muumini huwa usoni mwake na huzuni yake hukaa moyoni mwake."

Kwa maneno mengine, muumini wa kweli huwa mwenye huzuni na kulia sana anapokuwa mahali pa faragha pindi anapoyakumbuka makosa yake. Machozi yake pia ni chanzo cha nuru katika nyuso zao.

Jalal al-Din Rumi anaelezea hekima ya nuru katika uso wa muumini kama ifuatavyo:

"Ewe muumini wa miungu (zaidi ya mmoja)**,** (kama) **nisipoutazama uso** (uhalisia) **wangu mwenyewe, nitautazama uso wako nawe utautazama uso wangu. Yule autazamaye uso** (uhalisia) **wake mwenyewe - nuru yake ni kubwa kuliko nuru ya viumbe wote** (wa Mwenyezi Mungu)**."** [31]

31. Mathnawi, II, 883-884

Kwa maneno mengine, mojawapo ya sababu za nuru ya uso wa muumini ni kuwa na uwezo wa kuutazama kwa umakini uso wake mwenyewe na kuona makosa yake kabla ya kuangalia makosa ya watu wengine. Hili ndiyo chimbuko la nuru katika uso wa anayemtambua Mungu, ambaye huielewa vyema hekima ya maneno yasemayo: *"Wanaojitambua huweza kumtambua Mola wao."* Hii ndio sababu inaelezwa kuwa; *"Hakuna hekima (elimu) kama mtu kuyajua makosa yake mwenyewe."*

Abdulqadir Jilani anasema kuwa:

"Muumini hujifanya kuwa ana furaha awapo kati ya watu, lakini kiuhalisia ni mwenye huzuni... hutaamali, hutafakari na hulia sana, lakini hucheka kidogo. Huificha huzuni moyoni mwake kwa kuonyesha tabasamu usoni mwake. Kwa nje huonekana kana kwamba anafanya kazi kujipatia maisha yake, wakati moyo wake unashughulishwa na kumdhukuru na kumkumbuka Mola wake. Anaonekana kuwa yuko pamoja na watoto na wanafamilia yake, lakini kiuhalisia, moyo wake uko pamoja na Mola wake.

Acha tama , usafihi, ukaidi na kupendwa sana dunia. Punguza kidogo raha na furaha yako! Huzunika kidogo! Tambua kuwa Mtume wetu mpendwa ﷺ alitabasamu ili kuwachangamsha wale walio karibu naye."

Kucheka sana ni hali ya ukosefu wa uwastani. Wakati kuwa na uso mkali ni mwisho mwingine wa ncha. Hali zote mbili ni majanga ya kiroho kwa roho za waumini. Kutabasamu ni hali ya kadiri na ni tabia yenye kukubalika zaidi.

TABASAMU LA MTUME ﷺ

Tabasamu linaweza kuelezewa kama kucheka kwa kuonyesha sehemu ndogo tu ya meno. Hii ndio iliyokuwa cheko la Mtume ﷺ. Tabasamu lake kamwe halikuonyesha hali ya kupitiliza kama vile kucheka. Kuhusu jambo hili, bibi Aisha رضي الله عنها anasema kuwa:

"Kamwe sikuwahi kumuona Mtume akicheka kwa kiasi cha mtu kuona paa la kinywa chake, bali alikuwa akitabasamu tu." (Bukhari, Kitab al-adab, 68, Muslim, istisqā, 16)

Kwa mujibu wa hadithi nyingi za maswahaba, Mtume ﷺ alikuwa na adabu na tabia bora na alikuwa mpole na mtaratibu kuliko watu wote. Daima alikuwa akitabasamu na uso wake ulikuwa uking'aa kwa nuru ya tabasamu lake.

Abdullah bin Salam, mwanazuoni wa Kiyahudi, katika kudadisi alimuulizia Mtume ﷺ wakati wa hijra yake kutoka Makkah kwenda Madina. Alipoona uso wa Mtume ﷺ akasema:

"Mwenye uso kama ule hawezi kusema uongo" na kisha akasilimu. (Tirmidhi, Qiyāmah, 42/2485, Ibn Majah, At'imah, 1: Iqāmah, 174)

Uso na mavazi ya mtu ni kama dirisha lake. Kila kiumbe kina lugha ya tabia na adabu. Kwa maneno mengine, mtu huzungumza kupitia tabia yake, hata kama atakuwa ameufunga mdomo wake. Watu hubeba dalili za ulimwengu wao wa ndani kwenye nyuso zao. Nyuso ni mkalimani wa macho anayeuelezea ulimwengu wa ndani na kuyawezesha macho kuona (yaliyo ndani kutokana na ukalimani huo). Hii ndio sababu kwamba tabasamu lenye kuchomoza ni kioo kizuri cha ulimwengu wa ndani.

Jalal al-Din Rumi analielezea jambo hili kwa uzuri ndani ya tungo zifuatazo:

"Ukitaka kununua komamanga, linunue wakati likitabasamu (baada ya kaakaa lake kufunguka), ili kicheko chake (uwazi) kiweze kutoa taarifa za mbegu zake. Oh, Kibarikiwe kicheko chake, kwani kupitia kinywa chake kinapata kuuonyesha moyo, kama lulu zitokazo katika kijaluba cha roho... komamanga lenye kucheka hulifanya bustani kuwa lenye kucheka (kwa kupendeza na kuchanua): usuhuba na watu (watukufu) hukufanya uwe miongoni mwa watu (watukufu). Ikiwa wewe ni mwamba au jiwe, utabadilika kuwa kito utakapofika kwa mtu mwenye moyo (walii)." [32]

Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa akipita karibu na watu kwa utaratibu huku akitabasamu. Alikuwa akisikiliza mazungumzo ya maswahaba wake kwa umakini ili kuwafurahisha. Alitabasamu kwa kuonyesha sehemu ya meno. Maswahaba wake walifuata desturi na kuiga tabia zake.

Anasimulia Jarir b. Abdullah kuwa;

"Mtume hakuwahi kujificha dhidi yangu (kamwe hakuwahi kunizuia nisiingie kwake) tangu nilipoingia katika Uislamu, na kila aliponiona alinipokea kwa tabasamu." (Bukhari, Kitab Al-Adab, 68)

Abdullah bin Harith anasema kuwa:

"Sijaona mtu yeyote mwenye kutabasamu zaidi ya Mtume ﷺ." (Tirmidhi, Manāqib, 144)

Hapa kuna baadhi ya maneno ya Mtume ﷺ kuhusu ubora wa kutabasamu:

"Usikichukulie kitu chochote kuwa kisichokuwa na umuhimu katika mambo mema hata kama utakutana na ndugu yako ukiwa na uso wenye furaha." (Muslim, Kitab Al-Bir, 144)

32. Mathnawi, I, 718 -719, 721 -722

“ Kila tendo la wema ni sadaka. Kumpa ndugu yako uso wenye furaha na kumminia maji katika chombo chake ni katika wema” (Tirmidhi, Kitab Al-Bir, 45/1970. Ahmad B. Hanbal, Iii, 344; Bukhari, Al- Adab Al-Mufrad, No: 304)

Wakati Mtume ﷺ akiwa hana chochote cha kuwapa masikini alikuwa akiugeuzia uso wake kwa kuhisi aibu. Hapo aya ifuatayo ikateremka:

“Na ikiwa unajikurupusha nao, nawe unatafuta rehema ya Mola wako Mlezi unayoitaraji, basi sema nao maneno laini.” (17:28)

Baada ya amri hii kutoka kwa Mwenyezi Mungu, pindi Mtume ﷺ alipokuwa hana kitu cha kutoa, alikuwa akitabasamu na kuzungumza vizuri na masikini ili kuzivuta nyoyo zao.

Kwa hivyo basi, kutabasamu, kusalimia na kuzungumza vizuri havipaswi kudharauliwa. Hizi ni baadhi ya ibada za kijamii kwa kila roho ya muumini; kwa sababu, kutabasamu ni desturi aliyodumu nayo Mtume ﷺ na kuitilia mkazo.

TABASAMU LA MARAFIKI WA MWENYEZI MUNGU

Waumini wema, ambao wamejipamba kwa maadili ya Mtume ﷺ, hufuata nyayo za Mtume ﷺ katika kila kipengele cha maisha yao. Huwapa watu furaha na utulivu kwa nyuso zenye tabasamu. Kutazama kwao huwa ni ponyo ya nyoyo zenye maradhi. Nyuso zao zenye nuru huwakumbusha watu kuhusu Mwenyezi Mungu Mtukufu na maisha baada ya kifo; kwa maana wao huendelea kupokea baraka za Mtume ﷺ.

Kuwa na tabia ya uwaridi kama Mtume ﷺ na marafiki wa Mwenyezi Mungu ni sifa yenye faida kwa wafuasi wa Muhammad ﷺ. Kwa sababu waridi hustahimilia miiba kwenye matawi yake, na wakati huo huo likitabasamu kwa harufu yake nzuri na kuwaambia watu: “Fikiria kuhusu mimi na uwe kama mimi.”

Lengo la dini ni kulea watu kama hao wenye adabu, wazuri na wenye hisia. Waumini kamili daima huwa katika hali ya kuwasalimia viumbe wote kwa nyuo zenye tabasamu. Dirisha la ulimwengu wao wa kiroho huwafungukia viumbe wengine; kwa sababu, waumini waliokamilika ni watu wenye adabu na hisia kama maua na ni wakarimu kama matunda ya miti.

Junaid al- Baghdadi anasema kuwa sharti na tabia muhimu zaidi katika kuwa na urafiki na ndugu katika dini ni kukutana naye ukiwa na uso wenye tabasamu na kumfanya afurahi, wakati Abu Uthman Hari naye anasema kuhusu jambo hili kuwa ni kumuonyesha tabasamu anapokuwa hatendi dhambi. Abu Abdullah Salimah anaeleza kuwa mazungumzo mazuri na uso wenye bashasha ni sifa bainishi za marafiki wa Mwenyezi Mungu.

Harith al-Muhasib anasema kuwa;

“Tabia njema ni mambo manne:

- Kuwa na subira mbele ya mateso ya watu walioghafilika.

*- Kutokasirika sana (kuwa na uwezo wa kusema **amani** unapochokozwa na wajinga)*

- Kuwa na uwezo wa kuonyesha uso wa bashasha wa Uislamu.

- Kuwa na lugha nzuri na laini”.

Hassan al-Basrī anazungumzia kwa muhtasari tabia njema kama ifuatavyo:

"Kiini cha tabia njema ni kueneza wema, kutowasumbua watu na kuwa na uso wenye tabasamu."

Donge la ulimwenguni limetengenezwa kwa chachu ya upendo. Kila kitu, kuanzia kwenye kitu kidogo mpaka kwenye vitu vikubwa, utakapokichunguza kwa jicho la roho, utaona kuwa kuna upendo wa Mwenyezi Mungu katika kiini cha kila kitu. ishara na Mwenyezi Mungu Mtukufu katika ulimwengu huu, kama vile mabustani, chemchem, maua, vipepeo, ndege, n.k. vyote vinawakumbusha watu umuhimu wa tabasamu la kimungu. Inasikitisha kwa mja kutojua ukweli huu. Mja anachohitaji kufanya ni kulitambua hili tabasamu la kimungu na kuwaonyesha viumbe wengine tabasamu hili usoni mwake.

Muumini akiishi kwa kutenda matendo mema, basi atakutana na tabasamu zuri katika kitanda chake cha mauti. Hili limeelezwa katika aya ifuatayo:

"Hakika waliosema: Mola wetu Mlezi ni Mwenyezi Mungu! Kisha wakanyooka sawa, hao huwateremkia Malaika wakawaambia: Msiogope, wala msihuzunike; nanyi furahini kwa Pepo mliyokuwa mkiahidiwa." (41: 30)

Tena aya nyingine inasema:

"Hakika marafiki wa Mwenyezi Mungu - hawatakuwa na hofu wala hawatahuzunika." (10; 62)

Nani anajua aina ya baraka watakazopata waumini wenye ukomavu, ambao wana uwezo wa kuonyesha tabasamu la Kimungu kwa viumbe katika Akhera!

Sheikh Sadi anasimulia kisa katika *Bostān* yake:

“Hapo zamani alikuwepo mtu mwenye tabia njema. Alikuwa akiwalipa mema wale wanaomtendea ubaya. Baada ya kifo chake, mtu mmoja alimuona ndotoni na kumuuliza:

“Niambie nini kilichotokea baada ya kifo chako.”

Marehemu alitabasamu na kuanza kuzungumza kama ndege mwenye kuimba:

“Sijawahi kumfanyia madhara mtu yeyote katika maisha yangu na kamwe sikuwahi kuukunja uso wangu. Daima nilitabasamu. Ndiyo maana ninatendewa vizuri hapa.”

Huwezi kuona marafiki wa Mwenyezi Mungu wakiwa na uso mkali. Kuangalia nyuso zao kufanya watu wajisikie amani na utulivu na kuwapeleka katika ulimwengu wa kiroho. Hawa marafiki wa Mwenyezi Mungu huzipeleka roho zenye kuomboleza katika nafsi zao na kupunguza huzuni zao. Roho zao ni kama vituo vya amani na matengenezo.

Hekima ya kweli ya utulivu huu ni kuwa, kwa sababu wao huwakumbusha watu juu ya Mwenyezi Mungu na Akhera, huwaokoa dhidi ya wasiwasi,tamaa, matamanio mengi ya nafsi na ulimwengu huu wa mpito. Huwaonyesha watu kwamba amani na utulivu wa kweli vinaweza kupatikana kwa kufanya juhudi katika kuitafuta furaha ya milele.

Aina nyingine ya hekima inayowafanya marafiki wa Mwenyezi Mungu kuwa na nyuso zenye tabasamu ni kazi yao ya kufikisha ujume wa Uislamu. Kwa sababu kuwa na uso wa tabasamu na kutumia maneno mazuri na laini wakati wa kufikisha ujumbe wa Uislamu na kuwaonya watu ni amri ya Mwenyezi Mungu. Tabasamu ni nyenzo ya mawasiliano ya kiroho baina ya watu. Hii ndio sababu kwamba hakuna mbinu nyingine bora na mujarabu ya kuwaonyesha watu njia iliyon-

yooka ya Uislamu zaidi ya uso wenye tabasamu. Jambo hili limeelezwa katika aya ifuatayo:

"Basi ni kwa sababu ya rehema itokayo kwa Mwenyezi Mungu ndiyo umekuwa laini kwao. Na lau ungelikuwa mkali, mwenye moyo mgumu, bila ya shaka wangelikukimbia. Basi wasamehe, na waombee maghfira, na shauriana nao katika mambo. Na ukishakata shauri basi mtegemee Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wanao mtegemea." (3: 159)

Kuhusu umuhimu wa kuwa na uso wenye tabasamu, kutumia maneno mazuri, na kuwa na adabu katika kufikisha ujumbe wa Uislamu, Sadi anasimulia kisa kifuatacho katika kitabu chake *Bostān*:

"Kulikuwa na kijana mmoja, mwenye uso wa kutabasamu na maneno ya kupendeza, mwenye kuuza asali. Kila mtu alimpenda na alikuwa na wateja wengi. Alipendwa sana kiasi kwamba hata kama angeuza sumu badala ya asali, watu wangeendelea kuinunua.

Mtu mmoja mwenye uso mkali akaingiwa na wivu wa biashara yake na akataka kuuza asali. Alichukua gari nzima ya asali na kuanza kutembea mjini. Alipiga kelele "asali, asali", lakini uso wake mkali ilikuwa kana kwamba anauza siki. Achilia mbali kuwauzia watu asali, hata nzi hawakutua juu ya asali yake.

Jioni ilipofika alirudi nyumbani. Hakuweza kupata sarafu hata moja. Alipata hasira na kuketi katika kona ya nyumba yake. Mke wake akamwambia kwa mzaha:

"Asali ya uso mkali itakuwa chungu."

Watu wenye tabia mbaya hujipeleka motoni, wakati wale wenye tabia njema hutoka peponi.

Rafiki yangu! Tembea na kama ikibidi, kunywa maji moto kutoka mtoni; usinywe asali baridi na tamu kutoka mikononi mwa mtu mwenye uso mkali chini ya jua linalochoma. Ni uchafu wa kiroho kula chakula kutoka mikononi mwa mtu mwenye uso mkali.

Usifanye mambo kuwa magumu kwa kuwa mkaidi; kwa sababu, watu wakaidi daima huteseka. Tuchukulie kuwa humiliki chochote; je, huna hata maneno matamu?"

Unaona? Uso wenye bashasha na maneno matamu ni mtaji mkubwa katika kuwaongoza kwenye njia ya haki watu walio masikini wa imani na tabia njema. Hata uso chukivu hutabasamu wakati wa kutembea katika bustani la mawaridi miongoni mwa maua yenye rangi kwa sababu ya maua hayo kuakisi uzuri katika roho yake. Watu wenye jukumu la kuwaongoza wengine wanatakiwa wawe na uwezo wa kuzilainisha nyoyo ngumu na kuzifanya nyuso chukivu zitabasamu.

Waumini wenye ukomavu ni watu wenye kutabasamu, kuvumilia na kustahimili katika kubeba mizigo ya machungu ya watu wengine. Ni muhimu kuwa na moyo uliolelewa kwa hekima ya Qur'an na Sunnah na uso unaoakisi na kuonyesha sura ya tabasamu la Uislamu. Katika huduma za mafunzo ya kiroho, tabasamu na kushukuru vinatakiwa kuwa sifa ya asili.

Ewe Mola wetu! Tufanye kuwa wenye huruma, wenye upendo, adabu na waumini wenye ukomavu. Zibariki nyoyo zetu upendo wa imani na nyuso zetu zifanye kuwa nyuso zenye tabasamu la Uislamu.

Amin...



ADABU NA TABIA NJEMA

Tabia njema ni zawadi muhimu ya mtu anayesafiri katika njia iliyonyooka. Mtu hawezi kuwa mwema na mgomvi kwa wakati mmoja.

Hatutakiwi kusahau kuwa Ibilisi hakufukuzwa mbele ya Mwenyezi Mungu kwa sababu ya kutokuwa na elimu au matendo bali kwa sababu ya tabia mbaya. Ndiyo maana kitu bora kinachomuangamiza Ibilisi ni tabia njema.

Lengo la malezi ya kiroho ni kuwafanya watu wafikie hali ya utambuzi na kuelewa kwamba wanatazamwa na kamera za Mwenyezi Mungu wakati wote; ili kwamba sifa bora kama vile adabu, uzuri, tabia njema na staha viweze kuwa tabia zao za asili.

ADABU NA TABIA NJEMA

Kitu kinachomfanya mwanadamu kuwa bora kuliko viumbe wengine ni tabia njema. Mwanadamu hupata heshima mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa adabu, jamala, tabia njema na staha. Ndiyo maana kuna daraja maalumu ya tabia njema na adabu katika nyoyo za marafiki wa Mwenyezi Mungu. Kiukweli Masufi wengi huuelezea Usufi kuwa ni "Tabia njema na adabu."

Shah Naqshaband, ambaye alipata mafunzo chini ya uongozi wa kiroho wa Amir Kulal, alijitoa wakfu kuwahudumia wagonjwa na vikongwe katika miaka ya mwanzo ya uhusiano wake na maisha ya Kisufi ili kuondosha kiburi chake na kuelewa maana ya kweli ya hali ya kutokuwa chochote. Anasimulia hali yake ya wakati huo kama ifuatavyo:

"Nilimtumikia mwalimu wangu kwa muda mrefu. Kiburi changu kilishuka mpaka kwenye kiwango ambacho nilipoona kiumbe yeyote wa Mwenyezi Mungu njiani nilianza kusimama na kusubiri apite.Sikuwa naweza kutembea nyuma ya kiumbe husika. Utumishi wangu uliendelea kwa kipindi cha miaka saba. Matokeo ya utumishi wangu nilifikia hali ya kiroho ambayo nilianza kusikia dua za wanyama wakimuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu."

Kwa roho zenye hekima, kila kitu katika ulimwengu ni ishara ya uwezo na nguvu za Mwenyezi Mungu. Ili kufikia daraja hii ya kiroho, roho ya mwanadamu inatakiwa kupata mafunzo na kutakaswa kupitia malezi ya kiroho.

Hapo itakuwa na uwezo wa kuona mandhari ya kiroho na kuzama katika hekima, kwa sababu siri nyingi zisizowazika zinaweza kutatuliwa kwa hekima. Siri za kiroho haziwezi kuwa dhahiri mpaka hekima ifikie kiwango cha ukomavu. Tabia njema ni nyenzo muhimu ya mtu anayesafiri katika njia iliyonyooka. Mtu hawezi kuwa mwema na mgomvi kwa wakati mmoja. Kama imani, msingi wa kiroho wa Uislamu ni *Tawhid* au kuamini kuwepo kwa Mungu mmoja, na, katika matendo, kuna tabia njema, unyoofu, na huruma.

Kwa hali hii, tunaweza kusema kuwa Uislamu unajumuisha utaratibu na vigezo vya uzuri, adabu, usafi au "tabia njema." Jalal al- Din Rumi anauelezea ukweli huu katika tungo zifuatazo:

"Fungua macho yako na utazame kwa umakini kwenye maneno ya Mwenyezi Mungu kuanzia mwanzo mpaka mwisho. Qur'an nzima, aya zake zote, ni maelezo ya tabia njema."

Marafiki wa Mwenyezi Mungu wamefikia daraja hizo za juu za kiroho kwa tabia njema. Imam Rabbani anasema kuwa:

"Hakuna anayeweza kupiga hatua kwenda kuungana na Mwenyezi Mungu Mtukufu bila kuzingatia vigezo vya tabia njema. Njia ya Masufi wakubwa inaundwa na tabia njema kuanzia mwanzo mpaka mwisho."

Tabia njema za hali ya juu ni zile zinazotekelezwa na kuchungwa mbele ya Mwenyezi Mungu.

KUWA NA TABIA NJEMA MBELE YA MWENYEZI MUNGU MTUKUFU

Hatutakiwi kusahau kuwa Ibilisi hakufukuzwa mbele ya Mwenyezi Mungu kwa sababu ya kutokuwa na elimu au matendo bali kwa sababu ya tabia mbaya. Ndiyo maana kitu kinachomchukiza zaidi Ibilisi ni tabia njema.

Rumi analielezea hali hii kwa uzuri kabisa:

"Ibilisi alipokataa kusujudu mbele ya Adam na kutotii amri ya Mwenyezi Mungu, alisema: "asili yangu ni moto, wakati asili yake ni udongo. Je ni sahihi kwa mtu aliyejuu kumsujudia aliye chini?"

Kwa sababu ya tabia hii ya kijuvi, shetani alilaaniwa na kufukuzwa mbele ya Mwenyezi Mungu. Mbali na majibu yake haya ya ukaidi, ibilisi alijaribu kubishana na Muumba wake." (Fihi Ma Fīh, uk. 159)

Abu 'Ali Al-Daqqāq (Mwenyezi Mungu airehemu nafsi yake) anasema kwamba:

"Kuacha tabia njema kunahitaji uwe umefukuzwa mbele ya Mwenyezi Mungu. Yeyote aonyeshaye utovu wa tabia mbele ya Sultan, atapelekwa mlangoni; na akionyesha utovu wa adabu hapo mlangoni, atapelekwa ghalani."

Watangulizi wetu walituusia kuchukua mafunzo kutoka kwenye hali na hatima za wale wenye tabia mbaya kwa kusema: "Jifunze tabia kutoka kwa wale wenye tabia mbaya." Tunatakiwa kutafakari kuhusu mwisho wa shetani na kujifunza kutokana na mwisho huo.

Mja anayeonyesha tabia sahihi mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu hujiepusha na kila aina ya matendo maovu, na

huyatambua makosa na kughafilika kwake katika kufanya ibada na kuamiliana na watu. Hujilinda dhidi ya maradhi ya kuyategemea matendo yake kupita kiasi.

Tusisahau kuwa matendo yetu hata yakiwa mazuri kiasi gani, ni kama kumwaga ndoo ya maji kwenye bahari. Kamwe hatupaswi kuiona ibada na utumishi wetu kuwa vyenye kutosha kuliko baraka za Mwenyezi Mungu Mtukufu. Tunapaswa kufanya ulinganisho wa matendo yetu na yale ya maswahaba wa Mtume ﷺ, siyo kuyalinganisha na yale ya watu wa kawaida katika jamii tunayoishi, kwa sababu Mwenyezi Mungu amewaweka *Ansar* na *Muhajiriin* kama mfano kwetu. Kwa upande mwingine, wale wenye tabia sahihi za utiifu wanatambua kuwa mema yote hutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, na aina zote za udhaifu zinatokana na wao wenyewe.

Maneno ya wale wanaoitelekeza ibada na kupotoka wanaposema *"nifanye nini? Haya ni majaliwa yangu"* ni kauli za ubinafsi na kughafilika kutokana na uovu. Mwenyezi Mungu Mtukufu hutoa hamasa ya kufanya ibada kwa wale walio na nia ya kufanya ibada, wakati akiweka vizuizi mbele ya wale wasiokuwa na nia ya kufanya ibada. Ndiyo maana kutafuta kisingizio cha kutofanya ibada na kulaumu majaaliwa ni ujinga wa wazi na utovu wa heshima kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Tukumbuke kuwa shetani aliteleza na kupotea kwa sababu ya utovu huo wa heshima. Ndiyo maana jambo linalomtatiza sana shetani ni kuwaona waumini wanaoonyesha heshima, utiifu, na utayari kwa mameno mengine wale wanaoonyesha tabia na adabu kamili ya utii.

Mojawapo katika malengo makubwa ya Usufi ni kulea watu katika hali ya *ihsan* au hali ya mtu kutambua kuwa wakati wote yuko mbele ya Mwenyezi Mungu, na hivyo kuonyesha

tabia njema mbele ya Mwenyezi Mungu. Masufi wanasema kuwa:

"Shikamana na tabia njema nje na ndani. Kwa sababu mtu akifanya kosa kwenye tabia zake za nje, hupata adhabu ya nje; wakati wale wanaotenda makosa kwenye tabia zao za ndani wataadhibiwa kwa adhabu ya ndani. Yule anayezipoteza tabia zake njema huwa amejiweka mbali na Mwenyezi Mungu, hata kama anadhani kuwa anajiweka karibu naye na hata kama anadhani kuwa anaridhiwa, kiukweli anakuwa amekataliwa." (Bursevī, Ismail Hakki, Ruhul Bayan, X, 401)

Kwa hiyo, badala ya kuyakataa vikali mambo ambayo Mola wetu ameyakadiria kwa ajili yetu, tunatakiwa kuyaridhia. Tuyakubali kuwa ni kwa manufaa yetu na aina hii ya kufikiri ni miongoni mwa tabia muhimu sana za kiroho.

Siku moja, mwanazuoni mmoja wa Hadith alimuona kijana mdogo aitwaye Bayazid al-Bistami akapendezwa na matendo yake. Ili kuipima akili na uelewa wa Bayazid alimuuliza:

"Ewe kijana! Unajua namna ya kutekeleza swala?"

Bayazid akajibu:

"Kwa idhini ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, ninajua." Mwanzuoni huyo akamuuliza tena:

"Inatekelezwa vipi?"

Bayazid akasema:

"Ninaanza kuomba kwa hisia kubwa nikisema "Mola wangu! Nimekuja mbele yako ili kutekeleza amri yako." Kisha nitasema اَللّٰهُ اَكْبَرُ "Mwenyezi Mungu ni Mkubwa"; nitasoma aya kutoka katika Qur'an; nitainama kwa unyenyekevu; kisha nita-

sujudu kwa staha; na mwishowe nitamaliza kwa kusema *"al-salaam alaykum wa-rahmatullah."*

Mtu huyo alishangazwa sana na kuuliza:

"Kwa nini unawaruhusu watu wakipapase kichwa chako wakati una uelewa na ufahamu mkubwa kiasi hicho?" Mwanazuoni huyo alikuwa akidhani kuwa mapenzi na mahaba makubwa ya watu yanaweza kumpa kiburi Bayazid na akataka kumuonya.

Bayazid akampa mwanazuoni huyo wa hadith jibu lifuatalo lenye busara:

"Hawakipapasi kichwa changu bali wanaupapasa uzuri ambao Mola wangu amenijaalia. Nitawazuiaje wasipapase kitu ambacho siyo milki yangu?"

Muumini anatakiwa afikie daraja kubwa ambayo anakubali kuwa mazuri na mema yote hutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, na asikinasibishe chochote na nafsi yake.

Namna bora kabisa ya kuonyesha tabia njema mbele ya Mwenyezi Mungu ni kumnyenyekea. Na ishara bora ya unyenyekevu inajionyesha katika ufanyaji wetu wa ibada. Marafiki wa Mwenyezi Mungu wanaeleza kuwa:

"Ibada humpeleka mja peponi; wakati unyenyekevu na adabu katika ibada humpeleka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu na kumfanya kuwa rafiki Yake."

Anas bin Malik anasema kuwa:

"Kuonyesha adabu katika matendo ni alama ya kukubalika kwa matendo hayo."

Khidhr عليه السلام anausia kuomba dua ifuatayo:

"Mola wangu! Nipe baraka ya adabu katika kukuabudu."

Kwa kuwa marafiki wa Mwenyezi Mungu huishi wakitambua kuwa wakati wote wapo mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, huwa waangalifu sana kwenye adabu na tabia zao za nje pamoja na zile za ndani. Hili linaweza kuonyeshwa kwa kudumisha hali ya unyenyekevu na heshima hata nje ya ibada. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema ndani ya Qur'an Tukufu kuhusu jambo hili kuwa:

"Ambao wanadumisha Sala zao." (70: 23)

"Na ambao wanazihifadhi Sala zao." (70: 34)

Jalal al-Din Rumi anazitafsiri aya hizi kama ifuatavyo:

"Mja hudumisha hali yake katika swala na pia baada ya kuwa nje ya swala. Hivyo, hutumia maisha yake yote katika unyenyekevu, heshima na adabu na tabia njema; na huchunga ulimi na moyo wake. Hii ndiyo hali ya marafiki wa kweli wa Mwenyezi Mungu Mtukufu..."

Malengo ya mafunzo ya kiroho ni kuwafanya watu wafahamu na kuelewa kuwa wakati wote wanatazamwa na kamera za Mungu; ili kwamba tabia na sifa nzuri kama vile adabu, uzuri, tabia njema, na staha vipate kuwa tabia zao za kimaumbile.

Dawud al-Tai anasimulia kuwa:

"Nilikuwa pamoja na Abu Hanifah kwa miaka ishirini. Katika kipindi cha miaka yote hiyo, nilimuangalia kwa umakini na sikuwahi kumuona akiwa kichwa wazi iwe anapokuwa pekee yake wala anapokuwa pamoja na watu. Sikuwahi kumuona akiwa amenyoosha miguu yake hata anapokuwa amepumzika. Nikamuuliza:

"Kuna ubaya gani kunyoosha miguu yako ukiwa peke yako?" akasema: "Ni bora kuonyesha adabu yako unapokuwa mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu."

"Mahmud Sami Ramazanoglu hakuwahi kuonekana akiwa amenyoosha miguu yake au akila huku ameegemea kitu. Alikuwa akiwasomea tungo zifuatazo watu walio karibu naye:

"Adabu na tabia njema ni taji lililotengenezwa kwa nuru ya Mola

Vaa taji lake na usalimike dhidi ya taabu zote."

Watu hawawezi kutenda kwa uhuru wanapokuwa mbele ya mtawala au mtu mwenye daraja ya juu, kama wanavyofanya katika maeneo na nyakati nyingine. Marafiki wa Mwenyezi Mungu ni wale wanaotambua kuwa muda wote wapo mbele ya Mwenyezi Mungu na kuikubali hali hii bila ushahidi wowote. Kwa maneno mengine wanaishi wakifahamu maana ya aya ifuatayo:

وَهُوَ مَعَكُم اَيْنَ مَا كُنْتُمْ

"... Naye yu pamoja nanyi popote mlipo ..." (57; 4) Hii ni kwa sababu tabia njema hujumuisha nyanja zote za maisha yao.

Marafiki wa Mwenyezi Mungu wapo makini juu ya tabia zao hata wanapokuwa mbali na macho ya watu. Kwa mfano, marafiki wa Mwenyezi Mungu huwa waangalifu kuhusu uvaaji wa kofia wakati wote, ambazo huvaliwa kama alama ya heshima wakati wa ibada ya swala. Swahaba mmoja alipomuuliza Mtume ﷺ kama anaruhusiwa kuvaa chochote anapokuwa pekee yake, Mtume ﷺ akamwambia:

"Mwenyezi Mungu ndiye anayestahiki zaidi kuonewa haya kuliko watu." (Abu Dawud, Hammām, 2 / 4017)

Watangulizi wetu, ambao walilelewa kwa tabia na adabu za Kiislamu, walionyesha mfano bora wa tabia, unyenyekevu

na heshima. Salomon Schweigger, ambaye alikuwa kasisi wa Kiprotestanti, anaandika mistari ifuatayo katika kitabu chake cha safari kuhusu Waislamu:

"Waislamu hujisitiri hata wanapokuwa bafuni. Heshima iliyoje ya watu hawa! Tunapaswa kujifunza tabia njema na staha kutoka kwao, hao tunaodai kuwa ni makatili." [33]

Kujisitiri ni sifa na tabia ya binadamu. Hakuna jambo hilo kwa viumbe wengine. Kujistiri pia ni tabia ya asili ya waja wenye utii. Kwa hakika Adam na Hawa عليهما السلام walijisikia aibu na kutafuta kitu cha kujisitiri walipokuwa peponi, japokuwa walikuwa peke yao. Kwa hivyo, kujisitiri na kujifunika ni tabia za asili za binadamu.

Kuwa na heshima mbele ya Mwenyezi Mungu pia huwajumuisha viumbe wengine kulingana na ukaribu wao kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Heshima ya pili kwa umuhimu mkubwa inatakiwa kuonyeshwa mbele ya Mtume wa mwenyezi Mungu ﷺ.

KUWA NA ADABU MBELE YA MTUME WA MWENYEZI MUNGU ﷺ

Maswahaba walionyesha mifano bora ya tabia na adabu kwa Mtume ﷺ. Walielezea hali ya heshima yao kama ifuatavyo:

"Tulikaa chini mbele ya Mtume ﷺ kwa utulivu sana kana kwamba juu ya vichwa vyetu kuna ndege na kama tungetikisika wangeruka." [34]

33. Ortayli, Ilber, Osmanliyi, Yeniden Kesfetmek, 88.
34. Tazama Abu Dawud, Sunnah, 23 – 24/4753; Ibn Majah, Janaiz, 37.

Heshima ya Maswahaba kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ ilikuwa kubwa sana kiasi kwamba mara nyingi hawakuweza hata kumuuliza maswali kwa kudhani kuwa kufanya hivyo ni ukaidi. Kutokana na hali hiyo, walitamani bedui kutoka jangwani aje kumuuliza Mtume ﷺ maswali yaliyokuwa akilini mwao, ili waweze kufaidika na majibu yake.

Mbali na heshima yao hiyo, walikuwepo maswahaba wachache sana ambao waliweza kuutazama uso wa Mtume ﷺ. Imesimuliwa kuwa miongoni mwa maswahaba ni Omar na Abu Bakr ﷺ ndiyo walioweza kuutazama uso wa Mtume ﷺ wakati akitoa khutba. (Tirmidhi, Manāqib, 16/3668)

'Amr b. 'As, aliyeifungua Misri, anaelezea hii kama ifuatavyo:

"Na japokuwa hakuna niliyekuwa nikimpenda kama Mtume wa Mwenyezi Mungu na hakuna aliyekuwa muhimu katika macho yangu kuliko yeye, kamwe sikuwa na ujasiri wa kumtazama kikamilifu usoni mwake kwa sababu ya nuru yake. Hivyo, kama nikiombwa kuzielezea sifa zake, siwezi kufanya hivyo kwa maana sikumtazama kikamilifu." (Muslim, Kitab Al-Iman, 192)

Tunapothubutu kumuelezea Mtume ﷺ kwa uelewa wetu mdogo, tunamuomba msamaha Mwenyezi Mungu kwa makosa yetu yasiyokuwa ya makusudi pindi tunapomuelezea Mtume wake.

Kwa upande mwingine, kumtolea salamu na kumsifu Mtume ﷺ, pindi jina lake linapotajwa, ni miongoni mwa amri za Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa umma wa Kiislamu. Aya ifuatayo inasema;

"Hakika Mwenyezi Mungu na Malaika wake wanamsalia Nabii. Enyi mlio amini! Msalieni na mumsalimu kwa salamu." (33: 56)

Ni ajabu kuona kuwa wakati mitume wote ﷺ wametajwa kwa majina yao ndani ya Qur'an Tukufu, lakini Qur'an haimuiti Mtume ﷺ kwa "Ewe Muhammad!" bali "Ewe Nabii! Au Ewe Mtume wa Allah!". Mwenyezi Mungu Mtukufu anawataka wa-umini wote wafuate tabia hii katika maisha yao:

"Msifanye wito wa Mtume baina yenu kama wito wa nyinyi kwa nyinyi..." (24: 63)

Ibn 'Abbas ﷺ anasema kuhusu aya hii kwamba:

"Watu walikuwa wakimuita Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ kwa kusema "Ee Muhammad! Au Ee Abu al-Qasim!" Mwenyezi Mungu Mtukufu akawakataza kumuita hivyo. Baada ya hapo walianza kumuita "Ee Mtume wa Mwenyezi Mungu! Au Ee Nabii wa Mwenyezi Mungu!" (Abu Nuaym, Dalāil, I, 46)

Kwa hivyo, kama wafuasi wake, kulitaja tu jina la Mtume wetu ni kwenda kinyume na adabu na tabia sahihi. Sambamba na jina lake, tunatakiwa pia kutaja sifa zake tukufu. Vilevile tunatakiwa kukiheshimu kila kilicho karibu na Mtume ﷺ.

Hali ya Sultan wa Kiuthmaniya Yavuz Selim, ambaye alikuwa akimpenda Mtume ﷺ, ni mfano mwema kwetu. Aliifungua Misri mwaka 1517 na kuchukua ofisi ya Ukhalifa. Siku ya Ijumaa ya tarehe 20 Februari, pindi khatibu wa msikiti wa Malik Muayyad alipomuita ***"Hakim al-Haramayn al-sharifayn"*** yaani, mtawala wa miji miwili mitukufu ya Makkah na Madina, alimkatisha khatibu na kumwambia huku akitokwa na machozi:

"Hapana, hapana! Mimi siyo mtawala wa maeneo haya matukufu. Kinyume chake, mimi ni "*Khadimul Haramayn al-Sharifayn* au mtumishi wa miji miwili mitukufu ya Makkah na Madina."

Kisha akaliondoa zulia na kusujudu juu ya ardhi kumshukuru Mola wake. Na kuanzia siku hiyo aliweka juu ya kilemba

chake nyoya katika sura ya ufagio kama ishara ya utumwa wake.

Mfano mwingine mkubwa wa heshima ulionyeshwa na Sultan wa Kiuthmaniya aliyedhulumiwa na kuuawa kishahidi, Abdulaziz Khan. Siku moja alipokuwa mgonjwa kitandani mwake, aliambiwa kuwa: "Kuna ujumbe wake kutoka Madina."

Aliwaambia wasaidizi wake:

"Nisaidieni nisimame mara moja. Nataka kuyasikiliza maombi kutoka katika miji hii mitukufu nikiwa nimesimama. Ni utovu wa heshima kusikiliza maombi ya majirani wa Mtume ukiwa umelala."

Kisha kila alipopata barua kutoka Madina alikuwa akifanya udhu na kuzibusu kwa sababu kulikuwa na vumbi la Madina kwenye barua hizo na kisha humpa karani wake mkuu ili azifungue na kuzisoma.

KUWA NA ADABU MBELE YA MARAFIKI WA MWENYEZI MUNGU

Baada ya kuifafanua aya isemayo "**"Msifanye wito wa Mtume baina yenu kama wito wa nyinyi kwa nyinyi..."** (24: 63), Abu Lays (Mwenyezi Mungu amrehemu) alisema:

"Sisi pia tunaelewa kuwa kutokana na aya hii kwamba tunapaswa kuonyesha heshima kwa walimu. Imeelezwa kuwa haki za walimu na watu wema zinapaswa kuchungwa. Hii ndiyo sababu kwamba pindi majina yao yanapotajwa, bila kujali lugha, tunatakiwa pia kusema kitu kuonyesha heshima yetu kwao. Kwa kuwa imeharamishwa kuwaita baba zetu wa

kibaolojia kwa majina yao, itakuwaje kuhusu kuwataja baba zetu wa kiroho kwa majina yao". (Ruh al-Bayan, VII, 447)

Kwa maneno mengine, mojawapo ya ishara muhimu zaidi za heshima yetu kwa Mtume ﷺ ni kuonyesha heshima kwa marafiki wa Mwenyezi Mungu, wana hekima na wana-maarifa, ambao ni warithi wa Mtume ﷺ. Ili kupanda kiroho, tunahitaji kujielekeza kwenye muongozo wa marafiki (mawalii) wa Mwenyezi Mungu kwa heshima, kuwasikiliza na kufanya kila tuwezalo kufuata ushauri na wosia wao katika maisha yetu. Tunapaswa kukubali kuwa pamoja nao kama baraka. Kwa sababu wale wanaokuja mbele yao kwa heshima huondoka na baraka.

Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ anasema:

"Kuweni makini na busara ya muumini; kwa sababu hutazama kwa nuru ya Mwenyezi Mungu." (Tirmidhi, Tafsir, 15)

Onyo la "kuwa makini" katika maneno ya Mtume ﷺ aliyetajwa hapo juu linamaanisha kuwa "usiende mbele ya waumini waliokamilika ukiwa na ajenda za siri na nyoyo chafu." Ndiyo maana kuna maneno yasemayo "tazama unachosema mbele ya mwanachuoni, na tazama kile ulichonacho moyoni mwako mbele ya rafiki (walii) wa Mwenyezi Mungu."

Kwa hiyo, tunahitaji kuwa makini zaidi kuhusu tabia na adabu zetu kwa marafiki wa Mwenyezi Mungu. Kuzungumza, kukaa na kusimama mbele yao bila idhini yao, na kuwa na ukaidi kwao wote hupunguza faida yoyote ya kiroho na kuchochea adhabu ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Pindi Sultan wa Kiuthmaniya, Yavuz Selim Khan alipoingia mbele ya marafiki wa Mwenyezi Mungu, asingezungumza isipokuwa pindi inapobidi. Kwa kweli wakati alipomtembelea Muhammad Badahshī katika mji wa Dameski, hakuzungum-

za, alisikiliza tu kisha akaondoka. Vigogo waliokuwa pamoja naye walishtushwa na kumuuliza:

"Ewe Sultan wetu! Ulisikiliza tu. Kwa nini hukusema neno lolote?"Yavuz Selim Khan akajibu:

"Si sahihi kwa mtu yeyote, hata kwa Sultan, kuzungumza mbele ya Walii wa Mwenyezi Mungu. Hata kama sisi ni Masultani wa dunia hii, daima tunahitaji msaada wa Masultani wa ulimwengu wa kiroho. Kama ningehitajika kuzungumza, wangejua na wangeniruhusu nizungumze."

Hii ndiyo iliyokuwa adabu na tabia ya Yavuz Selim Khan kwa marafiki wa Mwenyezi Mungu.

Siyo masultani tu, bali pia watu wa kawaida walikuwa makini kuhusu tabia zao mbele ya marafiki wa Mwenyezi Mungu. Katika siku za mwisho wa Dola ya Uthmaniya, majemadari ambao walikuwa wameizunguka Bosporus walikuwa wakiwakaribisha abiria wao kuja kuwaombea dua Aziz Mahmud Hudāyī na Yahya Efendī walipokuwa wakipita karibu na makaburi yao.

Kwa muhtasari, tabia njema ni kitu muhimu sana katika Uislamu. Kuwa na hisia kuhusu tabia na adabu zetu huanza kwa kuwa wanyenyekevu mbele ya Mwenyezi Mungu, na kumheshimu Mtume wake ﷺ na Mawalii wake; na huendelea kuwa na heshima kwa wazazi, kwa waumini na viumbe wengine wote.

Mali ya kimaada inaweza kupotea lakini utajiri wa tabia njema daima hubaki pamoja nasi. Kwa hiyo waumini wanatakiwa kujifunza kanuni za tabia njema na kujitahidi kuzichunga. Wanatakiwa kuwa mfano wa kuigwa na wanadamu kwa kuzifanyia kazi kanuni hizo katika maisha yao. Ili kufikia lengo hili, tunahitaji kusoma na kujifunza vitabu kuhusu kanuni za

tabia njema; lililo muhimu zaidi, tunatakiwa kuwa karibu na Waumini wema wenye adabu na tabia njema.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu atubariki sisi wote maadili ya hali ya juu ya Mtume ﷺ. Atubariki kuwa miongoni mwa waumini wenye adabu, wazuri, na wenye heshima ambao hunufaika na ulimwengu wa kiroho wa marafiki na mawalii wa Mwenyezi Mungu.

Amin...



ADABU ZA KUONGEA KWA MUJIBU WA QUR'AN TUKUFU

Qur'an Tukufu ambayo ina njia madhubuti mno za kujieleza, inatutaka kuiga mfano wake kadiri iwezekanavyo. Ili kueleza madhumuni yetu kwa njia bora zaidi, ulaini na ufasaha wa lugha ni sharti kwa mzungumzaji yeyote; kwa sababu uzuri, umaridadi, na wema katika Uislamu vinatakiwa kuwasilishwa kwa maneno bora zaidi.

Hekima na siri za Qur'an Tukufu zina kina kirefu sana mfano wa bahari. Hata hivyo kila mtu anafaidika nazo kwa kadiri anavyoruhusiwa na vipawa vya moyo wake. Kama moyo wa mtu ni mdogo kama tondoo ya mshonaji, fungu lake katika bahari hii isiyokuwa na kikomo halitokuwa pana wala kubwa kuliko ukubwa wa moyo wake.

ADABU ZA KUONGEA KWA MUJIBU WA QUR'AN TUKUFU

Imani ni mtu kujifunga kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa dhati na kwa upendo. Rasilimali muhimu sana ya muumini katika njia yake ya kuelekea kwenye kuungana na Mwenyezi Mungu Mtukufu ni upendo wake. Hata hivyo, upendo pekee unaotamkwa bila kufika kwenye moyo hautoshi. Kiwango kamili cha upendo kinaweza kufikiwa kwa kudumisha tabia njema.

Tabia njema ni kama manukato mazuri ya waridi, ambayo huuburudisha moyo. Manukato haya yanatakiwa kupenya ndani ya kina cha moyo wa muumini na kufika katika kila kipengele cha maisha yake. Tabia njema zinapoutawala ubora wa mwenendo wa mtu, hali hiyo pia huashiria kuwa amefikia ukamilifu wa imani.

Jalal al-Din al-Rumi anasema;

"Akili yangu iliuuliza moyo wangu: imani ni kitu gani? Na moyo wangu ukaliinamia sikio la akili yangu na kusema; imani ni tabia njema."

Kwa hiyo, tabia na matendo yote ya marafiki wa Mwenyezi Mungu yanafundisha uzuri na tabia njema. Mola wetu pia anatuita kwenye tabia za utii kwa mujibu wa kanuni zilizoelezwa ndani ya Qur'an Tukufu.

"Kuzungumza" huwa mwanzo wa orodha ya mambo yanayotakiwa kupambwa na adabu na tabia njema. Kuzungumza kama kioo kilichong'arishwa, ambacho huakisi na kuonyesha hali ya moyo na akili ya mtu; na kiwango cha imani na maadili yake. Kama methali maarufu isemavyo: "Mtu amejificha chini ya ulimi wake." Hivyo, mazungumzo ya mtu maridadi na mwenye moyo safi yatakuwa maridadi na masafi. Ufuatao ni mfano bora wa hili:

Siku moja Qubaas bin Ushaym ﷺ alisema:

"Mimi na Mtume ﷺ tulizaliwa katika mwaka wa tembo."

'Uthman bin. Affan ﷺ akamwambia:

"Nani kati yenu mkubwa (katika umri), wewe au Mtume ﷺ". Akatoa jibu la mfano lifuatalo:

"Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ ni mkubwa sana kuliko mimi. Mimi nilifika mapema tu kufika katika dunia hii ... " (Tirmidhi, Manāqib, 2 / 3619).

Huu ni mfano wa uzuri wa kiroho wa kizazi cha maswahaba uliojionyesha katika mazungumzo yao. Tunapaswa kufikiria kuhusu aina ya malezi na mafunzo yaliyowafanya kutumia lugha hiyo nzuri, ya adabu na yenye kupendeza.

Viumbe wote katika ulimwengu huu huyakumbuka na kuyataja majina ya Mwenyezi Mungu kulingana na namna yao maalumu ya uzungumzaji. Mwanadamu amejaaliwa njia na namna bora ya kuzungumza. Jambo hili limeelezwa ndani ya Qur'an Tukufu kama ifuatavyo:

"Arrah'man, Mwingi wa Rehema, Amefundisha Qur'an. Amemuumba mwanadamu, akamfundisha kubaini (au mfumo wa kujieleza). " (55; 1-4)

Kuna pointi nzuri sana na yenye busara katika maneno hayo ya Mwenyezi Mungu. Tunapaswa kutafakari kwa nini Mwenyezi Mungu alitufundisha Qur'an na haki baadaye akatujaalia uwezo wa kujieleza.

Kwanza kabisa, Mola wetu anawataka waja wake wawe na mfumo wa kujieleza uliowekwa kwa misingi ya Qur'an Tukufu. Ndiyo maana mafunzo ya Qur'an huwa ya kwanza kabisa. Kwa upande mwingine, mojawapo ya tabia na sifa kubwa za Qur'an ni ufasaha na balagha yake, au mtindo wa fasihi yake ya kipekee. Wakati kazi za kifasihi zilizoandikwa na wanadamu huwachosha wasomaji baada ya kurudia rudia, lakini jinsi unavyozidi kuisoma Qur'an ndivyo unavyozidi kupata raha kwa kuisoma.

Qur'an Tukufu inasema:

"Mwenyezi Mungu ameteremsha hadithi nzuri kabisa, Kitabu chenye kufanana na kukaririwa; husisimua kwacho ngozi za wenye kumhofu Mola wao Mlezi. Kisha ngozi zao na nyoyo zao hulainika kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu..." (39: 23)

Historia inaeleza kuwa washairi wa Kiarabu, ambao walipata zawadi kubwa kwenye maonyesho ya fasihi ya Peninsula ya Arabia, waliposikia mtindo wa kipekee wa kibalagha na kifasaha wa Qur'an Tukufu, waliyaondoa mashairi yao waliyokuwa wameyaweka kwenye kuta za Kaaba.

Kwa hiyo, Waislamu ambao ndiyo wanaohutubiwa na maneno ya kimiujiza ya Qur'an Tukufu wanatakiwa kufanya juhudi ya kujipamba kwa kanuni zake za kimaadili na kujaribu kuuelewa uzuri wake wa kibalagha. Kwa maneno mengine, Qur'an, ambayo huakisi mtindo madhubuti wa kujieleza, inatutaka tutumie lugha hiyo nzuri na ya dhahiri. Ili kuelezea

madhumuni yetu kwa njia safi, mazungumzo mazuri na fasaha ni sharti kwa mzungumzaji yeyote; kwa sababu, uzuri, umaridadi na wema wa Uislamu unatakiwa kuwasilishwa kupitia maneno yetu safi.

KUWA NA MAZOEA YA KUTUMIA LUGHA YA HURUMA YA QUR'AN TUKUFU

Hekima na siri za Qur'an ni zenye kina kama bahari. Hata hivyo, kila mtu hufaidka nayo kwa kadiri moyo wake unavyoruhusu kufanya hivyo. Kama moyo wa mtu ni mdogo kama tondoo ya mshonaji, fungu lake kutoka katika bahari hiyo isiyokuwa na mwisho litakuwa sawa na moyo wake. Waislamu wote, wa hali ya juu na wa hali ya chini, hukaa kwenye dawati moja la kusomea na kuisoma Qur'an; hata hivyo kila mtu hunufaika nayo kwa kadiri moyo wake unavyomruhusu. Maana za Qur'an hujiweka wazi kulingana na kiwango cha ukaribu wa mja kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Kwa hiyo, tunapaswa kujiuliza kama manufaa na udadisi wetu kwenye Qur'an, ambayo kwa namna moja ni ujumbe kutoka kwa Mola kuja kwetu, ni zaidi ya ujumbe unaotumwa na wanadamu. Ni kwa kiwango gani tunafanya juhudi kuielewa hekima yake? Kwa mfano, je huwa tunakwenda kuwauliza wanaojua pindi tunapokuwa hatuelewi kitu ndani ya maneno hayo? Kwa muhtasari, je tunaipa umuhimu vya kutosha?

Tunaweza kuielewa lugha ya huruma ya Qur'an tukufu pale tutakapotoa majibu ya kuridhisha kwa maswali yaliyotajwa hapo juu.

Hebu tutafakari juu ya kiasi cha muda na juhudi tunazozitumia kujifunza lugha fulani ya kigeni. Hasa katika zama hizi,

tunaishi katika ulimwengu wa utandawazi. Ndiyo maana tunakwenda kwenye kozi za lugha, tunatumia kiasi kikubwa cha pesa na muda kujifunza lugha moja ya kigeni. Tunafikia hata kwenda na kuishi pamoja na wazungumzaji asilia wa lugha hiyo. Hii imekuwa ni sekta kubwa ya biashara katika siku za hivi karibuni.

Naam, kujifunza lugha nyingine ni jambo maridhawa, lakini Muumba wa lugha zote hizi anatutaka kwanza tujifunze "lugha ya Qur'an." Siyo kujifunza tu Kiarabu, bali kujifunza jinsi ya kuielewa lugha ya Qur'an ya huruma. Na njia ya kuielewa Qur'an hupitia kwenye kuyadhibiti maongezi yetu kupitia maonyo ambayo Qur'an Tukufu imetuwekea, na kuyapendezesha kupitia mafundisho kutoka kwa Mwenyezi Mungu.

Matatizo makubwa katika uhusiano wetu na watu wengine kwa kawaida hutokana na uelewa mbaya na matumizi mabaya ya lugha; kwa sababu lugha yaweza kuwa ufunguo wa kheri na shari. Ndiyo maana tunatakiwa kuwa waangalifu sana tusizibadilishe ndimi zetu kuwa miiba inayozichoma nyoyo za wengine. Imeelezwa katika mithali moja kwamba "Majeraha ya upanga hupona, lakini hisia zilizojeruhiwa kwa maneno makali haziponi."

Hivyo, tunatakiwa kufikiri mara mbili na kutaamali matokeo ya maneno yetu kabla ya kuanza kusema. Kwa sababu kuzungumza ni kama kutupa jiwe. Tuwe waangalifu kuhusu mahali ambapo jiwe hilo litatua.

Mtukufu Mtume ﷺ anaashiria jambo hili na kusema kuwa;

"usiseme kitu ambacho utatakiwa kuomba msamaha..." (Ibn Majah, Zuhd, 15)

Kuzungumza ni kama kutupa mishale, mshale unatoka kwenye upinde haiwezekani kurudi, vivyo hivyo, maneno ha-

yawezi kurudi pindi yanapotamkwa. Daima tunaweza kuzungumza maneno ambayo hatujayazungumza, lakini hatuweza kuyarudisha maneno ambayo yameshazungumzwa na tunayolazimika kuyazuia.

Waumini wenye ukomavu hutafakari kwanza kama maneno yao yatakuwa na faida, hivyo wakiona kama maneno yao yatawasababishia matatizo wao wenyewe au wanayemzungumzia, hupendelea kukaa kimya. Vile vile ni waangalifu kuhusu maneno watakayosema na jinsi watakavyoyasema.

Abu Bakr ﷺ anatuonya kuhusu jambo hili:

"Fikiri vyema kuhusu utakachosema, yule utakayemzungumzia na wakati utakaozungumza..."

Muumini anatakiwa kuwa na werevu na kuyarekebisha maneno yake kulingana na yule anayezungumza naye; kwa sababu maneno ambayo ni mazuri kwa baadhi ya watu yanaweza kuwaumiza wengine. Ndiyo maana kwanza hali ya kisaikolojia ya msikilizaji inapaswa kuangaliwa kabla ya kusema chochote. Hatua mbili tatu mbele zinatakiwa kutaamuliwa. Watu huwaamini na kuwapa umuhimu waumini wakomavu na wenye uelewa.

Ndiyo maana Mtume ﷺ alikuwa akiwaambia watu mambo yatakayowavutia na kuzungumza nao kwa kadri ya kiwango cha uelewa wao. Alikuwa hatumii lugha moja kwa bedui na kwa sahaba mwenye ujuzi. Alikuwa akiwaambia mabedui mambo mepesi ambapo angewaambia maswahaba wakomavu mambo ya kina ya kiroho.

Siku moja Omar ﷺ alishuhudia mazungumzo baina ya Mtume ﷺ na Abu Bakr ﷺ, japokuwa alikuwa miongoni mwa maswahaba wenye elimu na maarifa makubwa, alilazimika kukiri kuwa:

"Nilikuwa kama mtu asiyejua Kiarabu. Sikuelewa hata neno moja katika mazungumzo yao."

Hii ndiyo sababu kwamba Mtume ﷺ alimuonya Ibn Abbas ؓ akisema:

"Ewe Ibn Abbas! Usizungumze na watu kwa lugha wasiyoweza kuielewa; kwa sababu ukifanya hivyo, inaweza kuwapeleka kwenye uharibifu." (Daylamī, V, 359).

Rumi anashauri katika suala hili kwamba:

"Usiuze vioo katika soko la vipofu; na usighani katika soko la viziwi."

Siku moja Mtume ﷺ alikuwa juu ya ngamia wake na maswahaba wakitembea mbele yake. Mu'adh bin Jabal ؓ akamuuliza:

"Ewe Mtume wa Allah! Je utajali nikija karibu nawe?"

Mtume ﷺ alipomruhusu kumsogelea, Mu'adh akamuuliza tena:

"Ewe Mtume wa Allah! Wazazi wangu watolewe fidia kwa ajili yako. Raghba yangu kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu ni ayachukue maisha yetu kabla yako. Lakini kama Mwenyezi Mungu akiyachukua maisha yako kabla yetu, ni aina gani ya ibada unatushauri tuifanye baada yako?"

Mtume ﷺ hakujibu swali hili. Mu'adh akauliza tena:

"Je ni kupigana katika njia ya Mwenyezi Mungu?"

Mtume ﷺ akasema:

"Kupigana kwa ajili ya Mwenyezi Mungu ni jambo zuri kulifanya, lakini kuna matendo bora ya kufanya."

Mu'adh akauliza kuwa:

"Unamaanisha kufunga na kutoa sadaka?"

"Kufunga na kutoa sadaka ni matendo mazuri pia."

Mu'adh akahesabu matendo yote mema aliyoyafikiria, na kila mara Mtume ﷺ alikuwa akisema:

"Kuna matendo bora zaidi ya kufanya." Hatimaye Mu'adh alipouliza:

"Baba na mama yangu wawe fidia kwa ajili yako. Niambie, ewe Mtume wa Allah, ni lipi tendo bora?". Mtume ﷺ akaashiria kwenye mdomo wake na kusema:

"Kukaa kimya kama hautozungumza kitu kizuri."

Mu'adh akauliza:

"Je tutaulizwa kwa kile tulichozungumza?"

Mtume ﷺ akaligusa goti la Mu'adh na kumwambia;

"Allah akulipe mema ewe Mu'adh! Kitu gani baki kitakachowasukuma wanadamu motoni? Yule anayemuamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho azungumze maneno mazuri au akae kimya! Zungumza mema upate thawabu; pata amani na utulivu kwa kutozungumza maneno yenye kuumiza." (Hakim, IV, 319 / 7774).

Basi muumini kamwe hatakiwi kusahau kwamba maneno yake daima yanahifadhiwa na kamera za Mwenyezi Mungu. Qur'an Tukufu inasema:

"Hatamki neno ila karibu yake yupo mwangalizi tayari." (50; 18)

Hata kama tusipoulizwa kwa maneno yetu hapa duniani, hakika tutaulizwa huko Akhera. Ndiyo maana tunatakiwa kuwa waangalifu juu ya maneno yetu kama tunavyokuwa

waangalifu kuhusu kile tunachokula. Yawezekana kwa sababu ya jambo hili ndio maana Qur'an Tukufu ikatoa umuhimu mkubwa kwenye maadili ya kuzungumza, kwa maneno mengine, jinsi ya kuzungumza na kutozungumza.

QUR'AN INATAKA TUTUMIE LUGHA YA AINA GANI?

Awali ya yote, Qur'an inatulingania kwenye matumizi ya lugha fasaha na sahihi. Inawaamrisha watu kusema *"Qawl-i Hasan"* [35] au maneno mazuri.

Vile vile inatuamrisha kutotamka neno lolote la kuwadharau wazazi wetu na badala yake tusema قَوْلاً كَريماً *(qawlan Karima)* [36] kwa maneno mengine inatutaka tuwaambie maneno mema na mema, *qalan*, kilugha ina maana ya maneno, na *karima*, ina maana ya mazuri na mema.

Qur'an inatuamrisha kuwa, iwapo hatuna chochote cha kuwapa masikini, basi tuzungumze nao kwa قَوْلاً مَيْسُوراً *(qawlan maysura)* [37], au maneno yenye kutia faraja, laini na yenye kuwaridhisha.

Inatukumbusha kuwa maneno mema قَوْلٌ معْرُوفٌ *(qawlun ma'rufun)*[38] pamoja na kusamehe ni bora kuliko kutoa sadaka kuwapa maskini huku ikifuatiwa na maneno yanayochoma na kuziumiza hisia zao.

35. Qur'an 2: 83, Qur'an 17: 53
36. Qur'an 17: 23
37. Qur'an 17: 28
38. Qur'an 2: 263

Qur'an inatuambia tutumie maneno mema na mazuri قَوْلاً مَعْرُوفاً *(qawlan ma'rufa)*[39] kwa mayatima, masikini na jamaa wa karibu.

Kisha inatuambia tutumie maneno kauli sahihi, njema na ya kheri قَوْلاً مَعْرُوفاً *(qwalan ma'rufa)*[40] tunapozungumza na wale wenye maradhi ya kiroho katika nyoyo zao, ili kuzuia hali ya uelewa mbaya, uovu au ubaya.

Ili kuzilainisha nyoyo za madhalimu, Qur'an imetuamrisha kuzungumza nao kwa kutumia maneno laini قَوْلاً لَيِّناً *(qawlan layyina)* [41]. Inatukumbusha kuwa maneno makali na ya ukaidi huacha athari hasi kwa yule anayeambiwa. Ndiyo maana imetuusia kutumia lugha laini na ya upendo, isiyochochea chuki.

Sehemu nyingine, katika kufikisha ujumbe wa Uislamu, Qur'an Tukufu inatuambia tutumie *(qawlan baligha)* au maneno ya wazi, bayana na yenye kuleta athari, ambayo yataziathiri nyoyo za wale tunaozungumza nao. Ili kulifikia hili, kauli zetu zinatakiwa zitoke ndani ya vina vya nyoyo zetu; vinginevyo, maneno yanayotoka kwenye ndimi zetu pekee yatapita kwenye sikio moja na kutokezea kwenye sikio la pili. Qur'an Tukufu inatuonya kwamba muda wa kudumu maneno na kauli hizi utakuwa mfupi sana. Kuchagua maneno yetu kutoka ndani ya yale yenye athari badala ya yale ya kawaida ni amri nyingine kutoka kwa Mwenyezi Mungu juu yetu. Kuhusu suala hili, Qur'an Tukufu inasema kuwa:

"Waite waelekee kwenye Njia ya Mola wako Mlezi kwa hikima na mawaidha mema, na ujadiliane nao kwa namna iliyo bora..." (16: 125)

39. Qur'an 4: 5, 8
40. Qur'an 33:32
41. Qur'an 20: 44

Roho zinapenda sana hekima. Hekima ni chakula cha roho. Sayyidna Ali ﷺ anasema:

"Ipumzishe roho yako kwa maneno ya hekima na yenye kuburudisha na mwenendo mwema; kwa sababu kama ulivyo mwili wako, roho yako nayo huchoka."

Kwa maneno mengine, ulimi wa muumini unapaswa kuwa mto wa hekima ambao hutoa uzuri wa kiroho wa mambo ya kweli kutoka kwa Mwenyezi Mungu.

Kwa mara nyingine, Qur'an inatuamrisha kuwa wakweli na wanyoofu, na tuzungumze kwa قَوْلاً سَديداً *(qawlan sadida)*[42] au ukweli ikiwa tunataka kutendewa haki na njia sahihi, na kusamehewa na Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Kwa hakika kuzungumza ukweli na kutomdanganya mtu ni sharti la msingi la mtu kuwa Muislamu. Muumini daima anapaswa kusema ukweli hata kama utakuwa na madhara kwake. Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ, kamwe hakusema uongo, hata pale anapotania. Tukio lifuatalo ni mfano kamili unaotuonyesha ubora na usafi wa moyo wake.

Amesimulia Abdullah ibn Amir:

Siku moja mama yangu aliniita wakati Mtume ﷺ alipokuwa amekaa nyumbani mwetu. Akasema: "Njoo nitakupa kitu." Mtume wa Mwenyezi Mungu akamuuliza:

"Unakusudia kumpa nini?"

Akajibu: "Nimekusudia kumpatia tende."

Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ akasema;

42. Qur'an 4: 9; Qur'an 33; 70

"Kama hukukusudia kumpa chochote, uongo wako uta-andikwa dhidi yako." (Abu Dawud, Kitab al-Adab, 80/4991, Ahmad b. Hanbal, III, 447)

Hivyo basi, Qur'an Tukufu, muongozo wetu kutoka kwa Mwenyezi Mungu, unatulingania sisi waumini, katika aya nyingi, kutumia lugha sahihi, njema na laini na inatuonya ku-husu kutumia lugha iliyo kinyume.

AINA GANI YA LUGHA INAYOKATAZWA NA QUR'AN TUKUFU?

Qur;an Tukufu inatueleza kuwa maneno ya uongo ya washirikina na makafiri ndiyo maneno mabaya zaidi, [43] ma-neno matupu, [44] na mafundisho yanayohitilafiana [45]. Uislamu umekataza kila aina ya maneno ya uongo,[46] kama vile kuse-ma kuwa Mwenyezi Mungu ana washirika, ukafiri na unafiki. Na kitisho cha Qur'an dhidi ya kila moja kati ya hayo, yaani uongo, ni kikubwa mno.

Mwenyezi Mungu Mtukufu amekataza kusema maneno makali hadharani[47] na kufichua hadharani matendo mabaya isipokuwa katika mazingira maalumu kama vile mbele ya ha-kimu ili kulinda haki za mtu aliyeonewa. Kwa sababu kufichua na kuzungumzia mambo mabaya husababisha yajulikane na hivyo yanaweza kuenea katika jamii. Maneno yasiyokuwa na staha ni kama kuanika wazi matendo mabaya. Hadith ya Mtu-me ﷺ inasema:

43. Qur'an 17: 40
44. Qur'an 13; 33
45. Qur'an 51: 8
46. Qur'an 22: 30
47. Qur'an 4: 148

"Mazungumzo machafu ni sehemu ya unafiki." (Tirmidhi, Kitab al-Bir Wa al-Bila, 80)

Tunatakiwa kuwa makini ndimi zetu zisizoee kutumia lugha chafu. Kisa kifuatacho kinalielezea jambo hili kwa uzuri.

Siku moja Nabii Issa عليه السلام alikutana na nguruwe njiani. Akamwambia nguruwe: *"Tuache tupite kwa amani"* Wanafunzi wake wakamuuliza:

"Wazungumza na nguruwe?"

"Ninahofia ulimi wangu usije kuzoea lugha chafu." (Akimaanisha kuwa hata kuzungumza na mnyama, hakutaka kutumia lugha isiyokuwa ya kiungwana katika kumuelezea "nguruwe".) (Malik, Muwattā, Kalam, 4)

Kurudia maneno hayo hayo, iwe lazima au la, ni udhaifu wa kujieleza. Kama maneno hayo ni ya ukaidi na yasiyofaa, inakuwa ni tatizo kubwa sana. lugha hiyo inaumiza watu wenye haki na si sahihi kwa waumini. Kwa hakika, imeelezwa katika Hadith moja kuwa:

"Ewe Aisha! Je, umewahi kuniona nikizungumza lugha mbaya na chafu? (Kumbuka) watu wabaya zaidi mbele ya Mwenyezi Mungu siku ya Kiyama ni wale ambao watu huwakimbia kutokana na lugha zao mbaya na chafu." (Bukhari, Kitab al-Adab, 48)

Kwa mara nyingine, Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliwaonya wafuasi wake dhidi ya matumizi ya maneno ya jeuri na machafu na kuwausia kutumia lugha ya kiungwana na nzuri ili kuelezea maana husika.

Qur'an Tukufu pia inakataza kutumia maneno ya kupamba-pamba kwa udanganyifu kwa lengo la kuwahadaa watu.

Muumini anatakiwa kuangalia matumizi ya lugha inayoweza kuwa rahisi kueleweka.

Isisahaulike kuwa lengo la kuzungumza ni kueleza kwa uwazi kile ambacho mzungumzaji anakikusudia. Kupamba mazungumzo kwa maneno yasiyokuwa na ulazima na kujifanya kuwa mtu wa busara huiharibu sifa na uaminifu wa mzungumzaji machoni pa wasikilizaji. Siku moja Mtume ﷺ aliwaonya maswahaba wake kuhusu aina hii ya mazungumzo yanayomchukiza Mwenyezi Mungu na kusema:

"Siku ya Kiyama Mwenyezi Mungu hatoikubali toba au fidia kutoka kwa yule ambaye hujifunza ufasaha wa lugha na kuyarefusha mazungumzo yake bila ulazima wowote ili kwayo aziteke nyoyo za watu." (Abu Dawud, Kitab al-Adab, 86/5006)

Hii ndiyo sababu kwamba ni muhimu kwetu kujielezea kwa muhtasari na katika namna ambayo ni rahisi kueleweka. Maneno yetu yanapaswa kuwa wazi, yenye athari na fasaha. Kama asemavyo Jalal al-Din Rumi:

"Wale wasioweza kuelezea madhumuni yao ndiyo wanaorefusha mazungumzo."

Kurefusha mada, na kusema kitu hicho hicho tena na tena huwachosha wasikilizaji. Mazungumzo kama hayo huwa na maana ya kuwaona wasikilizaji kama watu wasioelewa.

Ili kuwa mzungumzaji mzuri, mtu anatakiwa kwanza kujifunza jinsi ya kuwa msikilizaji mzuri. Mwenyezi Mungu Mtukufu amewajaaliwa wanadamu masikio mawili na ulimi mmoja ili wasikilize zaidi na kuongea kidogo. Mazungumzo na maongezi yasiyokuwa na umuhimu humfanya mtu apoteze upendo wa watu. Kadhalika anatakiwa kujiepusha na upotezaji wa muda wake anaporefusha mazungumzo yake.

Imam Awzai (aliyefariki mwaka 157 H) anasema:

"Mwenyezi Mungu akitaka kuungamiza umma, huwafungulia milango ya mabishano yanayowazuia kufanya mambo mema."

Hii ndiyo sababu kwamba, mazungumzo matupu yasiyokuwa na umuhimu yanahesabiwa kama ni kupoteza muda. Mtume ﷺ anasema kuwa:

"Mazungumzo ya watu hayawi kwa ajili yao bali huwa dhidi yao, isipokuwa mazungumzo ya kuamrisha mema na kukataza mabaya." (Ibn Majah, Fitan, 64).

"Ewe Hafsa! Jizuie kuzungumza sana. Mazungumzo yasiyokuwa ya kuyadhukuru majina ya Mwenyezi Mungu, basi mazungumzo hayo huua moyo. Zitaje sifa za Mwenyezi Mungu kwa wingi uwezavyo kwani mazungumzo hayo huuhuisha moyo." ('Ali al-Muttakī, hakuna: 1896).

"... Kuzungumzia jambo jema ni bora kuliko kukaa kimya; na ukimya ni bora kuliko kuzungumza maovu." (Hakim, III, 343; Bayhakī, Shuab, 256/4993)

Basi, tunapaswa kuwa makini sana wapi, lini, na ni kiasi gani tunachotakiwa kuzungumza. Sheikh Sadi Shirazi anasema kuwa:

"Mambo mawili huonyesha udhaifu wa akili. Ukimya pindi mazungumzo yanapohitajika na kuzungumza pindi ukimya unapohitajika".

Kiwango cha sauti pia kinatakiwa kiwe kizuri kirekebishwe kulingana na hali ya wasikilizaji. Kuongea kwa sauti sana na kuumiza masikio ya wasikilizaji ni miongoni mwa mambo yaliyokatazwa na Qur'an Tukufu. Qur'an inasema:

"Na ushike mwendo wa katikati, na teremsha sauti yako. Hakika katika sauti mbaya zote bila ya shaka iliyozidi ni sauti ya punda." (31: 19)

Kwa hakika, baadhi ya maswahaba walikuwa wakinyanyua sauti zao mbele ya Mtume ﷺ, wakapokea onyo lifuatalo kutoka kwa Mwenyezi Mungu:

"Enyi mlioamini! Msinyanyue sauti zenu kuliko sauti ya Nabii, wala msiseme naye kwa kelele kama mnavyosemezana nyinyi kwa nyinyi, visije vitendo vyenu vikaharibika, na hali hamtambui." (49: 2)

Aya hii inaashiria pia kwamba kushusha sauti mbele ya wakubwa na watu wanaoheshimika ni katika tabia njema.

Vile vile tunatakiwa kuepuka kuichafua lugha yetu kwa usengenyaji, matusi, na tuhuma. Mambo haya ni miongoni mwa majanga ya lugha yanayoonyesha uovu wa moyo.

Kwa muhtasari, waumini waliojipamba kwa kanuni za kimaadili za Qur'an Tukufu ni kama maua, wanatakiwa kuzigusa roho za wengine kwa uzuri wao na harufu yao nzuri. Kila neno katika maneno yao linapaswa kuwa kirutubisho cha roho. Hawatakiwi kuacha kutabasamu na kueneza huruma katika jamii kwa maneno yao mazuri. Wanatakiwa kuwa miongoni mwa watu *ahsan*, *ajmal*, na *akmal* katika jamii kwa shakhsia na mwenendo wao.

Wanatakiwa kuwa *ahsan* inayomaanisha kuwa matendo yao yote yanatakiwa kuwa bora na kutawanya uzuri kila wakati.

Wanatakiwa kuwa *ajmal* yaani shakhsia zao zinapaswa kuleta amani na utulivu kwa watu wanaowazunguka.

Wanatakiwa kuwa *akmal*, yaani wawe wakomavu na wakamilifu zaidi katika jamii.

Matendo na kazi zote za waumini hao bora huakisi uzuri, ukuu, uchaji, amani, na wajihi wenye kutabasamu wa Uislamu.

kwa mujibu wa maelezo ya *Hilya -i Sharif*, Mtume ﷺ alikuwa na nuru ya uzuri katika uso wake; ufasaha katika mazungumzo yake; umaridadi katika matendo yake; na balagha na usafi katika maneno yake. Mazungumzo yake yalikuwa mazuri na yenye kugusa mno, maneno yake hayakuwa mengi sana wala mafupi sana.

Alikuwa akizungumza kwa uwazi na kila mtu aliweza kuielewa kila sentensi yake. Alikuwa hazungumzi kwa haraka haraka. Kwa ufupi, alikuwa fasaha zaidi, mchache wa maneno, na mzungumzaji mwenye hekima kuliko watu wote.

Abu Kursāfah ﵁ anasema kuwa:

Mimi, mama yangu, na shangazi yangu tulikwenda kwa Mtume ﷺ na kutoa kiapo cha utii wetu. Tulipoondoka, mama na shangazi yangu wakaniambia:

"Hatujawahi kuona mtu kama huyu katika maisha yetu. Hatumjui mtu yeyote mwenye uso mzuri zaidi kuliko yeye, mwenye nguo safi kuliko zake, na mwenye maneno fasaha mno kuliko yake. Mdomo wake mtukufu ni kama nuru yenye kuenea ulimwenguni." (Haythamī VIII, 279-280)

Mola wetu! Tujaalie tuwe wenye kuizoea lugha ya Mtume wetu ﷺ. Tupe baraka ya kupambwa na kanuni za kimaadili za Qur'an na utusaidie kuyarekebisha matendo na mwenendo wetu wote uendane na misingi ya Qur'an Tukufu.

Amin...

UKARIMU NA KUTOA SADAKA

Muumini anatakiwa awe na huruma kama upepo wa asubuhi na awe na ukarimu kama mvua. Awape amani na utulivu watu wa karibu naye na daima atafute radhi za Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Hii ndiyo sababu kwamba marafiki wa Mwenyezi Mungu ni wale ambao wamepambwa kwa usikivu, adabu, ithaar, huruma na ukarimu. Hawa huiangazia jamii yao kama mwezi unavyoangaza usiku wa giza. Ukarimu wao ni kama mto wa porini, ambao hutiririka kutoka mbali na kutoa amani kwa mimea, wanyama, na kila aina ya viumbe.

UKARIMU NA KUTOA SADAKA

Tunda la kwanza la imani ni huruma na ishara ya wazi zaidi na dalili kubwa ya huruma ni infaq au sadaka. *Infāq* ina maana ya kujitolea maisha na mali kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Maisha ya manabii, wasomi, Wana-hekima, na mawalii yamejaa visa vya huruma na kutoa sadaka.

SHINDANENI KATIKA UKARIMU

Siku moja Mtume ﷺ aliwageukia maswahaba wake baada ya kumaliza swala ya Ijumaa na kuwauliza:

"Je kuna mtu yeyote miongoni mwenu kafunga leo?" Omar رضي الله عنه akasema:

"Mimi sikufikiria juu ya kufunga jana usiku na hivyo mimi si mwenye kufunga leo."

Abu Bakr رضي الله عنه akasema:

"Mimi nilikuwa na mawazo kuhusu kufunga jana usiku na mimi ni mwenye kufunga hivi sasa."

Kisha Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ akauliza:

"Je, kuna mtu yeyote miongoni mwenu ambaye alitembelea mgonjwa leo?"

Omar ﷺ akajibu:

"Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Tulipomaliza kuswali swala ya alfajiri na wala hatujatoka msikitini. Inawezekanaje kumtembelea mgonjwa?"

Lakini Abu Bakr ﷺ akasema:

"Nimesikia kwamba ndugu yetu Abdurrahman bin Awf ni mgonjwa. Nilipokuwa nakuja msikitini, nilisimama nyumbani kwake kuangalia hali ya afya yake."

Tena Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ akauliza:

"Je, kuna mtu yeyote miongoni mwenu aliyemlisha masikini asubuhi ya leo?"

Omar ﷺ akajibu:

"Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Tumemaliza kuswali swala ya Alfajiri na hatujatoka msikitini."

Lakini Abu Bakr akasema:

"Nilipokuwa njiani kuelekea msikitini leo asubuhi, niliona mtu aliyekuwa akiomba chakula. Abdurrahman mwanangu alikuwa na kipande cha mkate mkononi mwake, nikauchukua mkate na kumpa yule masikini."

Mtume ﷺ aliposikia hilo akamwambia Abu Bakr ﷺ:

"Ewe Abu Bakar! Ninakupa habari njema ya Pepo."

Baada ya Omar ﷺ kusikia hayo, akashusha pumzi na kusema "Ah! Pepo" Ili kutuliza huzuni yake, Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ akamwambia:

"Mwenyezi Mungu amhurrumie Omar, Mwenyezi Mungu amhurumie Omar! Kila anapotaka kutenda mema Abu Bakr humpita". (Haythamī, III, 163-164 Angalia pia Abu Dawud, Zaka, 36/1670. Hakim, I, 571 / 1501).

Somo kubwa tunalopaswa kulichukua kutokana na hadithi hiyo iliyotajwa hapo juu ni kwamba wakati wote tunatakiwa kutafuta radhi za Mwenyezi Mungu Mtukufu; kwa maana imeelezwa katika aya kuwa:

"Na ukipata faragha, fanya juhudi. Na Mola wako Mlezi ndiyo mshughulikie." (94; 7-8)

Tena Mola wetu anasema juu ya waja wake wema ambao amewaridhia:

"... na wanakimbilia katika mambo ya kheri. Na hao ndiyo miongoni mwa watenda mema...." (3, 114)

Kukimbilia kufanya mambo ya kheri inapaswa kugeuka kuwa tabia ya asili ya muumini. Muumini anatakiwa awe na huruma kama upepo wa asubihi na mwenye ukarimu kama mvua. Awape amani na utulivu watu wa karibu naye na daima atafute radhi za Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Hii ndiyo sababu kwamba marafiki wa Mwenyezi Mungu ni wale ambao wamepambwa kwa usikivu, adabu, *ithaar*, huruma na ukarimu. Hawa huiangazia jamii yao kama mwezi unavyoangaza usiku wa giza.

Ukarimu wao ni kama mto wa mwituni, ambao hutiririka kutoka mbali na kutoa amani kwa mimea, wanyama, na kila aina ya viumbe. Infaq ya kweli ni kutafuta radhi za Mwenyezi Mungu kwa kuzigeukia roho zenye huzuni na zisizokuwa na matumaini kwa moyo uliojazwa ikhlas,huruma, upendo na *ithaar*. Yaani kukimbilia kuwasaidia wengine kwa njia yoyote ile ili kuondosha hali yao ya kunyimwa.

Mola wetu ameifanya *infaq* kuwa mojawapo ya majukumu muhimu ya kijamii. Bila shaka hiyo ni moja ya baraka zake za ajabu. Kwa maneno mengine, Mola wetu ametaka sehemu ndogo ya baraka zake itolewe kwake kama ishara ya kumshukuru kwa fadhila zake nyingine nyingi. Akaifanya *infaq* kama fidia ya dhambi na nyenzo muhimu ya kupata thawabu za kiroho kwa ajili ya wokovu wa milele.

TABIA NA SIFA YENYE KUMPANDISHA MTU: UKARIMU

Tabia pekee inayotakiwa kufanya kazi katika *infaq* ni ukarimu. Itakuwa kazi bure kutegemea matunda ya infaq yastawi katika mabustani ya nyoyo ambayo hayakupandwa mbegu za ukarimu.

Katika maneno ya Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ, ukarimu umeonyeshwa kuwa ni njia ya kuwa karibu na upendo wa Mwenyezi Mungu:

"Mwenyezi Mungu Mtukufu ni Mkarimu; na anapenda ukarimu na maadili ya juu …" (Suyūtī, Jami 'Al-Saghīr, I, 60)

Ukarimu, ambao ni ladha ya imani, humfanya mtu apendwe na Mwenyezi Mungu na watu. Imeelezwa katika Hadith al-Qudsi[48] kuwa:

"Hii (Uislamu) ndiyo dini niliyoiridhia na nimeichagua kwa ajili yangu. Ukarimu na tabia njema ndivyo vinavyofaa kwa ajili yake. Madamu mnaishi kama Waislamu, iinueni kwa tabia hizi." (Haythamī VIII, 20, Ali Al-Muttaqī, Kanz Al-'Ummāl, VI, 392)

48. Ni hadith ambazo Mwenyezi Mungu huwasiliana na Mtume Muhammad ﷺ

Ukarimu ni matokeo ya kukomaa katika imani ya kumuamini Mwenyezi Mungu na Akhera. Ali ﷺ analielezea hili kwa uzuri:

"Imani ni mfano wa mti; mizizi yake ni imani thabiti; matawi yake ni uchamungu; nuru yake ni staha na matunda yake ni ukarimu."

Sheikh Sadi Shirazi anasema kuwa:

"Mtu karimu ni kama mti wenye matunda; na mtu asiyekuwa na ukarimu ni mfano wa kama kuni kwenye milima." Na anaashiria kuwa ukosefu wa sifa ya ukarimu haina tofauti na kuni za moto.

MARADHI MAKUBWA MAWILI: UBADHIRIFU NA UBAKHILI

Ubadhirifu ni mtu kutumia sana kwa ajili yake mwenyewe; wakati ubakhili ni mtu mmoja kujilimbikizia sana. Yote mawili ni katika sifa na tabia za ubinafsi. Mwenyezi Mungu Mtukufu anaikataa aina hii ya utumwa. Hilo limetajwa katika aya zifuatazo:

"Wala usiufanye mkono wako kama uliofungwa shingoni mwako, wala usiukunjue wote kabisa, utabaki ukilaumiwa muflisi." (17: 29)

"Na wale ambao wanapotumia hawatumii kwa fujo wala hawafanyi ubakhili, bali wanakuwa kati kati baina ya hayo." (25: 67)

Ili kutimiza mahitaji ya mali, mtu anatakiwa kuacha kutumia mali yake kwenye maeneo yaliyokatazwa na Uislamu na kujitenga na tabia hizo mbili, yaani ubakhili na ubadhirifu. Ma-

janga ya kuwa tajiri ni uchoyo, tamaa na ubakhili. Na ukarimu ni dawa ya maradhi haya.

Ghazali anauelezea ukarimu kuwa ni hali iliyo baina ya ubadhirifu na ubakhili.

Kwa upande mwingine, janga la ukarimu ni ubadhirifu. Kwa maneno mengine, kutumia fadhila za Mola wako kwa ubadhirifu, wakati ukijaribu kuwa mkarimu, ni utumiaji mbaya.

Kuhusu *infaq*, tuashirie kuwa ubadhirifu hauna maana ya kutumia sana. Kutumia kwa ajili ya vitu visivyokuwa na umuhimu, viwe vingi au vichache, huhesabiwa kuwa ni ubadhirifu; kutumia kwenye vitu sahihi, bila kuangalia ukubwa wake, haichukuliwi kama ni israfu. Kinyume chake ni kitendo chenye kusifiwa. Msemo usemao: *"hakuna kheri katika ubadhirifu; na hakuna ubadhirifu katika kheri"* unaonyesha ukweli huu.

Mfano bora unaothibitisha kuwa utumiaji kwenye vitu sahihi hata uwe mkubwa kiasi gani, hauchukuliwi kuwa ni israfu, ni mfano wa Abu Bakr ﵁. Mara kadhaa alitoa mali zake zote kumpa Mtume ﷺ.

Kwa upande mwingine, ubakhili hauna maana ya kutoa kiasi kidogo, bali una maana ya kutoa chini ya uwezo; kwa sababu kila mtu anawajibika kutumia ndani ya mipaka ya uwezo wake. Sheikh Sadi analieleza hili kwa namna yenye kupendeza;

"'Mwenyezi Mungu hamfungii mtu mlango wa kutenda mema. Tambua vizuri kuwa wema wa kila mtu upo katika kiwango cha uwezo wake. Sahani ya dhahabu inayotolewa na tajiri siyo sawa na karati ya sadaka ya mtu masikini itokanayo na kazi ya mikono yake. Mguu wa panzi ni mzito sana kwa sisimizi."

Katika vita vya Yarmuk, glasi ya mai, ambayo mashahidi watatu walipeana wakati wa pumzi yao ya mwisho, inaweza kupita thawabu za matendo mengi makubwa; kwa sababu kitu muhimu siyo kiasi cha sadaka, bali utajiri wa moyo.

Vinginevyo, kama kutoa kidogo kungehesabiwa kuwa ni ubakhili, ukarimu ungependelewa kwa matajiri na wenye mali. Kinyume chake, mali na umasikini ni njia za mitihani ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Kuwa tajiri au maskini ni kitu kilicho nje ya mamlaka ya mja. Ndiyo maana ukarimu au ubakhili ni suala ambalo halina uhusiano na mali bali ni tabia ya moyo.

Kwa maneno mengine, muumini aliye masikini anaweza na anatakiwa kuwa mkarimu. Imani yetu inatutaka kuwa wakarimu katika hali yoyote ile. Kwa sababu ukarimu au ubakhili hautegemei tunatoa kiasi gani katika mali zetu bali unategemea uwiano, ambao tunaweza kuutumia.

Mtume ﷺ anamlingania kila muumini, masikini na tajiri, kutoa sadaka. Anawaambia wale wenye tende moja tu:

"(Enyi watu!) Jiokoeni na moto (wa Jahannam) hata kwa kipande cha tende (kinachotolewa sadaka), na kama hicho hakipo, basi (jiokoeni) kwa kusema maneno mazuri." (Bukhari, Kitab al-Adab, 34)

Hapa kuna baadhi ya mifano zaidi ya ushauri na uhamasishaji wa Mtume ﷺ katika suala hili. *"Ewe Aisha! Usimtoe mtu masikini mbali mikono mitupu, toa hata kama unachoweza kutoa ni nusu ya tende".* (Tirmidhi, Kitab al-Zuhd, 37)

"Kumuonyesha tabasamu ndugu yako katika Uislamu ni aina ya sadaka." (Tirmidhi, Kitab al-Bir, 36)

Abu Dharr رضي الله عنه anaripoti kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ alisema:

"Ewe Abu Dharr! Unapoandaa mchuzi, ongeza maji na umpe (zawadi) jirani yako." (Muslim, Kitab al-Bir, 143) Hadith Hii inaonyesha kwamba umasikini si kikwazo mbele ya ukarimu.

TIBA YA UGUMU WA MOYO: UKARIMU NA KUTOA SADAKA

Aina zote za Ibada huupa moyo uzuri mbalimbali, wema na malipo ya kiroho. Malipo ya kiroho yana duru muhimu kwa wanadamu ambao wako njiani kuileta imani yao kutoka kwenye hali ya kutokomaa kwenda kwenye hali ya ukomavu.

Omar bin Abdulaziz (Mwenyezi Mungu airehemu nafsi yake) anasema kuwa:

"Swala hukupeleka mpaka kwenye nusu ya safari yako; funga hukupeleka mpaka kwenye lango la Mfalme. Sadaka hukupeleka mpaka mbele ya Mfalme."

Maana ya *infaq* ikichunguzwa vizuri, itaonekana kuwa hekima iliyo nyuma ya ibada hii ni kuwaokoa binadamu kutoka kwenye utumwa wa maada (vitu) na kuufanya umaanawi (hali ya kiroho) kuwa juu na kuushinda umaada. Katika muktadha huu faida kubwa ya *infaq* ni kuipa faraja dhamiri.Ali Isfahani anauelezea vizuri ukweli huu:

"... nilitafuta wema na kutotenda dhambi nikavikuta katika uchamungu, kwa maneno mengine kujizuia kufanya mambo yaliyoruhusiwa kwa hofu ya kuangukia katika mambo yenye shaka. Nilitafuta urahisi wa kuuliza nikaukuta katika kukaa kimya. Nilitafuta faraja na utulivu nikaukuta katika kutoa sadaka."

Kwa sababu kila muumini anawajibikiwa kwa wale watu wanaomzunguka,hawezi kuyaziba masikio yake asisikie matatizo ya masikini na mafukara. Anapaswa awe amejawa na Ikhlasi, umaridadi, ithaar, na huruma ya *infaq* na kutoa sadaka.

Mweyezi Mungu Mtukufu amewafanya viumbe kuwa sababu ya wao kupata maisha yao. Hivyo, kuwaangalia wenye shida na kuweza kutenga fungu katika baraka ulizopewa na Mwenyezi Mungu ni wema wa hali ya juu na baraka kubwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Moyo wa muumini hauwezi kupata faraja isipokuwa kwa kutuliza vilio vya masikini.

Jalal al-Din Rumi anaufafanua ukweli huu kama ifuatavyo:

"Unajua kuwa kupungua kwa mwili na mali ni faida kwa moyo na huutoa katika madhara[49]*. Utajiri ukitumika katika mambo ya kheri, uhai mia moja huja katika moyo kama mbadala."*[50]

Mali zinatakiwa zitafutwe kwa lengo la kuwasaidia wenye shida kwa kuanza na jamaa wa karibu mpaka kwa wanyonge, masikini, na masikini wengine katika jamii. Hivyo mali inapaswa kutafutwa kwa lengo la kupata faraja na wokovu wa milele. Hili likiwa lengo la kuchuma mali, basi ugumu, msongo na msukosuko utokanao na wasiwasi wa kidunia huondoka na mahala pake huchukuliwa na utulivu mzuri na amani ya moyo.

Tusikilize tiba ya ugumu wa moyo, ambao ni tatizo la watu wote katika ulimwengu wa sasa, kutoka kwenye kinywa cha Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ:

"Ukitaka moyo wako ulainike, walishe masikini, na kipapase kichwa cha yatima..." (Ahmad b. Hanbal, Musnad, II, 263)

49. Mathnawi, III, 3395
50. Mathnawi, IV, 1758

Rumi, katika namna fulani, anaitafsiri hadith hii kama ifuatavyo;

"Nyoyo za masikini ni kama nyumba iliyojaa moshi. Ufungulie dirisha kwa kusikiliza na hivyo moyo na nafsi yako vitasafika."[51]

Roho zilizokomaa na kusafika kwa kutoa sadaka zitafurahia kuona kwamba sadaka zao zimegeuka kuwa ulinzi kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Hivyo, zitageuka kwa hiari kuelekea kwenye utoaji wa sadaka.

Rumi analifafanua hili kama ifuatavyo:

"Kamwe utajiri haukupungua kwa kutoa sadaka: kwa hakika vitendo vya kheri ni njia bora ya kuifungamanisha mali na mtu husika. Katika zaka kuna mafuriko na ongezeko la dhahabu (ya mtu): katika swala kuna ulinzi dhidi ya zinaa na uovu. Zaka ni mlinzi wa mfuko wako, swala ni mchungaji anayekuokoa dhidi ya mbwa mwitu." [52]

Mali haipungui wala kutoweka kwa kutoa sadaka. Kinyume chake, huongezeka kutokana na kiwango cha Ikhlas katika kitendo hicho cha sadaka. Japokuwa Abu Bakr ﵁ alifikia kwenye hatua ya kufilisika kifedha kutokana na kutoa mali yake yote kwa Mtume ﷺ, aliongeza mali yake tena na tena kwa fadhila za Mwenyezi Mungu, kwa sababu mali iliyotolewa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu huongezeka kama iliopogolewa.

Aya ifuatayo inabainisha kuwa:

"Mfano wa wanaotumia mali zao katika Njia ya Mwenyezi Mungu ni kama mfano wa punje moja iliyo chipuza mashuke saba. Katika kila shuke zimo punje mia. Na

51. Mathnawi, III, 485
52. Mathnawi, VI, 3573 - 3576

Mwenyezi Mungu humzidishia amtakaye, na Mwenyezi Mungu ni Mwenye wasaa na Mwenye kujua." (2: 261)

Mali isiyotumika kwa ajili ya Mwenyezi Mungu inafanana na maji yaliyotuama yanayotoa harufu mbaya baada ya kuwa katika sehemu moja kwa muda mrefu. Kwa uzuri kabisa Sheikh Sadi anasema:

"Usidhani ya kuwa fedha itaongezeka kwa kuirundika. Hata maji hutoa harufu mbaya. Jaribu kusamehe. Mbingu husaidia kutiririsha maji. Mvua, zinatuma mafuriko na haziiachi ikauke."

Jalal al-Din Rumi anauweka wazi ukweli huu kama ifuatavyo: *"Pindi mtu anapopanda mbegu, ghala lake hukauka (mbegu), lakini kuna uzuri katika shamba lake; na kama akiziacha (mbegu) ghalani na kuziweka, wadudu na panya na majanga (ya zama na kuoza) vitazimaliza*." [53]

Sadaka na Zaka huzisafisha na kuzitwaharisha mali. Huwa ngao dhidi ya matatizo. Hayo yameelezwa katika hadith ifuatayo ya Mtume ﷺ:

"Fanyeni haraka kutoa sadaka; kwa sababu matatizo hayawezi kwenda mbele ya sadaka." (Haythamī, Majma 'Al-Zawāid, Iii, 110)

Maneno kama *Infāq* ambayo yana maana ya kujitolea mali na maisha kwenye njia ya Mwenyezi Mungu Mtukufu yametajwa katika zaidi ya sehemu mia mbili ndani ya Qur'an Tukufu. Amri ya *infaq* ni matokeo ya huruma ya Mola wetu isiyokuwa na kikomo kwa waja wake. Kwa sababu, kwa kutulingania kwenye kutoa sadaka, kiukweli, Mola wetu anatuita kwenye kufaidika na fadhila, baraka, na amani ya kiroho inayopatikana katika kutoa sadaka.

53. Mathnawi, I, 2239 - 2240

TOA KILICHO NJE YA MAHITAJI YAKO

Hali ya kujinyima anasa za mwili huanza pale nyoyo zinapofika kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa upendo. Mali hupoteza thamani yake katika macho na nyoyo. Thamani yake hupatikana pale zinapokuwa kama nyenzo ya kuwa karibu na Mwenyezi Mungu Mtukufu. Muumini anayetafuta ridhaa ya Mwenyezi Mungu Mtukufu anajua jinsi ya kuendesha maisha ya wastani na ya kawaida ili aweze kutafuta njia za kuwasaidia masikini.

Kizazi cha Maswahaba, ambao walilelewa katika mazingira ya Qur'an na Sunna, hawakuelekea kwenye anasa na utawala wa dunia hii, ingawa walipata utajiri mkubwa kupitia ngawira zilizomiminika katika mji wa Madina kutoka katika ardhi walizozifungua. Hawakubadilisha mtindo wa maisha yao ya wastani (staha) na wala hata kuzipamba nyumba zao. Kwa kutoa sadaka katika mali zao, waliendesha maisha ya amani na utulivu wa kweli wa mali. Kizazi cha Maswahaba hakikujua mtindo wa maisha ya ubadhirifu, ulafi, anasa na majivuno, ambayo ni maradhi sugu ya dunia ya kisasa. Kwa sababu waliishi kwa kufahamu ukweli wa kwamba **"kesho kaburi litakuwa ndiyo makazi ya roho zao."**

Imam Malik aliandika katika barua yake kwa Khalifa wa wakati wake kuwa:

"Omar ﷺ alikwenda kuhiji mara kumi. Kwa kadiri nijuavyo alikuwa akitumia dinari kumi na mbili tu katika hijja yake moja kwa sababu ya mtindo wa maisha yake ya staha. Alikuwa akikaa chini ya mti badala ya hema. Alikuwa akibeba kiriba cha maziwa yake mabegani mwake. Alikuwa akitembea sokoni na kuulizia hali zao." (Iyad Qadhi ', Tartīb al-Madārik, uk. 271)

Kwa maneno mengine, Omar ﷺ alikuwa akiridhika kutumia tu kile kinachohitajika kwa ajili ya hijja yake, na mali iliyobaki alikuwa akiitoa sadaka. Kwa sababu Mwenyezi Mungu ameeleza kuwa kiasi kinachotolewa katika sadaka ni **"kilicho nje ya mahitaji."**[54] Kulingana na hili, kiwango cha chini cha ukarimu ni kutoa kiwango kilichozidi katika mali, ambacho hakihitajiki.

Kwa hali hii, Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ anasema kwamba:

"Ewe mwana wa Adamu, ni bora kwako ukitumia ziada yako (mali), lakini ukiizuia, ni mbaya kwako. (Hata hivyo) hakuna lawama kwako (kama kuizuia kuna umuhimu) kwa ajili ya maisha. Na anza (kutuoa sadaka) kwa wategemezi wako; na mkono wa juu ni bora zaidi kuliko mkono wa chini." (Muslim, Kitab al-Zaka, 97; Angalia pia Tirmidhi, Kitab al-Zuhd, 32)

Basi, tusizidishe kiasi cha haja na kutathmini kiasi cha haja ndani ya mipaka ya usawa. Na pia tunapaswa kutumia kiasi kilicho nje ya mahijtaji yetu kwa kukitoa sadaka.

JUHUDI ZA KUONGEZA UKARIMU

Ahmad bin Abu Ward (Mwenyezi Mungu aihurumie nafsi yake) anaelezea kwa muhtasari hali ya marafiki wa Mwenyezi Mungu kama ifuatavyo:

"Kuna mambo matatu ambayo yakiongezeka kwa rafiki wa Mwenyezi Mungu, hali yake nzuri nayo huongezeka:

1. Kadri daraja yake inavyopanda, ndivyo staha yake inavyoongezeka.

54. Qur'an 2: 219.

2. Kadri anavyozidi kuishi ndivyo anavyozidi kuwahudumia wengine

3. Kadri mali yake inavyoongezeka ndivyo ukarimu wake unavyoongezeka."

Ramazanoğlu Mahmud Sami (q.s) alikuwa katika hamasa kubwa ya *infaq* kiasi kwamba aliona kuwa sadaka yake haitoshi, akawa anatembea kwa miguu kwenda kazini na kuiweka akiba nauli yake ya gari ili apate kuitoa sadaka. Kwa maneno mengine, alikuwa akiitoa muhanga furaha yake ili aongeze kiasi cha sadaka yake.

Kila kitu kinachotolewa kama sadaka ni mtaji wa wokovu wetu wa milele huko Akhera. Ili kupata furaha hii ya milele Rumi anatoa ushauri ufuatao:

"Punguza kiasi unachokula na kunywa katika dunia hii upate kuongeza sadaka yako ili uweze kupata chemchem (ya ziada ya mali). Inawezekanaje mtu aliyedondosha tone kwenye ardhi ya uaminifu akose bahati ya mawindo?"

Leo kila mtu ajaribu kuishi kulingana na kanuni hii kadri awezavyo, hata kwa kutoa sadaka ndondogo kutokana na furaha binafsi, urahisi, mapambo ya nyumba zetu, au matumizi yetu ya kila siku. Hali ya masikini, mafukara na kadhalika, ni picha ya mfano kwa wale wenye ufahamu.

Waumini wenye mali, ambao hutenda kulingana na kanuni hii, hujiweka mbali na utafutaji wa anasa na raha. Lakini, wale wenye kughafilika juu ya ukweli huu hujifanyia matumizi makubwa sana kwa ajili ya nafsi zao. Hao ni wale wasemao "ni mali yangu, naweza kuitumia nitakavyo" na ni wale ambao Qur'an Tukufu imewaita kama **ndugu wa mashetani.** [55]

55. Tazama Qur'an 17: 27.

UPOFU WA UBAKHILI

Ili kuwa watu halisi wa utoaji sadaka, utiifu wetu unatakiwa kufikia ngazi ya *ihsan*, yaani kumuabudu Mwenyezi Mungu kana kwamba unamuona. Kuwa na uwezo wa kuona ukuu wa Mwenyezi Mungu kila mahali na kila wakati kunategemea macho ya moyo wetu yawe wazi. Ili kufikia ukarimu wa kweli, lazima tuwe na imani thabiti na kutoa sadaka zetu kana kwamba tunaziona thawabu zetu tutakazopata huko Akhera.

Rumi anaelezea jambo hili kama ifuatavyo;

"Mtume ﷺ alisema, "Yule ajuaye kwa uhakika malipo yake siku ya Kiyama - kwamba malipo yake yatakuwa kumi kwa moja - kila wakati atafanya (kitendo cha) ukarimu mkubwa." Ukarimu wote mkubwa unatokana na kuona malipo; kwa hiyo, kuona malipo kunaondoa hofu (na woga wa kufanya ukarimu). Ubakhili hutokana na mtu kutoona malipo: matarajio ya kupata lulu humfanya mzamiaji aendelee kuwa na furaha. Hivyo hakuna aliye bakhili duniani; kwa sababu hakuna anayetoa bila (kuona) kile atakachopata kama badala. ukarimu basi, huja kutoka machoni, siyo mkononi: ni kile kinachoona mambo ndicho kinachomuokoa mwenye kuona dhidi ya ubakhili."[56]

kwa hakika ubakhili ni upofu wa moyo na kutokuwa na uwezo wa kukiona kifo na kile kitakachokuja baada ya kifo. Pia ni utovu wa shukrani kwa baraka za Mola wetu zisizokuwa na kikomo.

Katika suala hili Rumi anatoa onyo la kutisha kuwa:

56. Mathnawi, II, 895 - 900

"Kwenye ukingo wa mto, maji huonewa kinyongo na yeye (peke yake) ambaye ni kipofu wa mkondo wa maji." [57]

Mola wetu pia anatuonya kuhusu kupatwa na upofu huo wa moyo na utovu wa shukrani katika aya zifuatazo:

"Na mna nini hata hamtoi katika Njia ya Mwenyezi Mungu, na hali urithi wa mbingu na ardhi ni wa Mwenyezi Mungu?... " (57; 10)

"... Na Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye hazina za mbingu na ardhi, lakini wanafiki hawafahamu." (63; 7)

"Angalieni! Nyinyi mnaitwa mtumie katika njia ya Mwenyezi Mungu, na wapo katika nyinyi wanaofanya ubakhili. Na anaye fanya ubakhili basi anajifanyia ubakhili mwenyewe. Na Mwenyezi Mungu si mhitaji, na nyinyi ndiyo wahitaji. Na mkigeuka atawaleta watu wengine badala yenu, nao hawatakuwa kama nyinyi."(47; 38)

Kwa maneno mengine tunatakiwa kutafakari kuwa tunaishi katika ardhi ya nani, tunakula riziki za nani, na ni mali ya nani ambayo tunajaribu kuizuia?

Bila shaka Mwenyezi Mungu Mtukufu ndiye mmiliki halisi wa mali. Ametupa amana ya baraka zake katika hii dunia. Waja wake ni kama mawakala wa kusambaza mali yake katika hii dunia. Mja pia ana jukumu kwa masikini na wenye shida. Wale wanaoutambua ukweli huu hawawezi kuwa wageni wa yale yanayotokea katika jamii yao.

57. Mathnawi, II, 894

TOA MSAADA ILI NAWE UPATE KUSAIDIWA PINDI UTAKAPOUHITAJIA

Kuwahurumia na kuwasaidia viumbe, Mwenyezi Mungu Mtukufu ni mfano bora wa jinsi anavyowapenda viumbe. Njia bora ya kuonyesha shukrani kwa baraka tunazopewa na Mola wetu ni kutoa msaada na kuwa wakarimu kwa waja wa Mola wetu wenye haja kama tunavyohitaji huruma na fadhila zake; kwa sababu fadhila hizo ni mtihani kwetu hapa duniani.

Imeelezwa katika hadithul - Qudsi kuwa:

"Mwenyezi Mungu alisema (kumwambia mwanadamu), 'toa (sadaka), kwa maana nitakufidia (kwa wingi)." (Bukhari, Kitab Al-Tawhīd, 35)

Katika hadith nyingine, Mtume ﷺ anasema kuwa:

"Toa kulingana na uwezo wako; usizuie fedha yako kwa kuihesabu (yaani kwa kuilimbikiza), (kwani ukifanya hivyo), Mwenyezi Mungu naye ataizuia baraka yake kwako." (Bukhari, Kitab Al-Zaka, 21 ; Muslim, Kitab al-Zaka, 88)

Kwa maneno mengine ili kuwa muumini aliyekomaa ambaye Mwenyezi Mungu Mtukufu amemridhia, tunawajibika kuwasaidia kwa wingi waja wake wenye shida kama anavyotusaidia na kututeremshia baraka Zake.

Tunamuomba Mola wetu atupe ladha ya nyoyo na furaha ya imani. Tunamuomba atupe baraka ya raha ya ukarimu na amani ya kuwasaidia wengine.

Amin...

ADABU ZA KUTOA

Muumini ni mtu karimu. Ukarimu wa kweli ni kuwa na uwezo wa kutoa bila hisia ya majuto na bila kusimulia. Kinyume chake ni kuwa na uwezo wa kutoa kwa furaha. Muumini anapaswa awe kama maua, ambayo kwa hiari hutoa harufu yake nzuri. Kwa hivyo basi, ili sadaka yake ipate kukubaliwa kikamilifu mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Sheikh Saadi anasema kwamba:

"Kwa kuwa huna lazima ya kwenda kwenye mlango wa mtu, ili kutoa shukrani, usimmkatae masikini anayekuja mlangoni kwako na kutana naye kwa uso wenye tabasamu..."

ADABU ZA KUTOA

Tunapochunguza msingi na lengo la Usufi, tunagundua kwamba njia kuu inayotumiwa na Usufi kwa ajili ya mafanikio ya kiroho ni “upendo”, na kilele cha mafanikio ya kiroho ni kuzingatia misingi ya tabia njema. Katika suala hili, muumini anakuwa katika njia ielekeayo kwenye kuungana na Mwenyezi Mungu kwa kiasi kwamba humuweka Mwenyezi Mungu na Mtume wake katika kitovu cha moyo wake. Alama kuu ya hili ni kujipamba kwa misingi ya kimaadili ya Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ.

Hisia ya kuzingatia misingi ya tabia njema inaunda msingi wa maadili ya kitume. Kwa mujibu wa maelezo ya maswahaba, Mtume wa Mwenyezi Mungu alikuwa na soni sana kuliko bikira aliyefunikwa. Kwa mara nyingine anasema Mtume ﷺ kuhusu tabia zake: *“Mola wangu alinifundisha tabia njema na akaniadabisha vizuri.”* (Suyūtī, Jami ‘al-Saghīr, I, 12)

Jalal al-Din Rumi anasema yafuatayo kuhusu tabia njema:

“Kama unataka kukitiisha kichwa cha Shetani, fungua macho yako na utaona kwamba kinachomuumiza sana ibilisi ni tabia njema. Kama mtu hana tabia njema basi huyo si binadamu wa kweli...”

Hii ndiyo sababu kwamba hapo zamani miongoni mwa ishara na onyo katika nyumba za madarweshi na wale waliosilimu palisomeka: «اَدَبْ يَا هُو» . Alama hii ina maana mbili. Maana moja ni kwamba inawaonya na wakati huo huo inawalingania madarweshi kuwa waangalifu kuhusu tabia zao. Maana nyingine ni kwamba dua kwa Mwenyezi Mungu ili kupata tabia njema.

Tabia njema ambazo ni msingi wa imani, zinakusanya vipengere vyote vya maisha ya muumini, hususan ibada yake na maisha yake ya kila siku.

Mwenyezi Mungu Mtukufu anaeleza kuwa hakuwaumba waja isipokuwa kwa lengo la kumuabudu Yeye peke yake. Kwa muktadha huu, aina zote za ibada na miamala ya kila siku ni kama hatua muhimu ya utiifu wetu. Kwa maneno mengine,, hatuwezi kufikiria maisha ya utiifu bila ibada na miamala ya kila siku.

Kwa upande mwingine, namna tunavyotekeleza wajibu wetu wa utumwa ni muhimu sana kama utekelezaji wake wenyewe. Kwa sababu uzingatiaji wa tabia njema na adabu katika ibada na miamala ndiyo sharti la pekee la kuufikia upendo na radhi za Mwenyezi Mungu. Ndiyo maana ibada inayotekelezwa bila kuzingatia adabu na misingi sahihi hupoteza thamani yeke yote na kumuacha mtekelezaji akiwa hana kitu zaidi ya uchovu wa kimwili.

Kuhusu ukweli huu, Mtukufu Mtume ﷺ ameeleza katika hadith tukufu:

“Kuna watu wengi wanaofunga hawapati chochote kutokana na funga zao isipokuwa njaa na kiu, na kuna watu wengi wanaoswali usiku lakini hawapati chochote zaidi ya uchovu” (Ibn Majah, Şiyām, 21)

Kama ilivyo kwa swala, ambayo ni nguzo ya Uislamu, ina masharti ambayo lazima yatekelezwe kwa unyenyekevu, Zaka na sadaka navyo vinapaswa kutolewa kwa kuzingatia kanuni fulani za adabu. Vinginevyo wale wanaotoa sadaka zao hovyo watakumbana na hatima yao huko Akhera sawa na onyo la Mwenyezi Mungu **"ole wao wanaosali..."** (107: 4) kwa wale wanaozipuuza swala zao.

USIPOTEZE SADAKA YAKO

Mola wetu anatuhabarisha kuhusu adabu tunazotakiwa kuzichunga katika kutoa sadaka kama ifuatavyo:

"Wanaotoa mali zao kwa Njia ya Mwenyezi Mungu, kisha hawafuatishii masimbulizi wala udhia kwa walichotoa, wana ujira wao kwa Mola wao Mlezi, wala haitakuwa hofu juu yao wala hawatahuzunika.

Kauli njema na usamehevu ni bora kuliko sadaka inayofuatiliwa na maudhi. Na Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye kujitosha na Mpole.

Enyi mlioamini! Msiharibu sadaka zenu kwa masimulizi na maudhi, kama anayetoa mali yake kwa kuwaonyesha watu, wala hamuamini Mwenyezi Mungu wala Siku ya Mwisho. Basi mfano wake ni kama mfano wa jabali ambalo juu yake pana udongo, kisha likapigwa na mvua kubwa, ikaliacha tupu. Basi hawatakuwa na uweza wowote kwa walivyochuma. Na Mwenyezi Mungu hawaongoi watu makafiri." (2, 262-264)

Katika aya zilizotajwa hapo juu, Mola wetu anatuonyesha njia sahihi tunazotakiwa kuzichunga katika kutoa Zaka na sadaka. Kwa maneno mengine vitendo vya hisani vinavyo-

fanywa kwa unyanyapaa, matusi, na kuwadharau masikini na kuvunja mioyo yao, havina thamani mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Wale wasiofuata kanuni hizi na kutoa sadaka yao kwa moyo wa kipumbavu na baridi huziharibu thawabu zao kwa mikono yao wenyewe.

Kusimulia sadaka na wema siyo tu kwamba husababisha kupoteza thawabu zake, bali pia husababisha kughadhibikiwa na Mwenyezi Mungu.Kuhusu suala hili Mtume ﷺ anasema kwamba;

*"Watu watatu ambao Mwenyezi Munu hatozungumza nao siku ya Kiyama, hatowatazama na wala hatowasamehe na watapata adhabu kali. Mtume ﷺ akairudia mara tatu.*Abu Dharr رضي الله عنه akasema:

"Wamepata hasara na wamepotea; ni watu gani hao ewe Mtume wa Allah?"

Hapo Mtume ﷺ akasema:

"Hao ni: mkokotaji wa nguo ya chini, muuzaji wa bidhaa kwa kiapo cha uongo na yule anayekumbushia wema wake kwa ubaya." (Muslim, Kitab Al-Iman, 171)

Kama tunavyoona, wema usiokuwa na Ikhlas ndani yake na unaofuatiwa na maudhi na unyanyapaa ni miongoni mwa dhambi kubwa ambazo mwenye kuzitenda ataadhibiwa badala ya kupata thawabu. Kwa kuwa nyoyo ni mahali panapotazamwa na Mwenyezi Mungu, hazitakiwi kuvunjwa.

Aidha, zaka na sadaka ambazo Mwenyezi Mungu ameamrisha zitolewe, ni haki ya asili ya masIkini iliyo mikononi mwa matajiri. Kwa hivyo, kuchukua sadaka katika mali ya tajiri na kumpatia masikini haipaswi kuangaliwa kama fadhila ya tajiri kwa masikini bali ni kukabidhi kitu kumpa mwenye nacho. Kusahau ukweli huu na kujaribu kukwepa kufikisha ama-

na ya baraka za Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa waja wake na kuwanyanyasa masikini ni upuuzaji, uchanga na ujinga.

Hivyo basi, hatupaswi kujivunia sadaka zetu, kuwadharau masikini; kinyume chake tunapaswa kujiweka katika daraja yao na kuwaza kuwa siku moja tunaweza kuwa kama wao; kwa sababu hata kama kufanya kazi kwa bidii kuna nafasi fulani katika utajiri au umasikini, kwa kiwango kikubwa ni mambo ya majaliwa.

Mwenyezi Mungu anaweza kumfanya tajiri kuwa masikini na masikini kuwa tajiri. Vitu hivyo (utajiri na umasikini) siyo vipimo vya ubora mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Bali ni nyenzo za majaribu hapa duniani. Ubora wa mtu mbele ya Mwenyezi Mungu hutokana na uchamungu na unyoofu pekee. Kujivuna kuhusu kuwasaidia masikini hutokana na kughafilika juu ya siri za mitihani katika hii dunia.

Sheikh Saadi anasema katika *Bostān* Yake:

"Unapomfanyia wema mtu, usijivunie kwa kusema "mimi ni bwana, yeye ananihitajia." Usiuambie upanga wa zama umkate huyu masikini. Kwa sababu upanga huo bado haujaingia kwenye ala yake. Inawezekana siku moja ukakukata nawe pia."

Matajiri wanatakiwa kujua kujiweka mahali pa masikini na wanatakiwa wawe na uwezo wa kusema: "Mola wetu angeweza kutufanya tuwe wao na wao wawe sisi. Kwa kuwa ametupa baraka zake, hiyo ina maana kuwa ametupa kama amana. Na pia ametupa jukumu la kuwaangalia masikini. Na ametutaka tuwasaidie kama ishara ya kumshukuru."

Kwa mara nyingine ushauri wa Sheikh Saadi katika kitabu hicho hicho ni wa kushangaza sana:

"Masikini akija mlangoni kwako, usimfukuze. Mungu apishe mbali, siku moja unaweza kuwa masikini na ukalazimika kwenda kwenye milango ya watu wengine.

Ulizia hali ya wale wenye nyoyo zilizovunjika. Siku moja unaweza kuwa kama wao.

Kwa kuwa huna lazima ya kwenda kwenye mlango wa mtu, ili kutoa shukrani, usimmkatae masikini anayekuja mlangoni kwako na kutana naye kwa uso wenye tabasamu..."

Kwa hakika aya tukufu ya Qur'an yasema:

"Akakukuta mhitaji akakutosheleza? Basi yatima usimwonee! Na anayeomba au kuuliza usimkaripie! Na neema za Mola wako Mlezi zisimlie." (93; 8-11)

Sehemu muhimu katika kuwafanyia fadhila masikini siyo kuwakumbusha wema huo kwa ubaya vibaya na njia bora ya kulifikia hilo ni kusahau fadhila hizo mara tu baada ya kuzifanya. Lugman al- Hakim analielezea jambo hili kwa uzuri kabisa:

"Usisahau mambo mawili: Mwenyezi Mungu Mtukufu na kifo.

Sahau mambo mawili: fadhila zako kwa wengine na mabaya unayotendewa na wengine."

Kuwa mhisani wa kweli ni baraka kubwa katika dunia hii na kesho Akhera. Wale wanaoweza kutekeleza ibada hii kwa usahihi, kwa mujibu wa habari njema kutoka kwa Mola wetu, hawatokuwa na hofu wala huzuni siku ya hukumu. Ndiyo maana Mwenyezi Mungu na Mtume wetu mpendwa ﷺ katika aya na *hadith* nyingi wanatushajiisha kupata amani na utulivu wa kuwasaidia watu wengine.

Mwenyezi Mungu Mtukufu alituonya, sisi waja wake, kutopoteza baraka hiyo kubwa kama *infaq* na akatuamrisha kuchunga adabu zake.

Muumini ni mtu karimu. Ukarimu wa kweli ni kuwa na uwezo wa kutoa bila hisia ya majuto na bila kusimulia. Kinyume chake ni kuwa na uwezo wa kutoa kwa furaha. Muumini anapaswa awe kama maua, ambayo kwa hiari hutoa harufu yake nzuri. Kwa hivyo basi, ili sadaka yake ipate kukubaliwa kikamilifu mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Aya tukufu inasema kuhusu jambo hili: **"...Mwenyezi Mungu anazikubali sadaka zao"** (9: 104)

Rumi anaelezea baraka za *infaq* iliyotolewa kwa njia nzuri;

"Toa kwa uzuri mali, milki yako na ufanye moyo ufurahike ili kwamba dua za moyo huo zipate kuwa nuru katika kaburi lako, na kuiangaza njia yako katika usiku wenye giza."

Kwa hiyo tusikatae tabasamu la kawaida kutoka kwa masikini, kama tusivyozikataa mali na milki zetu.

Pindi Ramazanoğlu Mahmud Sami (Mwenyezi Mungu aibariki roho yake) alipokuwa akimuona masikini, kama yupo katika gari, angesimamisha gari, akashuka, akatabasamu na kutoa sadaka yake. Ithaar, adabu na huruma zinapaswa kuwa sifa bainishi za Muislamu.

KUTOA SADAKA PAMOJA NA HISIA YA SHUKRANI

Tabia na adabu za Kiislamu zinataka uione sadaka kama baraka. Mtoaji anatakiwa pia amshukuru mpokeaji. Kwa sababu anakuwa amemuokoa mtoaji kutokana na jukumu na kumfanya achume thawabu.

Katika aya moja, imeelezwa kuwa;

"Si juu yako wewe kuwaongoa, lakini Mwenyezi Mungu humwongoa amtakaye. Na kheri yoyote mnayotoa ni kwa nafsi zenu. Wala msitoe ila kwa kutafuta wajihi wa Mwenyezi Mungu. Na kheri yoyote mtakayotoa mtalipwa kwa ukamilifu, wala hamtadhulumiwa." (2: 272)

Hii ina maana kwamba wale wanaotoa ndiyo watakaoona baraka za kweli za wema wao. Kwa hakika atapokea thawabu za wema wake kikamilifu zaidi na zaidi kulingana na kiwango cha Ikhlas yake. Kwa maneno mengine, infaq inaweza kuonekana kama ni fadhila kwa mpokeaji lakini kiukweli ni fadhila kwa mtoaji. Ndiyo maana kwamba mtoaji anatakiwa amshukuru mpokeaji badala ya yeye kushukuriwa.

Upendo wa baba yangu kwa masikini ulikuwa kama bahari kubwa. Wakipokea sadaka yake alikuwa akienda huku akishukuru. Akitoa pesa, alikuwa akiiweka katika bahasha na kuandika juu yake **"ahsante kwa kuipokea."** Alikuwa akifanya kila awezalo kutoumiza hisia zake. Haya ni matokeo ya neema ya kiroho na fadhila za kuwasaidia viumbe kwa ajili ya Muumba wao.

Rumi analielezea jambo hili katika tungo zake za hekima;

"Masikini ni kioo cha fadhila, jihadhari! Usipumue juu ya kioo kwa kusema mambo mabaya kwenye uso wa kioo. [58]

Wito wenye sauti ulimjia (masikioni mwake): "Njoo, ewe mtafutaji! fadhila inamhitaji muombaji: (inahitaji) kama muombaji. Fadhila inawatafuta waombaji na masikini, kama wazuri wanavyotafuta kioo kisafi.[59]

58. Mathnawi, I, 2750
59. Mathnawi, I, 2744-2745

Kwa vile masikini ni kioo cha fadhila, tahadhari! Pumzi huumiza wajihi wa kioo. Kwa upande mmoja, fadhila yake (mtoaji) humfanya muombaji ajitokeze (humfanya aombe), huku kwa upande mwingine yeye (mtoaji), (bila kuombwa), humjaza muombaji (zaidi ya anachohitajia).” [60]

Ndiyo maana inatupasa kuikubali kama baraka mahsusi kutoka kwa Mola wetu pale mtu anapotujia na kuomba msaada wetu. Na tunatakiwa pia kuichukulia fursa hiyo kuwa ni heshima ya utiifu wetu.

Ali ﷺ anaufafanua ukweli huu kama ifuatavyo:

“Kuna baraka mbili ambazo sijui ni ipi kati yake inayonifurahisha zaidi. Moja ni pale mtu anapokuja kwangu na kwa dhati kabisa akaniomba msaada wangu kwa mategemeo kuwa nitamkidhia mahitaji yake. Ya pili ni pale Mwenyezi Mungu Mtukufu anapomsaidia mtu kupitia kwangu. Kumfariji muumini kwa kumuondolea matatizo ni bora kwangu kuliko kuwa na dunia iliyojaa dhahabu na fedha.” (‘Ali al-Muttaqī, Kanz al-Ummāl, VI, 598 / 17049)

Mtoaji wa sadaka akihisi fahari kwa kitendo chake na akatarajia kushukuriwa, basi thawabu na baraka za kitendo chake hicho huharibika. Mtoaji hatakiwi kutarajia chochote zaidi ya radhi za Mwenyezi Mungu. Isisahaulike kuwa kutarajia hata kuombewa dua na kushukuriwa na masikini ni vitu vinavyofifiza na kuharibu Ikhlas ya sadaka.

Katika suala hili, aya ifuatayo iliyoshuka kusifu sadaka iliyotolewa na Ali na fatima ﷺ yatakiwa kuwa mfano mzuri kwa waumini:

“Na huwalisha chakula, juu ya kukipenda kwake, masikini, na yatima, na wafungwa. <u>Hakika sisi tunakulisheni</u>

60. Mathnawi, I, 2748 - 2749

kwa wajihi wa Mwenyezi Mungu. Hatutaki kwenu malipo wala shukrani. Hakika sisi tunaiogopa kwa Mola wetu Mlezi hiyo siku yenye shida na taabu. Basi Mwenyezi Mungu atawalinda na shari ya siku hiyo, na atawakutanisha na raha na furaha." (76: 8-11)

Hali ifuatayo ya akinamama wa umma wa Kiislamu kuhusu kutoa sadaka kwa ajili ya Mwenyezi Mungu tu na kutotarajia chochote kutoka kwa mpokeaji isiyopunguza thawabu za sadaka ni mfano mzuri sana.

Pindi Aisha na Umm Salamah ﵂ wanapotuma kitu kwenda kwa masikini, walikuwa wakimtaka waliyemtuma akumbuke namna mpokeaji alivyowaombea ili nao wamuombee masikini huyo. Walitaka hata kufidia dua za masikini. Kamwe hawakuwa wakitarajia kuombewa na masikini, kwani dua hiyo itaonekana kama ni fidia ya sadaka yao.

NJIA YA KUFIKIA WEMA

Mola wetu anatuonyesha lengo la juu la utumwa wetu katika aya ifauatayo:

"KABISA HAMTAFIKIA wema mpaka mtoe katika vile mnavyovipenda. Na kitu chochote mnachokitoa basi hakika Mwenyezi Mungu anakijua." (3: 92)

"Kutoa katika vile tunavyovipenda" ni tabia tunayopaswa kuichunga katika sadaka zetu. Kwa sababu, umuhimu katika suala hili unaonyesha kiwango cha upendo alionao mja kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Kwa hivyo basi, tunatakiwa kutoa katika vile tunavyovipenda zaidi na ambavyo tukipewa tutavifurahia. Kwa namna hiyo tunaweza kusonga mbele katika njia itakayoifanya sa-

daka yetu iwe kamilifu. Tujiweke katika nafasi ya masikini na pale tunapotoa kitu, tuwaze kuwa kama tungekuwa ndiyo wapokeaji tungefikiria nini. Kwa mara nyingine aya tukufu inatueleza:

"Enyi mlioamini! Toeni katika vile vizuri mlivyovichuma, na katika vile tulivyo kutoleeni katika ardhi. Wala msikusudie kutoa vilivyo vibaya, hali nyinyi wenyewe msingevipokea ila ingekuwa mmefumba macho. Na jueni kwamba Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujitosha na Msifiwa." (2: 267)

Mtu asidhani kwamba atatimiza wajibu wake kwa kumpa masikini vitu visivyo na thamani na vikuukuu. Aina hii ya sadaka haiwezi kuhesabiwa kama ni sadaka ya kweli.

Muumini ni mtu karimu, na ukarimu wa kweli hauweki sadaka kwenye vitu visivyokuwa na thamani na vilivyochoka, bali vitu vya thamani, vyenye manufaa na vinavyopendwa ambavyo vinaweza kutatua tatizo la masikini.

SAIDIANENI KATIKA WEMA NA UCHAMUNGU

Lengo katika kutoa sadaka ni kupunguza kabisa matatizo ya masikini. Bila shaka mtu mmoja peke yake hawezi kufikia lengo hili, kwa sababu kila mtu ana bajeti ndogo yenye kikomo. Ndiyo maana tunatakiwa tusaidiane na kuungana katika kutenda mema. Mwenyezi Mungu anatuambia katika aya ifuatayo:

"...Na saidianeni katika wema na uchamungu..." (5:2)

Kwa maneno mengine kusaidiana katika wema ni amri ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Hii ina maana kwamba tunahitaji kupata umoja na hata kuanzisha taasisi hasa katika huduma, ambayo mtu hawezi kuifanikisha akiwa peke yake.

Katika suala hili, tujaribu kutimiza amri ya Mola wetu ya "Na saidianeni katika wema na uchamungu" kwa kuwashajiisha watu wanaotuzunguka kusaidiana katika mambo ambayo hatuwezi kuyakabili tukiwa peke yetu.

Jambo linalofaa kwa muumini wa kweli ni daima kutafuta njia za kutenda wema. Muumini mwenye kiwango hiki cha dhamiri kama hana cha kutoa, basi anaweza kujitolea muda na nguvu yake. Kwa namna hiyo anaweza kuwa njia ya kufanya wema mkubwa zaidi.

Leo hii hatupaswi kukamatwa na maradhi ya kuzifariji dhamiri zetu kwa kutoa kiasi kidogo, ambacho hakiwezi kutatua tatizo lolote la masikini. Tunahitaji kufikiria ni asilimia ngapi ya baraka za Mola wetu tunayoitoa katika njia yake? Ni upi uwiano wa misaada yetu na kiasi tunachokitoa kwa matumizi yetu wenyewe? Au tunazifariji dhamiri zetu na kiasi kidogo kwa kulinganisha misaada yetu na sadaka ndogo za watu wengine?

Hata hivyo, sisi kama waumini, tunatakiwa tujilinganishe na Mtume wa Allah ﷺ na maswahaba wake watukufu; kwa sababu Mwenyezi Mungu Mtukufu anatuamrisha kuwafanya waja hawa wema kuwa mifano kwetu katika aya ifuatayo:

"Na wale waliotangulia, wa kwanza, katika Wahajiri na Ansari, na waliowafuata kwa wema, Mwenyezi Mungu ameridhika nao, na wao wameridhika naye; na amewaandalia Bustani zipitazo mito kati yake, wadumu humo milele. Huko ndiko kufuzu kukubwa." (9: 100)

Kizazi cha maswahaba, ambacho Mwenyezi Mungu anakileta mbele yetu kama kizazi cha mfano, kililipa thamani ya imani yao kwanza kwa kuadhibiwa katika mji wa Makkah; pili walistahimili na kuvumilia mashambulizi na hujuma za makafiri katika mji wa Madina. Na mwishowe wakabeba nuru ya uongofu na kuufikisha ujumbe wa Uislamu kwa muda mrefu. Walikusanya kila walichokuwa nacho kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Kwa sababu daima waliishi katika kuitaamali na kuitafakari aya ifuatayo:

"Tena bila ya shaka mtaulizwa siku hiyo juu ya neema." (102: 8)

Nasi pia tunatakiwa kukifanya kizazi cha maswahaba kama mfano kwetu na kujaribu kuishi kulingana na misingi mitatu iliyotajwa hapo juu.

MWENYE KUJULISHA KHERI NI KAMA ALIYEIFANYA

Tunatakiwa kuhakikisha kuwa sadaka zetu zinatatua tatizo la jamii. Na kama sisi wenyewe hatuwezi kulitatua, basi tutafute watu wengine kwa kuwaza *"Je ninaweza kumpata mtu anayeweza kumsaidia huyu masikini?"* badala ya kusema "*nifanye nini sasa? Hiki ndicho ninachoweza kufanya."* Kwa namna hiyo tunaweza kuwa daraja linalowaunganisha watu masikini na wale wenye fursa za kuwasaidia.

Kwa sababu Mtume ﷺ anasema:

"Wale wanaosababisha jambo la kheri kufanyika ni sawa na wale waliolifanya." (Tirmidhi, 'Ilm, 14)

Kwa sababu ya ukweli huu, Marafiki wa Mwenyezi Mungu huwahamasisha watu kufanya wema ili waweze kuwa sehemu ya wema wao. Kuhusu suala hili mfano wa mwalimu wa Sultan Mehmed, Akşemseddîn ni wa muhimu sana:

Ijumaa ya kwanza baada ya kuifungua Istanbul, kulikuwa na gwaride la ushindi na ufunguzi katika uwanja wa Ok mraba Meydani. Baadaye Sultani Mehmet, ambaye kamwe hakusahau msaada wa watu wa karibu naye, alisema kuwa:

"Rehma iwe juu ya Mashahidi wetu, utukufu na heshima ziende kwa maveterani wetu na sifa na shukrani kwa watu wangu ..." akawagawia zawadi, mali, na ardhi kwa askari na raia laki moja na elfu sabini waliokuwa naye. Baada ya hapo kiongozi wake wa kiroho Akşemseddîn akawausia maveterani kama ifuatavyo:

"Enyi maveterani! Mnapaswa kujua kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu aliwaita kama "askari wa ajabu ..." natumaini nyote ni wenye kusamehewa na Mwenyezi Mungu Mtukufu. Sasa msipoteze mali zenu na zitumieni katika mambo mema. Mtiini Sultan wenu na mumpende... "

Hivyo alitaka kuimarisha nguvu ya jeshi la ushindi kwa nguvu nyingine na kuwahamasisha kuujenga mji na kuwasaidia wakazi wa mji huo. [61]

Sisi ni dhuria wa umma mkubwa, ambao umezalisha ustaarabu wa sifa na tabia njema. Mpaka leo hii tunaishi katikati ya kazi zao njema kama vile wakfu, visima, nyumba za kheri n.k Tunapaswa kuzilinda kazi zao na kujaribu kuzalisha kazi mpya za hisani zinazofanana na zao. Awali ya yote tunahitaji kuupamba ulimwengu wetu wa ndani kwa sifa na tabia njema; na kisha tunahitaji kulea vizazi vipya vitakavyokuwa na imani

61. Tazama Ayverdi, Samiha, Turk Tarinde OSMANLI ASIRLARI, Istanbul 1999, uk. 227 - 228.

na viweze kulinda kazi za wahenga wao. Vinginevyo, Uislamu utapoteza nguvu zake, vizazi vitapotea na hata taifa letu kubadilika. Tunapaswa kuwa waumini wahisani na wanaotambua majukumu na wajibu wao.

Kwa muhtasari, muumini mhisani ni mtu anayetanguliza shida za wengine mbele ya shida yake. Yeye pia ni mtu anayejua kwamba kupata wokovu wa milele kesho katika mahakama ya Mwenyezi Mungu kunataegemea katika kuwasaidia wengine; kwa sababu, Mola wetu ametukataza kuwa wabinafsi, wakaidi na mabakhili. Kuhusu suala hili, hatupaswi kusahau kuwa mtihani wetu utakuwa rahisi kulingana na hisia zetu za kuwajibika mbele ya watu wengine.

Tunamuomba Mola wetu atupe baraka ya msukumo wa kuishi kwa ajili ya dini yetu. Ajaalie katika nyoyo zetu mapenzi ya kuwasaidia wengine kwa ajili Yake. Ayafanye matendo yetu ya hisani yaendane na kanuni za tabia njema.

Amin...

USAFI WA MOYO KATIKA KUTOA

Kuna kanuni ya mvuto katika pesa, ambayo hubadilika kulingana na ilivyochumwa. Pesa ni kama nyoka. Huenda katika shimo ilikotokea. Chumo la halali ni nyenzo ya kutekeleza mambo mema, wakati chumo la haramu huyeyuka na kutoweka kwa ajili ya mambo maovu. Hivyo tunaweza kuelewa pesa zinachumwa kutoka wapi na zinatumika wapi.

Hali yetu ya kiroho huathiriwa na mambo mawili:

1. Vyakula vya halali au vya haramu na hata vile vyenye shaka.

2. Tabia na shakhsia za watu wanaosuhubiana na sisi.

USAFI WA MOYO KATIKA KUTOA

Usafi wa moyo una maana ya Ikhlas katika utumishi na usafi wa nia. Uchamungu na Ikhlas ni siri za utumishi ambazo haziwezi kutenganishwa.

Ni kama maneno mawili yenye maana moja. Ni muunganо wa mja na Mola wake ndani ya moyo wa mja. Kwa maneno mengine, ni dhihirisho la sifa kama vile rehema, huruma, msamaha, na ulaini wa moyo. Ni hali ya mja kumtafuta Mwenyezi Mungu katika kila hali, katika kila tabia, hata katika kila pumzi.

Nyoyo zenye upungufu wa Ikhlas huanza kusikiliza na kufuata matama nio ya nafsi. Kilele cha kufuata huku ni upumbavu wa kuabudu kitu kingine zaidi ya Mwenyezi Mungu Mtukufu hata kama ni kwa moyo tu. Hili limeelezwa katika aya ifutayo:

“Je! Umemwona aliyeyafanya matamanio yake kuwa ndiyo mungu wake? Basi je, wewe utakuwa ni wakili wake?” (25; 43)

Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ anaelezea matokeo yenye kuhuzunisha ya ukosefu wa Ikhlas katika matendo kama ifuatavyo:

"Ninachohofia zaidi kwa ummah wangu ni kumshirikisha Mwenyezi Mungu Mtukufu. Siyo kwamba wataabudu mwezi au jua. Kinachonihofisha zaidi ni matendo yatakayotekelezwa kwa malengo mengine tofauti na kutaka radhi za Mwenyezi Mungu na furaha zilizojificha (hisia za ubatili" (Ibn Majah, Zuhd, 21)

Kwa hiyo, ibada inayotekelezwa kwa nia ya kujifaharisha, kujionyesha au kwa lengo lingine tofauti na kutaka radhi za Mwenyezi Mungu haiwezi kuleta manufaa yoyote ya kiroho. Inakuwa ni harakati za bure tu za mwili. Kama anavyosema Mtume ﷺ:

"Thawabu ya matendo hutegmea nia na kila mtu atapata thawabu kulingana na kile alichonuia." (Bukhari, Iman, 41)

Kama ilivyo katika ibada zote, ikhlas (usafi wa moyo) ni muhimu sana katika kutoa sadaka. Sadaka inatakiwa kutolewa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu tu. Mtume wa Mwenyezi Mungu anasema kuwa:

"Mtu akitoa sadaka inayolingana na tende kutokana na chumo la halali; kwa maana Mwenyezi Mungu hupokea kilicho halali, ataipokea kwa Mkono Wake wa Kuume, na hata kama ni tende, itaendelea kukua mikononi mwa Mola, kama mnavyokuza mtoto, mpaka ikawa kubwa kuliko mlima." (Muslim, Kitab al-Zaka, 63)

"Hakika sadaka hupokelewa na Mwenyezi Mungu kabla haijapokelewa na mpokeaji." (Munāwī, Kunūz al-Haqāiq, uk. 34)

Kwa maneno mengine Mwenyezi Mungu Mtukufu anakuwa mhusika halisi wa sadaka. Hii ndiyo sababu kwamba kuwa na moyo wa dhati ni jambo muhimu sana katika matendo ya uhisani. Inatakiwa kutoa sadaka bila kutarajia kupata chochote kutoka kwa kiumbe na useme "Mola wangu, nimetoa hii ni kwa ajili yako tu." Huu ndiyo msingi mkuu wa kutoa sadaka.

ALAMA YA IKHLAS: KUMTAFUTA MHITAJI WA KWELI

Kujaribu kumpa sadaka yule anayestahiki kweli ni adabu muhimu ya *infaq*. Kwa maneno mengine, badala ya kuchagua njia rahisi na kuitoa bila mpangilio, tunatakiwa kuhisi kwamba ni ibada na tufanye juhudi kama ilivyoelezwa katika aya ifuatayo;

"...Na ambao wanatoa Zaka..." (23: 4)

Kama tunavyokuwa makini wakati wa kununua kitu kipya, tunatakiwa kutumia muda na nguvu hiyo hiyo katika kumtafuta mstahiki wa kweli wa sadaka yetu. Kwa sababu *infaq* ni muamala wa kiroho, ambao ndani yake tunatoa katika vile tulivyobarikiwa na Mola wetu na mbadala wake tunapata baraka za akhera zisizokuwa na kikomo. Na utekelezaji bora wa muamala huu hupatikana kwa kumtafuta mhitaji wa kweli. Hili pia huonyesha kiwango cha Ikhlas na usafi wa moyo katika sadaka yetu.

Tumeamrishwa katika aya ya Qur'an kumtafuta mhitaji wa kweli kama ifuatavyo:

"Na (kutoa huko) wapewe mafakiri waliozuilika katika njia za Mwenyezi Mungu, wasioweza kusafiri katika nchi kutafuta riziki. Asiyewajua hali zao huwadhania kuwa ni matajiri kwa sababu ya kujizuia kwao. <u>Utawatambua kwa alama zao</u>; hawang'ang'anii watu kwa kuwaomba. Na kheri yoyote mnayotoa, basi kwa yakini Mwenyezi Mungu anaijua." (2: 273)

Kwa maneno mengine, kuwapa sadaka watu wanaostahiki hueneza usikivu katika moyo na kuuwezesha kuwatambua wahitaji wa kweli kwa nyuso zao.

Imeelezwa katika hadith nyingine kuwa:

"Masikini siyo yule anayeomba kipande kimoja au viwili kutoka kwa watu, bali masikini ni yule asiyekuwa na kitu na ni mwenye kuona aibu kuwaomba watu." (Bukhari, Kitab al-Zaka, 53)

Rumi anatoa ushauri ufuatao katika suala hili:

"Nenda na utafute moyo! Mhudumie mnyonge. Mlinde mnyonge na aliyevunjika moyo. Hao ndiyo watu ambao hawachumi kutoka kwa watu wengine. Lakini, wana utulivu kamili wa moyo. Watafute na uwapate."

Tabia bora ya kweli ni kushikilia mikono ya wale wanaohitaji. Kwa maneno mengine kuwatafuta masikini ambao hawawezi kuomba kwa sababu ya staha na kuwatambua kupitia nyuso zao ni amri ya Mola wetu. Bila shaka kufikia aina hii ya utambuzi hutegemea chakula chetu ni halali kwa kiwango gani na nguvu ya Ikhlas iliyo katika nyoyo zetu.

Sadaka inayotolewa kutokana na chumo halali, na ikatolewa kwa hiari kwa ajili tu ya Mwenyezi Mungu Mtukufu haitopotea; kwa hakika Mwenyezi Mungu ataifikisha kwa wale wanaostahili kuipata.

Kumsaidia mtu mmoja anayestahiki kusaidiwa wakati mwingine ni sawa na kuwasaidia maelfu ya watu; kwa sababu kutoa kiwango kikubwa kumpa mtu huyo haitohesabiwa kuwa ni ubadhirifu.

Mtume ﷺ alitoa umuhimu maalumu kwa maswahaba masIkini wajulikanao kama "As-haab al-Suffah" na akawahamasisha maswahaba wenye mali kuwasaidia.

Rumi anasema kuhusu nani na wapi tunapotakiwa kutoa sadaka zetu:

“Uadilifu ni nini? Kuipa miti maji. Dhulma ni nini? kuipa miiba maji.” [62]

Kwa hiyi tunatakiwa kuwa makini kuhusu kila kinachopewa uhai na sadaka zetu, kama ni bustani la hali ya kiroho au miiba ya ubinafsi.

Thamani ya infaq hutegemea uhalali wa mali husika. Kwa idhini ya Allah Mtukufu, sadaka inayotolewa katika mali halali itaangukia katika fungu la anayeistahiki kweli. Kwa hali hiyo sadaka huwa ni aina ya mashine ya x-ray ya mapato yako.

Mwanafunzi mmoja mwenye mali wa Abu Abbas Nihāwandī alikuja kwake na kumuuliza kuhusu mtu anayetakiwa kumpa sadaka yake. Akajibu:

“Mpe yule ambaye moyo wako unahisi kuwa anastahiki.”

Baada ya kuondoka, mwanafunzi huyo alikutana na kipofu aliyekuwa akiomba msaada. Akadhani kuwa ni mtu anayefaa kumpa sadaka yake. Hivyo basi akachukua mfuko wa dhahabu na kumpa kipofu huyo. Baada ya kipofu kuliangalia begi na kuona lina dhahabu aliondoka akiwa mwenye furaha.

Siku ya pili alipopita jirani na eneo hilo, akamuona yule kipofu aliyempa sadaka yake akizungumza na kipofu mwingine. Alikuwa akisema:

“Jana, mtu mmoja alinipa mfuko wa dhahabu nikaenda kwenye kilabu cha pombe na kunywa.”

Mwanafunzi alifadhaishwa na hali hiyo. Akaenda haraka kwa mwalimu wake, Abu Abbas Nihāwandī. Kabla ya kumwambia kilichotokea, Abu ‘Abbas akampa sarafu ya fedha na kumwambia aitoe sadaka kwa mtu wa kwanza atakayekutana naye njiani.

62. Mathnawi, V, 1089

Mwanafunzi akaondoka kwa ajili ya kutekeleza amri ya mwalimu wake kabla hajamuelezea tatizo lake. Akafanya kama mwalimu wake alivyomwambia afanye na kumpa pesa mtu wa kwanza kukutana naye.

Lakini akataka kufanya udadisi kuhusu mtu huyo na hivyo akaanza kumfuata. Baadaye yule mtu akaingia kwenye jengo lililotelekezwa kisha akatoa ndege aliyekufa kwenye nguo zake na kumuacha sakafuni. Alipoanza kuondoka, mwanafunzi akatokezea mbele yake na kumuuliza:

"Bwana, kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, naomba unifafanulie yote haya yanayotokea. Huyu ndege mfu ni wa nini?"

Masikini huyo alipomuona mtu aliyempatia pesa, akashikwa na hofu na kuanza kuzungumza kwa kigugumizi:

"kwa muda wa siku saba sikuweza kupata kitu cha kuwalisha wanangu. Mimi na mke wangu tumekuwa tukivumilia lakini watoto wetu hawana nguvu tena za kuvumilia njaa. Lakini ingawa tulikuwa katika hali hiyo, niliona soni kuomba omba na kuwataka watu wanisaidie. Ndipo nilipopata huu mzoga wa ndege ambaye ni kama ameoza. Nilipanga kuwapelekea wanangu. Kwa upande mwingine nilikuwa namuomba Mola moyoni mwangu aniokoe. Ndipo ulipokuja na kunipa hii sarafu ya fedha. Nilimshukuru Mola wangu na kuja hapa kuutupa huu mzoga wa ndege. Na sasa nitakwenda sokoni kuwanunulia chakula wanangu...."

Mwanafunzi akachanganyikiwa na kurudi kwa mwalimu wake. Kabla ya kusema chochote, Abu 'Abbas Nihāwandī akamwambia:

"Mwanangu, inaonekana kwamba kabla ya kutoa sadaka yako, hukuzingatia wapi ulipoipata pesa yako. Ndiyo maana, pamoja na kwamba ulijaribu kumtafuta mtu sahihi, sadaka

yako ilitumika kwenye pombe; kwa sababu chumo hutumika kutegemeana na jinsi lilivyopatikana. Kwa sababu ya sarafu yangu ya fedha kuwa halali ilipata mtu sahihi, lakini begi lako la dhahabu lilikwenda kwa mtu asiyestahili..."

Kwa maneno mengine, upatikanaji wa mtu sahihi wa kupokea sadaka yetu una uhusiano na mahali tulipozipata mali zetu. Kana kwamba kuna kanuni ya uvutano katika pesa, ambayo hubadilika kulingana na ilivyochumwa. Pesa ni kama nyoka. Huenda katika shimo ilikotokea. Chumo la halali ni nyenzo ya kutekeleza mambo mema, wakati chumo la haramu huyeyuka na kutoweka kwa ajili ya mambo maovu. Hivyo tunaweza kuelewa pesa zinachumwa kutoka wapi na zinatumika wapi.

Upande wa kiroho wa infaq hujionyesha waziwazi. Ni kwa sababu ya uhalali wa mali na Ikhlas ya moyo ambayo kwa baadhi ya watu sadaka huwapa utulivu kamili wa moyo.

Jambo jingine muhimu ni kwamba Uislamu unahamasisha kutoa sadaka pale inapowezekana. Kama tukiweza kutoa sadaka yetu kwa moyo safi, basi Mwenyezi Mungu atajaalia baraka zake juu yetu. Wakati mwingine hata kama sadaka yetu yaonekana kama haikupewa kwa mtu sahihi, inaweza kumfanya mtu huyo aamke kutoka usingizini mwake na kuitafuta njia sahihi ya Uislamu.

Mtume ﷺ analiashiria hili katika hadith yake. "Mtu mmoja alionyesha nia yake ya kutoa sadaka, hivyo akatoka na sadaka yake na kuiweka mikononi mwa mwanamke mzinifu. Asubuhi watu wakawa wakijadiliana na kusema: usiku wa wa jana sadaka ilitolewa kwa mzinifu. (mtoaji wa sadaka) akasema: Ewe Mwenyezi Mungu, himidi ni zako, sadaka yangu ilikwenda kwa mzinifu. Kisha kwa mara nyingine akaonyesha nia yake ya kutoa sadaka; hivyo akaenda na sadaka yake na

kumpa mtu tajiri. Asubuhi watu wakawa wanazungumza na kusema kuwa: tajiri kapewa sadaka. Akasema: “Ewe Mwenyezi Mungu, himidi ni zako, hakika sadaka yangu imekwenda mikononi mwa mtu tajiri.”

Baada ya hapo akaonyesha nia yake ya kutoa sadaka, akatoka na sadaka yake na kumpa mwizi. Asubuhi, watu wakawa wanazungumza na kusema: mwizi kapewa sadaka. Hivyo (mmoja wa watu hao) akasema:

“Ewe Mwenyezi Mungu, himidi ni zako (bahati mbaya iliyoje kwa sadaka kupewa) mwanamke mzinifu, mtu tajiri na mwizi!”

Hapo (malaika akaja) na kumwabia:

“Sadaka yako imepokelewa. Kuhusu mwanamke mzinifu (sadaka hiyo yaweza kuwa njia) ambapo anaweza kuachana na uzinifu. Mtu tajiri huwenda akajifunza na kutoa katika kile alichoruzukiwa na Mwenyezi Mungu, na mwizi anaweza kuacha wizi.” (Bukhari, Kitab AL-Zaka, 14, Muslim, Kitab AL-Zaka, 78).

Tunaona tukio kama hilo katika maisha ya Ramazanoğlu Mahmud Sami. Siku moja alipokuwa ziarani katika mji wa Anatolia, mtu mmoja alisimamisha gari lake na kuomba fedha ya sigara. Hata kama rafiki zake hawakubaliani naye, anasema:

“Kwa kuwa ameomba, tunatakiwa kumpa fedha” na bila wasiwasi akatoa pesa huku marafiki zake wakitazama kwa mshangao. Masikini huyo alifurahishwa na kile alichokiona akasema:

“Sasa nitakwenda kununua chakula kwa pesa hii” akaondoka akiwa ni mwenye furaha.

Huu ni mfano mzuri unaoonyesha jinsi sadaka iliyotolewa kwa moyo safi inavyoweza kuwa na athari chanya kwa

masikini. Itakuwa furaha kubwa kwetu kama tukianza kabisa kufikiria hisia za masikini badala ya hisia zetu.

Hii ndiyo sababu kwamba Sheikh Sadi anatoa onyo lifuatalo:

"Usiweke uhisani na sadaka yako katika mfuko na kuufunga. Usikatae kutoa hisani yako kwa mtu. Usiseme "huyu ni mnafiki, huyu ni mdanganyifu." Waache wawe wanavyotaka. Ni kitu gani kwako?"

KAMA UNA NIA YA DHATI, MWENYEZI MUNGU ATAKUJAALIA BARAKA ZAKE

Mwenyezi Mungu Mtukufu hukiongeza kile kidogo kilichotolewa kwa moyo safi. Huwalipa waja thawabu kubwa kwa matendo yao madogo. Hii ndiyo maana kwamba sarafu moja inayotolewa kwa moyo safi ina thamani kubwa kuliko mamia ya sarafu yanayotolewa bila moyo wa dhati. Kwa maneno mengine, kiwango cha sadaka siyo muhimu, bali jambo muhimu ni pale inapolinganishwa na mali ya mtoaji, ina uwiano gani na kama imetolewa kwa Ikhlas na kwa nia ya dhati. Mtume wa Mwenyezi Mungu anasema kuhusu suala hili:

"Nia ya muumini (lengo na usafi wake wa moyo) ni muhimu zaidi kuliko matendo yake." (Şuyūtī, Jami 'al-Saghīr, II, 194)

Hii ndiyo sababu kwamba amali ndogo huwa kubwa inapotekelezwa kwa Ikhlas na sadaka ndogo huwa ni fidia ya dhambi za mtoaji. Hilo linapatikana katika hadith ifuatayo ya Mtume ﷺ:

"Mtu mmoja alikabiliwa na kiu kali akiwa safarini, akaona kisima. Aliteremka kisimani na kunywa kisha akatoka nje na

kumuona mbwa ameupinda ulimi wake kutokana na kiu na huku akila udongo laini. Mtu huyo akasema;

"Mbwa huyu ameteseka na kiu kama nilivyoteseka."

Akateremka kisimani, akajaza maji kwanye kiatu chake, akakishikilia kwa mdomo wake mpaka akapanda juu na kumnywesha mbwa. Hivyo Mwenyezi Mungu akakitambua kitendo hiki na kumsamehe dhambi zake. Hapo (maswahaba waliokuwa karibu naye) wakasema:

"Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, tunapata thawabu hata kwa (kuwahudumia) wanyama kama hao? Akasema:

"Ndiyo kuna thawabu kwa kumhudumia kila kiumbe hai."

Hapa amali ndogo iliyofanywa kwa Ikhlas imemuokoa mtu kutokana na moto, wakati katika hadith nyingine, mwanamke muumini wa dini lakini mwenye ukatili alikwenda motoni kwa sababu ya kumuacha paka wake afe kwa njaa. (Angalia Muslim, Kitab al-Salam, 151-153)

Ndiyo maana, ili kuwa waumini kamili, tunatakiwa kufanya juhudi kwa Ikhlas kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, na kufanya kila amali nzuri tunayoweza bila kujali udogo wake. Tunatakiwa kuwanyooshea mikono yetu ya huruma hata wanyama na mimea na kufikia uwezo wa kuwaangalia kupitia jicho la Mwenyezi Mungu.

Ishara nyingine ya baraka za sadaka ni urefu wa muda wa huduma wa taasisi ya hisani. Taasisi zinazoanzishwa kwa Ikhlas kwa vipato halali zitadumu sana kwa sababu ya umadhubuti na uimara wa misingi yake.

Kuhusu hili tunaweza kutoa mfano wa msikiti wa Suleymaniye na majengo yake, ambao umekuwa ukiwahudumia watu kwa karne nyingi. Muasisi wa eneo hili, Sultan Suleiman,

alikuwa mtu mwema, ambaye alikuwa mwenye kujali haki za watu. Alijaribu kuwa mtawala mwadilifu. Msingi wa eneo hili, ulioanzishwa na Sheikh al –Islam Abussuud Efendi, ulipokamilika, Sultan alitaka watu wote waliofanya kazi katika kulijenga wakusanyike. Baada ya kutoa shukrani zake kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu alisema maneno yafuatayo:

"Ndugu zangu katika Uislamu! Kwa idhini ya Allah tumekamilisha jengo hili. Ikiwa kwa bahati mbaya au wa kusahau kuna mtu ambaye hajalipwa kwa kazi yake, tunamuomba aje na achukue sasa hivi. Huenda kuna wale ambao hawapo sasa hivi, ninawaomba muwape taarifa waje kuchukua haki zao..."

Katika ujenzi wa msingi wa jengo hili palikuwepo pia na wanyama kama vile farasi na punda ambao walikuwa wanafanya kazi. Utaratibu wa kuwapumzisha na kuwapa chakula ulizingatiwa.Uangalifu mkubwa wa kutovunja haki ya kiumbe yeyote ulishadidiwa. Huenda hali ya kiroho ya jengo hili la Suleymaniye imo ndani ya siri ya uangalifu na umakini huu.

Sinan ndiye aliyekuwa mhandisi wa jengo hili adhimu. Naye pia alikuwa mtu mwema. Alikuwa mwangalifu sana wale wasiokuwa wasafi wasihusike kuweka tofali. Ndiyo maana msitari ufuatao ukawa ndiyo msemo maarufu miongoni mwa umma:

"Suleymaniye ni ya Sultan Suleiman; Sinan ndiye mjenzi na imani ndiyo udongo wake..."

Wakati wa sherehe za ufunguzi wa jengo, Sultan alisema kuwa: "Sinan ndiye atakayeufungua msikiti huu ili utoe huduma, kwa sababu amefanya kazi kubwa katika kuukamilisha." Sinan Mhandisi akajibu:

"Sultan wangu, mwana-kaligrafia Karahisārī apewe heshima hii, alipoteza macho yake wakati akifanya kazi za kalig-

rafia za msikiti huu...” Hivyo Karahisārī akafungua jengo hilo kwa ajili ya kuanza huduma.

Unapotembelea Suleymaniye, unahisi hali ya kiroho iliyopenya ndani ya jengo. Ndani ya msikiti kuna giza kidogo, ambalo humpeleka muumini kwenye ulimwengu wa ndani wa kiroho. Ni mfano wa maji matakatifu. Mawe na udongo wake vina hali tofauti ya kiroho. Huu msikiti huuakisi Uislamu katika maada. Ni kama mwanadamu aliye kimya, anayeelezea mambo kwa ukimya wake.

Athari za kiroho za msikiti huu juu kwenye saikolojia ya binadamu ni rahisi kuonekana. Hata watalii wa dini mbalimbali roho zao hupata pumziko ndani ya mazingira ya utulivu na amani ya msikiti wa Suleymaniye.

Hizi ni baraka zitokanazo na juhudi zenye Ikhlas za waasisi wa jengo hili. Kwa zaidi ya karne tano, limeendelea kuwa salama na imara licha ya matetemeko mengi ya ardhi.

MKONO WA KUSHOTO USIJUE KINACHOTOLEWA NA MKONO WAKO WA KULIA

Sadaka isiyotolewa kwa moyo wa dhati, kutokana na ubatili wake, haina thamani ya kiroho. Hatari kubwa zaidi kwa mtoaji katika suala hili ni kwamba anajifikiria yeye katika sadaka yake. Kwa namna hiyo huifunika sadaka yake na mawazo ya kidunia. Njia mujarabu ya kumuokoa mtu dhidi ya maradhi hayo ya kiroho ni “kuzingatia usiri katika sadaka.”

Qur’an Tukufu inasema:

“Mkizidhihirisha sadaka ni vizuri; na mkizificha mkawapa mafakiri kwa siri basi hivyo ni kheri kwenu, na yata-

kuondoleeni baadhi ya maovu yenu. Na Mwenyezi Mungu anazo habari za mnayo yatenda." (2: 271)

Mtume ﷺ anasema:

"Mwenyezi Mungu huziandika thawabu za usiri wa amali njema ambayo mja ameifanya kwa siri. Akiifanya kwa uwazi, Mwenyezi Mungu huiandika katika matendo aliyoyatenda kwa uwazi. Iwapo mja atasema kuwa amefanya amali fulani, basi amali hiyo huandikwa katika kitabu cha unafiki.".(Ghazalī, Ihyā 'Ulūm Al-Din, I, 595)

Sehemu nyingine, kwa mujibu wa aya na hadith mbalimbli za Mtume ﷺ, wale wanaotoa sadaka zao kwa siri watakuwa miongoni mwa wale waliosamehewa dhambi zao na wale watakaokuwa chini ya kivuli cha Mwenyezi Mungu siku ambayo hapatokuwa na kivuli kingine. (Tazama Qur'an 2: 271 na Bukhari, Adhān, 36)

Hata hivyo, wakati mwingine huenda kukawa na faida katika kufanya *infaq* kwa uwazi. Kwa kufanya hivyo watu wanaweza kuhamasika kutoa sadaka. Kwa hakika, wafasiri na wachambuzi wameitafsiri aya isemayo "**Mkizidhihirisha sadaka ni vizuri; na mkizificha mkawapa mafakiri kwa siri basi hivyo ni kheri kwenu"** (2: 271) kwamba Zaka inatakiwa kutolewa kwa dhahiri ili kuwahamasisha watu, na aina nyingine zote za sadaka zinatakiwa kutolewa kwa siri.

Kwa muhtasari, *infaq* inatakiwa itolewe kwa dhahiri au kwa siri kutegemeana na mazingira yanavyobadilika. Kama mtu ataweza kutunza usafi wa nia yake, basi hakuna tatizo kuitoa kwa dhahiri. Inaweza kuwa bora pia kuitangaza kama njia ya kuhamasisha watu kutoa sadaka. Msingi mkuu katika njia zote mbili ni kuujenga moyo dhidi ya unafiki na ubatili, na kuimarisha uchaji na usafi wa moyo.

Kutoa sadaka kwa uwazi kunaweza kusababisha staha ya mpokeaji kudhoofika, na wakati mwingine wanaweza kuweka matarajio ya kuendelea kupokea sadaka, jambo litakalodhoofisha juhudi zao na kupoteza utashi wa kufanya kazi. Sadaka ya wazi pia ina hatari mbili: inaweza kumpeleka mtu kwenye ubatili na kuna uwezekano kwa mpokeaji kuumia. Katika hali hiyo, itakuwa bora kutoa sadaka kwa siri.

Kutokana na hali hiyo, inapofika usiku Omar ﷺ alikuwa akibeba mfuko wa unga mgongoni kwake na kuupeleka katika maeneo ya watu maskini mjini. Wakati wa kuwasaidia maskini, alikuwa hafichui utambulisho wake, na alikuwa akiwafurahisha.

Kila usiku, mjukuu wa Ali ﷺ, Imam Zayn al-Abidin alikuwa akibeba kiroba cha chakula mgongoni mwake na kukiacha mlangoni mwa masikini na kisha huondoka bila wao kujua kama yeye ndiye aliyekwenda. Asubuhi ya siku moja masikini wa mji wa Madina hawakuona viroba vya chakula mbele ya milango yao.

Baadaye wakazi wa Madina wakasikia kuwa Imam Zayn al-Abidin amefariki dunia.Wakati wa kumuosha, watu wakaona sugu mgongoni mwake. Walipotafuta sababu ya sugu hizo, wakagundua siri yake. Sugu hizo zilitokana na kubeba viroba vya chakula. [63]

Hisia hii inaweza kuonekana vyema katika amali ya wakfu ya Sultan Mehmed II:

“Mimi, mfunguzi wa Istanbul na mtumwa mnyenyekevu Sultan Mehmed, nimetoa wakfu vyumba 136 katika eneo la Taşlik la Istanbul, ambavyo nilivinunua kwa mali yangu, kwa masharti yafuatayo:

63. Tazama Ibn Kathir, *al-Bidāyah*, IX, 112, 122; Abū Nuaym, *Hilyah*, III, 136.

Kwa mali zilizotajwa hapo juu, nimewateua watu wawili kwa kila mtaa wa Istanbul. Watu hawa watapita katika mtaa na ndoo ya majivu na ndimu, wataondosha mate ya watu kwa majivu na ndimu. Watapata akchas 20 kila siku kwa kazi yao.

Aidha, mimi nimeteua madaktari 10 wa upasuaji, madaktari 10 na matabibu (orderlies) 3 watakaoshugulikia majeraha ya watu. Watakwenda katika siku maalumu za mwezi, na watagonga mlango wa kila mtu bila kubagua. Watachunguza iwapo kuna mgonjwa yeyote, na kama yupo, watamsaidia. Kama hawana tiba kwa ugonjwa husika, watamchukua mgonjwa na kumpeleka hospitali ya Dar al-Ajaza bila malipo yoyote.

Kama ikitokea tukawa na njaa. Katika hali hiyo, silaha 100 zitatolewa kwa wawindaji. Watakwenda kuwinda wanyamapori isipokuwa wakati wa msimu wa kuatamia mayai na wakati wakiwa na watoto katika milima ya Balkan, hivyo wataendelea kuwapatia chakula wagonjwa.

Aidha, familia za mashahidi na watu masikini wa Istanbul watakula katika mgahawa maalumu wa wakfu wangu. Kama hawakuweza kuja kwenye mgahawa maalumu wao wenyewe, watapelekewa chakula majumbani mwao wakati wa giza bila mtu yeyote kujua ....”

Kama inavyoonekana kutokana na tendo hili, Sultan Mehmed aliweka kanuni kadhaa nzuri za namna ya kuwasaidia watu masikini.

Mababu zetu walikuwa wakiweka sadaka zao ndani ya bahasha na kuziacha chini ya jiwe la kuwekea sadaka msikitini; watu wenye shida walikuwa wakienda na kuchukua kiasi wanachohitaji bila kukutana na mtoaji wa sadaka hiyo. Kwa kufanya hivyo, mtoaji hakuhisi fahari na wala nyoyo za wapokeaji hazikuumizwa.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu atufanye sisi wote kuwa waja wema wanaotekeleza matendo yao kwa Ikhlasi na nia safi. Tunamuomba atupe baraka ya kupata fungu kutoka katika sifa njema za maswahaba, marafiki wa Mwenyezi Mungu na waumini wema.

Amin...



ITHAAR - KUWATANGULIZA WENGINE

Ithaar au kuwatanguliza wengine, ni kipimo cha upendo na mahaba. Watu hujitolea mno kwa ajili ya wale wanaowapenda.

Upendo wa Mwenyezi Mungu unahitaji kujitoa kwa dhati. Unaweza kufikiwa tu kwa kuacha mapenzi ya kidunia. Pindi upendo unapofikia kwenye ukamilifu wake, hali ya kujitolea kwa ajili ya unayempenda hufikia kilele chake. Kwa kufanya hivyo, maumivu hubadilika kuwa raha na furaha.

Heshima na utu wa muumini ni kuwa huitanguliza amani na furaha ya ndugu zake katika Uislamu kabla ya furaha yake mwenyewe. Kwa maneno mengine, hupiga hatua kutoka kwenye ubinafsi kwenda kwenye ithaar na anaweza kusema “Wewe kwanza” au “yeye kwanza” badala ya “Mimi kwanza.”

ITHAAR - KUWATANGULIZA WENGINE

Ithaar, ambayo ni kilele cha kujitolea na ukarimu, ni tabia na sifa maalumu ya mitume na marafiki wa Mwenyezi Mungu. Ina maana ya kuwa na uwezo wa kujitolea, kuachana na haki yako mwenyewe, na kuwapa wengine kitu ambacho wewe mwenyewe wakihitajia. Ina maana ya mtu kufikiria amani na furaha ya ndugu zake katika Uislamu katika mazingira na hali yoyote ile. Kwa maneno mengine, mja hutoka kwenye hali ya umimi kwenda kwenye kuwatanguliza wengine, na kuweza kusema **"wewe kwanza**" au badala ya kusema "**mimi kwanza**".

Hakim Tirmidhi anatoa jibu lifuatalo kuhusu swali la **"infaq ni nini?"**

"Infaq ni kutafuta amani kwa kuwafurahisha wengine."[64]

Sababu kubwa inayowapeleka marafiki wa Mwenyezi Mungu tabia hii njema ni sifa yao ya huruma. Daima huishi kwa mujibu wa ujumbe wa Mwenyezi Mungu unaopatikana katika aya isemayo: **"Hakika Waumini ni ndugu**..." (49: 10)

Ithaar ni kiwango cha juu kabisa cha ukarimu; kwa sababu ukarimu ni kutoa mali usiyoihitajia. Ina maana ya kuinyamazisha nafsi ya ndani na kuvishinda vipingamizi na raghba zake.

64. Dânâ, Sâdık, Altınoluk Sohbetleri, v. 3, uk. 48

Mola wetu Mtukufu anasema kuhusu tabia hii njema:

"Na huwalisha chakula, juu ya kukipenda kwake, masikini, na yatima, na wafungwa. Hakika sisi tunakulisheni kwa wajihi wa Mwenyezi Mungu. Hatutaki kwenu malipo wala shukrani. Hakika sisi tunaiogopa kwa Mola wetu Mlezi hiyo siku yenye shida na taabu. Basi Mwenyezi Mungu atawalinda na shari ya siku hiyo, na atawakutanisha na raha na furaha." (76: 8 - 11)

Ni rahisi mtu kutoa pale anapokuwa na kila kitu. Kwa kuwa anatoa kitu cha ziada, nafsi ya ndani haimshinikizi sana. Ugumu hasa ni kuwa na uwezo wa kutoa wakati wa ukata.

Uzuri ulioje wa maelezo ya Ali ﷺ pale anaposema:

"Mali za kidunia zinapokujia, utajua jinsi ya kutoa. Kwa sababu kuitoa hakupunguzi wingi wake. Mali za kidunia zinapokukimbia, endelea kutoa. Kwa sababu hazitokaa na wewe milele."

Katika *Ithaar* au kutoa kitu unachokihitajia, mtu huvumilia mashinikizo ya nafsi ya ndani na kujitoa muhanga kwa hiari na kwa utiifu. Hiki siyo kitu ambacho kila mtu anaweza kukifanya. Kuweza kuonyesha sifa hizo za kimaadili kunahitajika ukomavu wa kiroho, usafi wa moyo na nafsi.

Malipo ya kila tendo jema hutegemea ugumu wake. Hii ndiyo sababu kwamba malipo ya *ithaar* ni makubwa kuliko aina yoyote ya sadaka. Marafiki wa Mwenyezi Mungu walizichukulia thawabu tabia hii ya kimaadili kama hazina isiyomithilika na walitoa sadaka "bila kuhofia kufukarika" hapa duniani ili wapate furaha na manufaa yake makuu huko Akhera.

Uzuri ulioje wa maneno ya Rumi kuhusu hili pale anaposema:

"Kama majani ya mbuyu huu yatadondoka, Muumba ataujalia zawadi ya kutokuwa na majani (umasikini wa kiroho). Kama kwa sababu ya zawadi yako mali haitobaki mikononi mwako, fadhila za Mungu zitawezaje kukuacha ukiwa umelala chini". [65]

Kwa hiyo, ithaar ina maana ya mtu kuweza kutoa katika hali ya ukata. Ina maana ya kuonyesha ukuu wa kumpa ndugu yako bila kukhofu kufukarika na kwa kuikabili njaa. Ina maana ya kutoa ukiwa na furaha bila kuonyesha uso mkali bila kujali ugumu wa jambo hilo ndani ya nafsi yako.

KUTOA KATIKA KILA AINA YA BARAKA

Ithaari haihusu pesa au mali pekee. Ni kuwa na uwezo wa kutoa chochote tulichojaaliwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu. Kwa maneno mengine, *ithaar* ni kutoa kwa dhati katika kila aina ya baraka za kimaada na za kiroho, vipawa, ujuzi, na hekima. Ili litawezekana tu kwa kuifanya *ithaar* kuwa kitu muhimu ndani ya moyo.

Kwa mfano, mwalimu wa Qur'an hapaswi kusema "nina kitu gani? Nitoe nini?" Badala yake anatakiwa kuona kuwa kuitumikia Qur'an ni hazina, na anaweza kujitolea muda wake wa ziada kufundisha Qur'an. Kwa namna hiyo atakuwa ameungana na watu wa *ithaar*.

Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ alipigwa mawe na watu wa Taif alipokuwa akiwafikishia ujumbe wa Uislamu. Hata hivyo hatua ya mtumwa (Addaas) kuingia katika Uislamu ilimpunguzia huzuni yake.

65. Mathnawi, I, 2233-2234

Baada ya safari hii yenye machungu, Mtume ﷺ aliwaendea watu wa makabila ya washirikina wa Arabia waliokuja kwa ajili ya hijja. Aliwaelezea yale ambayo watu wa Makkah walikuwa wakiwatendea waumini na kuwaambia: *"Nipelekeni kwenye kabila lenu ili niwafikishie ujumbe wa Uislamu."* Anakimbia tatizo moja na kuingia katika tatizo jingine ili tu awafundishe watu kuhusu Uislamu. Alisahau kabisa faraja na mapumziko, kama isemavyo aya ifuatayo:

"Na ukipata faragha, fanya juhudi. Na Mola wako Mlezi ndiyo mshughulikie." (94: 7-8)

Kwa hivyo tukiweza kujitolea mapumziko yetu kwa ajili ya fursa zisizokuwa na kikomo za njia ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, nasi pia tunaweza kuungana na watu wa *Ithaar*.

ITHAAR YA MTUME WA MWENYEZI MUNGU NA MASWAHABA WAKE

Kama ilivyo katika mambo mengine yote ya Uislamu, Mtume ﷺ na maswahaba wake ni mfano bora kwetu juu ya *ithaar*. Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ kamwe hakumkatalia mtu aliyetaka msaada wake. Kama hana kitu wakati huo, alikuwa akitafuta njia ya kumsaidia, na kamwe hakujiweka nyuma katika kusaidia. Siku moja mtu mmoja mwenye shida alimjia. Mtume ﷺ akasema:

"Sina kitu sasa hivi cha kukupa, lakini nenda kanunue unachotaka kwa jina langu, nitalipa baadaye."

Omar رضي الله عنه aliposikia hivyo akasema:

"Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Kama unacho utampa, kama huna basi Mwenyezi Mungu hajakukalifisha vitu vilivyo nje ya uwezo wako."

Mtume ﷺ hakupendezewa na maneno ya Omar. Mmoja wa waumini wa Madina akasema:

"Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Baba na mama yangu wawe fidia kwa ajili yako! Toa! Usiogope kwamba mali za dunia hii zitapungua."

Mtume ﷺ alipendezewa na maneno haya. Akatabasamu na kusema:

"Hivyo ndivyo nilivyoamrishwa." (Haythamī, X, 242)

Kwa maneno mengine Mtume wa Mwenyezi Mungu alikuwa karimu mno kiasi kwamba aliwasaidia watu hata kwa kukopa pesa. Tabia na hisia yake vinapaswa kuwa mfano kwetu.

Siku nyingne Mtume ﷺ alipoletewa bakuli la maziwa, alikuwa akianza kuipeleka kwa watu wa Suffa (as-hab al-suffa). Alikuwa hajifikirii mwenyewe pindi maswahaba wake wanapokuwa na njaa; kwa sababu, kwake yeye furaha ya kuwasaidia maswahaba wake ilipita furaha zote.

Uzuri ulioje wa jinsi mshairi anavyoielezea sifa ya Mtume ﷺ ya *ithaar* kwa njia ya ulinganisho:

" Siku moja mtu akikulinganisha na mawingu kwa ukarimu, atakuwa anafanya kosa katika kusifia kwake huko. Kwa maana mawingu hulia pindi anapotoa; lakini wewe unatabasamu."

Mtume ﷺ na Abu Bakr ؓ walipofariki dunia, walizikwa katika chumba cha Aisha. Aisha ؓ alikuwa akitarajia kwamba atazikwa katika eneo la mwisho lililobaki katika chumba chake. Lakini Omar ؓ alipochomwa mkuki na kuwa katika hali

mbaya, alimtuma mwanaye kwa Aisha ﵂ na kumuomba nafasi iliyobaki chumbani kwake ili apate kuzikwa humo. Aisha ﵂ aliachia haki yake na kumpa nafasi Omar ﵁.

Masikini mmoja alimuomba kitu Aisha, mke wa Mtume ﷺ, hali ya kuwa amefunga na alikuwa na kipande kimoja tu cha mkate katika nyumba yake. Akamwambia mtumishi wake wa kike "*mpe*". Mtumishi akasema, "Hutokuwa na kitu cha kufuturu leo." Aisha akarudia, "*mpe*," na hivyo akafanya kama alivyoambiwa. Ilipofika jioni, watu wa nyumba moja au mtu mmoja ambaye haikuwa kawaida kwake kuwapa, akawapatia kondoo na chakula. Aisha, mama wa waumini, akamuita mtumishi wake na kumwambia "*Kula hiki. Hiki ni bora kuliko kipande chako cha mkate."* (Maalik, Muwattā, Sadaqah, 5)

Kwa sababu maswahaba walijua vyema kuwa Mwenyezi Mungu ni karimu kuliko waja wake na asingewaacha waja wake wanaootoa kwa dhati kwa ajili yake. Hutoa kitu bora zaidi ya kile kinachotolewa.

Imeelezwa katika aya kuwa:

"... Na chochote mtakachokitoa (kwa ajili ya kheri) Yeye atakilipa..." (34:39)

Infaq ni furaha kubwa kwa waumini wanaojua malipo ya kuwasaidia wengine. Jalal al-Din Rumi analielezea hili katika maneno yafuatayo;

"Anapoona kipande cha bidhaa kilichozidi katika faida (yake mwenyewe), mapenzi yake kwa ajili ya mali yake hufifia; (maana hata sasa) bado anavutiwa nazo, kwa sababu anajua hakuna faida kuliko mali yake mwenyewe." [66]

66. Mathnawi, III,4107-4108

"Mali haitopungua kwa kutoa sadaka; kinyume chake kuwasaidia watu kuilinda mali isipotee"

Swahaba mmoja aitwaye Jabir ﷺ anasimulia *ithaar* ya waumini wa Madina (ansaar) kwa ndugu zao wahamiaji kutoka Makkah (Muhajirina):

"Pindi Ansar walipovuna tende, walikuwa wakizigawa sehemu mbili na kuweka katika nusu moja tende kidogo kuliko nusu ya pili. Kisha walikuwa wakiweka matawi ya tende chini ya fungu lenye tende kidogo ili lionekane kubwa kuliko la pili. Kisha huwaambia muhajirin "chukua fungu unalotaka." Muhajirin walikuwa wakichagua fungu dogo na kuliacha lile kubwa kwa Ansar. Kwa hivyo Ansar walikuwa wakiwapendelea Muhajirin kuliko nafsi zao na kupata tende kidogo." (Haythamī, X, 40)

Ukubwa ulioje wa jambo lililofanywa ili kupata raha ya kiroho ya ithaar! Uzuri ulioje wa hali ya udugu na ithaar unaoacha nyuma maslahi ya kimaada na kidunia!

Vile vile, Sahaba Abu Ubaydah bin Jarrah ﷺ, ambaye alikuwa kamanda wa jeshi la Kiislamu, alipoletewa maji baridi na mkate mzuri jangwani, aliuliza: "Je askari wangu wamepata vitu hivi?" alipogundua kuwa vitu hivyo vililetwa maalumu kwa ajili yake, hakuvikubali. Alisema kwamba "Nitakula kile ambacho askari wangu wanakula." Kwa sababu alikuwa miongoni mwa wale wasiosema "mimi kwanza" bali "ndugu zangu kwanza."

Mtu mmoja alikuja kwa Mtume. Mtume akamtuma mjumbe kwenda kwa wake zake (kumletea chakula mtu yule) lakini wakasema kuwa hawakuwa na chochote zaidi ya maji. Hapo Mtume ﷺ akasema:

"Nani atakayemchukua mtu huyu awe mgeni wake?"

Mtu mmoja katika Ansari akasema, "Mimi".

Akaenda naye mpaka kwa mke wake na kumwambia: *"Mhudumie vizuri mgeni wa Mtume wa Mwenyezi Mungu."*

Mkewe akasema: *"Hatuna chochote zaidi ya chakula cha wanangu*."

Naye akasema: andaa chakula chako, washa taa yako na wakiulizia chakula cha usiku wabembeleze walale."

Mkewe akaandaa chakula chake, akawasha taa na akawalaza wanaye, na kisha akasimama na kufanya kama anazima taa, lakini akaizima. Kisha wote wawili wakajifanya kama wanakula, kumbe wamelala njaa. Asubuhi yule Ansari akaenda kwa Mtume ﷺ, Mtume akamwambia: "Usiku wa jana Mwenyezi Mungu alipendezewa na ulichofanya." (Tazama Bukhari, Manāqib al-Ansari, 10, Tafsir, 59 / 6)

ITHAAR YA MARAFIKI WA MWENYEZI MUNGU

Marafiki wa Mwenyezi Mungu ambao wamepambwa na misingi ya kimaadili ya Mtume ﷺ walionyesha ithaar kama iliyoonyeshwa na maswahaba wa Mtume ﷺ. Mojawapo imesimuliwa na Antakyali Abu al-Hasan kama ifuatavyo;

"Siku moja watu wapatao thelathini walikusanyika kwenye mji wa Ray. Walikuwa na mkate ambao usingewatosheleza wote. Wakaukata mkate, wakazima taa kisha wakakaa kwa ajili ya kula. Baada ya muda walipowasha taa ili wasafishe meza, wakaona mkate wote ukiwa vilevile kwenye meza. Kila mmoja alimpendelea mwenzake ale kuliko nafsi yake." (Ghazālī, Ihyā, III, 572)

Katika suala hili, mfano mwingine wenye kushangaza ni wa Dawud Al-Tai. Siku moja mmoja wa wanafunzi wake alimwambia:

“Nimechoma kiasi cha nyama, tafadhali waweza kula kiasi?”

Kwa kuwa Dawud Al-Tai hakujibu, mwanafunzi wake akadhani kuwa mwalimu wake alikuwa amekubali na hivyo akamletea. Dawud Al-Tai aliitazama nyama na kuuliza:

“Kuna habari zozote kuhusu yatima fulani na fulani?”

Akimaanisha hali mbaya ya yatima, mwanafunzi akajibu: “Kama unavyojua” Kisha Dawud AL-Tai akamwambia mwanafunzi wake: “Basi wapelekee hii nyama” Lakini mwanafunzi alitaka mwalimu wake ale nyama, na akasisitiza akisema: “Ewe bwana, hujala nyama kwa muda mrefu” Dawud Al-Tai hakukubali akasema: “Mwanangu! Nikila hii nyama, baada ya muda mfupi itanitoka; lakini wale yatima wakiila, itapelekwa mbinguni na kukaa huko milele.”

Ubaydullah Ahrār anasimulia:

“Siku moja nilikwenda sokoni. Mtu mmoja akanijia na kusema; “Nina njaa. Je waweza kunipa chakula kwa ajili ya Mwenyezi Mungu?” Sikuwa na kitu cha kutoa isipokuwa kilemba kikuukuu. Tukaenda kwenye mgahawa na kumwambia mpishi: “Chukua hiki kilemba. Ni kikuukuu lakini nikisafi. Unaweza kukitumia kukaushia vyombo vyako. Je waweza kukichukua na kumpa chakula mtu huyu?” Mpishi akampa chakula masikini yule, na hakutaka kukichukua kilemba changu. Lakini nilikataa. Nilisubiri mpaka masIkini yule alipomaliza kula, ingawa nami nilikuwa na njaa.” (Hadāiq Al-Wardiyyah, uk. 651)

Baadaye Ubaydullah Ahrar akawa tajiri sana ambapo aliwaajiri maelfu ya watu katika ranchi yake. Hata hivyo, hakuac-

ha kuwahudumia watu. Huduma yake kwa kila mtu, kuanzia mwanzo mpaka mwisho wa safari ya kiroho, ilikuwa kubwa. Anasimulia mojawapo ya huduma zake kama ifuatavyo:

"Nilkuwa nikiwahudumia wagonjwa wanne katika Madrasah ya Maulana Qutbuddin mjini Samakand. Kwa sababu ya hali yao ya kuharisha kuwa mbaya, walianza kulowanisha vitanda vyao. Nilikuwa nikiwasaidia kuwapeleka bafuni na kuwafulia nguo zao. Kwa sababu ya kuendelea kuwahudumia niliambikizwa maradhi na kuuguwa. Pamoja na hivyo niliendelea na huduma yangu na kuwasafishia nguo na vitanda vyao." *(Hadāiq Al-Wardiyyah, uk. 653)*

Mfano bora ulioje wa hali wa Ubaydullah al-Ahrār! Angetaka angewaajiri watu wakafanya kazi zote hizi. Lakini hakupenda kukosa thawabu za ithaar na akajitolea furaha yake mwenyewe.

Abbas b. Dahkān anasimulia:

"Miongoni mwa watu ambao mimi nawajua ni Bishr bin Harith pekee ndiye aliyeondoka hapa duniani kama alivyokuja. Alizaliwa mtupu na akaondoka mtupu. Alipokuwa kwenye kitanda cha mauti, mtu mmoja alikuja kumuomba kitu. Hakuwa na chochote zaidi ya kanzu yake. Aliitoa na kumpa huyo masikini. Aliazima kanzu kutoka kwa mtu na akafariki dunia. Kwa maneno mengine, alipofariki dunia alikuwa hana hata kanzu. Alikuja hapa duniani bila nguo na akaondoka bila nguo."

Kwa upande mwingine, jambo muhimu katika kutoa huduma kwa ajili ya Mwenyezi Mungu ni kuifanya pindi inapokuwa hakuna mtu anayetaka kuifanya; na kumsaidia masikini pindi inapokuwa hakuna mtu mwingine wa kumsaidia. Hiyo ina maana ya kuielewa siri ya manano yasemayo *Marafiki wa Mwenyezi Mungu hununua katika masoko ambayo hakuna anaye-*

nunua. Linaweza kufikiwa kwa kujitolea vitu ambavyo hakuna mtu anayetaka kujitolea, hata kama ni kujitolea maisha.

KILELE CHA ITHAAR: KUJITOLEA MAISHA

Ithaar ni mfano wa kazi ya kuvutia kutokana na juhudi za kidini. Ina maana ya mtu kuweza kuupandisha upendo wake kwa Mwenyezi Mungu na Mtume wake juu ya upendo wa aina yoyote ile. Ndiyo maana Mtume ﷺ akamwambia Omar ؓ kwa niaba ya wafuasi wake wote:

"Hapana, Naapa kwa yule ambaye nafsi yangu iko mikononi mwake, (hutokuwa na imani kamili) mpaka niwe kipenzi zaidi kwako kuliko nafsi yako."[67] Na Omar akatoa thamani ya upendo wake kwa Mwenyezi Mungu na Mtume wake kwa uhai wake na akafa kishahidi.

Upendo wa Mwenyezi Mungu unahitaji kuitolea halisi. Mtu anaweza kuupata kwa kuutoa muhanga upendo wa kidunia. Watu hutoa mhanga wa hali ya juu kwa ajili ya wale wanaowapenda. Kila mtu huutoa mhanga wake kulingana na yule ampendaye. Upendo unapofikia ukamilifu wake, mhanga wako kwa ajili ya unayempenda hufikia kilele chake. Hapo maumivu hubadilika na kuwa furaha.

Wale wanaoishi katika imani zao wakiwa na upendo huo madhubuti hakuna kitakachowazuia hata kutoa maisha yao.

Usiku ambao Mtume ﷺ alikuwa akihama kuelekea Madina, nyumba yake ilivamiwa na maadui zake. Alimuacha Ali ؓ kalala kitandani mwake na kuanza safari ya kuelekea Madina. Ali ؓ alikubali kubeba hatari ya kufa na bila hofu akalala kwenye kitanda cha Mtume ﷺ.

67. Tazama Bukhari, Kitab al-ayman, 3.

Qur'an Tukufu inasema kuhusu waumini ambao ni kilele cha ithaar:

"Na katika watu yupo ambaye huiuza nafsi yake kwa kutaka radhi za Mwenyezi Mungu; na Mwenyezi Mungu ni Mpole kwa waja wake." (2: 207)

Uzuri ulioje wa maneno ya Rumi katika kuelezea hali hii pale anaposema:

"Pindi panapokuwa hakuna kitu bora kuliko maisha, maisha huwa na thamani kubwa; pindi kitu bora zaidi kinapotokea, jina la maisha huwa kitu chenye kuteleza (kisichokuwa na maana). Bidhaa (za ulimwengu huu) na mwili ni theluji yenye kuyeyuka isiyokuwa na chochote; (lakini) Mungu ndiye mnunuzi, kwani Mungu amevinunua. [68]" [69]

Ghulam Khalil ambaye alikuwa mtu muovu aliyeupiga vita Usufi alikuwa akionyesha uadui wake kwa Masufi. Alikula njama ya kumtia nguvuni Abu al-Husayn al- Nuri na baadhi ya Masufi wengine wakatumwa kwenye mji mkuu wa dola. Kwa amri rasmi, wote wakapewa adhabu ya kifo. Mnyongaji alipotaka kumkata kichwa mmoja wa Masufi, Abu al-Husayn al-Nuri kwa hiari kabisa alisogea mbele kwa ajili ya adhabu. Kila mtu alishangaa. Mtoa adhabu akamwabia:

"Ewe jasiri! Unataka kuadhibiwa lakini huu upanga siyo kitu kinachotakiwa kupendwa. Bado haijafika zamu yako, kwa nini wafanya haraka kiasi hicho?"

Abu al-Husayn akajibu;

"Njia yangu ni njia ya ithaar na kitu cha thamani zaidi ni uhai wa mtu. Ningependa kuzitoa mhanga dakika zangu za mwisho katika ulimwengu huu kwa ajili ya ndugu zangu. Kwa

68. At-Tawbah, 9:111
69. Mathnawi, III, 4110, 415

Sufi, pumzi moja katika hii dunia ina thamani kubwa kuliko miaka elfu moja ya Akhera; kwa sababu hii dunia ni mahali pa kuchuma radhi za Mwenyezi Mungu, wakati Akhera ni mahali pa kuwa karibu na Mwenyezi Mungu Mtukufu. Ukaribu naye hupatikana kwa kuwatumikia wengine. Ndiyo maana najitolea pumzi yangu ya mwisho kwa ajili ya ndugu zangu." [70]

Mali, uhai na watoto ni baraka, ambayo binadamu huitamani sana na hawataki kuvitoa sadaka. Ndiyo maana mtihani wetu katika hii dunia kuhusu baraka hizi tatu umekuwa mgumu kuliko mitihani yote. Mwenyezi Mungu Mtukufu huwajaribu sana waja wake kuhusu vitu hivi na kuangalia Ikhlas yao katika kumtumikia.

Nabii Ibrahimu عليه السلام alifaulu mitihani yake katika mambo haya yote na kuwa "Khalil au Rafiki" wa Mwenyezi Mungu. Alitoa mali yake bila kuhofu kufukarika. Alitupwa ndani ya moto na Namrudh kwa sababu ya mapambano ya kufikisha ujumbe wa Mwenyezi Mungu, kwa hiyo akathibitisha kuwa alikuwa tayari kuyatoa maisha yake kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Na miongoni mwa mitihani yake mizito kuhusu mwanaye, alitii na kujisalimisha kwa Mola wake.

Watoto wana nafasi muhimu sana katika maisha ya watu. Watoto ni njia ya kuhalalisha tamaa ya mwanadamu ya kuendelea kuwepo, kwa sababu ukoo wake huendelea kupitia kizazi. Ndiyo maana wanadamu huwashikilia watoto wao kwa upendo mkubwa. Kwa namna moja watoto ni sehemu yenye kuendelea ya wazazi wao.

Katika suala hili, Nabii Ibrahimu عليه السلام aliukabili mtihani mzito zaidi pale alipotakiwa kumtoa dhabihu mwanawe Ismail عليه السلام kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Malipo ya utiifu na ku-

70. Ḥujwīrī, *Kashf al-Mahjūb*, kilichotafsiriwa na Süleyman Uludağ, Istanbul 1996, uk. 302

jisalimisha kwao kwa kipekee, kwa amri ya Mwenyezi Mungu, malaika Jibril alimleta kondoo kutoka peponi. Kumbukumbu ya sadaka zao imeendelea kuwa hai na itaendelea kuishi baina ya waumini katika mfumo wa ibada mpaka siku ya mwisho.

Katika jambo hili, lengo halisi la ibada ya kuchinja ni mja kumuahidi Mola wake kuwa atatoa dhabihu hata ya maisha yake, pindi itakapohitajika. Vile vile ibada ya kuchinja ina maana ya kufaulu mtihani wa uchamungu na kusajili utiifu na kujisalimisha kwetu mbele ya Mwenyezi Mungu. Kuhusu sadaka za kuchinja, imeelezwa katika aya ifuatayo kuwa:

"Nyama zao hazimfikii Mwenyezi Mungu wala damu zao, lakini unamfikia uchamungu wenu..." (22: 37)

Uzuri ulioje wa maelezo ya Rumi kuhusu faida za sadaka ya maisha:

"Mtume alisema, "kwa ajili ya kukumbusha, daima malaika wawili hutoa tangazo zuri wakisema 'Ewe Mwenyezi Mungu, wafanye watumiaji sana waridhike kikamilifu, walipe mara laki moja kwa kila dirham wanayotumia." [71]

"Ee Mungu, wewe ndiwe unayemlipa mtumiaji neema, na Wewe ndiwe unayemlipa bakhili mateso." Hasa (hili humhusu) mtumiaji ambaye ameitumia nafsi (uhai) yake kwa hiari na kuifanya koo yake kuwa sadaka kwa Muumba. Analitoa koo lake, kama Ismali: kisu hakiwezi kufanya chochote kwenye koo lake. [72]

Ukitoa mkate kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, utalipwa mkate; ukitoa maisha yako kwa ajili ya Mungu, utapewa maisha (kama malipo). [73]

71. Mathawi, I, 2223-2224
72. Mathnawi, II, 381-383
73. Mathnawi, I, 2236

Kama aliyaona, vipi atasita kutoa maisha yake? Vipi atahuzunishwa na uhai mmoja? Kwenye ukingo wa mto, maji yanawekewa kinyongo naye (yeye pekee) ambaye kwamba haoni mkondo wa maji." [74]

BARAKA KUBWA YA *ITHAAR*

Kujitolea na kutoa sarafu moja ni kitu chenye thamani zaidi kuliko kutoa mamia kwa maelfu ya sarafu yanayotolewa bila kujitoa. Hili limefafanuliwa katika maneno yafuatayo ya Mtume ﷺ:

Siku moja Mtume ﷺ aliwaambia maswahaba wake:

"Sarafu moja ilishinda sarafu elfu moja."

Maswahaba wakamuuliza;

"Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Vipi hayo yakawezekana?" Mtume ﷺ akawajibu:

"Mtu mmoja alikuwa na sarafu mbili za fedha. Akatoa sadaka sarafu moja. Mtu mwingine (ambaye alikuwa tajiri sana) akachukua sarafu laki moja na kuzitoa kama sadaka." (Nasā'ī, Zaka, 49)

Kwa maneno mengine, jambo muhimu katika sadaka siyo kiasi chake, bali ni kiwango cha kujitoa kinachofanywa na mtoaji. Mali ya kweli siyo ukubwa wa vile unavyovimilki bali kuridhika kwa moyo. Na ukarimu wa kweli ni kulazimishana na njia na kutoa kwa moyo mmoja.

Sahl b. Abdullah al-Tustarī anasimulia: Nabii Musa عليه السلام alimuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu akisema:

74. Mathnawi, II, 893 - 894

"Mola wangu nionyeshe daraja za baadhi ya wafuasi wa Muhammad ﷺ peponi."

Mwenyezi Mungu akamwambia:

"Ewe Musa! Wewe siyo madhubuti wa kutosha kwa jambo hili, lakini nitakuonyesha mmoja wa wale wenye daraja ya juu kabisa miongoni mwao. Kwa daraja hii, nimemfanya kuwa bora juu yako na juu ya viumbe wengine wote."

Kisha mlango wa mbingu ukafunguliwa. Alipoona nuru yake na alivyo karibu na Mwenyezi Mungu, Musa akazimia. Baadaye Musa akamuuliza Mwenyezi Mungu Mtukufu jinsi mtu huyo alivyofikia daraja hiyo.

Mwenyezi Mungu akajibu:

"Kwa njia ya msingi wa maadili ya hali ya juu niliyompatia"

Musa alipouliza msingi huu wa kimaadili, Mwenyezi Mungu akamwambia:

"Msingi huo ni Ithaar au kuitoa nafsi kwa ajili ya mahitaji ya wengine. Atakayekuja kwangu na Mwenendo huu, nitamuonea soni kumuuliza na nitampatia mahali popote atakapo peponi." (Ghazālī, Ihyā, 570-571)

Kwa kweli si kila mtu anaweza kupata daraja ya namna hiyo, lakini kadiri tunavyokaribia anga hii ndivyo tunavyozidi kupata baraka.

Tusisahau kuwa hatua ndogo katika kufanya ithaar huenda ukawa mlango wa milele wa faida kwetu.

Pia imeelezwa katika hadith ya Mtume ﷺ:

"Si muumini wa kweli yule ashibaye hali ya kuwa jirani yake ana njaa."

(Hakim, II, 15) Hadith hii inatukumbusha ukubwa wa jukumu letu. Kama ambavyo pindi kiungo kimoja cha mwili kinapouma, mwili wote hupata maumivu; kila muumini huhisi maumivu ya ndugu yake ndani ya moyo.

Hivyo, tunapaswa kuhisi maumivu ya ndugu zetu kuanzia wale wa karibu na kufika kwa wale walioko Afrika, Aceh na maeneo mengine ya ulimwengu.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu ayape maisha yetu baraka ya mazingira ya kiroho ya zama za furaha na hali ya kiroho ya marafiki zake. Tunamuomba azipe nyoyo zetu baraka ya amani ya kuwasaidia ndugu zetu kwa kutuliza maumivu yao. Tunamuomba aifanye amani ya moyo katika dunia hii kuwa ishara ya utulivu atakaotujaalia huko Akhera.

Amin...

KUHARAKISHA KUTENDA WEMA

Mola wetu Mtukufu anasema ndani ya Qur'an Tukufu "Naapa kwa alfajiri"[1] na wakati wa alfajiri una maana maalumu kwa maisha yetu. Tutayajaza vipi maisha yetu? Ni muda gani tutautumia kwa ajili yetu na kiasi gani cha muda tutakachotumia kwa ajili ya masikini na wenye shida? Malaika wanaoandika matendo yetu wataandika nini katika vitabu vyetu kwa ajili ya Akhera? Muumini anatakiwa kutafakari kwa makini majibu ya maswali haya na kuutumia muda wake kwa matendo mazuri.

1. Qur'an, 89: 1

KUHARAKISHA KUTENDA WEMA

Mwenyezi Mungu Mtukufu ameapa kwa “wakati” na anatutaka tuwe makini na jinsi tunavyotumia uhai wetu.

Wakati ni mfano wa kisu chenye makali kotekote. Wakati ukitumika kulingana na moyo wa Qur’an na Sunnah, huwa ni njia ya kufika peponi. Lakini kwa wale wanaoutumia wakati wao katika dunia hii kinyume na moyo wa Uislamu, huwa kama mafuriko. Muumini hatakiwi kuangamia katika gharika hii.

Haiwezekani kurudisha yaliyopita au kurudi nyuma. Muda hauwezi kuwekwa, kuazimwa au kuuzwa. Hata kama tukitoa mali yetu yote kama dhamana, hatuwezi kuahirisha au kuharakisha muda wa mauti yetu hata kwa sekunde moja.

Maisha yetu katika hii dunia, ambayo ni maandalizi ya awamu ya Akhera, ni kama hazina. Ndiyo maana yanatakiwa kutunzwa na kutumika kwa umakini, kwa sababu hakuna fidia pale tunapoipoteza baraka hii. Kutumia hovyo muda wetu kama matamanio ya kibinafsi yanavyotaka hakumalizika na kuyatelekeza na kuyasahau majukumu yetu mbele ya Mwenyezi Mungu itakuwa sababu ya kujuta.

Maisha ambayo ni barabara yenye matuta iliyo baina ya uchanga na kaburi ndiyo idadi ya pumzi zetu. Idadi hii haijulikani kwa mwanadamu lakini yajulikana kwa Mwenyezi Mun-

gu Mtukufu. Pumzi ya mwisho ndiyo ya muhimu sana katika pumzi zetu hapa duniani.

Pumzi ya mwisho ni kivuko cha maisha yetu katika hii dunia kuelekea kwenye maisha mapya na ya milele huko Akhera. Ni njia yenye mikunjomikunjo na yenye mwinuko mkali kati ya dunia hizi mbili. Kila muumini mwenye tafakuri anapaswa kutafakari kwa kina kuhusu njia hiyo ngumu na ajaribu kuyaweka maisha yake kwenye njia iliyonyooka ya Uislamu.

Pumzi ya mwisho ambayo ni sehemu ya mwisho ya mchezo wa maisha ni kama kioo kisafi kinachomuonyesha kila mtu mwisho wake. Katika kioo hicho binadamu watapata kujua wao ni akina nani. Wakati tukitumia pumzi hizi zenye thamani za uhai wetu kwenye dunia hii ya muda hatupaswi kusahau kwamba tunaendelea kurikodiwa na kamera za Mwenyezi Mungu. Siku moja mkanda wa maisha yetu utawekwa mbele yetu na kutakiwa kuungalia kwa amri ya **“** اقْرَأْ كِتَابَكَ **Soma kitabu chako.”** Hapo kwa mara nyingine tutajitambua.

Kwa kuwa hatujui wakati wa kupumua pumzi yetu ya mwisho, leo ndiyo siku ya kujiandaa kwa ajili ya wokovu wa milele. Leo ndiyo siku ya kutenda mambo mema, yatakayokuwa akiba yetu siku ya Kiyama.

Katika maneno ya Mtume ﷺ, tunakumbushwa kwamba tutaulizwa siku ya Kiyama kila kitu katika matendo yetu tuliyoyafanya hapa duniani. Mtume wa Mwenyezi Mungu anatuusia kuachana na mghafala kama ifuatavyo:

“Unyayo wa mja hautosogea siku ya kiyama mpaka aulizwe mambo manne: uhai wake - aliutumiaje, elimu yake - aliitumikisha je, mali yake - aliipata wapi na alivyooitumia, na mwili wake - aliutumiaje.” (Tirmidhi, Kitab Sifat Al-Qiyamah Wal Raqa’iq, 1).

"Faidika na mambo matano kabla ya mambo matano: ujana wako kabla ya uzee wako, afya yako kabla ya maradhi yako, mali yako kabla ya ufukara wako, muda wako wa faragha kabla ya kushughulishwa, na uhai wako kabla ya mauti yako." (Bukhari, Riqāq, 3, Tirmidhi , Zuhd, 25)

UMUHIMU WA KUHARAKISHA MAMBO MEMA

Mtume wa Mwenyezi Mungu alitoa ujumbe kuhusu umuhimu wa kuharakisha kutenda mambo ya kheri kwa mifano mingi katika maisha yake. Moja wapo imesimuliwa na 'Uqbah bin Harith:

"Niliswali Alasiri pamoja na Mtume ﷺ na baada ya kumaliza swala akasimama haraka na kwenda kwenye nyumba ya mmoja wa wake zake na kisha akatoka. Akaona kuwa nyuso za watu zina mshangao kutokana na kasi yake. Kisha akasema:

"Nilipokuwa nikiswali nilikumbuka kuwa kulikuwa na kipande cha dhahabu ndani ya nyumba yangu na sikupenda kiendelee kuwepo usiku mzima, na hivyo nimeagiza kuwa kitolewe sadaka." (Bukhari, Adhān, 158, Al-'Amal Fi Al-Salat, 18; Nasaī, Sahw, 104)

Katika Hadith nyingine, anasema kuwa:

"Harakisheni kutoa sadaka; kwani sadaka huzuia matatizo." (Haythamī, Majma 'Al-Zawāid, Iii, 110)

Kama ambavyo swala bora ni ile iliyoswaliwa kwa wakati wake, sadaka bora ni ile inayotolewa bila kuahirishwa. Kitendo hiki cha Mtume ﷺ kimeonyesha katika maisha ya wanazuoni na mawalii, ambao ni warithi wa Mitume.

Kisa kutoka katika maisha ya Hassan al-Basri ni mfano mzuri mno kwetu.

Darwesh mmoja aliomba kitu kwa Hassan al-Basri. Akasimama hapo hapo na kumpa kanzu yake. Watu wakamuuliza Hassan al-Basri:

"Ewe Hassan! Kwa nini hukwenda nyumbani na kumletea kitu kutoka nyumbani kwako?"

Hassan al-Basri akajibu:

"Siku moja mwenye haja alikuwa msikitini na kuniambia kuwa alikuwa na njaa. Tulifanya siri na tukawa hatujampatia kitu kwa haraka. Tuliondoka msikitini na kwenda majumbani mwetu. Tulipokuja kuswali Alfajiri, tulimkuta masikini yule akiwa amefariki dunia. Tulimuandalia sanda na kumzika. Siku ya pili niliota ndoto na kuiona sanda tuliomzikia yule masikini ikiwa na maneno yafuatayo: *"Chukua sanda yako, haikukubaliwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu."* Kuanzia siku hiyo niliapa kwamba sitochelewa kukidhi haja ya mtu." [75]

Mwenyezi Mungu Mtukufu huwaonyesha baadhi ya mambo marafiki zake kwa lengo la kuacha athari kubwa kwenye nafsi zao na kuwaelekeza kwenye njia iliyonyooka. Kama inavyoweza kueleweka kutokana na kisa kilichotajwa hapo juu, thamani ya amali njema inapatikana katika kuitekeleza haraka bila kuichelewesha hata kidogo.

75. See Darir Mustafa Efendi, Yüz Hadis Yüz Hikâye, edited by S. Yıldırım - N. Yılmaz, Istanbul 2001,. 157uk

MANDHARI YENYE MFANO WAKATI WA PUMZI YA MWISHO

Rabi' bin Haytham anaelezea hali yenye kusikitisha ya mtu mmoja wakati wa kuvuta pumzi yake ya mwisho ambaye aliahirisha mambo mema na akawa hajaitakasa nafsi yake;

"Mtu huitoa roho yake kutokana na vitu anavyovipenda katika dunia hii. Siku moja nilikuwa pamoja na mtu katika kitanda chake cha mauti. Wakati nikirudiarudia kalimah al-Tawhid (la ilaha illallah) ili afuatishe ninavyotamka, yeye alikuwa akihesabu vidole vyake kana kwamba anahesabu pesa."

Kwa maneno mengine, mara nyingi watu huahirisha kutenda mambo mema kwa kusema kuwa watayafanya baadaye, lakini hata hiyo "baadaye" inapokuja, bado hawawezi kupata nafasi ya kuyatenda. Ndiyo maana mawalii wameelewa maana ya maneno yasemayo *"wale wanaosema tutafanya baadaye wameangamia."*

Abu Hurayra ﵁ anasimulia kuwa:

"Mtu mmoja alikuja kwa Mtume ﷺ na kumuuliza, "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Ni sadaka ipi iliyo bora katika malipo?" Akajibu:

"*Sadaka unayoitoa wakati ukiwa mwenye afya njema, bakhili na mwenye kuhofia ufakiri na unatamaani kuwa tajiri. Usiichelewesha mpaka wakati kifo kinapokaribia ukasema, "Mpeni kingi fulani na fulani, na mpeni kingi yule na yule.' Na hicho kingi tayari ni mali ya yule na yule (kwa maana muda umekwishapita."* (Bukhari, Zakat, 11)

Katika hadith nyingine imeagizwa kuwa:

"Mtu anayetoa sadaka ya dirham moja wakati wa uhai wake ni bora kuliko kutoa sadaka dirham mia moja wakati wa umauti." (Abu Dawud, Wasaya, 3/2866)

Kutokana na ukweli uliotajwa hapo juu, Sheikh Saadi anatoa ushauri ufuatao:

"Jiandalie mwenyewe akiba yako kwa ajili ya Akhera ukiwa bado uko hapa duniani. Kwa sababu baada ya kufa, ndugu zako wataingiwa na uchoyo na hawatoifanyia chochote roho yako. Toa mwenyewe dhahabu zako na baraka nyingine leo! Baada ya kufa, utavipoteza vyote.

Wale wanaojifanyia maandalizi kwa ajili ya Akhera ndiyo wanaopata ustawi. Hakuna mtu tofauti na mimi anayeweza kunikuna mgongoni mwangu kwa kufikiria manufaa yangu mwenyewe.

Weka mali yoyote uliyo nayo katikati ya kiganja chako na ipeleke mahali unapotaka kuitoa. Kama ukishindwa, kisha utang'ata kidole chako kwa sababu ya majuto."

Ni ukweli kwamba kutotoa sadaka ya mali kwa wakati wake na kuiacha kwa warithi, ambao hawakulelewa katika mafunzo sahihi ya kiroho na haijulikani mahali zitakapotumika, husababisha mtu husika kuwajibika siku ya kiyama. Na hiki siyo kitu ambacho waumini wenye wakili wanaweza kukifanya.

Swahaba wa Mtume ﷺ, Abu Dharr رضي الله عنه anatoa ushauri mzuri:

"Kuna washirika watatu katika mali. Wa kwanza ni mmiliki wa mali, yaani wewe; wa pili ni hatima. Haikuulizi kuwa ikuletee kheri au shari. Na wa tatu ni mrithi wako ambaye anasubiri ufariki dunia. Unapokufa, anachukua mali yako na utahesa-

biwa kwa mali hiyo. Kama una uwezo, usiwe mshirika dhaifu kuliko washirika wote wa mali hii." (Abu Nuaym, Hilyah, I 163)

Watu wanadhani kuwa ni matajiri katika ulimwengu huu wa kuwazika, watajikuta wakiwa muflisi pindi watakapokufa. Watakuja kushituka asubuhi baada ya kifo na kutambua kuwa hawana chochote mikononi mwao. Tajiri wa kweli hafilisiki baada ya kifo. Badala yake, anakuwa na himaya na mali ya milele.

Jalal al-Din Rumi anasema kuwa:

"Maisha katika dunia hii ni ndoto tu. Kuwa mmiliki wa mali katika dunia hii ni sawa na kupata hazina katika ndoto. Mali katika dunia hii hubakia katika dunia hii kwa kuhama-hama kutoka kizazi kimoja hadi kingine. "

"Kifo humuamsha tajiri aliyeghafilika kwa kuyachukua maisha yake. Mtu hulia kwa uchungu na maumivu aliyoyapa katika kutafuta kitu ambacho hakukimiliki na huanza kujuta; lakini anakuwa kachelewa mno". [76]

Baada ya kuzikwa katika ardhi, chochote kinachotokea kwa masikini, ndicho hicho hicho kinachomtokea tajiri. Huko kila mtu hukuta kile alichofanya hapa duniani. Mtaji wa wale walioondoka duniani, awe mtumwa au mfalme katika dunia hii, ni kile walichojiandalia kwa ajili ya Akhera. Ulimwengu huo ni mahali pa kila mtu kukutana na kile anachostahiki. Wale waliokuwa masultani waonevu hapa duniani watakuwa wa-tumwa huko Akhera; na wale waliokuwa watumwa wema hapa duniani watakuwa masultani. Daraja na vyeo vyote vya ulimwengu huu havitakuwa na nafasi huko Akhera. Hakuna kitakachomfaa mtu zaidi ya utii na nyoyo zenye Ikhlas.

76. Mathnawi, III, 2641

Vitu vikubwa ambavyo Mwenyezi Mungu hutujaribu navyo katika hii dunia, ni uhai, mali na watoto. Vitu hivi vinapotumiwa kwa wema, huwa ni baraka; lakini vikitumiwa kwa uovu, huwa ni chanzo cha maumivu na huzuni. Sauti ya dini ndiyo pekee inayoweza kutufanya tujue kipi chema na kipi kibaya, ipi baraka na ipi nakma kwetu.

Qur'an Tukufu inasema:

"Enyi mlioamini! Yasikusahaulisheni mali yenu, wala watoto wenu, kumkumbuka Mwenyezi Mungu. Na wenye kufanya hayo ndiyo waliokhasiri. Na toeni katika tulichokupeni kabla hayajamfikia mmoja wenu mauti, tena hapo akasema: Mola wangu Mlezi! Huniakhirishi muda kidogo nipate kutoa sadaka, na niwe katika watu wema?" (63: 9-10)

Hali ya wale wanaoyaharibu maisha yao imeelezwa katika aya ifuatayo:

"Na humo watapiga makelele: Mola wetu Mlezi! Tutoe tufanye mema siyo yale tuliyokuwa tukiyafanya.Kwani hatukukupeni umri wa kutosha kukumbuka mwenye kukumbuka? Na akakujieni Mwonyaji? Basi onjeni! Kwani waliodhulumu hawana wa kuwanusuru." (35: 37)

Imam Ghazali anatoa ushauri na usia ufuatao:

"Mwanangu! Fikiria kwamba umekufa leo na umerudishwa tena duniani. Fikiria jinsi utakavyokuwa na msisimko katika hali kama hiyo. Kwa hiyo kaa mbali na dhambi na kila kitu ghairi ya Mwenyezi Mungu na usipoteze hata sekunde moja leo; kwa sababu kila pumzi unayovuta ni baraka kubwa."

Hii ina maana kwamba tunapaswa kuuchukulia kila ukurasa unaofunguliwa katika kalenda ya maisha kuwa ni fursa

tuliyopewa na Mwenyezi Mungu na kwa hivyo tunatakiwa kuharakisha kutenda mema.

KILA MTU HUJUTA

Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ anatuonya kama ifuatavyo: "Hakuna mtu anayekufa asijute." Alipoulizwa majuto hayo ni ya nini, akasema kwamba:

"Kama (aliyefariki) ni mtu muhsin (mtu mwema), atajuta kwa kutozidisha matendo yake mema; na kama ni muovu, atajuta kwa kutoacha maovu yake na kujisahihisha." (Tirmidhi, Kitān Al-Zuhd, 59/2403)

Kwa maneno mengine, hata watu wema watajuta kwa kutotumia zaidi baraka na neema walizokuwa nazo hapa duniani kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Hatuwezi kupata hata maneno ya kuelezea majuto ya watu walioghafilika.

Behlul Dana anauliza kwamba:

"NI jambo gani kubwa linaloweza kupatikana chini ya ardhi?" Kisha analijibu swali lake mwenyewe:

"Majuto ya wafu ndiyo vitu vikubwa vinavyopatikana chini ya ardhi."

Kwa hiyo tunapaswa kuharakisha kufanya matendo yanayompendeza Mwenyezi Mungu na kuacha kupoteza muda wetu kwa matendo yasiyokuwa na manufaa yoyote. Tunatakiwa kuiona kila siku moja kana kwamba ni siku yetu ya mwisho kuishi hapa duniani na kutumia muda wetu kikamilifu.

Mwenyezi Mungu Mtukufu anaonyesha hali ya wale walio katika hali ya kuhuzunika kuhusu kutumia kikamilifu muda wao na anawaonyesha njia ya kujiokoa kutoka katika hali

ya kutumia vibaya muda wao na kupata baraka kutoka kwa Mwenyezi Mungu:

"Na ukipata faragha, fanya juhudi. Na Mola wako Mlezi ndio mshughulikie." (94: 7-8)

Kwa maneno mengine, tunapomaliza kufanya ibada au amali njema, tunapaswa kufanya haraka kutekeleza amali nyingine na tusiache hata dakika moja ipite bila kufanya ibada au kufanya amali njema.

Rumi anaeleza kuwa:

"Alama ya kukubaliwa ibada yetu ni kwenda kutekeleza matendo mengine mema, na kutoka kwenye amali moja kuikimbilia nyingine."

Anasema tena mahali pengine:

"Kabla kifo hakijachukua kila kitu tulichopewa, tunapaswa kutoa kila kitu kinachotakiwa kutolewa."

Kwa sababu imeelezwa katika aya ifuatayo:

"Enyi mlioamini! Toeni katika tulivyo kupeni kabla haijafika Siku ambayo hapatakuwapo biashara, wala urafiki, wala uombezi. Na makafiri ndiyo madhalimu." (2: 254)

Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ anasema kuwa:

"Harakisheni kufanya matendo mema (Kabla ya hamjadirikiwa) na zahma ambayo itakuwa kama sehemu ya usiku wa giza. Wakati huo mtu atakuwa Muislamu asubuhi na kuwa kafiri jioni au atakuwa muumini jioni na kuwa kafiri asubuhi, na ataiuza dini yake kwa vitu vya kidunia." (Muslim, Kitab Al-Iman, 186, Tirmidhi, Kitab Al-Fitan, 30: Kitab Al-Zuhd, 3)

Kwa hiyo wakati tukiwa bado tuna nafasi, tunapaswa kufanya haraka katika kufanya mambo mema. Kufanya maan-

dalizi kwa ajili ya Akhera linatakiwa liwe lengo la kila muumini. Ni muhimu tusidanganywe na raha za muda za ulimwengu huu na tusisahau kwamba mali ni sawa na hazina inayopatikana ndotoni.

MALI HALISI YA MTU NI ILE ANAYOIANDAA KWA AJILI YA AKHERA

Siku moja familia ya Mtume ﷺ ilichinja kondoo na kuigawa nyama yake. Mtume ﷺ akauliza: "Kuna nyama yoyote iliyobaki?"

Aisha رضي الله عنها akasema:

"Mfupa wa bega ndiyo uliobaki."

"Hivyo nyama yote tumebaki nayo isipokuwa ile ya mfupa wa bega!" (Tirmidhi, Sifat Al-Qiyamah, 35)

Abdullah bin Shihhīr anasimulia:

Siku moja Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa akisoma Sura ya Takāthur (102). Alipomaliza kusoma, akasema:

"Mwanadamu anadai: mali yangu, mali yangu. Hapo (Mtume s.a.w) akasema: Ewe Mwanadamu, je kuna chochote chako zaidi ya kile ulichokula, kile ulichotumia, au kile ulichovaa na kisha kikachakaa au ukakitoa kama sadaka na kupelekwa mbele?" (Muslim, Kitab Al-Zuhd Wa Al-Raqāiq, 3 -4)

Katika Hadith nyingine, Mtume wa Mwenyezi Mungu anaonyesha moja ya mandhari ya Siku ya Kiyama kama ifuatavyo:

"Na (bila shaka) kila mmoja wenu atasimama mbele ya Mwenyezi Mungu na hapatokuwa na pazia wala mkalimani baina yake na Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi Mungu ata-

muuliza, 'Je sikukupa mali?' atajibu kwa kukubali. Kisha atamuuliza tena, 'je sikukuletea mjumbe?' na kwa mara nyingine mtu huyo atajibu kwa kukubali kisha ataangalia upande wake wa kulia ataona moto, na kisha ataangalia kushoto na kuona moto. Na hivyo, kila mmoja wenu anapaswa kujiokoa kutokana na moto kwa kutoa (sadaka) hata kipande cha tende, na ikiwa hana kipande cha tende, basi (afanye hivyo) kwa kusema maneno mazuri (kwa ndugu yake). (Bukhari, Zaka, 9, 10: Riqāq, 31: Tawhīd, 36).

Hivyo kila kitu tutakachokabiliana nacho siku ya Kiyama, kikiwa kizuri au kibaya, kinatokana na yale tuliyoyatenda katika hii dunia. Ndiyo maana Mola wetu anatuonya katika Qur'an:

"Enyi mlioamini! Mcheni Mwenyezi Mungu, na kila nafsi iangalie inayoyatanguliza kwa ajili ya Kesho. Na mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu anazo habari ya mnayoyatenda." (59: 18)

Sheikh Sadi anasema kuwa:

"Watu wenye akili wanapokwenda katika ulimwengu mwingine huondoka na mali na pesa zao. (Yaani hutoa sadaka kwa ajili ya Mwenyezi Mungu) lakini wale wenye ubakhili huziacha mali zao hapa hapa duniani wakati wanazitamani."

JIOKOENI NA MARADHI YA UBAKHILI

Ubakhili na kujitenga na *infaq* ina maana ya kuyatupa maisha yetu ya Akhera katika hatari. Katika Qur'an Tukufu Mola wetu anatuonya kama ifuatavyo:

"Na toeni katika njia ya Mwenyezi Mungu, wala msijitie kwa mikono yenu katika maangamizo. Na fanyeni

wema. Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wafanyao wema." (2: 195)

Mali na baraka, isiyotumiwa kama sadaka, ni kama rafiki asiyeaminika. Muda unapofika na maisha yakafikia kikomo, itaonyesha uasi wake na kumuacha mmiliki wake peke yake na akiwa mnyonge. Wale wanaotarajia kupata utiifu kutoka kwenye mali na miliki zao wanapaswa kuzitoa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mtukufu na kuzituma mali huko Akhera ili wakutane nazo huko pindi watakapoondoka katika huu ulimwengu. Ili kulifikia hili, ni lazima kuondokana na ubakhili wa nafsi.

Umuhimu wa kuushinda ubakhili kwa ajili ya kupata wokovu wa milele umeelezwa ndani ya aya kama ifuatavyo:

"...Na mwenye kuepushwa uchoyo wa nafsi yake, basi hao ndiyo wenye kufanikiwa." (59:9)

Hata hivyo Ibilisi hukimbilia kutumia aina mbalimbali za mbinu na kupandikiza mbegu za upotevu ndani ya nyoyo. Hujaribu kuwahadaa wanadamu japokuwa Mwenyezi Mungu ndiye mpaji pekee wa baraka. Hili limeeelezwa ndani ya aya ifuatayo:

"Shet'ani anakutieni hofu ya ufakiri na anakuamrisheni mambo machafu. Na Mwenyezi Mungu anakuahidini msamaha na fadhila zitokazo kwake. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye wasaa, Mwenye kujua." (2: 268)

'Ali ﷺ, ambaye alizijua vizuri sana mbinu za Ibilisi, alikuwa akiwausia magavana wake kuwa na ithaar na ukarimu na akiwaonya kwa kusema:

"Msiwaruhusu watu wafuatao kuingia katika baraza lenu la ushauri; mtu bakhili anayekuhofisheni na ubakhili na kuwakatisheni tamaa ya kutoa sadaka, mtu mwoga anayeyadho-

ofisha maamuzi yenu ya kufanya mambo makubwa, na mtu mwenye tamaa anayewaelekeza kufanya dhulma na kuwashauri kwamba uchoyo ni kitu kizuri."

Wale wanaoweza kujiokoa na ubakhili wa nafsi na vishawishi vya shetani wanajua vizuri sana kwamba sadaka yao haipotei; kinyume chake inawasubiri huko Akhera. Jambo hili limeelezwa katika hadith kwamba:

"Kuna sifa tatu ambazo naweza kuzizungumzia kwa kuapa, zitambue vizuri: Kwa kutoa sadaka, mali ya mtu haipungui. Mwenyezi Mungu ataiongeza heshima ya wale wanaovumilia pindi wanapoonewa.

Mwenyezi Mungu huwafungulia mlango wa umasikini wale wanaofunga milango ya kuomba-omba." (Tirmidhi, Zuhd, 17)

Rumi anaonyesha kwamba kutoa sadaka hakupunguzi kiasi cha mali kama ifuatavyo:

"Upandaji wa mbegu safi katika ardhi ya Mungu, na hakuna mapato (hiyo haiwezekani)." [77]

"Kwa kuwa ardhi hii ya kifo haiwezekani bila kuzalisha, itakuwa vipi ardhi ya Mungu iwepo (bila mazao)? Hiyo (ardhi ya Mungu) ni mahali penye wasaa." [78]

"Kwa hakika, mazao ya ardhi hii (ya Mungu) hayana kikomo: hata (zao) dogo la mbegu moja ni mara mia saba." [79]

Kila dakika moja ya maisha, ambayo ni mtaji usiokadirika kwa ajili ya Akhera, ni mbegu ya maisha ya peponi ambayo itabadilika kuwa almasi za milele. Lakini hizi mbegu zisizokadirika tukizitumia vibaya kwa ajili ya matamanio ya nafsi, basi

77. Mathnawi, IV, 1759
78. Mathnawi, IV, 1761
79. Mathnawi, IV, 1763

zitabadilika kuwa mazao ya moto. Huzuni iliyoje kwa wale wasiokuwa na furaha! Nyakati ambazo zimepambwa kwa moyo wa Qur'an na Sunnah, ni mbegu za furaha ambazo zitaota katika mabustani ya peponi.

Mali ambayo haikutolewa sadaka ni sawa na wale wasiokuwa waaminifu kwa marafiki zao. Wakati mali inayotolewa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu ni kama rafiki mwaminifu na mzuri. Ukweli huu umeelezwa katika maneno yafuatayo ya Mtume ﷺ:

"Mali ni rafiki maridhawa wa muumini iwapo ataitoa kwa ajili ya masikini, yatima na msafiri." (Ahmad, III, 21)

"Siku ya Kiyama kila mtu atakuwa chini ya kivuli cha sadaka yake." (Ghazālī, Ihyā, I, 626)

'Ubayd bin Umayr anaelezea ukweli huu kama ifuatavyo:

"Watu watafufuliwa na njaa kubwa sana, kiu, na bila mavazi. Hata hivyo Mwenyezi Mungu atawalisha wale waliowalisha masikini katika dunia; Mwenyezi Mungu atawaondolea kiu wale walioondokana na kiu kwa ajili ya Mwenyezi Mungu."

Mola wetu anawapa habari njema wale wenye kuifikia kwa ukali Siku ya Kiyama:

"Wale wanaotoa mali zao usiku na mchana, kwa siri na dhahiri, wana ujira wao kwa Mola wao Mlezi; wala haitakuwa hofu juu yao, wala hawatahuzunika." (2, 274)

Kwa kifupi tunapaswa kuigeuza infāq kuwa tabia yetu ya asili, tujaribu kuwa katika kufanya jitihada za infāq, kujua thamani ya muda wetu na kuutumia katika kufanya wema.

Mola wetu Mtukufu anasema ndani ya Qur'an Tukufu " وَالْفَجْرِ *Naapa kwa Alfajiri*" [80] na wakati wa alfajiri una maana maalumu kwa maisha yetu. Tutayajaza vipi maisha yetu? Ni muda gani tutautumia kwa ajili yetu na kiasi gani cha muda tutakachotumia kwa ajili ya masikini na wenye shida? Malaika wanaoandika matendo yetu wataandika nini katika vitabu vyetu kwa ajili ya Akhera? Muumini anatakiwa kutafakari kwa makini majibu ya maswali haya na kuutumia muda wake kwa matendo mazuri. Anapaswa kuyakubali maneno yafuatayo kutoka kwa Omar ﷺ kama msingi wa maisha yake: *"Jiulize kabla hujaulizwa".*[81]

Kama asemavyo Omar b. Abd al-Aziz:

"Ukitaka kwenda Akhera, fanya maandalizi kulingana na eneo hilo."

Tumalizie sura hii kwa kuitikia Amin kwenye dua ifuatayo ya Abu Bakr ﷺ:

"Ewe Mwenyezi Mungu! Eneo bora la maisha yetu ni mwisho wake; na eneo bora la matendo yetu ni matokeo yake; na siku bora ya maisha yangu ni siku nikapounganana nawe!" [82]

Amin...

80. Qur'an, 89: 1
81. Ibn Kathir, *Tafsir*, I, 27
82. Suyuti, Tarikh al- Khulafa, uk. 103



UDUGU

Anas bin Malik ﵁ anasimulia:

"Mtume ﷺ ilikuwa kama hajamuona mmoja katika ndugu zake katika Uislamu kwa muda wa siku tatu humuulizia. Kama ndugu yake yuko mbali humuombea dua; kama yupo nyumbani humtembelea; kama yu mgonjwa humtakia afya njema (Haythami, II, 295)

Hivyo basi sharti la kwanza la kuwa ndugu katika Uislamu ni kuacha kuwa mzigo. Kwa maneno mengine ni kujaribu kutokuwa mzigo wa lazima kwa ndugu yake katika Uislamu; kinyume chake anatakiwa ajaribu kumpunguzia uzito ndugu yake.

UDUGU

Udugu katika Uislamu ni sheria ya hali ya juu ambayo iliwekwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu baina ya waumini na iwapo masharti yake yakizingatiwa vizuri basi thawabu zake ni kubwa. Ni chimbuko la amani, utulivu na furaha. Vile vile udugu wa Kiislamu ni kuwa na uwezo wa kuwapenda waumini wote; kuwa rafiki wa dhati na muwazi, kushiriki katika furaha na machungu ya ndugu zako, na ni kuwa na uwezo wa kujitolea nafsi kama na pindi inapohitajika.

Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ anasema:

"Kuna watu miongoni mwa waja wa Mwenyezi Mungu ambao siyo mitume wala mashahidi lakini mitume na mashahidi wote watawatazama kwa wivu siku ya kiyama kwa sababu ya daraja yao mbele ya Mwenyezi Mungu."

Maswahaba wakauliza:

"Ni watu gani hawa ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, na wamefanya nini wakapata malipo hayo? Tuambie ili tuwapende na tuwafanye kuwa marafiki zetu."

Mtume wa Mwenyezi Mungu akajibu:

"Ni wale watu ambao japokuwa hawana udugu au uhusiano miongoni mwao, wanapendana tu kwa ajili ya Mwenyezi

Mungu, nyuso zao zitakuwa na nuru na watakaa kwenye viti vylivyotengenezwa kwa nuru. Watu watakapokuwa na hofu (siku ya kiyama), wao hawatokuwa na hofu; watu watakapokuwa na huzuni, wao hawatokuwa na huzuni."

Kisha akasoma aya zifuatazo:

"Jueni kuwa vipenzi vya Mwenyezi Mungu hawatakuwa na hofu wala hawatahuzunika. Hao ni ambao wameamini na wakawa wanamcha Mungu. Wao wana bishara njema katika maisha ya dunia na katika Akhera. Hapana mabadiliko katika maneno ya Mwenyezi Mungu. Huko ndiko kufuzu kukubwa." (10: 62 -64) (Abu Dawud, Kitab al-Buy'u, 76/3527; Hakim, Iv 170)

Katika maelezo mengine Mtume ﷺ anaeleza kuwa kuwapenda ndugu katika Uislamu humfurahisha Mwenyezi Mungu Mtukufu:

"Mtu mmoja alimtembelea ndugu yake katika mji mwingine na Mwenyezi Mungu akamtuma Malaika kwenda kumsubiri njiani na alipomjia akasema: unakusudia kwenda wapi? Akasema: Ninakwenda kwa rafiki yangu katika mji huu. Akasema: je kuna wema uliomfanyia (na unakwenda kuchukua malipo yake)? Akasema: hapana, ninampenda tu kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, Mtukufu. Hapo akamwambia: Mimi ni kiumbe kutoka kwa Mwenyezi Mungu (nimekuja kukupa habari) kuwa Mwenyezi Mungu anakupenda kama unavyompenda (kwa ajili yake)."

Hadith hii imepokelewa na Hammid bin. Salama kwa mtiririko huo huo. (Muslim, Kitab al-Birr, 38; Ahmad b. Hanbal, II, 292)

Mtume wa Mwenyezi Mungu anasema kwamba:

"Mwenyezi Mungu atawapa kivuli watu saba siku ya kiyama, wakati ambapo hakutakuwepo na kivuli isipokuwa kivuli

chake. (Watu hawa saba ni) mtawala mwadilifu, kijana aliyekulia katika kumuabudu Mwenyezi Mungu (yaani anamuabudu Mwenyezi Mungu kwa ikhlas tokea utotoni), mtu ambaye moyo wake umeshikamana na msikiti (yaani anaswali swala za faradhi msikitini kwa jamaa), watu wawili wanaopendana kwa ajili ya Mwenyezi Mungu tu na wanakutana na kushirikiana kwa ajili ya Mwenyezi Mungu tu, mtu anayekataa wito wa mwanamke mzuri wa kumtaka afanye naye zinaa naye akasema: Ninamuogopa Mwenyezi Mungu, mtu anayetoa sadaka kwa siri sana kiasi kwamba mkono wake wa kushoto haujui kinachotolewa na mkono wa kulia (yaani hakuna mtu ajuaye kiasi gani mtu huyo katoa sadaka), na mtu anayemkumbuka Mwenyezi Mungu katika faragha na macho yake yanatiririsha machozi." (Bukhari, Adhan, 36)

Lengo kuu la waumini wenye ukomavu la kuwapenda ndugu zao katika dini ni kupata radhi za Mwenyezi Mungu Mtukufu. Njia pekee ya kuwa karibu na ndugu katika Uislamu na kunufaika na dua zake ni kuwa mja bora wa Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Katika Usufi, udugu au usuhuba katika njia moja ina maana ya kusaidiana kwenye safari ya kwenda kwa Mwenyezi Mungu na kusaidiana katika mambo ya kidini na ya kidunia. Vile vile ni kupunguza mahitaji ya ndugu yako na kushirikiana naye katika matatizo yake, jambo ambalo huonyesha njia bora na ya mfano ya kuishi katika udugu wa Kiislamu.

Siku moja Bishr Khafi alimtuma Aswad bin. Salim kwenda kwa Ma'ruf al-Karhi. Aswad akamwambia Ma'ruf kuwa:

"Bishri Khafi anataka kuwa ndugu yako. Kwa sababu ya kuona aibu kukuomba binafsi, amenituma kwako. Anatumaini kuwa utakubali wazo lake la udugu ; lakini pia ana baadhi

ya maswali kuhusu kama ataweza kuchunga majukumu ya udugu .”

Hapo Ma’ruf al-Karhi akasema:

“Nisingependa kumuacha ndugu yangu peke yake na kuwa pamoja naye usiku na mchana” na kisha akasimulia maneno kadhaa wa kadhaa ya Mtume ﷺ kuhusu ubora wa hali ya juu wa udugu katika Uislamu. Ili kumfafanulia asili na jinsi udugu wa kweli unavyopaswa kuwa akasema:

‘Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ alimfanya Ali kuwa ndugu yake, kwa sababu hiyo Ali akawa mshirika wake katika elimu. Akamuozesha binti yake mtukufu. Kwa kuwa Bishr amekutuma, basi shuhudia kuwa nimemkubalia kama ndugu yangu kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Hata kama hawezi kunitembelea, nitamtembelea. Mwambie kuwa tunaweza kuonana kwenye mikusanyiko ya Kisufi. Mwambie asinifiche matatizo yake; anatakiwa anijuze matatizo yake…”

Ibn salim alimposimulia kilichotokea, Bishr Khafi alifurahi sana na kulikubali pendekezo la Ma’ruf al-Karhi.

UDUGU KATIKA UISLAMU NI BORA KULIKO UDUGU WOTE

Udugu katika Uislamu ni mfungamano wa juu kabisa ambao hauwezi kulinganishwa na urafiki wa muda au wa maisha, wala hauwezi kulinganiswa na udugu wa damu na nasaba.

Mtume ﷺ ambaye ni muasisi wa mfumo wa udugu wa kipekee katika historia, anasema kwamba:

“Kama ningetakiwa kuchukua rafiki katika wanadamu bila shaka ningemchukua Abu Bakr lakini udugu na urafiki wa Kiislamu ni bora zaidi.” (Bukhari, Salat, 80)

Kwa maneno mengine, udugu katika Uislamu ndiyo kilele cha urafiki. Mtume wa Mwenyezi Mungu aliufanya udugu katika Uislamu kuwa wenye kupendeza kwake kuliko urafiki wake na Abu Bakr, ambaye alikuwa miongoni mwa maswahaba wakubwa na alisifiwa na Mtume mwenyewe mara nyingi. Abu Bakr naye pia alijua thamani ya udugu huu na yeye mwenyewe alionyesha mfano bora wa udugu wa Kiislamu.

Udugu wa nasaba ni kitu cha muda na kinahusu huu ulimwengu. Tulipokuja hapa duniani, hatukuwa na nafasi ya kuchagua wazazi au ndugu zetu. Lakini tunaweza kuchagua yupi anayeweza kuwa ndugu yetu katika Uislamu. Hiki ndicho kitakachomsaidia mtu huko Akhera.

Hassan al-basri anasema kwamba:

"Marafiki na ndugu zetu ni muhimu sana kwetu kuliko wanafamilia wetu; kwa sababu wanafamilia wetu hutukumbuka katika hii dunia, lakini marafiki zetu watatutafuta siku ya Kiyama." (Ghazali, Ihya, II, 437)

Muhammad bin Yusuf Isfahani anasema kuwa:

"Watoto wako wanawezaje kuwa kama ndugu zako katika wema? Watoto wako watachukua urithi wako na kuutumia katika furaha na anasa. Wakati ndugu zako wema watakulilia baada yako, watafikiria kuhusu hali yako kaburini na kukuombea mema."

Kwa hiyo, sharti muhimu zaidi la udugu ni uaminifu. Kwa maneno mengine, tunatakiwa kuendelea kuwapenda ndugu zetu katika Uislamu wanapokuwa hai, na baada ya mauti yao tunatakiwa kuwa karibu na wanafamilia wao na kuwaombea mema katika maisha ya Akhera.

UDUGU WA *MUHAJIRIN* (WAHAMIAJI) NA *ANSAAR* (WASAIDIZI)

Mwenyezi Mungu Mtukufu anatupa udugu baina ya waumini waliohama kutoka Makka kwenda Madina au Muhajirun (wahamiaji) na waumini wa Madina au Ansar (wasaidizi) waliofungua mikono yao kwa ajili ya wahamiaji kutoka Makka kama mfano bora wa udugu katika Uislamu. Anatutaka tuyaratibu maisha yetu kulingana na mfano wao.

Ududu uliowekwa na Mtume ﷺ kati ya *Ansaar* na *Muhajirun* ni picha ya kipekee ya ubora. Kwa kutoa mali zao, Ansaar kwa wema kabisa waliweka mali zao zote na wakaeleza kwamba wako tayari kushirikiana mali hizo na ndugu zao kutoka Makkah. Kwa upande mwingine, *Muhajrun* walionyesha mfano bora wa kuridhika na kuwaambia ndugu zao wa madina:

"Ndugu yangu, unaweza kuhifadhi mali yako, nionyeshe tu njia iendayo sokoni."

Walionyesha mifano mingi ya kwamba udugu katika Uislamu ni muhimu zaidi kuliko udugu wa nasaba.

Katika vita vya Badr, ambavyo ni vita vya kwanza vya imani dhidi ya ukafiri, Abu Bakr ؓ alipambana dhidi ya mwanaye; Abu Ubayda bIn. Jarrah akapigana dhidi ya baba yake; na Hamza ؓ akamkabili kaka yake. Kwa maneno mengine udugu wa Kiislamu ulivunja aina zote nyingine za uhusiano.

Zubayr bin Awwam anasimulia mfano mwingine wa udugu wa kidini kutoka katika vita vya Uhud:

"Mama yangu Safiyyahh alileta sweta mbili na kusema:

"Nimekuleteeni hizi mzitumie kwa ajili ya sanda ya kaka yangu Hamza."

Tukazichukua na kwenda nazo kwa Hamza. Pembezoni mwa mwili wa Hamza alikuwepo mtu mwingine wa Ansaar aliyekufa shahidi na hakukuwa na sanda kwa ajili ya mwili wake. Tukaona kuwa siyo jambo zuri kutumia sweta zote mbili kwa ajili ya mwili wa Hamza na kumzika mtu yule bila sanda. Tuliwaweka karibu mno kwa sababu sweta moja ilikuwa ndogo na nyingine ilikuwa kubwa." (Ahmad bin. Hanbal, I,165)

Tabia hii ya udugu imesifiwa pia na Mwenyezi Mungu ndani ya Qur'an Tukufu kama ifuatavyo:

"Na walio na masikani zao na Imani yao kabla yao, wanawapenda waliohamia kwao, wala hawaoni choyo katika vifua vyao kwa walivyopewa (Wahajiri), bali wanawapendelea kuliko nafsi zao, ingawa wao wenyewe ni wahitaji. Na mwenye kuepushwa uchoyo wa nafsi yake, basi hao ndiyo wenye kufanikiwa" (59: 9)

Aya hii imejumuisha masharti ya udugu . Kwa mujibu wa hii aya, lengo halisi la udugu wa Kiislamu siyo kuwa marafiki wakati wa raha na furaha bali ni urafiki, ukaribu na kushirikiana matatizo ya ndugu zetu katika nyakati za shida. Pia ina maana kuwatanguliza ndugu zetu juu ya mahitaji yetu wenyewe na kujitolea nafsi zetu kwa ajili yao.

UWE RAFIKI, USIWE MZIGO

Mtu mmoja alimwambia Junaid al- Baghdadi:

"Hatuoni tena udugu wa kweli. Udugu wa zamani umekwenda wapi?" Junaid akajibu:

"Kama unamtafuta ndugu atakayebeba matatizo yako na kuangalia mahitaji yako huwezi kumpata katika zama hizi; lakini kama unamtafuta mtu utakayemsaidia, na kustahimilia matatizo yake kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, basi wapo wengi."

Mtume ﷺ anasema:

"Muumini ni yule aliye mzuri kwa watu na watu wanaweza kuchangamana naye. Hakuna kheri kwa wale wasiokuwa wazuri kwa watu wengine na ambao hakuna awezaye kuchangamana naye." (Ahmad b, Hanbal, II, 400; V, 335; Hakim, I, 73/59)

Kwa hiyo sharti la kwanza la kuwa ndugu katika Uislamu ni kuacha kuwa mzigo. Kwa maneno mengine ni kujaribu kutokuwa mzigo wa lazima kwa ndugu yake katika Uislamu; kinyume chake anatakiwa ajaribu kumpunguzia ndugu uzito ndugu yake.

Kuna baadhi ya masharti ya udugu wa Kiislamu ambayo yanatakiwa kuchungwa. Nayo ni haki za ndugu zetu wa Kiislamu juu yetu. Mtume wa Mwenyezi Mungu عليه السلام anazielezea kwa muhtasari haki hizi kama ifuatavyo:

"(Mambo) sita ni haki za Muislamu juu ya Muislamu mwenzake. Akaambiwa: ewe Mtume wa Allah ni yepi hayo? Akasema: unapokutana naye, msalimie; anapokualika karamu itika. Anapokutaka ushauri mshauri, na anapopiga chafya na akasema : "Alhamdulillah," wewe sema , "Yarhamuk Allah (Mwenyezi Mungu akuhurumie); na anapoumwa mtembelee; na anapofariki lisindikize jeneza lake." (Muslim, salaam, 5)

"Enezeni salaam baina yenu, wapeni chakula masikini na wenye shida; na kwa hivyo mtakuwa ndugu kama alivyokuamrisheni Mwenyezi Mungu." (Ibn Majah, At'imah, 1)

Anga yetu inatakiwa iwe pana sana kuhusiana na masharti ya udugu ; kwa sababu kiwango chetu cha udugu huonyesha kiwango cha ukomavu wetu.

1. Msaada wa muumini mwenye mali kwa ndugu yake mwenye shida ni hatua ya kwanza ya udugu . Imeelezwa katika aya ifuatayo: **"…Nawe fanya wema kama Mwenyezi Mungu alivyokufanyia wema wewe…"** (28: 77)

2. Hatua ya pili ni kuielewa maana ya aya isemayo **"… Utawatambua kwa alama zao…"** (2: 273) na kuyaangalia mahitaji ya masikini bila kusubiri wakuombe. Aya hii inatupa mafunzo ya kufikia daraja ya kiroho ambayo tunaweza tukawatambua ndugu zetu wenye shida ambao hawawezi kuwaambia marafiki zao kwa sababu ya staha yao. Hii ni hali ya juu sana ya udugu.

Watangulizi wetu wa Kiuthmaniya walikuwa wakitoa chakula kwenye nyumba za wageni na hoteli kuwapa wageni wote. Wasafiri walikuwa wakikaa hapo kwa muda wa siku tatu na wanapoondoka walikuwa wakipewa jozi mpya ya viatu iwapo walivyo navyo vikiwa vikuukuu.

Matajiri walikuwa wakitembelea magereza na kuwatoa watu ambao walifungwa kwa sababu ya madeni. Matajiri wa jamii ya Kiuthmaniya walikuwa wakienda kwenye duka la mboga na kuchagua kuangalia ukurasa wowote kwenye kitabu cha mikopo. Kisha hulipa madeni ya watu walio kwenye ukurasa ule bila hata kuwajua majina yao. Kwa kufanya hivyo waliwasaidia watu kwa ajili ya Mwenyezi Mungu.

Kutokana na uelewa huu wa udugu , wakfu zilienea kila mahali katika jamii ya Kiuthmaniya kama utandu wa buibui. Kulikuwa na wakfu zaidi ya elfu 26 zilizoanzishwa katika zama za Wauthmaniya, jambo ambalo ni uthibitisho mzuri unaoon-

yesha namna walivyotilia umuhimu udugu na mshikamano wa kijamii. Kwa mfano, wakfu wa Bezmialem Valide Sultan mjini Damascus ni ya kushangaza mno. Lengo la wakfu huu lilikuwa kufidia uharibifu uliosababishwa na wafanyakazi ili kulinda utu wao. Ni vigumu sana kwa jamii za leo zenye ubinafsi kuelewa namna watangulizi wetu walivyotilia umuhimu jambo hili.

3. Hatua ya tatu ya udugu ni kufikia kiwango cha *birr* inayomaanisha kupenda ndugu yako apate kile unachokipata wewe. Kuhusu suala hili Mtume ﷺ anasema kwamba, *"Miongoni mwenu hakuna atakayekuwa na imani mpaka ampendelee ndugu yake (Muislamu) kile anachoipendelea nafsi yake."* (Bukhari, Kitab al-iman, 7)

Mojawapo katika mifano bora kuhusu hili ulitolewa na Uthman رضي الله عنه. Ulipotokea upungufu wa maji katika mji wa Madina, alinunua kisima cha Rumah kwa kiasi kikubwa cha pesa na kukitoa wakfu kwa matumizi ya waumini. Kwa mujibu wa nukuu mbalimbali, alikuwa akisubiri kwenye mstari pamoja na Waislamu wengine wakati wa kuchota maji kwenye kisima hicho.

Wakati wa zama za Uthmaniya, watu waliweka maua mekundu mbele ya nyumba kama ishara kwamba katika nyumba hiyo kuna mgonjwa, hivyo kila mtu aliyepita karibu na eneo hilo alijua kwamba anatakiwa kukaa kimya asisababishe usumbufu, na pia aheshimu haki za nyumba husika.

4. Kiwango cha juu kabisa cha udugu wa Uislamu ni *ithaar*, yenye maana ya kuyatanguliza mahitaji ya ndugu yako katika Uislamu juu ya mahitaji yako mwenyewe. Ina maana ya kuridhika na hali mbaya uliyo nayo na kujaribu kutatua tatizo la ndugu yako pindi inapobidi. Hii ni sifa ya waumini wema, wachamungu, wakweli na wanyoofu na ni kiwango cha juu kabisa cha upendo wa udugu .

Mtume ﷺ alikuwa akiwafikiria watu wake kabla ya kujifikiria mwenyewe. Alikuwa hali wala kuilisha familia yake kabla ya maswahaba wake. Chochote alichokuwa nacho alikitoa kuwapa masikini. Wakati mwingine alikaa bila chakula kwa siku kadhaa.

Abu Hurairah ؓ anasimuliwa kuwa:

"Ninaapa kwa yule ambaye hakuna anayestahiki kuabudiwa ili yeye, (wakati fulani) nilikuwa nikilala chini kwa kulalia tumbo langu kwa sababu ya njaa, na (wakati mwingine) nilikuwa nikibandika jiwe kwenye tumbo langu kwa sababu ya njaa. Siku moja nilikaa kwenye njia ambayo wao (Mtume na Maswahaba) walikuwa wakipita. Abu Bakr alipopita nilimuuliza kuhusu aya fulani katika kitabu cha Mwenyezi Mungu na nikamuuliza kama anaweza kuniondolea njaa yangu, lakini alinijibu swali langu kisha akaondoka, hakuniondoshea njaa yangu.

Kisha akaja Omar na kupita karibu yangu nikamuuliza kuhusu aya fulani katika kitabu cha Mwenyezi Mungu, na nikamuomba kuniondoshea njaa yangu, lakini akapita bila kufanya hivyo, kwa sababu wote wawili hawakuwa na kitu cha kutoa.

Hatimaye alipita Mtume ﷺ na aliponiona akatabasamu, kwa maana alijua kilichokuwa moyoni na usoni mwangu. Akasema, "Ewe Aba Hirr (Abu Hurayra)! Nikaitika, "Labbaik, Ee Mtume wa Mwenyezi Mungu!" Akaniambia, "Nifuate." Akaondoka nami nikamfuata.

Kisha aliingia ndani nami nikaomba ruhusa ya kuingia nikaruhusiwa. Alikuta maziwa katika bakuli na kusema, "Maziwa haya yametoka wapi?" Wakasema, "Umeletewa kama zawadi na mtu fulani." Akasema, "Ewe Aba Hirr!" Nikasema, "Labbaik, Ee Mtume wa Mwenyezi Mungu!"

Akaniambia, “Nenda uniitie watu wa Suffa.” Hawa walikuwa wageni wa Uislamu ambao hawakuwa na familia, pesa, wala mtu wa kumtegemea, na pindi Mtume ﷺ alipokuwa akiletewa kitu kama sadaka alikuwa akiwatumia chote bila yeye kuchukua hata kidogo, na akiletewa kitu kama zawadi alikuwa akichukua baadhi na baadhi kuwatumia.

Agizo la Mtume ﷺ lilinihuzunisha, na nikajisemea, “Maziwa haya madogo yatawatoshaje watu wa al-suffa?” ingawa nilistahiki zaidi kunywa yale maziwa ili nipate nguvu, lakini nilivumilia! Mtume alikuja kuniagiza kuwapa maziwa. Nilishangaa iwapo nitapata hata kidogo katika yale maziwa, lakini, vyovyote vile, sikuwa na jinsi isipokuwa kumtii Mwenyezi Mungu na Mtume wake, hivyo nikaenda kuwaita. Walikuja na kumuomba Mtume ruhusa ya kuingia. Waliruhusiwa kuingia na wakakaa ndani ya nyumba.

Mtume ﷺ akasema, “Ewe Aba Hirr!” Nikasema, “Labbik, Ee Mtume wa Mwenyezi Mungu!” Akasema, “yachukue na uwape.” Hivyo nikalichukua bakuli (la maziwa) na kuanza kumpa mtu mmoja ambaye angekunywa kiasi chake na kunirudishia, kisha humpatia mwingine naye akanywa na kisha hunirudishia. Hatimaye baada ya kundi lote kunywa kiasi chao, nilifika kwa Mtume ﷺ ambaye alilichukua bakuli na kulishika kwa mkono wake, akanitazama na kutabasamu kisha akasema, “Ewe Aba Hirr!” Nikasema “Labbaik, Ee Mtume wa Mwenyezi Mungu!” Akasema, “umebaki wewe na mimi” Nikasema, “umesema kweli Ee Mtume wa Mwenyezi Mungu!” Akanambia, “kaa na unywe.” Nikakaa na kunywa. Akasema, “Kunywa,” nami nikanywa. Akaendelea kuniambia ninywe mapaka nikasema, “Hapana. Naapa kwa Mwenyezi Mungu aliyekutuma kwa haki, sina nafasi ya kuyaweka (tumboni mwangu)” akasema, “nipatie.” Nilipompa bakuli, alimsifu na

kumtaja Mwenyezi Mungu na kisha akanywa maziwa yaliyobaki.” (Tazama, Bukhari, Riqa, 17)

Kwa mara nyingine tena, tukio lifuatalo katika Vita vya Khandaq ni tukio la mfano.Imesimuliwa na Jabir ﷺ: tulikuwa tukichimba handaki siku ya vita vya Handaki na kukakutana na jiwe kubwa gumu. Tulikwenda kwa Mtume ﷺ na kusema, “kuna mwamba unaonekana kwenye handaki.” Akasema, “ninakuja huko chini.” Kisha akasimama, na hali yakuwa amefunga jiwe kwenye tumbo lake kwa maana hatukuwa na kitu cha kula kwa muda wa siku tatu. Hivyo Mtume ﷺ akachukua sepeto na kuupiga ule mwamba ukawa kama mchanga. Nikasema

“Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Naomba ruhusu niende nyumbani.” (Mtume aliponiruhusu) nilimwambia mke wangu kuwa, “Nimemuona Mtume katika hali ambayo siwezi kuivumilia. Una chakula chochote?”

Akajibu, “nina ngano na mbuzi.” Hivyo nilimchinja mbuzi naye akasaga ngano, kisha tukaiweka kwenye chungu. Kisha nikaenda kwa Mtume ﷺ na nikamwambia, “Kuna chakula kidogo kimeandaliwa kwa ajili yako, hivyo inuka ukale ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, waweza kuja na mtu mmoja au wawili.” Mtume ﷺ akauliza, “chakula hicho kina wingi gani?” Nikamuelezea. Akasema, “Ni kingi na kizuri. Mwambie mkeo asiondoe chungu kwenye moto na asiondoshe mkate wowote jikoni mpaka nifike huko.”

Kisha akasema (kuwaambia maswahaba wake wote), “Inukeni.” Muhajirin na Ansaar wakainuka. Nilipofika kwa mke wangu nikamwambia, “rehema ya Mungu iwe juu yako! Mtume amekuja pamoja na Muhajirina na Ansaar na wale waliokuwa pamoja nao.” Akasema, “je Mtume alikuuliza (una cha-

kula kiasi gani)?" Nikajibu, "ndiyo." Kisha Mtume ﷺ akasema, "ingieni na msisongamane."

Mtume ﷺ akaanza kukata mkate vipandevipande na kuweka juu yake nyama iliyopikwa. Alikuwa akifunika chungu na oveni kila alipochukua kitu. Alikuwa akiwapa maswahaba chakula na kuchukua nyama kwenye chungu. Aliendelea kukata mkate na kuwachotea nyama (maswahaba) mpaka wakala na kushiba, na hata hivyo, chakula kikabaki. Mtume ﷺ akasema (kumwambia mke wangu), "Kula na uwape wengine kwani watu wamekabiliwa na njaa." (Tazama Bukhari, Maghazi, 29; Waqidi, II, 452)

Ibn Omar ﷺ anaelezea kujitolea nafsi kwa ajili ya ndugu katika Uislamu na ukomavu wa watu kiroho wakati wa Mtume ﷺ kama ifuatavyo;

"Tuliishi katika zama hizo ambapo hakuna aliyewaza kuwa alikuwa na thamani kwa dhahabu na fedha kuliko ndugu yake katika Uislamu; ambapo leo watu wanapenda mali za kidunia kuliko ndugu zao katika Uislamu. " (Haythami, x, 285)

Hali hii hushitadi katika jamii ambazo uwiano wa maada na umaanawi vimeharibiwa kwa ajili ya kuipendelea maada. Kwa sababu ya mali na maslahi madogo ya kidunia, waumini hukasirikiana na nyoyo zao kuvunjika. Kutokana na ujinga, ubinafsi, ugumu wa moyo udugu wa Kiislamu umedhoofika.

Mtume ﷺ aliwaagiza wafuasi wake kuwapenda ndugu zao na kuwapendelea juu ya mahitaji yao wenyewe. Kwa kufanya hivyo aliwaamrisha kutengeneza jamii yenye upendo wa dhati.

Hata hivyo, upendo hauwezi kuwa maneno tupu. Hatuwezi kuzungumzia upendo wa kweli bila kujitolea nafsi, kushirikiana maumivu, kusamehe makosa, na kuwa na ithaar. Katika

hali hii udugu katika Uislamu unatakiwa kuwa wa matendo siyo wa maneno tu. Waumini wa kweli, ambao wamefikia upendo wa kweli, watakuwa ndugu wa Mtume ﷺ siku ya Kiyama.

Siku moja Mtume ﷺ alisema:

“Napenda kuwaona ndugu zangu.”

Maswahaba wakasema:

“Je sisi siyo ndugu zako ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu?”

Akasema:

“Nyinyi ni maswahaba wangu, na ndugu zangu hawajazaliwa.” (Muslim, Taharah, 39; Fadail, 28)

Ili tupate hadhi ya kuwa ndugu wa Mtume ﷺ, tunatakiwa kushirikiana katika matatizo ya waumini na kujitahidi kuyatatua matatizo yao. Kwa sababu kuwahudumia waja wa Mwenyezi Mungu ni kama kumtumikia Yeye; na kuwatumikia wafuasi wa Mtume ﷺ ni sawa na kumtumikia Mtume ﷺ.

Tunamuomba Mola wetu atufanye kuwa katika waja wake wenye furaha ambao wanachunga masharti ya udugu na kufaulu mitihani ya majukumu ya udugu . Tunamuomba azijaze nyoyo zetu kwa upendo na udugu wa Uislamu.

Amin...



KUHUISHA UDUGU

"…Nawe fanya wema kama Mwenyezi Mungu alivyokufanyia wema wewe…" (28: 77)

Mola wetu Mtukufu anatutaka tuwe kama mikono miwili inayosafishana, kwa maana ya kukidhiana haja za kila mmoja wetu za kimaada na kiroho; kushirikiana maumivu na furaha; kushauriana na kumuona ndugu katika Uislamu kama mtu mzuri.

KUHUISHA UDUGU

Mwenyezi Mungu Mtukufu aliwatangaza waumini wote kuwa na ndugu na akamfanya Mtume Wake ﷺ kuwa mfano bora wa kuonyesha masharti na mahitaji ya udugu huu. Vilevile akawafanya maswahaba wa Mtume ﷺ na marafiki wa Mwenyezi Mungu kuwa dhihirisho bora la moyo na dhamiri ya udugu. Kuilinda hazina hii ya kipekee ya furaha ni miongoni mwa majukumu muhimu mno ya waumini; kwa sababu mali hiyo haitokaa mikononi kwa muda mrefu kama haikutunzwa kikamilifu.

Kuutunza msingi wa udugu kunategemea sisi tuishi kwa huruma, upendo, adabu na dhamiri ya uwajibikaji. Kupuuza na kughafilika katika suala hili kutakuwa na maana ya kuuacha mlango wazi ili shetani apate kutafuta fursa za kuubomoa uhusiano wa waumini. Shetani anapopata fursa, haitochukua muda mrefu kwa yeye kuchochea matamanio binafsi ya waumini na kuuvunja uhusiano wao.

KUHAMASISHA AMANI BAINA YA WAUMINI

Kwa mujibu wa kanuni za Kiislamu, ni dhambi kubwa kuwa na hisia ngumu kwa ndugu yako Muislamu na kuen-

delea kumkasirikia. Kuhusu suala hili Mtume ﷺ anawaonya wafuasi wake akisema:

"Mtu akiendelea kutengana na ndugu yake (katika Uislamu) kwa muda wa mwaka mmoja, ni kama kumwaga damu yake." (Abu Dawud, Adab, 47/4915)

"Haijuzu kwa muumini kukaa mbali na muumini kwa zaidi ya siku tatu. Siku hizi tatu zikipita, anapaswa kukutana naye na kumpa salamu, akiitikia watakuwa washirika katika thawabu; lakini kama hakuitikia atabeba dhambi zake na yule aliyetoa salamu atakuwa ametoka katika dhambi ya kutengana." (Abu Dawud, Adab, 47/ 4912)

"Jiepusheni na tuhuma, kwani tuhuma ni uongo mbaya katika maongezi na msidadisiane na msichunguzane na msioneane wivu, na msijizoeze uovu, na msiwe na chuki na uadui baina yenu, kuweni ndugu na waja wa Mwenyezi Mungu." (Muslim, Birr, 30)

Abu Hurayra anasimuliwa kuwa Mtume ﷺ alisema:

Milango ya pepo haifunguliwi isipokuwa siku mbili, Jumatatu na Alkhamisi. Na kisha kila mja (wa Mwenyezi Mungu) asiyemshirikisha Mwenyezi Mungu na chochote hupewa msamaha isipokuwa yule ambaye ndani ya moyo wake kuna hisia ngumu dhidi ya ndugu yake. Malaika huambiwa: "Ahirisheni msamaha wao mpaka watakapofikia maridhiano baina yao." (Muslim, Kitab al-Birr, 35-36; Abu Dawud, Kitab al-Adab)

Kuvunja mafungamano ya udugu kunaelezwa katika aya zifuatazo kuwa ni mojawapo ya vyanzo vya kunyimwa huruma ya Mwenyezi Mungu:

"Hakika Waumini ni ndugu, basi patanisheni baina ya ndugu zenu, na mcheni Mwenyezi Mungu ili mrehemewe." (49: 10)

"…Basi mcheni Mwenyezi Mungu na suluhisheni mambo baina yenu, na mtiini Mwenyezi Mungu na Mtume wake ikiwa nyinyi ni Waumini. " (8: 1)

Katika aya zilizotajwa hapo juu, waumini wameagizwa kusuluhisha baina ya Waislamu ambao mafungamano yao yamelegea. Kwa maneno mengine udugu katika Uislamu una maana ya kuwa na uwezo wa kusahau mabishano na kujitolea nafsi kwa ajili ya udugu katika Uislamu. Kwa sababu kuendelea kumkasirikia ndugu yako katika Uislamu ni kuasi amri ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Na muumini mkomavu hawezi kuasi amri ya Mola wake kwa makusudi.

Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ anaeleza muungano baina ya imani na udugu katika Uislamu kama ifuatavyo:

"Hamtoingia peponi mpaka muwe na imani thabiti na hamtaamini (kikamilifu) mpaka mpendane. Je niwaonyesheni kitu ambacho mkikifanya mtapendana: toleaneni salamu baina yenu kwa kusema as-salaam alaykum." (Muslim, Kitab al-Iman, 93)

Kwa hiyo sharti la mtu kuwa muumini ni kuwa na uangalifu mkubwa katika kudumisha udugu katika Uislamu na kutosababisha vyanzo vya kuchukiana. Ahnaf bin Qays anasema kuwa: "Udugu ni kitu chembamba na laini, usipokilinda, kitaharibika. Daima unatakiwa kukilinda kwa kudhibiti hasira yako kiasi kwamba wale wanaokuonea watakuja na kukuomba msamaha. Ridhika na kile ulichonacho; usijitafutie zaidi kwa ajili yako binafsi na wala usitafute mapungufu ya ndugu yako." (Ghazali, Ihya, II, 466)

Kwa namna maalumu kabisa, jambo lifuatalo limeelezwa kuwa miongoni mwa sifa za muumini:

"…na wanajizuia ghadhabu, na wasamehevu kwa watu…" (3: 134)

Katika mistari ifuatayo Jalal al-Din Rumi anaashiria kuwa muumini anatakiwa kusamehe makosa ya ndugu zake, kuwatendea wema, na kuufanya udugu wao uendelee kuwa hai:

"Unapokutana na udhia kutoka kwa ndugu yako, kumbuka kwamba ameshakufanyia maelfu ya mema; kwa sababu wema ni kama muombezi wa dhambi zake."

Ni lazima kwetu kuyakumbuka mema ya ndugu yetu Muislamu na kumsamehe pale tunapoona makosa yake badala ya kumkasirikia. Vile vile tunatakiwa kujua kwamba wakati huo anahitaji msaada wetu sana.

KUCHUKIA DHAMBI; KUWAHURUMIA WAKOSAJI

Kwa mujibwa wa simulizi moja, walikuwepo ndugu wawili, mmoja akateleza na yule mwingine akaambiwa aachane na ndugu yake; lakini akasema:

"Simuachi ndugu yangu. Badala yake, sasa hivi anahitaji msaada wangu. Je ni sahihi kumuacha katika hali hiyo? Sasa hivi ninakwenda kumpa ushauri na kumuomba Mwenyezi Mungu amuongoze kwenye njia iliyonyooka."

Junayd al-Baghdadi alikuwa na mwanafunzi. Siku moja mwanafunzi alikamatwa akiwa anafanya dhambi. Aliona aibu sana kiasi kwamba aliondoka kwenye makazi ya kiroho na hakurudi. Baada ya muda, Junayd al-Baghdadi alimuona wakati akitembea sokoni. Mwanafunzi alipomuona mwalimu wake, alijisikia aibu na kutembea haraka kwenda mbali.

Junayd (Mwenyezi Mungu aibariki nafsi yake) akawageukia watu waliokuwa pamoja naye na kusema:

"Nendeni, nina ndege wangu ametoroka nyumbani"; kisha akamfuata mwanafunzi wake. Mwanafunzi alipogundua kuwa mwalimu wake anamfuata akaanza kutembea haraka. Lakini alipokuwa akikimbia akajigonga kichwani. Alipomuona mwalimu mbele yake, aliinamisha kichwa kwa aibu. Junayd akamwambia:

"Mwanangu! Unakwenda wapi? Unamkimbia nani? Mwalimu anatakiwa kumsadia mwanafunzi wake hasa katika wakati mgumu kama huu."

Kisha akamchukua mwanafunzi wake na kumpeleka kwenye nyumba ya mafunzo ya kiroho. Mwanafunzi alimuomba msamaha mwalimu na kutubu. Hali hii ni mojawapo ya matunda ya ukomavu wa kiroho katika kuwaongoza watu kwenye njia ya kweli ya Uislamu.

Udugu katika Uislamu ni kama ndugu wa damu, bali udugu wa Kiislamu ni mkubwa zaidi. Kwa mujibu wa Uislamu, kama ambavyo haturuhusiwi kuwaacha jamaa zetu kwa sababu ya makosa yao, hatupaswi pia kuwafukuza ndugu zetu kwa sababu ya dhambi zao. Linalotakiwa ni kuwashika mkono wale wanaoanguka. Hii ndiyo sababu kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu akasema kuhusu jamaa wa Mtume ﷺ:

"Na ikiwa watakuasi basi sema: Mimi najitenga mbali na hayo mnayoyatenda." (26: 216) Cha kushangaza katika aya hii Mtume ﷺ naye pia anaagizwa kuwaambia jamaa zake "Najitenga na mnayoyatenda" siyo "Najitenga na nyinyi". Kwa maneno mengine, chuki ya kuichukia dhambi isipelekwe kwa wakosaji. Muumini hapaswi kuzungumzia mambo kuhu-

su ndugu yake Muislamu ambayo hatopenda yazungumziwe, akiwa yupo au hayupo.

Hata hivyo hairuhusiwi kukaa kimya katika kumuamrisha yaliyo sawa na kumkataza mambo mabaya anayoyafanya. Kwa maneno mengine, wakati mwingine ni muhimu kumshauri ndugu yako Muislamu katika faragha. Wakati huo, siyo muhimu alipende hili au la; na japokuwa maonyo yetu yanaweza kuonekana kama yanamuumiza, kwa hakika yatakuwa ni msaada mkubwa kwake.

Siku moja Abdullah bin Mubarak alisafiri na mtu mwenye tabia mbaya. Safari yao ilipofikia tamati, Abdullah bin Mubarak akaanza kulia. Marafiki zake walishangaa kwa nini alikuwa akilia. Akawajibu huko macho yake yakiwa yamejaa machozi:

"Japokuwa tulisafiri pamoja, sikuweza kurekebisha makosa ya rafiki yangu. Sikuweza kubadilisha tabia yake mbaya. Na sasa ninawaza kama mimi ninaweza kuwa na ufanisi kwa sababu ya mapungufu yangu. Asipopata njia sahihi kwa sababu ya makosa yangu, nitakuwa katika hali gani siku ya Hukumu?" na akaendelea kulia.

Jambo lifuatalo limeelezwa katika hadith ya Mtume ﷺ:

"Ndugu wawili, wanaopendana kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, wanapokutana, wanakuwa kama mikono miwili inayosafishana. Waumini wawili wanapokuwa pamoja, Mwenyezi Mungu humfanya mmoja wao kunufaika na mwingine." (Ghazali, ihya, II, 394)

Mola wetu anatutaka tuwe kama mikono miwili inayosafishana, kwa maana ya kusaidiana katika haja za kimaada na kiroho, kushirikiana katika maumivu na furaha, kushauriana na kumuona ndugu katika Uislamu kama mtu bora.

Kuwa na mtazamo mzuri kuhusu ndugu katika Uislamu anapoonekana akifanya kitu kibaya na kuchukulia kwamba huwenda kuna uelewa mbaya au ana sababu nzuri za kufanya jambo husika, nayo ni miongoni mwa adabu za udugu . Waumini daima wanapaswa kuamiliana vyema; wasiwadharau ndugu zao badala yake wawaone kama waja wazuri kuliko wao mbele ya Mwenyezi Mungu.

MSINGI WA AWALI WA UMOJA: UDUGU WA KIISLAMU

Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliamiliana na Waislamu wa mwanzo kwa huruma; makabila ya Kiarabu ambayo hapo mwanzo yalikuwa na uadui dhidi yake, yakawa na urafiki naye wa karibu. Aya ifuatayo inaashiria urafiki huu:

"Na shikamaneni kwa Kamba ya Mwenyezi Mungu nyote pamoja, wala msifarikiane. Na kumbukeni neema ya Mwenyezi Mungu iliyo juu yenu: vile mlivyokuwa nyinyi kwa nyinyi maadui naye akaziunganisha nyoyo zenu; kwa neema yake mkawa ndugu. Na mlikuwa ukingoni mwa shimo la Moto, naye akakuokoeni nalo." (3: 103)

Uzuri ulioje wa maelezo ya jalal al-Din Rumi kuhusu udugu wa Kiislamu:

"Mtume Muhammad ﷺ anasema kuhusu Waislamu, "Wao ni kama nafsi moja." Wamekuwa nafsi moja kupitia kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu; kabla ya hapo, walikuwa maadui wakubwa, wanaochukiana. Makabila mawili ya Aws na Khazraj walikuwa na nyoyo zenye kiu ya damu za wao kwa wao. Kupitia (mahubiri ya) Mustafa [Muhammad ﷺ] uhasama wao wa muda mrefu ukafutwa na nuru ya Uislamu na usafi (wa

moyo). Kwanza, maadui hao wakawa ndugu kama matunda ya (mkungu wa) zabibu katika bustani; na (kisha) kwa maneno yaliyoagizwa, waumini wa kweli ni ndugu, waliungana (na kuchanganyikana) wakawa mwili mmoja." [83]

Majangwa ya Arabia ambayo yalikuwa maziwa ya damu kutokana na dhulma, machafuko, ujinga na uhasama mkubwa wa umwagaji damu kabla ya kudhihiri kwa Uislamu, yalibadilika kuwa mabustani adhimu ya ustaarabu kupitia nuru ya Uislamu. Udugu wa Kiislamu ni urithi wetu mtakatifu tulioachiwa na zama za furaha *(asrus Saadah)*. Kwa maadili ya udugu katika Uislamu waumini wameishi katika amani na umoja kwa karne nyingi licha ya tofauti zao za rangi, kabila, madhehebu na uelewa. Kuupoteza umoja wetu wa kijamii ni hasara kubwa mno kwa mtu mmoja mmoja na kwa jamii yote. Udugu wa Kiislamu ndiyo tiba pekee ya maradhi mbalimbali kama vile matamanio binafsi, migogoro ya kisiasa, chuki na hasira.

Udugu wa kweli wa Kiislamu ni kama miili miwili tofauti inayoishi na moyo mmoja. Rehema na baraka za Mwenyezi Mungu huwa pamoja na wale wanaosimama na kukaa pamoja. Nguvu na mafanikio ni mazao ya umoja.

Kisa kifuatacho ni maarufu sana. Mtu mmoja mwenye hekima aliwaita wanawe alipokuwa katika dakika za mwisho za uhai wake hapa duniani na kuwataka walete vijiti. Kisha akawafunga pamoja vijiti hivyo na kuwaambia wanawe;

"Haya vunjeni vijiti hivi." Waliposhindwa kuvivunja alivitenganisha na kuwaambia wanawe:

"sasa chukueni kijiti kimoja kimoja na mkivunje." Wakafanya kama walivyoambiwa na baba yao na kuvivunja. Hapo mzee huyo mwenye busara akawageukia na kuwaambia:

83. Mathnawi, II, 3711 - 3716

"Wanangu! Nyinyi ni kama hivi vijiti. Mkikaa pamoja hakuna atakayeweza kuwashinda; lakini mkitengana, mtashindwa." Kwa namna hiyo akawausia kuwa pamoja kwa kutumia mfano hai.

Wale wanaoungana na kupendana kwa ajili ya Mwenyezi Mungu wanasifiwa katika aya ifuatayo:

"Kwa hakika Mwenyezi Mungu anawapenda wanaopigana katika Njia yake kwa safu kama jengo lililokamatana." (61: 4)

Suala la waumini kutakiwa kuwa wamoja linaelezwa katika maneno yafuatayo ya Mtume ﷺ:

"Mfano wa hali ya Muumini kwa muumini mwenzake ni kama matofali ya ukuta, yanayokamatana." Wakati akisema maneno haya aliifumbata mikono yake kwa kuingiza vidole ndani ya vidole vingine. (Bukhari, Salat, 88, Muslim, Kitab al-Bir, 65)

Rumi anasema katika suala hili kwamba: *"Kama wao (watukufu) ni maelfu (kwa nje), siyo zaidi ya mmoja (katika uhalisia) ..."* [84]

KUHISI MAUMIVU YA NDUGU YAKO MUISLAMU

Ndiyo maana kwamba waumini hufurahi pale ndugu zao Waislamu wanapokuwa na furaha na uhuzunika pale wanapokuwa na maumivu. Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ anaelezea ukweli huu katika maneno yafuatayo:

"Waumini katika kuhurumiana, kupendana na kutendeana wema, utawaona kama mwili mmoja, ambapo kiungo kimoja

84. Mathnawi, III, 35

cha mwili kinapoumwa mwili wote hushirikiana nacho kwa kukesha na kuhisi homa." (Bukhari, Adab, 27, Muslim, Kitab al-Bir, 66).

Kusikia maumivu ya muumini mwenzako na kutafuta ufumbuzi wake ni aina ya ibada ya kijamii, ambayo huvuta radhi za Mwenyezi Mungu Mtukufu. Ndiyo maana kwamba kila muumini anatakiwa kuhisi huzuni ya ndugu yake muumini katika moyo wake.

Kwa hali hiyo, hali ya Abu al-Hasan al-Haraqānī ni mfano kamili kwetu. Anasema kuwa:

"Kama kidole cha ndugu yangu wa Kiislamu kutoka Turkistan mpaka Damascus kikichomwa na mwiba, huhisi maumivu ya mwiba ule; Jiwe likiugonga mguu wake, huugonga mguu wangu pia na huhisi maumivu yake. Kama kuna huzuni katika moyo, moyo huo ni kama moyo wangu."

Hivi ndivyo moyo wa muumini unavyotakiwa kuwa na hisia kuhusu ndugu yake Muislamu. Mtume wa Mwenyezi Mungu anatuambia kutohisi maumivu ya ndugu zetu katika Uislamu ni kinyume na maadili ya Kiislamu. Anasema kuwa:

"Siyo katika sisi yule anayelala ameshiba na hali ya kuwa jirani yake ana njaa." (Hakim, II, 15)

Katika hadith kama hiyo anasema:

"Wale wasioshiriki huzuni za waumini siyo katika sisi." (Tazama Hakim, IV, 352; Haythamī, I, 87)

Kwa hiyo, kwa mujibu wa kanuni za Kiislamu, kutojali matatizo ya muumini ni dhambi kubwa. Sariyy al-Saqatī, ambaye siku moja alitenda dhambi hiyo kubwa kwa sababu ya uzembe wake wa muda mfupi tu, anasema yafuatayo kuhusu majuto yake:

"Siku moja soko la Baghdad liliungua. Mtu mmoja akaja kwangu akikimbia na kuniambia kwamba: "Bwana we! Kuna habari njema, soko lote limeungua isipokuwa duka lako." Nikasema bila kufikiria machungu ya ndugu zangu kuhusu hasara walioipata: "*Alhamdulillah* -Himidi zote ni za Mwenyezi Mungu." Kwa muda wa miaka thelathini, nimekuwa nikitubu dhambi yangu hii." (Hatīb al-Baghdādī, Tarikh, IX, 188, Dhahabi, Siyar, XII, 185-86)

Kutubu kwa kipindi cha miaka thelathini kwa kosa la muda mfupi tu! Tafakari iliyoje!

Mke wa Omar bin. Abdulaziz, Fatimah, anasimulia yafuatayo kuhusu hali ya moyo wa mume wake, uliolelewa katika malezi ya hisia ya udugu wa Kiislamu:

"Siku moja nilikwenda katika chumba cha Omar bin. Abdulaziz. Alikuwa amekaa kaiweka mikono yake juu ya mashavu akilia. Akasema;

"Fatimah! Ninahisi uzito wa watu wangu mabegani mwangu. Masikini, mafukara, wagonjwa wote wanahitaji tiba lakini hawaipati, wanaohitaji mavazi lakini hawawezi kumudu gharama, yatima, wajane, wanyonge, mateka Waislamu walio katika ardhi za makafiri, vikongwe wasiokuwa na nguvu wameachwa wafanye kazi, familia zenye watu wengi wanaohitajia kulishwa…Ninapofikiria kuhusu watu hawa, nahisi kuangamizwa chini ya uzito wa majukumu. Kesho nitamjibu nini Mola wangu akiniuliza kuwahusu?" (Ibn Kathir, 9 / 201)

Mfano uliotajwa hapo juu unaonyesha hisia wanayotakiwa kuwa nayo walio katika nyadhifa za uongozi. Hata hivyo moyo wa muumini unatakiwa kuwa pamoja na ndugu zake katika imani. Mojawapo ya mifano isiyokuwa na kikomo kutoka katika maisha ya maswahaba ni huu ufuatao:

Katika miaka ya mwanzo ya Uislamu, baadhi ya waumini walihamia Abyssinia (Ethiopia). Huko walikutana na mambo mema. Baada ya muda, walirudi Makka baada ya kusikia habari zisizokuwa sahihi kwamba washirikina wa Makka wameukubali Uislamu. Washirikina wa Makka waliposikia kwamba Waislamu wamepokelewa Abyssinia, waliongeza mateso yao dhidi ya Waislamu.

Uthman bin. Madh'un ﷺ ambaye alikuwa chini ya ulinzi wa ndugu yake Walid bin. Mughirah, alipoona mateso na unyanyasaji wa watu wa Makka dhidi ya Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷻ na wafuasi wake, alianza kutafakari:

"Naapa kwa Mwenyezi Mungu, ni kosa kubwa kwangu kuishi chini ya ulinzi wa ndugu yangu Walid badala ya kukabiliana na mateso wanayokumbana nayo. Ulinzi wa Mwenyezi Mungu ni bora na wa salama kwangu." Hivyo akaenda kwa Walid ambaye alikuwa akimlinda na kumwambia;

"Ewe mwana wa Ami yangu! Ulinipatia ulinzi wako na umetekeleza ahadi yako vizuri sana. Sasa ningependa kuacha kuwa chini ya ulinzi wako niende kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ. Yeye na maswahaba wake ni mfano bora kwangu. Nipeleke kwa Makuraish na uwaambie kuwa kwa sasa siishi chini ya ulinzi wako tena." [85]

Uthman bin Madh'un ﷺ aliona kuwa ni bora akae na ndugu zake na kushirikiana nao katika matatizo na shida. Alifikiria kuwa haitokuwa sahihi kwake kukaa kwa raha hali ya kuwa ndugu zake wapo katika taabu. Kwa sababu hakuweza kufanya chochote kingine, alifanya kile alichoweza kufanya, ambacho ni kushirikiana maumivu. Katika wakati wetu huu tunapaswa kuzijenga fikra zetu katika kutafakari hali za Waislamu wanyonge na masikini duniani kote.

85. Ibn Ishak, *siret*, Konya 1981, uk. 158; Haythami, VI, 34.

SWAHABA ALIYEACHA IBADA YA ITIKAFU KWENDA KUMSAIDIA MUUMINI

Muumini hutafuta njia za kufika kwenye radhi za Mwenyezi Mungu kwa kutatua matatizo ya ndugu zake. Mtume wa Mwenyezi Mungu *anasema;*

"…Mwenyezi Mungu humsaidia mja madamu mja huyo anamsaidia ndugu yake …" (Muslim, Kitab al-Dhikr, 37-38)

"…Muislamu ni ndugu wa Muislamu. Hamdhulumu, hamdhalilishi na wala hamdharau. Uchamungu upo hapa, (alisema hivyo huku) akiashiria kifuani mwake mara tatu. Ni uovu mkubwa kwa Muislamu kumdharau Muislamu mwenzake. Mambo (hayo) yote ya Muislamu ni haramu kwa Muislamu mwenzake: damu yake, mali yake na heshima yake." (Bukhari, Mazālim, 3, Muslim, Kitab al-Bir, 58).

Hii ndiyo sababu kwamba muumini anapaswa kuhisi ndani ya moyo wake huzuni ya ndugu yake na kufanya lolote analoweza kulifanyia kazi. Amali bora ambayo Mwenyezi Mungu anairidhia ni kujitolea nafsi kwa ajili ya ndugu katika imani na kuyatanguliza mahitaji yao juu ya mahitaji na furaha yako binafsi.

Kwa kuwa maswahaba walilelewa na Mtume ﷺ, waliokolewa na maradhi ya kusema "mimi mwenyewe, mimi mwenyewe" wakafikia daraja ya kusema "watu wangu, watu wangu." Ufuatao ni mfano kutoka katika maisha ya maswahaba:

Ibn Abbas رضي الله عنه alipokuwa katika *I'tikaf* ndani ya msikiti wa Mtume ﷺ, mtu mmoja alimjia na kumtolea salamu. Ibn Abbas رضي الله عنه akaitikia salamu yake na kusema:

"Ndugu yangu, nimekuona ukiwa mwenye huzuni na kuchoka.'

Akajibu:

"Ndiyo, Ewe binamu wa Mtume, nina huzuni. Kuna mtu nina haki yake, lakini naapa kwa Mwenyezi Mungu, sina uwezo wa kuilipa." Ibn Abbas ﷺ akasema:

"Je ungependa nizungumze na mtu huyo?" Alipojibu kwa kukubali, Ibn Abbas aliondoka msikitini haraka. Yule mtu akamuita kwa sauti:

"Umesahau kuwa umo ndani ya *I'tikaf*" Ibn Abbas ﷺ akamjibu:

"Nilimsikia mwenye hili kaburi (akiashiria kaburi la Mtume) akisema kwamba:

"Mwenye kufuatilia haja ya ndugu yake na kuishuguhulikia, ana thawabu zaidi kuliko kukaa ndani ya *I'tikaf* kwa miaka kumi; na kukaa *I'tikaf* kwa siku moja kwa ajili ya Mwenyezi Mungu hutengeneza fuo (mahandaki/mitaro) tatu baina ya muumini na moto. Upana wa kila ufuo ni sawa na umbali baina ya mashariki na magharibi." (Bayhaqi, shuab, III, 424 -25)

Maneno yafuatayo ya Mtume yanaelezea thamani ya kushughulikia mahitaji ya muumini mbele ya Mwenyezi Mungu:

"Mwenyezi Mungu amewaumba waja ambao hukimbiliwa na watu kwa haja zao. Watu hao ndiyo wenye kusalimika na adhabu za Mwenyezi Mungu Siku ya Kiyama." (Haythami, VIII, 192)

BARAKA KUTOKA KWA MWENYEZI MUNGU: MWEZI WA RAMADHAN

Siku za mwezi wa Ramadhan ni baraka za aina yake kuishi kulingana na misingi ya udugu wa Kiislamu. Katika mwezi

huo wenye baraka, waumini wanapaswa kuchukulia uzito suala la kutekeleza masharti ya udugu wao.

Mtume ﷺ alikuwa mkarimu zaidi na kuzidisha ibada na kutoa sadaka zaidi katika kipindi cha Mwezi wa Ramadhan. Alipoulizwa:

"Ni sadaka gani yenye thawabu kubwa zaidi?" akajibu:

"Ile inayotolewa katika mwezi wa Ramadhan…" (Tirmidhi, Zakat, 28/663)

Mwezi wa Ramadhan ni msimu ambao mema yote hulipwa maradufu zaidi. Mwezi wa Ramadhan una usiku wa (laylatu) Qadr, ambao ni bora kuliko miezi elfu moja. Kwa hali hiyo basi, wale wanaotekeleza kikamilifu masharti ya mwezi huu hupata baraka zisizokuwa na kikomo. Kwa upande mwingine, wale wanaokwenda kinyume nayo, watakumbana na matokeo mabaya. Mtume ﷺ anasema kuhusu suala hili:

"…Malaika Jibril alinijia na kusema "Wale wanaofika mwezi wa Ramadhan na wakawa hawajasamehewa wawe mbali na rehema za Mwenyezi Mungu." Nikasema "Amin" kwa dua yake…" (Hakim, IV, 170 / 7256. Tirmidhi, Da'awāt, 100/3545)

Kama ambavyo mvua za mwezi Aprili zinazodondokea kwenye miamba haziwezi kuleta faida, ni muhumu kuelewa maana halisi ya mwezi wa Ramadhan ili kupata faida kubwa itokanayo na mwezi huu. Tunapaswa kuuchukulia Mwezi wa Ramadhan kama fursa ya kufidia hasara zetu za mwaka mzima na kufanya kila tuwezalo kufaidika na kunufaika na rehema na baraka zake.

Katika zama za Uthmaniya, wakati wa mwezi wa Ramadhan nyumba zilijaa wageni kwa ajili ya futari.kila usiku watu kutoka kada mbalimbali walikuwa wakialikwa kwenye futari. Baada ya futari wageni walikuwa wakiletewa zawadi zilizoitwa

"zawadi kwa ajili ya meno." Kutegemea na na wageni husika, zawadi hii wakati mwingine ilikuwa ni nguo na wakati mwingine pesa katika bahasha. Baada ya swala ya *tarawih*, wageni walileteweа asali. Waumini matajiri walishirikiana na masikini katika shida zao kwa kuwapatia sadaka na zaka. Kwa hali hiyo wanajamii walikuwa wakifurahiana, wakichangamana na kuzisafisha nyoyo zao.

Furaha iliyoje kwa wale wenye kuzithamini baraka za mwezi wa Ramadhan na wakastahiki kupata baraka ya wokovu wa milele! Furaha iliyoje kwa wale wanaouchukulia kila usiku kama usiku wa (laylatul) Qadr na kuzitumia vizuri kila fursa wanazozipata!

Tunamuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu atujaalie kuwa waumini wema tunaoishi na kuwasaidia kwa dhati waumini wengine wanaoishi kulingana na misingi ya udugu wa Kiislamu! Atupe baraka ya maisha yaliyojaa matendo mema yatakayomridhisha na kutufanya tupate wokovu wa milele!

Amin…

KUPENDA NA KUCHUKIA KWA AJILI YA MWENYEZI MUNGU

Wale walio mafaqiri wa muongozo wa imani na hawajui kupenda ni kama meli iliyo katikati ya bahari bila usukani.

Kupenda mno vitu visivyostahiki kupendwa ni hasara kubwa katika ulimwengu huu. Upendo uliobanwa kwenye maslahi rahisi na yasiyokuwa na maana ya dunia hii ni kama maua yanayoota kwenye lami, ambayo muda mfupi au baadaye yatakanyagwa na kuharibiwa. Bahati mbaya iliyoje kwa almasi iliyotupwa mtaani! Hasara kubwa iliyoje kwa almasi hiyo kumilikiwa na mtu asiyestahiki!

KUPENDA NA KUCHUKIA KWA AJILI YA MWENYEZI MUNGU

Upendo huibuka kutokana na mtazamo wa sifa alizonazo mpendaji kwa yule anayempenda. Kadri Mwenyezi Mungu Mtukufu anavyozidi kuona sifa zake kwa mja Wake, ndivyo anavyozidi kumpenda. Kwa maneno mengine, kadiri mja anavyozidi kujipamba na tabia njema zilizoamrishwa na Mwenyezi Mungu na Mtume Wake ndivyo anavyozidi kupata upendo kutoka kwa Mwenyezi Mungu.

Vituo vyote ulimwenguni vipo kutokana na vinyume vyake. Kwa kuwa kinyume cha upendo ni chuki, kuchukia kile kinachochukiwa na Mwenyezi Mungu ndiyo njia halisi ya kuonyesha upendo wetu kwake.

Katika sura moja ya Qur'an Tukufu, Mwenyezi Mungu Mtukufu anamlaani Abu Lahab, ambaye alimuonea Mtume Wake. Katika sura hii maalumu Mwenyezi Mungu anatoa tangazo kwa wanadamu wote. Hivyo basi, tunaweza kusema kwamba upendo wako wa kukipenda kitu utakuwa pungufu na usiokuwa wa dhati bila kukichukia kilicho kinyume na kitu hicho.

Mwenyezi Mungu Mtukufu ndiye Muumba, Chanzo, na kituo cha mwisho cha upendo. Muumini anapaswa kukubali kuwa upendo wake wote ni upigaji hatua kuulekea upendo

wa Mwenyezi Mungu, kwa sababu upendo wa kweli huanza baada ya kupita juu ya vizuizi vyembamba vya kupenda vitu visivyodumu. Furaha ya muda ya upendo wa vitu visivyodumu (vyenye kufa) ikilinganishwa na furaha ya upendo wa Mwenyezi Mungu, ni dhaifu na hafifu kama mwanga wa taa ukilinganishwa na mwanga wa jua. Uzuri ulioje wa maneno ya Jalal al-Din Rumi katika mistari ifuatayo:

"Mwenyezi Mungu ameupa nguvu upendo wa Kimungu kiasi kwamba anayekunywa tone moja ataondokana na wasiwasi wa ulimwengu huu na wa baadaye." [86]

Marafiki wa Mwenyezi Mungu ni mifano halisi ya kufikia kilele cha upendo wa Mwenyezi Mungu. Waumini wa kweli, wanaoonja ladha ya upendo wa Kimungu, humpenda Mwenyezi Mungu, Mtume Wake, na kila kitu wanachokipenda. Kwa hali hiyo kila aina ya upendo huyeyuka ndani ya upendo huu.

Kuwapenda wazazi, watoto, mali, uhai, marafiki na jamaa, majirani, taifa, bendera, nchi, n.k kwa ajili ya Mwenyezi Mungu ni dalili ya kuufikia uhalisia wa upendo. Aina zote hizi za upendo huupa moyo amani na utulivu, japokuwa vinaelekezwa sehemu nyingine tofauti na Mwenyezi Mungu, kwa sababu vinapendwa kwa ajili Yake.

MATUNDA YA MTI WA UTUME

Kwa mujibu wa hadith moja, siku moja Mtume wa Mwenyezi Mungu alimuuliza Ali ﷺ:

"Ewe 'Ali! Je, unampenda Mwenyezi Mungu Mtukufu? "

'Ali akajibu: "Ndiyo, nampenda."

86. Mathnawi, IV, 2683

"Je, unampenda Mtume wake, pia?"

"Ndiyo, ninampenda."

"Je, unampenda binti yangu Fatimah?"

"Ndiyo, nampenda"

"Vipi kuhusu Hassan na Hussein, je, unawapenda?"

"Ndiyo, ninawapenda Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu."

Basi Mtume wa Mwenyezi Mungu akasema:

"Ewe 'Ali! Una moyo mmoja tu, lakini unawapenda wanne. Unawezaje kuyapanga mapenzi mengi katika moyo mmoja? "

'Ali hakuweza kujibu swali hili. Alikwenda nyumbani kwake kuwaza juu ya jibu lake. Fatimah alipomuona mume wake akiwa na wasiwasi kuhusu kitu, akaja kutaka kujua sababu yake. Akamuuliza kwa upole.

"Unaonekana kuwa mwenye mawazo. Kuna kitu kibaya kimekutokea? Kama una wasiwasi na kitu chochote cha dunia hii, basi hutakiwi kuwa na wasiwasi nacho; kama ni kitu kinachohusu Akhera, basi niambie ni kitu gani?"

Ali ﷺ alimwambia kilichotokea. Fatimah ﷺ alipoelewa kila kitu, alitabasamu na kusema:

"Nenda kwa baba na umjibu swali lake kama ifuatavyo." Akampa Ali baadhi ya nukta kuhusu jibu la swali hilo. Ali alipendezwa na jibu lake akaenda moja kwa moja kwa Mtume ﷺ:

"Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Binadamu wana mielekeo mbalimbali kama vile Kaskazini, Kusini, Mashariki na Magharibi. Moyo nao pia una uelekeo. Ninampenda Mwenyezi Mungu kwa akili yangu; ninakupenda kwa roho na imani yangu; ninampenda Fatimah kwa nafsi yangu ya kibinadamu;

ninawapenda Hassan na Hussein kwa sababu ya hisia ya kimaumbile ya mimi kama baba.

Mtume wa Mwenyezi Mungu aliposikia jibu hili akatabasamu na kusema:

"Ewe Ali! Haya maneno ni matunda yaliyochukuliwa kutoka katika mti wa utume." [87]

MAJARIBU NA VISHAWISHI VYA DUNIA

Kumsahau Mola na furaha ya milele aliyowaahidi waja Wake kwa kutekwa na tamaa za vitu visivyodumu ni upumbavu mkubwa. Ni kama mfano wa mbwa mwindaji wa sultani katika kisa cha Fariduddin Attar, aliyesahau mmiliki wake akakimbilia kipande cha mfupa wakati wa sherehe ya kuwinda. Maisha katika dunia hii yamejaa mifupa na vyambo sawa na hivyo vilivyotajwa katika mfano huo.

Jalal al- Din Rumi anasema:

"Oh, ni samaki wangapi walio salama baharini ambao, kwa sababu ya uroho wa koo zao wamekamatwa na ndoana!"[88]

Hili halitofautiani sana na mja kumsahau Mola wake kutokana na kuwa mtumwa wa tamaa za nafsi. Kudanganyika na uzuri bandia wa ulimwengu huu na kupoteza daraja za juu mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu ni kama upumbavu wa kubadilisha chombo kilichopambwa kwa almasi ghali na kipande kidogo cha bati kisichokuwa na thamani yoyote. Jalal al- Din anaelezea kudanganywa huko kwa istiari ifuatayo:

87. Tazama Türkiye Gazetesi İslâm Âlimleri Ansiklopedisi, Juz. I, uk. 145.
88. Mathnawi, III, 1695

"Siyo ajabu kwamba kondoo amemtoroka mbwa mwitu; ajabu ni kuona kwamba kondoo huyu kauweka moyo wake (kafanya urafiki) kwa mbwa mwitu." [89]

Muumini wa kweli ni kiumbe mtukufu zaidi miongoni mwa viumbe. Hapaswi kujishusha hadhi kwa kuuelekeza upendo wake kwenye uelekeo usiokuwa sahihi. Hapaswi kusahau utu na shakhsia yake kwa funda moja ya anasa za hii dunia. Hapaswi kudhani kuwa matamanio ya dunia hii ya muda ndiyo chimbuko la furaha ya kweli.

Qur'an Tukufu inasema:

"Je! Umemwona aliyeyafanya matamanio yake kuwa ndiyo mungu wake? Basi je, wewe utakuwa ni wakili wake?" (25: 43)

Katika hadith moja ya Mtume ﷺ imeelezwa kuwa:

"Mbaya zaidi miongoni mwa miungu ya uongo katika dunia hii, ambayo Mwenyezi Mungu anaichukia mno, ni matamanio ya nafsi na mawazo ya ajabu ajabu." (Haythami, I, 188)

Zunnun al-Misri anaeleza njia sahihi ya kutumia chuki na upendo kama ifuatavyo:

"Tunahitajika kuwa marafiki wa Mwenyezi Mungu na maadui wa nafsi; siyo marafiki wa nafsi na maadui wa Mwenyezi Mungu."

Ili kuwa marafiki wa Mwenyezi Mungu tunatakiwa kulindwa dhidi ya utumwa wa nafsi. Kwa maneno mengine hatutakiwi kushindwa na kuzidiwa na matamanio ya nafsi ili tuweze kufikia urafiki wa Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Lakini, wale walio mafukara wa muongozo wa imani na hawajui upendo ni nini ni kama meli katikati ya bahari bila

89. Mathnawi, I, 1293

usukani. Tamaa za nafsi huwavuta watu hawa. Huiharibu akili, uelewa wao na dhamiri; kwa sababu moyo usioshughulishwa na vitu sahihi, hujazwa mawazo mabaya na ya batili. Kama nchi iliyokaliwa na majeshi ya adui, kadhalika hapawezi kuwa na amani katika moyo uliotiwa utumwani na tamaa chakavu.

Upendo unaokwenda kinyume na hadhi ya imani unaweza kusababisha mgogoro kati ya muumini na nafsi yake na kuiharibu imani yake. Upendo huo unaweza hata kumpeleka kwenye ukafiri. Kisha, kama ambavyo tunakuwa waangalifu juu ya vile tunavyokula na kuwa makini juu ya uhalali wa chakula chetu, ndivyo tunavyotakiwa kuwa waangalifu juu ya upendo tunaouruhusu kuingia katika nyoyo zetu. Ili kulinda imani yetu tunahitaji:

KUWAPENDA WALE WANAOSTAHIKI KUPENDWA NA KUWACHUKIA WALE WANAOSTAHIKI KUCHUKIWA

Kama hisia za kupenda na kuchukia kwetu siyo kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, na kama tunawapenda wale tunaohitaji kuwapenda na kuwachukia wale tunaohitaji kuwachukia, basi hili ni janga kubwa la kiroho kwetu. Ndiyo maana kupenda na kuchukia vinapaswa kuelekezwa kwa watu sahihi.

Qur'an Tukufu inasema kuwa:

"Enyi mlioamini! Mcheni Mwenyezi Mungu, na kuweni pamoja na wakweli." (9: 119)

Kwa sababu, daima tunapata baraka, hali ya kiroho, na nishati chanya kutoka kwa watu wema; na kinyume cha mambo haya, kuwapenda maadui wa dini na watenda dhambi, huleta balaa. Aya tukufu inasema kuhusu suala hili:

"… jitenge nao mpaka waingilie mazungumzo mengine…" (6: 68)

Kusifia kitu kilichofanywa na adui wa Uislamu, hata kama hakihusiani na dini kama vile kujenga ukuta, huleta taathira hasi kwenye moyo wa muumini; kwa kuwa kuistaajabia kazi yake kutainua heshima yake binafsi, itasababisha ghadhabu ya Mwenyezi Mungu. Kwa bahati mbaya Waislamu wengi walioghafilika hawaelewi kwamba msimamo huo hudhoofisha shakhsia yao na utambulisho wao wa Kiislamu.

Katika suala hili, tuuchukue werevu wa Sultan wa Kiuthmaniya, Bayazid II, kama muongozo kwetu. Kipindi cha sultan Bayazid II, ndiyo kipindi ambacho iliwekwa misingi ya utamaduni na ustaarabu wa Kiuthmaniya.

Mchoraji na mbunifu maarufu wa Kiitaliano Leonardo da Vinci alituma barua kwa sultan Bayazid na kumpa wazo la kuchora ramani za ujenzi wa misikiti na minara mingine katika mji wa Istanbul. Wazo hili lilipokelewa kwa furaha na msisimko kutoka kwa mawaziri wa Ikulu ya Topkapi, lakini Sultan alilikataa na kusema:

"Tukikubali pendekezo hili, nchi yetu itatawaliwa na mtindo wa ubunifu unaofanana na makanisa ambapo mtindo wetu wenyewe hautoweza kustawi na kuendelea."

Mtazama huo unaonyesha jinsi waumini wakomavu wanavyotakiwa kufikiri. Kwa hakika, sanaa ya Kiuthmaniya ilistawi baada ya Bayazid II. Kutokana na mtazamo huu, roho ya Uislamu ilipata kuingizwa katika jiemetri na minyororo ya minara kama ilivyojengwa Suleymaniye.

Watangulizi wetu wasingeonyesha hisia hii, tusingekuwa na minara hiyo mizuri na yenye kupendeza, na tusingekuwa na uwanja wa ustaarabu ulioibua wasanii wakubwa kama vile

Sinan msanifu, msanifu maandishi Hamdullah na Karahisari. Ndiyo maana tunapaswa kulinda utambulisho wetu na kuacha kunakili mitindo ya maisha ya makafiri.

Marafiki wa Mwenyezi Mungu hujizuia kuchukua msaada kutoka kwa madhalimu, watenda dhambi, makafiri achilia mbali kujifananisha nao; kwa sababu, binadamu anaweza kuwa mtumwa wa fadhila kirahisi. Hisia ya ukaribu na kuvutwa na aliyekufadhili inaweza kuota ndani ya moyo. Ndiyo maana muumini anapohitaji msaada anatakiwa kwenda kwa watu wema na kumuomba Mwenyezi Mungu asiwe masikini wa kudharaulika.

Mtume ﷺ alimwambia swahaba mmoja aliyemuuliza kama anaruhusiwa kuomba msaada wa watu wengine:

"Hapana, ni vizuri usiombe. Lakini ukilazimika kuomba, angalau nenda kwa watu wachamungu na wema." (Abu Dawud, Zakt, 28)

Katika suala hili, uzuri ulioje wa hali ya wachawi wa Fir'aun. Wachawi ambao hapo mwanzo walimsifu na kumheshimu Fir'aun, waliukubali ujumbe wa Nabii Mussa عليه السلام walipoona miujiza yake. Fir'aun aliwaghadhibikia na kuanza kuwatisha kuwa atawaua. Lakini wachawi walilinda imani yao na hawakuyakubali matakwa yake ya batili. Walimwambia mateso yako ni hapa duniani na **"Sisi ni wenye kurejea kwa Mola wetu Mlezi."** [90] Kisha wakainua mikono yao na kumuomba Mwenyezi Mungu asiwafanye waonyeshe unyonge wowote kwa sababu ya mateso ya Fir'aun, wakasema:

"Ewe Mola Mlezi wetu! Tumiminie uvumilivu na utufishe hali ni Waislamu." (7: 126) Mwishoni walipata heshima ya kuuawa kishahidi.

90. Qur'an 7: 125.

Mfano ufuato kutoka katika zama za mwanzo za Uislamu unatuonyesha kuwa muumini anatakiwa kufanya nini mbele ya wale wanaostahiki kughadhibikiwa na Mwenyezi Mungu.

Washirikina walivunja mkataba miaka miwili baadaye kwa kuwaua Waislamu kadhaa. Aidha, hawakutilia umuhimu juu ya mapendekezo mapya ya amani yaliyotolewa na Mtume. Baadaye wakaogopa na kumtuma kiongozi wao Abu Sufiyan kwenda Madina. Hakuna mtu yeyote katika mji wa Madina aliyemsikiliza Abu Sufyan. Hata mke wa Mtume ﷺ Umm Habibah ambaye alikuwa binti wa Abu Sufyan hakumsikiliza na akauondosha mkeka aliokuwa ameukalia. Abu Sufyan alishangazwa na kuuliza:

"Binti yangu! Je mimi sina hadhi ya kupata mkeka wako au siyo stahili yangu?"

Umm Habibah akamjibu:

"Mkeka huu ni wa Mtume ﷺ. Kwa sababu wewe ni mshirikina usiye msafi, haustahiki kuukalia." Abu Sufyan aliposikia maneno haya aliingiwa na baridi na kumwambia binti yake:

"Umekuwa mtu wa ajabu baada ya kuondoka kwetu." Umm Habibah akaeleza umuhimu wa imani kama ifuatavyo:

"Sijawa mtu wa ajabu bali Uislamu umenipa heshima." (Ibn Hisham, IV, 12- 13)

Kwa maneno mengine heshima na hadhi ya imani ni ya juu kuliko vitu visivyodumu. Imani ya muumini mkomavu ndiyo inayomuongoza kutompenda mtu iwapo mtu huyo anatakiwa kutopendwa, bila kujali ni nani.

Mfano mwingine ni huu ufuatao:

Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ alimtuma Uthman رضي الله عنه kwenda Makka kama mjumbe kabla ya mkataba wa Hudaybi-

yah. Japokuwa Uthman ﷺ aliwaambia watu wa Makkah kuwa nia yao ni kuizuru Kaaba, washirikina hawakuwaruhusu kuingia mjini Makka. Wakamwambia pia Uthman ﷺ kwamba:

"Ukitaka kuizuru Kaaba wewe mwenyewe, unaweza kufanya hivyo."

Waislamu wote walikuwa wakisubiri kuizuru Kaaba, na baadhi yao walimuonea wivu hata Uthman ﷺ kwa kudhani kuwa alikuwa amepata bahati ya kuizuru. Lakini swahaba huyu ambaye alikuwa amejitolea nafsi yake kikamilifu kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na Mtume Wake aliwaambia washirikina wa Makkah:

"Siwezi kuizuru Kaaba kabla ya Mtume kuizuru. Nitalizuru eneo hili tukufu baada yake. Siwezi kukaa sehemu ambayo Mtume hapokelewi." (Ahmad bin. Hanbal, IV, 324)

Sisi kama wafuasi wa Mtume ﷺ tunatakiwa kubeba hisia aliyokuwa nayo katika moyo wake. Na hili linaweza kufikiwa tu kwa kupenda kile anachokipenda na kukichukia kile anachokichukia.

DALILI ZA UPENDO WA KWELI

Katika mkusanyiko mmoja, Thawban alikuwa akimuangalia sana Mtume ﷺ kiasi cha kuvuta umakini wa Mtume ﷺ. Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ akamuuliza;

"Ewe Thawban, una nini?"

Thawban ﷺ akajibu:

"Wazazi wangu wawe fidia yako ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Mimi hukukumbuka sana kiasi kwamba nahisi uc-

hungu wa kuwa mbali nawe kila mara ninapokuwa mbali na nuru yako. Hizi ndizo hisia zangu katika hii dunia, na nilikuwa nikitafakari maumivu nitakayokuwa nayo siku ya Kiyama. Siku hiyo utakuwa pamoja na Mitume wengine, nami sijui nitakuwa wapi. Kama sitoingia peponi, sitoweza kukuona. Mawazo haya yananihuzunisha sana ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu."

Mtume ﷺ akamwambia Thawban:

"Kila mtu atakuwa pamoja na wale aliowapenda." (Bukhari, Kitab al-Adab, 96)

Dalili ya kumpenda Mwenyezi Mungu na Mtume Wake ni kujisalimisha na kutii maamrisho yao.

Kama hatufuati kwa dhati kabisa maamrisho ya Mtume wetu mpendwa ﷺ, hatuwezi kupata uombezi wake. Hili limeelezwa katika aya ifuatayo:

"Sema: Ikiwa nyinyi mnampenda Mwenyezi Mungu basi nifuateni mimi, Mwenyezi Mungu atakupendeni na atakufutieni madhambi yenu…" (3: 31)

Kwa maneno mengine, madai ya kwamba unampenda Mwenyezi Mungu na Mtume Wake ni maneno matupu mpaka madai hayo yakupeleke kwenye kutii maagizo yao. Madai ya wale wasioweza kujitolea nafsi kwa ajili ya wanaowapenda hayana maana.

Hassan al-Basri anasema kuwa:

"Enyi watu! Msiitafsiri vibaya hadith isemayo "kila mtu atakuwa pamoja na wale aliowapenda." Bila kutenda matendo ya watu wema hamtokuwa miongoni mwao. Kwa sababu Wayahudi na Wakristo wanawapenda mitume wao lakini hawako pamoja nao."

Fudayl bin. Iyad alikuwa akiiuliza nafsi yake maswali yafuatayo:

"Unapenda kuingia pepo ya Firdaus pamoja na Mitume na waja wema, lakini umefanya nini kustahili kuingia? Ni matamanio mangapi ya nafsi umeyadhibiti? Ni hasira gani umeidhibiti? Umewatembelea jamaa ambao hawakutembelei? Ni makosa mangapi ya ndugu zako umeyasamehe? Umekaa mbali na nani kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na umekurubiana na nani?" (Ghazali, Ihya, 402)

Kupenda kwa ajili ya Mwenyezi Mungu ni kutotarajia malipo zaidi ya upendo. Aina hii ya upendo huimarisha imani yetu. Hadith ifuatayo inaelezea jinsi tunavyoweza kupata ladha ya imani.

"Mwenye kuwa na sifa tatu zifuatzo atapata utamu (furaha) wa imani:

1. Yule ambaye Mwenyezi Mungu na Mtume Wake wanapendeza kwake kuliko chochote.

2. Anayechukia kurudi kwenye ushirikina (ukafiri) kama anavyochukia kutupwa motoni.

3. Kupenda kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na kuchukia kwa ajili yake." (Tazama Bukhari, kitab al-Iman, 9, 14)

Naam, ili kuhisi utamu wa imani, upendo unatakiwa kuwa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu tu. Na kwa hili, kuna baadhi ya dalili. Sahl anauelezea ukweli huu kama ifuatavyo;

"Alama ya kumpenda Mwenyezi Mungu ni mtu kuipenda Qur'an. Na alama ya kumpenda Mwenyezi Mungu na Qur'an ni kumpenda Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.). Alama ya kumpenda Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ ni kuzipenda sunnah zake. Alama ya kupenda sunnah zake ni kuipenda Akhe-

ra. Alama ya kuipenda Akhera ni kuichukia dunia (kwa maneno mengine kutodanganywa na vishawishi vyake). Alama ya kutoipenda dunia ni kujitenga nayo isipokuwa kile kidogo kinachohitajika kwa ajili ya kuipata Akhera."

Kwa muhtasari, mpendaji wa kweli huwapenda wale wanaopendwa na mpendwa wake; huvichukia vitu vinavyochukiwa na mpendwa wake; na humkumbuka mpendwa wake sana. Kuhusu suala hili Mtume ﷺ alijibu swali kuhusu imani bora kama ifuatavyo:

"Kupenda kwa ajili ya Mwenyezi Mungu; kuchukia kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na kuushughulisha ulimi na kumdhukuru Mwenyezi Mungu…" (Ahmad b. Hanbal, Musnad, 5/247)

KUPENDA NA KUCHUKIA KWA AJILI YA MWENYEZI MUNGU

Kwa mujibu wa riwaya moja, Mwenyezi Mungu Mtukufu alimuuliza Mussa عليه السلام:

"Ewe Mussa! Una amali safi iliyofanywa kwa ajili yangu tu?"

Mussa عليه السلام akajibu:

"Mola wangu! Nimetekeleza swala, nikafunga, nikatoa sadaka, na kusujudu kwa ajili yako. Nimekushukuru; nimesoma kitabu chako na kulitaja jina lako."

Mwenyezi Mungu Mtukufu akasema:

"Ewe Mussa! Swala ni muongozo wako; funga ni ngao yako; sadaka itakuwa kivuli chako na himidi wakati wa sijida zitakuwa mti kwa ajili yako peponi. Kusoma kitabu changu kutakupatia makazi na wake peponi. Kulikumbuka jina langu itakuwa nuru yako. Umefanya nini kwa ajili yangu tu?"

Hapo Mussa ﷺ akasema:

“Mola wangu! Niambie amali gani nikiifanya itakuwa kwa ajili yako tu.”

Mwenyezi Mungu akajibu:

“Ewe Mussa! Umekuwa na urafiki na mtu yeyote kwa ajili yangu? Na umemchukia mtu kwa ajili yangu? Hapo Mussa ﷺ akaelewa kwamba kupenda na kuchukia kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mtukufu ndiyo amali inayokubali zaidi mbele ya Mwenyezi Mungu. (Mukisha fat al-Qulub, 86)

Kuhusu suala hili, imesimuliwa kuwa Nabii Issa ﷺ alipewa wahyi ufuatao:

“Ukifanya ibada kwa uhai wote na iwapo ibada hizo hazitojumuisha kupenda na kuchukia kwa ajili yangu, hazitokuwa na maana yoyote.”

Ukamilifu wa ibada na miamala yetu unategemeana na undani wetu wa kiroho. Ndiyo maana kupenda na kuchukia ndani ya nyoyo zetu vinatakiwa viwe kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Hakika Mtume ﷺ alikuwa hakasiriki isipokuwa pale haki inapokiukwa na ukweli unapozuiliwa. Haki inapokiukwa, hasira yake isingetulia mpaka tatizo litatuliwe. Alikuwa hakasiriki na angejadiliana na mtu yeyote kwa mambo binafsi.

Kwa maneno mengine, muumini hapaswi kuchanganya suala la kuchukia kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na hasira ya kawaida; na anatakiwa kujua wakati gani, wapi na namna ya kukasirika. Anatakiwa kuwa makini kuhusu chanzo cha hasira yake, je ni imani yake au nafsi yake? Kwa sababu, kama hasira ikitokana na nafsi, kinachukuliwa kama kitu kibaya. Hapo hasira huitawala akili na Ibilisi kuanza kuishambulia. Kama

hasira hiyo ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, humaanisha ukomavu na jambo zuri.

Wakati wa vita, Ali ﷺ alikaribia kumuua adui. Mara adui akamtemea mate usoni na Ali karudi nyuma akawa hajamuua. Adui hakuelewa sababu ya kitendo hicho cha ajabu kutoka kwa Ali akamuuliza:

"Ewe Ali! Kwa nini umesita? Kitu gani kimetokea na kukufanya utulie? Mabadiliko hayo ya ghafla yametokana na nini? Tafadhali niambie."

Ali akamjibu:

"Ninapambana kwa ajili ya Mwenyezi Mungu tu. Ndiyo maana nawaua maadui wa Uislamu. Kamwe sichanganyi hisia zangu katika mapambano yangu. Lakini ulinitemea mate usoni na kujaribu kunifanya nikasirike. Kama ningekukasirikia, pambano langu lingekuwa kwa ajili ya nafsi yangu; wakati ninapambana kwa ajili ya kutaka radhi za Mola wangu pekee."

Kutokana na jibu hili adhimu, adui yule akapata heshima ya kuingia katika Uislamu.

Kwa muhtasari, hasira inayoishinda akili na kusababisha makosa, ni aina ya hasira inayotokana na nafsi na inatakiwa kudhibitiwa. Lakini haina maana ya kutojali na kudhibiti hasira pindi inapotokea dhulma au shambulizi dhidi ya dini, imani, maadili au hali ya kiroho. Kinyume chake, msimamo kama huo unahesabiwa kuwa ni hali ya kughafilika. Ili kupata radhi za Mwenyezi Mungu, kukasirika, pindi inapohitajika, ni muhimu kama kuidhibiti hasira.

Umar ﷺ alikuwa mwepesi wa hasira sana dhidi ya ukafiri, uonevu na dhulma. Ndiyo maana hakuna aliyethubutu kufanya dhulma mbele yake. Kwa sababu ya hasira ya Umar ﷺ, hata shetani angebadilisha njia pindi amuonapo Umar.

Mtu mmoja alikwenda kwa Junayd al- Baghdadi na kumuona shetani akikimbia mbali. Mtu huyo aliposogea karibu na Junayd al-Baghdadi, aligundua usoni mwake kuwa Junayd alikuwa amekasirika sana na akamuuliza:

"Ewe Junayd! Kama tujuavyo, shetani humkurubia mtu anapokuwa na hasira, kwa nini ameonekana akikukimbia, pamoja na kwamba ulikuwa umekasirika sana? Unaweza kuniambia hekima ya jambo hili?"

Junayd akajibu:

"Hujui kwamba hatukasiriki kwa ajili ya nafsi zetu? Watu wanapokasirika kwa sababu binafsi, shetani huwadhibiti? Kwa kuwa hasira yetu ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, tunapokasirika, shetani hukimbia bali nasi kuliko tunapokuwa tumetulia."

Tunamuomba Mwenyezi Mungu azibariki nyoyo zetu kwa daraja hiyo ya ukomavu! Akufanye kupenda na kuchukia kwetu kuwe kwa ajili yake! Atujaalie uwezo wa kuliona lililo sahihi na la batili na tulifuate la sahihi na kuliacha la batili!

Amin...

IKHLAS KATIKA KUPENDA NA KUCHUKIA

Watu wengi wasiojali, ambao wameathiriwa na nafsi zao, hudhani, bila kujua, kwamba taabu zao ni furaha. Kwa sababu hawajui kuanguka kwao na mapungufu yao, hawafanyi juhudi kuyarekebisha.

Mtume wa Mwenyezi Mungu r anasema:

"Hakika, ninaapa kwa Mwenyezi Mungu, lazima muamrishe mema na kukataza mabaya, mjaribu kumzuia mtenda dhulma, mumfungamanishe na yaliyo sahihi, na kumfanya ashikamane moja kwa moja na haki. La sivyo Mwenyezi Mungu atazifanya nyoyo zenu kufanana na zile za watenda dhambi ambao aliwalaani." (Abu Dawud, Kitab al-malahim, 17/4336)

IKHLAS KATIKA KUPENDA NA KUCHUKIA

Kama kumpenda Mwenyezi Mungu na vile anavyovipenda, kadhalika kujizuia na vitu asivyovipenda ni sharti la moyo salama, kutoonyesha chuki na upinzani dhidi ya matendo ya batili na maovu kwa kiwango hicho hicho cha kupenda matendo mema ni dalili ya udhaifu na upungufu wa imani. Mtume ﷺ anasema:

"Anayependa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na kuchukia kwa ajili ya Mwenyezi Mungu; akatoa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na akajizuia kutoa kwa ajilia Mwenyezi Mungu huipeleka imani yake kwenye ukamilifu. (Tirmidhi, Sifat al-Qiyamah, 60)

Kwa hiyo, muumini mkomavu huweka siyo tu mawazo yake bali pia hisia zake kulingana na radhi za Mwenyezi Mungu. Anapopenda kitu, hukipenda kwa ajili ya Mwenyezi Mungu; na anapokichukia kitu, hukichukia kwa ajili tu ya Mwenyezi Mungu. Kipimo cha hisia zake ni "kuendana na radhi za Mwenyezi Mungu."

Abdullah bin. Abbas anazungumza nasi karne nyingi zilizopita:

"Penda unachokipenda kwa ajili ya Mwenyezi Mungu; acha unachokiacha kwa ajili ya Wenyezi Mungu; tambua kwamba hii ndiyo njia ya kupata radhi za Mwenyezi Mungu. Vinginevyo, mtu hawezi kupata faida ya swala, funga, hijja

yake, nk. Kwa bahati mbaya watu wa sasa wamevutika sana kwenye ulimwengu huu. Kupenda na kuchukia kwao ni kwa ajili ya manufaa ya kidunia tu …"

HISIA YA IMANI INAPOPOTEA

Uwezo wa kutafuta radhi za Mwenyezi Mungu katika kupenda na kuchukia unapopotea, mtu husika hugeuka kuwa mwanasesere anayechezewa na nafsi yake. Huyatanguliza maslahi ya kidunia kabla ya mambo ya imani. Kisha huanza kuyachukulia mabaya na maovu kwa urahisi akidhani kuwa anafanya subira; hapigi hatua ya kuyakomesha akidhani kuwa kufanya hivyo kutaumiza mahusiano yao. Kitendo hicho siyo tu kwamba kina madhara kwake mwenyewe bali pia kina adhara kwa huyo mtu anayemvumilia kwa makosa yake.

Katika jambo hili Sufyan al-Thawri anaeleza kuwa:

"Mtu anapofanya makosa, na yule anayedai kuwa ni ndugu yake akawa hakumuonya kwa upole, jueni kwamba upendo wake siyo kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Kama ungekuwa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, angemuonya mja huyo anayemuasi Allah kwa kutumia lugha nzuri."

Uvumilivu wa ubinafsi unaoonyeshwa kwa wale walio kwenye njia ya batili husababisha kuenea kwa dhambi katika jamii. Kisha dhambi hizi huanza kuonekana kama mambo ya kawaida na wanajamii kuyatenda bila kujali. Kuanguka kwa Wana wa Israeli kulianza baada ya kuridhia dhambi kwa hofu ya kupoteza maslahi yao.

Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ anatuhabarisha jambo hili kama ifuatavyo:

"Katika siku za mwanzo, wana wa Israeli walikuwa wakimwambia mtu wanapomuona akitenda dhambi:

Walikuwa wakimuonya kwa kumwambia "Tazama rafiki yangu! Muogope Mwenyezi Mungu na acha kufanya dhambi hiyo. Kwa sababu, jambo hili siyo halali kwako." Kisha siku ya pili wanapomuona mtu huyo huyo katika hali hiyo hiyo (wanafikiria maslahi yao), wanaacha kumuonya ili wapate kukaa na kula pamoja naye. Kisha Mwenyezi Mungu Mtukufu akazichanganya nyoyo zao pamoja."

Wakati Mtume ﷺ akisema maneno haya alikuwa ameegemea kitu, mara akanyooka na kumalizia maneno yake kama ifuatavyo:

"Hakika, ninaapa kwa Mwenyezi Mungu, lazima muamrishe mema na kukataza mabaya, mjaribu kumzuia mtenda dhulma, mumfungamanishe na yaliyo sahihi, na kumfanya ashikamane moja kwa moja na haki. La sivyo Mwenyezi Mungu atazifanya nyoyo zenu kufanana na zile za watenda dhambi ambao aliwalaani." (Abu Dawud, Kitab al-malahim, 17/4336)

ENEO DHAIFU LA WAISLAMU: KURIDHIA MAOVU

Kuridhia kitu unakofanywa kwa sababu za manufaa ya kidunia hudhoofisha imani. Leo hii, maridhiano mengi, yanayohatarisha imani, yanafanywa bila kupima mambo ya kidunia na kidini kwenye msingi wa Qur'an na Sunnah. Lakini, lililo baya zaidi ni kwamba watu wengi wasiojali, ambao wameathiriwa na nafsi zao, hufikiri, bila kujua, kwamba taabu zao ni furaha. Kwa sababu hawajui kuanguka kwao na mapungufu yao, hawahisi haja ya kujirekebisha.

Kuzorota jamii yetu, kwa sababu ya uvamizi wa kidunia wa kiutamaduni, kwa bahati mbaya kumeleta mambo mengi yaliyo kinyume na roho ya Uislamu. Hatua muhimu sana za maisha zimechanganywa na matendo yasiyokuwa ya Kiislamu na shetani amefanywa kuwa mshirika wao. Lakini, maelezo yafuatayo ya Mwenyezi Mungu kuhusu shetani, aliyefukuzwa na Mwenyezi Mungu, ni onyo muhimu sana kwa wanadamu:

"Na wachochee uwawezao katika wao kwa sauti yako, na wakusanyie jeshi lako la wapandao farasi na waendao kwa miguu. Na shirikiana nao katika mali na wana, na waahidi. Na Shetani hawapi ahadi ila ya udanganyifu." (17: 64)

Kwa hakika Waislamu wengi wameisahau dini yao katika sherehe muhimu sana za maisha yao, kama vile harusi, kutahiri, mazishi, n.k Kinyume chake sikukuu hizi zinapaswa kuwa nyakati muhimu zaidi za maisha ambapo Waislamu huikumbuka dini yao na kuwa na mwenendo unaoendana na utambulisho wa Kiislamu. Kwa sababu dini siyo kitu cha kipindi fulani cha maisha, bali inapaswa kuwa mtindo wa maisha unaopenya katika vipengere vyote vya maisha. Kwa hiyo, haiwezi kuwa kitu kinachofuatwa kipindi fulani na kuachwa katika kipindi kingine.

Badala ya kuishi maisha yetu kulingana na misingi safi ya Kiislamu, kuzifunika nyakati muhimu za maisha yetu kwa matendo yasiyokuwa ya Kiislamu ni kitendo kibaya ambacho ni kama kudondosha kipande cha uchafu katika glasi ya maji safi na kuyafanya yasifae kunyweka.

.Wakati wa zamani, sherehe za harusi na kutahiri zilikuwa zikifanyika katika misikiti au bustani, na tenzi na sura za Qur'an zilikuwa zikisomwa katika sherehe hizi. Masikini na matajiri nao walialikwa bila ya ubaguzi wowote. Baada ya karamu hizo, dua zilikuwa zikiombwa. Hasa masikini na mafuka-

ra walikuwa wakialikwa na watu walikuwa wakifaidika na dua zao kwa kufurahisha hapa duniani na Akhera; kwa sababu watu walikuwa waangalifu sana kuhusu kufuata onyo lifuatalo kutoka kwa Mtume ﷺ:

"Chakula kibaya zaidi ni kile cha karamu ya harusi ambacho matajiri tu ndiyo wanaoalikwa na masikini hawaalikwi." (Bukhari, Nikāh, 72)

Kwa namna hiyo kila mtu alishiriki katika sherehe ya kiroho na utulivu. Lakini leo hii wale wenye mali wanashindana kuonyesha uwezo wao wa mali, na hufanyia sherehe zao katika mahoteli na migahawa ya kifahari ambayo masikini hapigwa marufuku kuingia.

Kundi dogo tu la vibopa ndiyo wanaoalikwa katika sherehe hizi; matumizi mabaya na ya kifahari yanayohamasisha ulafi na ubadhirifu. Baadhi yao hutoa pombe, kitu ambacho ni haramu kabisa ndani ya Uislamu, na hunywewa bila kujali kana kwamba zinaruhusiwa katika sherehe hizo. Wazazi wengi wanaojifanya kuwa wanyoofu na makini wanastahimilia sherehe za watoto wao zinazotoa pombe, wacheza muziki, na zilizojaa mambo mengine mengi yanayokwenda kinyume na mwenendo wa Kiislamu; kwa hali hiyo hupingana na masharti ya imani zao.

Ujumbe unaopatikana katika wosia na ushauri unaotolewa kwa maharusi, nao pia umeanza kubadilika. Wazazi walikuwa wakiwaambia mabinti wao:

"Unatoka katika nyumba hii ndani ya nguo nyeupe ya harusi na unapaswa kutoka katika nyumba ya mumeo ndani ya sanda nyeupe."

Kwa namna hiyo, wazazi walikuwa wakiwausia uaminifu na kujitolea kwa ajili ya waume zao na kuzihamasisha nyoyo

za binti yao kuhusu nyumba yake mpya. Pia walikuwa wakiwausia kuwa na subira kwa mambo ya kifamilia. Hivyo walikuwa wakitengeneza jamii imara na yenye siha; wakati ambapo kwa bahati mbaya wazazi wa leo wanawapa ushauri watoto wao kana kwamba ni marafiki wanaopeana ushauri. Huwaambia:

"Usikubali kuzidiwa; mume wako akikwambia jambo moja, usikubali kushindwa na mjibu na mambo mawili na zaidi." Hivyo wanatengezwa na kujazwa chuki kuanzia siku ya kwanza ya ndoa yao. Bila shaka siyo jambo gumu kukisia ni aina gani ya ushauri unaotolewa kwa bwana harusi.

Hatupaswi kusahau kwamba sababu ya kuongezeka kwa kiwango cha talaka, mafarakano, vita, matatizo ya kisaikolojia zinatokana na kuzorota kiroho kwa zama tulizonazo. Isisahaulike kuwa kila sababu ya dhahiri ina sababu ya ndani.

Hata shughuli za mazishi, mojawapo ya nyakati za maana katika maisha, zimekuwa sehemu ya watu kuonyesha uwezo wao. Watu wameanza kuona fahari kwa shughuli zao za mazishi kuhudhuriwa na watu wenye uwezo katika jamii. Kuchapisha kwenye magazeti ya kila siku majina ya watu muhimu waliohudhuria mazishi na kuwashukuru ni kitu kinachokwenda kinyume na roho ya mazishi.

Mbali na hayo, badala ya kuwasaidia masikini kwa niaba ya marehemu na kuombewa dua na watu mafukara, watu wameanza kufuata desturi za Kikristo na kutuma mashada ya maua kwenye shughuli za mazishi; wakati ambapo waumini wanatakiwa kwenda kwenye mazishi kwa lengo la kupata radhi za Mwenyezi Mungu. Wanatakiwa kumuombea mema marehemu, kutoa sadaka kwa niaba yake, na kutoa heshima zao za mwisho kwa ndugu yao huyo. Mtukufu Mtume ﷺ alikuwa akiwashajiisha maswahaba wake kutembelea nyumba

zilizopatwa na msiba na kushiriki katika huzuni za ndugu zao Waislamu. Alikuwa akiwaambia: “Kuna yeyote miongoni mwenu aliyekwenda kwenye mazishi?”

Leo hii, baadhi ya watu wanahudhuria mazishi ili tu waonekane na kwa lengo la kulinda heshima yao. Ndiyo maana watu wamekuwa wakihudhuria mazishi ya matajiri badala ya mazishi ya watu masikini.

Kwa bahati mbaya, katika dunia ya sasa, wakati ambapo maradhi ya umaada na kupenda dunia yamepenya katika kila sehemu ya jamii, baadhi ya watu wamezoa kutathmini kila jambo kwa mtazamo wa kimaada. Wanaupima utu wa mtu kwa daraja na mali yao. Kwa namna moja, shughuli za harusi, kutahiriwa, na mazishi ni maeneo ya kuupima mtazamo huu; wakati ambapo kwa muumini, kuilinda imani yake, uchamungu, na tabia njema vinapaswa kuwa vipimo vya utu na hadhi ya mtu.

Kupenda mno na kutopea katika ufahari, kuonyesha mienendo mibaya katika shughuli za harusi, mazishi, ubadhirifu, kukiuka haki za wengine, n.k yote hayo ni athari mbaya zitokanazo na tamaduni za kigeni kwa jamii yetu. Katika utamaduni wetu wa Kiislamu, tabia hizo zilizokithiri hazina nafasi.

RADIAMALI YA IMANI

Mojawapo ya tabia na sifa za waumini ni kuwa waharakiaji wa mambo mema na wazuiaji wa maovu. Kwa maneno mengine kama ambavyo kueneza mema na kuamrisha haki, kuzuia maovu na kukataza mabaya nayo pia ni sharti la imani.

Kwa mfano, muumini anayealikwa mahali ambapo dhambi zinatendwa wazi wazi anatakiwa akatae mwaliko kama huo

bila kujali nani anayemualika. Onyo la aya ifuatayo liko wazi sana:

"HAKIKA wamefanikiwa Waumini, ambao ni wanyenyekevu katika Sala zao, na ambao hujiepusha na mambo ya upuuzi." (23: 1-3)

Katika aya hii waumini wameagizwa kujiepusha na mambo ya upuuzi; kwa hiyo haiwezekani kufikiria kuwa muumini atakubali mialiko ya kwenda maeneo ambayo dhambi zinafanyika. Muumini akikumbana na hali hiyo, anatakiwa kuikataa na kumuonya kikamilifu mualikaji. Iwapo mualikaji ataongea na muumini kwa maneno yafuatayo yenye kumshawishi: "Tusipoteze muda wetu na kujilazimisha na mambo hayo katika zama wakati huu wa kisasa. Nisikilize mimi na sahau kanuni hizo zisizokuwa na maana." Maneno kama hayo ni hatari sana kiasi kwamba yanaweza kumfanya mtu apoteze imani yake. Muumini kamwe hawezi kukubali fikra kama hizi na daima huonyesha upinzani dhidi yake; kwa sababu waumini ni mashuhuda wa Mwenyezi Mungu Mtukufu kama inavyosema aya ifuatayo:

"Na vivyo hivyo tumekufanyeni muwe Umma wa wasitani, ili muwe mashahidi juu ya watu, na Mtume awe ni shahidi juu yenu…" (2: 143)

Mfano mwingine ni kuhusu kwenda kwenye maduka na masoko yanayouzwa pombe na vileo. Muumini wa kweli anatakiwa kuachana na maduka hayo haraka na kumfanya mmiliki wa duka husika anakosa wateja kwa sababu ya kuuza pombe. Na radiamali kama hiyo inapaswa kuonyeswa dhidi ya aina zote za dhambi.

Kwa sababu ya kuonyesha kuchukizwa kwetu na matendo maovu yanayoweza kuacha athari chanya kwenye moyo

wa mtu aliyetenda jambo husika. Na inatarajiwa kuwa inaweza ikamuongoza kwenye unyoofu na wema na kusababisha kuokolewa siku ya Kiyama.

Hata hivyo kuvumilia ukiukwaji wa sheria za Mwenyezi Mungu huwafanya watendaji wa dhambi waone kuwa matendo yao hayo ni ya kawaida. Wanaweza hata kuanza kujifaharisha kwa dhambi zao.

Aidha, ni muhimu kusema kuwa kutoonyesha radiamali yoyote dhidi ya ukiukwaji wa sheria za Mola wetu, wakati tukionyesha upinzani mkubwa dhidi ya njaa na kupambana na faida ndogo za kidunia, ni ishara ya udhaifu wa imani.

MARADHI YA KUIGA

Suala jingine ambalo linaiweka imani yetu katika hatari ni kujaribu kujifananisha na makafiri au watenda dhambi na maradhi ya kuiga mtindo wa maisha yao. Uharibifu katika msingi wa imani na uzorotaji wa kiakili na kimaadili kwa kiasi kikubwa huanza na kuiga. Hatimaye kuiga hubadilika na kuwa tabia na mazoea. Kisha kufanana katika muonekano hugeuka kuwa kufanana kifikra; na kufanana kifikra hugeuka na kuungana kwa nyoyo. Ndiyo maana Mtume ﷺ anasema kwamba:

"Anayejaribu kujifananisha na watu basi mtu huyo ni mmoja wao." (Abu Dawud, kitab al-Libas, 4/4031)

Kama ambavyo ni vibaya kujifananisha na makafiri katika alama za kidini, kadhalika ni makosa kujifananisha nao katika mambo ya kidunia. Kupendelea kuiga ni mara kunapatikana zaidi au kidogo katika maumbile ya mwanadamu. Leo tunashuhudia uharibifu mkubwa katika muundo wa kimaadili wa jamii ya Kiislamu.

Kwa kuwa mifano mibaya ni mingi zaidi kuliko mifano mizuri katika jamii yetu, sasa tunapaswa kuwa makini zaidi kuhusu maradhi ya kuiga. Mamilioni ya watu wanapoteza muda wao bure kwa kutazama midahalo ya kisiasa na mashindano ya michezo kwa sababu tu ya maradhi ya kuiga. Hili pia lina dalili kubwa lakini hazijagunduliwa:

Kwa mfano, vijana wa Kiislamu wanaovaa *t-shirt* yenye picha mbaya au tangazo la kigeni, wanakwenda msikitini. Kwa kuwa hawaonywi na Waislamu wenzao, hata hawajui makosa yao. Waumini wanaonekana kusahau sifa na tabia zao zilizoelezwa katika aya ifuatayo**: "Na uwe kutokana na nyinyi umma unaolingania kheri na unao amrisha mema na unakataza maovu…"** (3: 104) ambapo kukataza na kuzuia maovu na kulingania kheri kwa maneno mazuri yenye athari ni wajibu juu ya waumini wote. Hili limeelezwa katika aya ifuatayo:

"Hao ndio wale ambao Mwenyezi Mungu anayajua yaliyomo ndani ya nyoyo zao. Basi waachilie mbali, uwape mawaidha na uwaambie قَوْلاً بَلِيغاً **maneno ya kuathiri na kuingia katika nafsi zao."** (4: 63)

Kwa kuwa kutojifananisha na makafiri ni mojawapo ya masharti muhimu mno ya kulinda utambulisho na hadhi ya Waislamu, Mtume ﷺ aliwaagiza wafuasi wake kufunga tarehe 10 ya mwezi wa Muharram pamoja na siku moja ya kabla yake au moja ya baada yake au siku zote tatu. Sababu ya kuongeza siku moja au mbili kwenye funga ya tarehe 10 ya mwezi wa Muharram ni ili kwenda kinyume na matendo ya Wayahudi. Kwa maneno mengine, alituamrisha kutojifananisha nao hata katika masuala ya ibada.

Hisia ya kuchukia kitu kwa ajili ya Mwenyezi Mungu inapokufa ndani ya nyoyo zetu, tunaanza polepole kuiga mitindo ya masiha ya kidunia ya makafiri na kujifananisha nao. Tuki-

linganisha imani yetu na kipande cha kamba, nyuzi za kamba hiyo bila shaka zitaanza kukatika moja baada ya nyingine pindi tunapohisi upinzani kwa ajili ya Mwenyezi Mungu ukianza kudhoofika katika nyoyo zetu.

Wauthmaniyya walikuwa wakiishi pamoja na watu kutoka dini, lugha, na jamii mbalimbali kwa karne nyingi, hata hivyo daima waliendelea kuufanya utambulisho, utu, na desturi zao za Kiislamu kuwa hai. Achilia mbali kujifananisha na makafiri, waliiwakilisha dini yao na kuwaathiri makafiri kwa kuishi kulingana na misingi ya Uislamu. Desturi za Kiislamu zikaenea miongoni mwa makafiri.

Kwa bahati mbaya leo, kutokana na kushuka kwa uchumi wa Waislamu, tumeanza kuruhusu desturi nyingi tofauti na utamaduni wetu kuingia katika maisha yetu. Kujifananisha na makafiri katika mavazi, sherehe, sikukuu, n.k kumeanza kuongezeka kwa kasi.

Upepo wa mitindo ya mavazi umewachukua waumini na kuwaweka chini ya taathira yake angamizi. Ni muhimu kwa waumini wasijielekeze huko. Kinyume chake wanatakiwa kuunga mkono kila juhudi ya kuhuisha utamaduni wetu wenyewe na kusimama imara dhidi ya mielekeo hiyo haribifu.

Mtindo wa uvaaji wetu, upambaji wa nyumba zetu, namna tunavyoishi, n.k. vinatakiwa kuendana na misingi ya Uislamu. Kuhusu suala hili, onyo la Omar ﷺ kwa askari wa jeshi la Kiislamu, waliokuwa wakienda Azerbaijan na Dagestan, la kutoiga desturi za washirikina ni mfano muhimu sana kwetu.

MAZUNGUMZO NA WASIO-WAISLAMU

Ili kuelewa istilahi za uvumilivu na majadiliano kwa usahihi, kwanza tunahitaji kujua mtazamo wa Kiislamu kuhusu

binadamu. Uislamu unawafundisha wafuasi wake kuwaona binadamu wote kama viumbe wa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Katika suala hili siyo muhimu kuwa watu hao ni waumini au la. Uislamu unawaamrisha waumini kuwa waangalifu kuhusu kuchunga haki za wale ambao hawajapata heshima ya muongozo wa Uislamu. Mkataba uliosainiwa na Mtume ﷺ pamoja na wakazi wa Kiyahudi katika mji wa Madina ni mfano wa aina yake katika suala hili.

Kwa hiyo, hakuna tatizo kuhusu kusaini mikataba na makafiri kuhusu haki za wananchi na maslahi ya jamii maadamu katika mikataba hiyo hakuna maridhiano yanayoridhia maovu katika mambo ya dini. Uislamu unahubiri huruma na upendo katika mahusiano ya kibinadamu. Ya'la' bin Murrah anasema kuwa:

"Nilihudhuria safari nyingi pamoja na Mtume ﷺ. Kila alipoona maiti ya mwanadamu njiani alikuwa akiagiza azikwe bila kuuliza kama ni muumini au la." (Hakim, I, 526/1374)

Siku moja jeneza lilipita mbele ya Mtume wa Mwenyezi Mungu. Mara akasimama wima. Maswahaba wakamwambia:

"Ee Mtume wa Mwenyezi Mungu, ni mazishi ya Mayahudi."

Mtume ﷺ akasema:

"Je, yeye si mwanadamu?" (Bukhari, Janaiz, 50)

Uislamu unaagiza uangalifu kuhusu haki za wasiokuwa Waislamu. Uzuri ulioje wa maagizo yafuatayo ya Sultani wa Kiuthamniyya, Mehmed II kwa askari wake kuhusu ukweli huu. Siku ambayo askari hao walipoifungua Istanbul aliwaambia:

"…Msiwaguse wale wanaoomba huruma yenu. Msiwaguse wanawake, watoto, vikongwe na wagonjwa…"

Wakati huo hata jina la tamko la haki za binaadamu halikuwepo kabisa, pindi Sultan Mehmed II alipoonyesha uvumilivu wa mfano. Pindi kiongozi wa familia za Kikristo mjini Istanbul aliposikia amri ya Sultan Mehmed II, alipiga magoti mbele yake kumshukuru. Sultan akamuinua na kumwambia:

"*Katika dini yetu, ni haramu kumsujudia mtu. Tafadhali nakuomba usimame. Ninakupa wewe na wakazi wengine wa kikristo wa Istanbul haki zenu. Kuanzia leo na kuendelea, msinihofie mimi kuhusu maisha na uhuru wenu.*"

Kwa sababu ya haki na uvumilivu, Wauthmaniyya waliweza kuwafanya Wabalkan waishi katika amani na utulivu japokuwa walizidiwa na wasiokuwa Waislamu kwa idadi. Tabia hii iliwafanya makafiri wengi waweze kuipata njia ya haki. Qur'an tukufu inasema:

"Wala msijadiliane na Watu wa Kitabu ila kwa njia iliyo nzuri kabisa, isipokuwa wale waliodhulumu miongoni mwao. Na semeni: Tumeyaamini yaliyoteremshwa kwetu na yaliyo teremshwa kwenu. Na Mungu wetu na Mungu wenu ni Mmoja. Na sisi ni wenye kusilimu kwake." (29: 46)

Sehemu nyingine, familia za Waislamu zilizokuwa zimepelekwa Kosovo na Bosnia ziliwakilisha vizuri tunu za Kiislamu kwa kuishi kulingana na maana ya aya iliyotajwa hapo juu na aya nyingine mfano wake. Hivyo wakawa sababu ya makafiri wengi kuongoka.

Kuwatendea dhulma na uonevu waumini au makafiri, kitendo hicho ni mzigo mkubwa siku ya Kiyama. Kuhusu suala hili, maelezo kuhusu kwamba sultani wa Kiuthamniyya Mehmed II alisimama mahakamani na msanifu majengo asiyekuwa muumini na hukumu ikatolewa dhidi yake (sultan) ni mfano kamili wa utoaji wa haki katika Uislamu.

KANUNI ZA MSINGI ZA MAZUNGUMZO NA MAJADILIANO NA WASIO WAISLAMU

Dunia nzima ni lengo kwa ajili ya kufikisha ujumbe wa Uislamu. Mtume wa Mwenyezi Mungu alituma wajumbe kwenda kwa viongozi wa nchi jirani na kuanzisha mazungumzo nao. Maswahaba ﷺ, kwa upande mwingine, walikwenda kwenye maeneno ya mbali zaidi ili kufikisha ujumbe wa Uislamu.

Kutokana na maendeleo ya nyenzo za kiteknolojia za jamii ya sasa, waumini wana wajibu mkubwa wa kujibu tuhuma na madai ya uongo yanayotolewa dhidi ya Uislamu na kuwaeleza watu kuwa Uislamu siyo dini ya ugaidi. Kuwafundisha watu kuwa kipindi chote cha miaka 23 ya utume kilikuwa kimejaa mifano ya mapambano dhidi ya uhasama wa kigaidi na umwagaji damu. Mafunzo yanahitaji kiwango fulani cha majadiliano. Tunapaswa kuzipa kipaumbele kanuni zifuatazo za kujadiliana na wasio Waislamu:

1. Tusisahau kuwa Uislamu ndiyo dini ya haki mbele ya Mwenyezi Mungu. Japokuwa Uyahudi na Ukristo kwa asili zilikuwa dini kutoka mbinguni, kwa bahati mbaya zilifisidiwa na kuharibiwa. Kutokana na uharibifu huu, Ukristo ukaanza kuamini utatu, wakati Uyahudi ukianza kuwafundisha wafuasi wake mtazamo wa Mungu kuwa na sifa kama za mwanadamu. Uislamu pekee ndiyo dini ya kweli ya tawhid, inayolinda imani ya umoja na upekee wa Mwenyezi Mungu. Ndiyo maana hakuna namna ya kuunganisha Uislamu na dini nyingine.

2. Jambo jingine muhimu ni kulinda Ikhlasi. Majadiliano baina ya Musa ﷺ na Fir'aun yametolewa kama mfano wa jambo hili ndani ya Qura'n Tukufu. Musa ﷺ alikwenda kwa Fir'aun na kuzungumza naye kwa lugha laini. Lakini Musa ﷺ kamwe hakwenda kinyume na mipaka ya Uislamu wala kulai-

nika. Kutokana na Ikhlasi yake, wachawi wa Fir'aun walihatarisha maisha yao na kuukubali ujumbe wa Uislamu.

3. Uislamu unafundisha matumizi ya njia na mbinu halali ili kufikia malengo halali. Hatuwezi kufikia malengo halali kwa kutumia njia haramu. Hili ni mojawapo ya umakini wa Uislamu. Kipindi cha miaka 23 ya mahubiri ya Mtume ﷺ ni mfano bora wa jambo hili. Kamwe hakukimbilia kutumia njia ambazo hazijahalalishwa na Mwenyezi Mungu.

Mfano mmoja wa hili ulitokea wakati wa vita vya Badr. Kama ijulikanavyo, idadi ya makafiri ilikuwa mara tatu ya Waislamu. Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ, Ali na Lubabah walikuwa wakienda Badr wakitumia ngamia mmoja kwa kupokezana. Walipofika eneo la (Harrat-ul-Wabara (Maili nne kutoka Madina) mtu mmoja aliyekuwa akijulikana kwa ukakamavu na ujasiri alikutana nao. Maswahaba wa Mtume ﷺ walifurahi kumuona.Mtume wa Mwenyezi Mungu akamuuliza:

"Umekuja pamoja nasi?"

Hapana, lakini wewe ni mwana wa dada yetu na pia wewe ni jirani yetu. Nimekuja nikufuate ili niweze kupata sehemu katika ngawira." Mtume wa Mwenyezi Mungu akamuuliza tena:

"Unamuamini Mwenyezi Mungu na Mtume Wake?"

Akasema: Hapana.

Mtume ﷺ akamwambia:

"Rudi, hatuhitaji msaada kutoka kwa mshirikina."

Mtu huyo akasisitiza akisema:

"Mimi ninajulikana kwa ushujaa wangu katika vita. Unaonaje kama nikipigana pamoja nanyi na nipate ngawira kama malipo badala ya kuukubali Uislamu?" Mtume ﷺ akajibu:

"Rudi, hatuhitaji msaada kutoka kwa mshirikina. Kwanza ukubali Uislamu kisha uje na ushiriki nasi katika mapambano." Hatimaye mshirikina huyo akaingia katika Uislamu. Mtume ﷺ akamuuliza kama alivyomuuliza mwanzo:

"Unamuamini Mwenyezi Mungu na Mtume Wake?"

Akajibu: ndiyo.

Mtume wa Mwenyezi Mungu akamwambia: "Sasa waweza kuja pamoja nasi." *(Tazama Muslim, Jihad, 150)*

Kwa muhtasari, hatutakiwi kufanya maridhiano yatakayoiharibu dini yetu katika kujadiliana na wasio Waislamu. Hatupaswi kusahau kuwa maridhiano kidogo tu yanaweza kuiangamiza imani yetu. Hili limeelzwa katika Aya zifuatazo:

"Mwenye kumtii Mtume basi ndio amemtii Mwenyezi Mungu…" (4: 80)

"Enyi mlioamini! Msitangulie mbele ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia, Mwenye kujua." (49:1)

Kwa upande mwingine, hatupaswi kusahau pia kwamba kulainika ni udhaifu wa mtu husika na siyo jamii nzima ya Kiislamu. Tunapaswa kujiepusha kuishusha hadi jamii yote ya Kiislamu kwa sababu ya udhaifu wa mtu mmoja.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu azibariki nyoyo zetu ziwe na sifa nzuri!

Mola wetu! Tufanye kuwa wenye kuipenda imani na uzijaze nyoyo zetu baraka ya imani. Tufanye tuwe wenye kuuchukia ukafiri na dhambi; tuonyeshe njia ya kujizuia navyo. Tusaidide kuungana na wale wanaoharakisha mema na kuyazuia maovu.

Amin...

TUSISAHAU KUFA

Hatujui namna tutakavyokutana na malaika wa mauti. Tutakwenda vipi kwenye makutano yetu ya mwisho? Tutakutana na Mola wetu tukiwa katika hali ya kusujudu au tukiwa katika hali ya kutenda dhambi? Daima tunatakiwa kutafakari kwamba yepi yatakayokuwa maneno yetu ya mwisho.

Junayd al-Baghdadi anasema:

"Siku moja katika dunia hii ina thamani sana kuliko miaka elfu moja katika Akhera. Kwa sababu ukiwa duniani una nafasi ya kupata radhi za Mwenyezi Mungu, hali yakuwa huko Akhera hutopata fursa ya kutenda matendo mema. Katika Akhera tutaulizwa kuhusu matendo yetu."

TUSISAHAU KUFA

Shetani na nafsi zetu za kihayawani ndiyo changamoto ngumu zaidi katika ulimwengu huu ambazo lazima tuzishinde ili kupata wokovu wa milele. Nafsi ya kihayawani kwa kawaida inawakilisha mielekeo hasi ambayo mwanadamu yuko chini yake. Mingi ya mielekeo hii ni matokeo ya "uasi dhidi ya umauti" na hamu ya "kuwa wa milele".

Hakika binadamu kamwe hawataki kupoteza baraka walizonazo. Daima wanatamani umilele na kutokufa. Wengine huutafuta umilele katika watoto wao na kutamani kizazi chao kiendelee mpaka siku ya mwisho. Wengine wanatishika na uimara wao wa kimwili na kiafya. Wanatamani waishi karne nyingi katika hali hiyo hiyo. Wengine huutafuta umilele katika kuacha athari na kutamani umashuhuri wao uendelee kuishi hata baada ya kifo chao. Na wengine wanautafuta umilele katika kukusanya mali na kutegemea nguvu za vile wanavyovimiliki. Jambo hili limeelezwa katika aya ifuatayo:

" Anadhani ya kuwa mali yake yatambakisha milele!" (104: 3)

Wakati ambapo kutafuta umilele katika dunia hii yenye kuondoka au kudhani kuwa siku za furaha hazitofikia kikomo na baraka hazitopotea ni mawazo tupu na matarajio ya bure kama kuona sarabi katika jangwa.

Uzuri ulioje wa maneno ya rafiki mmoja wa Mwenyezi Mungu pale anaposema:

"Usiiombe dunia kubaki milele. Itawezaje kukupa kitu ambacho haina?"

Kwa hiyo hatupaswi kusahau kwamba sisi ni wageni katika dunia hii na siku zetu zitafikia kikomo katika tarehe isiyojulikana. Maisha ya kweli na ya milele ni maisha ya Akhera, kwa sababu, hakuna hata kiumbe mmoja mabaye hatokufa. Kusahahu mauti ni upumbavu kama kuzika kichwa cha mtu mchangani na kudhani kuwa atapona dhidi ya hatari. Lakini, kwa bahati mbaya, msimamo wa watu wengi kuhusu kifo hautofautiani sana na hali hii. Watu wengi wanaishi bila kuujua ukweli huu, badala ya kukipamba kifo kwa matendo mazuri katika dunia hii.

HALI MBILI TOFAUTI KUHUSU KIFO

Bin Wahb Munabbih anasimulia:

Siku moja Sultan mmoja alikuwa akijiandaa kwa safari akachagua nguo zake bora na farasi bora kwa ajili ya safari yake. Kisha akiwa na watu wake huku akijigamba, alianza safari. Akiwa njiani, mtu mmoja aliyevaa nguo chakavu akaishika hatamu ya farasi wake. Sultan akamfokea masikini huyo:

"Wewe ni nani? Toka njiani." Mtu yule akamjibu kwa upole:

"Nina jambo muhimu sana nataka kukwambia. Ni jambo muhimu kwako…"

Sultani, nusu akiwa mwenye udadisi na nusu akiwa mwenye ghadhabu, akamwambia:

"Sawa niambie, ni jambo gani hilo." Mtu yule akasema:

"Ni siri. Nitakunong'oneza sikioni."

Sultani akainama na yule mtu akamnong'oneza:

"Mimi ni Azrail, Malaika wa Mauti na niko hapa kuchukua uhai wako."

Sultani akashikwa na woga na kuanza kuomba huruma ya Azrail:

"Tafadhali nakuomba unipe muda kidogo zaidi."

Lakini malaika akamwambia:

"Hapana, huna muda. Hutoweza kwenda kwenye familia yako" hapo hapo akauchukua uhai wa sultani.Kisha Malaika wa mauti akaendelea na safafri yake na kukutana na mtu mwema njiani. Akamsalimia na kumwambia:

"Nina siri nataka nikwambie" akainama na kumnong'oneza mtu mwema akamweleza kuwa yeye ni malaika wa mauti. Muumini huyo akafurahi sana na kumwambia:

"Karibu,nilikuwa nakusubiri. Nimefanya kila kitu ninachoweza ili kuifanya siku hii kuwa nzuri. Daima nilikuwa na wasiwasi juu ya siku zangu za mwisho katika dunia."

Malaika wa mauti akamwambia:

"Basi malizia yale ambayo umekuwa ukiyafanya." Mtu mwema akajibu:

"Jukumu langu muhimu ni kukutana na Mwenyezi Mungu Mtukufu."

Malaika akasema:

"Nitachukua uhai wako kwa njia unayotaka." Mtu mwema kamuuliza kama hilo linawezekana, na malaika akamwambia:

"Ndiyo, inawezekana na nimeamrishwa kufanya hivyo." Mtu mwema akasema:

"Hivyo ngoja nichukue tena udhu wangu na nianze kuswali. Chukua uhai wangu wakati nikiwa namsujudia Mwenyezi Mungu." Malaika akauchukua uhai wake hali ya kuwa ni mwenye kusujudu. (Ghazali, Ihya, IV, 834-5)

Hali mbili tofauti kutoka katika wakati wenye kutisha katika maisha… kwa upande mmoja, kuna mtu ambaye hajui kwamba siku moja maisha yake yatafikia kikomo; kwa upande mwingine, kuna mtu mwema ambaye wakati wote yuko tayari kwa ajili ya nyakati zake za mwisho na ambaye anafikia dakika zake za mwisho kwa amani na utulivu. Kwa baadhi ya watu kifo ni jinamizi, na kwa wengine, kama asemavyo Rumi, ni ishara ya muungano unaosubiriwa kwa hamu na ni sawa na usiku wa harusi.

Uzuri ulioje wa maneno ya Abu Bakr ﷺ anaposema:

"Ukimbie umaarufu ili heshima ikufuate. Jiandae na mauti ili ujaaliwe maisha ya milele."

Jalal al-Din Rumi anaelezea hali za marafiki wa Mwenyezi Mungu kama ifuatavyo:

"Kifo cha mwili ni zawadi kwa kkini cha siri: uharibifu ni (unaofanywa na) mkasi kwenye dhahabu safi?" [91]

Tunapaswa kufikiri jinsi tutakavyokutana na malaika wa mauti. Tutakwenda vipi kwenye makutano yetu ya mwisho? Tutakutana na Mola wetu tukiwa katika hali ya kusujudu au tukiwa katika hali ya kutenda dhambi? Daima tunatakiwa kutafakari kwamba yepi yatakayokuwa maneno yetu ya mwisho.

MSIMLILIE MAREHEMU ZILILIENI NAFSI ZENU...

Hassan al-Basri anasema kuwa:

"Azrail huyachukua maisha ya wale ambao wamemaliza muda wao duniani. Wanafamilia humlilia na kumuomboleza marehemu; lakini malaika wa mauti hujaribu kuwaambia:

91. Mathnawi, IV, 1681

"Kwa nini mnalia? Sikuchukua uhai wa mtu huyu kabla ya wakati wake. Siku zake zimefikia kikomo, amri ya Mungu imekuja na mimi nimefanya kazi yangu! Msilie bure. Muda utakapofika, nitarudi kuchukua maisha yenu pia."

Hassan al-Basri anaendelea kuelezea:

"Lau kama wanafamilia wangemuona malaika wa mauti na kusikia anachosema, wangesahau kumililia marehemu na wangeanza kujililia wenyewe!"

Mwenyezi Mungu Mtukufu, ambaye ana hekima maalumu katika matendo yake yote ametuficha muda wa mauti yetu ili muda wote tuwe tayari kwa siku husika, lakini wakati huohuo, tuweze kutekeleza majukumu yetu ya kidunia mpaka wakati wetu unapofika. Hii yote ni kwa sababu ya huruma yake isiyokuwa na kikomo kwa waja wake. Kwa mfano, kama mtu angejua muda wa kifo chake angeacha kazi, marafiki na familia yake, na kuuweka muda wake wote kwa ajili ya ibada. Maisha yangekosa mizania. Kama watu wangejua muda wao wa kufa, wasingefurahia maisha yao. Fikiria nini kingetokea iwapo mama angejua kwamba mtoto wake atakufa akiwa na umri wa miaka ishirini.

Kwa muhtasari, kutojua muda wa kufa ni baraka kutoka kwa Mwenyezi Mungu kwa sababu Mwenyezi Mungu Mtukufu aliumba maisha katika dunia hii kama mtihani na kwa sababu ya hilo akaiacha hatima na "muda wa kufa" kuwa siri. Ndiyo maana muda wote tunatakiwa kujiandaa kwa kifo:

Qur'an Tukufu inasema:

" Kila nafsi itaonja mauti. Kisha mtarudishwa kwetu." (29: 57)

Kuna aya nyingine nyingi kama hizo ndani ya Qur'an Tukufu. Aya hizo ni maonyo kutoka kwa Mungu yanayokaririwa ili kutukumbusha kuwa dunia hii si ya kudumu.

Wauthmaniyya walikuwa wakijenga makaburi yao katikati ya miji na mbele ya misikiti ili watu wanaopita jirani wapate kukumbuka kifo, wachukue mazingatio na warekebishe makosa yao.

Tunapaswa pia kukumbuka kwamba matangazo ya vifo tunayoyasikia na habari za vifo tunazozisoma katika magazeti kila siku siku moja zitatuhusu sisi. Tunatakiwa pia kuchukua mazingatio ndani yake. Hapo tunaweza kwenda kwa Mola wetu tukiwa na moyo uliojaa amani na utulivu.

Mtume wa Mwenyezi Mungu anasema kwamba:

"Mara zote kumbukeni kitu (kifo) kinachokomesha furaha." (Tirmidhi, Zuhd, 4)

Katika maneno mengine ya Mtume ﷺ, kutafakari mauti wakati wa swala kumeashiriwa kama ifuatavyo:

"Swali kama mtu anayeondoka ulimwenguni." (Ibn Mjah, Zuhd, 15)

Kwa maneno mengine, swala ni mfano wa safari ya kiroho kutoka katika ulimwengu huu wa muda kwenda kwenye maisha ya milele. Inawakilisha utiifu, kujisalimisha, na utumwa wetu kwa Mola wetu mara tano kwa siku. Kwa namna moja, ni njia ya kiroho ya kunufaika kwa kuwa pamoja na Mwenyezi Mungu katika Akhera tukiwa bado tupo duniani.

Kutokana na mtazamo huu, swala ni safari ya Miraji kati ya Ulimwengu huu na Akhera. Wale wanaotekeleza swala zao kwa umakini na unyenyekevu na kisha wakarudi kwenye maisha ya kila siku wanaishi maisha yenye umakini kana kwamba wamerejea baada ya kufa. Swala kama hiyo hutulinda dhidi ya kutenda madhambi na maovu. Swala ya kweli ni njia adhimu ya kutafakari kifo kwa vitendo.

Kila muumini anayeswali kama mtu anayekaribia kuondoka duniani anauona ulimwengu huu kupitia dirisha la Akhera.

Anapofikia ukomavu huu, je anaweza kuwa mweza wa ibilisi? Je anaweza kuathiriwa na matamanio ya nafsi? Je moyo wake unaweza kuelekea kwenye tamaa za kidunia?

Watu walimuuliza Ibrahim bin Adham (q.s) kuhusu sababu ya dua zao kutopokelewa na Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Akajibu:

"Mnamjua Mwenyezi Mungu, lakini hamfuati maamrisho yake. Mnamjua Mtume, lakini hamuishi kulingana na sunnah zake. Mnaisoma Qur'an, lakini hamtekelezi yale yaliyoandikwa ndani yake. Mnanufaika na baraka za Mwenyezi Mungu lakini hamshukuru. Mnaijua pepo lakini hamfanyi juhudi kuipata. Mnaujua moto lakini hamna wasiwasi nao. Mnasema kuwa kuna mauti, lakini hamjiandai nayo. Mnawaweka wazazi, ndugu zenu n.k makaburini kwa mikono yenu lakini hamchukui mazingatio. Kwa hiyo, mnawezaje kutegemea dua za watu hao wenye kughafilika zipokelewe?" (Tadhkirat al-awliyah, uk.40)

JAMBO MUHIMU LISILOJULIKANA: PUMZI YA MWISHO

Marafiki wa Mwenyezi Mungu hutumia maisha yao wakitafakari mauti na kuwa na wasiwasi kuhusu pumzi yao ya mwisho, kwa sababu wanajua vyema kuwa shetani, ambaye hujaribu kuwahadaa wanadamu katika maisha yao yote, atafanya kila awezalo kuwafanya wapotee njia wakati wa pumzi zao za mwisho. Shetani huweza kuwadanganya wale wenye shaka katika nyoyo zao, kisha huwaacha peke yao na mateso na ukafiri wao.

Qur'an Tukufu inasema:

" Ni kama mfano wa Shetani anapomwambia mtu: Kufuru. Na akikufuru humwambia: Mimi si pamoja nawe. Ha-

kika mimi namwogopa Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa walimwengu wote." (59: 16)

Ndiyo maana tunamuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu azilinde imani zetu mwishoni mwa uhai wetu. Dakika za mwisho za maisha yetu ni dakika hatari sana na wasiwasi wetu unatakiwa kujikita kwenye kutopoteza imani yetu katika sekunde za mwisho.Jambo hili limeelezwa katika aya ifuatayo:

" Enyi mlioamini! Mcheni Mwenyezi Mungu kama ipasavyo kumcha; wala msife ila nanyi ni Waislamu." (3:102)

"Um al-'ala, mwanamke wa Kiansari ambaye alikuwa amekula kiapo cha utii kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu aliniambia: "Muhajirun (Waislamu waliohama kutoka Makkah) waligawanywa miongoni mwetu kwa kura, nasi tulimpata Uthman bin Madh'un katika fungu letu. Aliishi pamoja nasi katika nyumba yetu. Kisha akashikwa na maradhi yaliyopelekea kifo chake. Alipokufa, akaoshwa na kuvikwa sanda.

Mtume wa Mwenyezi Mungu alikuja, nami nikasema (nikiuambia mwili wa marehemu), "Ewe Aba As-Saib! Mwenyezi Mungu akurehemu! Ninashuhudia kuwa Mwenyezi Mungu amekupa heshima." Mtume wa Mwenyezi Mungu akasema, "Unajuaje kwamba Mwenyezi Mungu amempa heshima?"

Nikasema, "Wazazi wangu wawe fidia yako ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Nani mwingine ambaye Mwenyezi Mungu atampa heshima yake?" Mtume wa Mwenyezi Mungu akasema:

"Ama yeye (marehemu), naapa kwa Mwenyezi Mungu, mauti yamemfika. Naapa kwa Mwenyezi Mungu, namtakia yote mema (kutoka kwa Mwenyezi MUngu). Naapa kwa Mwenyezi Mungu, licha ya ukweli kwamba mimi ni Mtume wa Mwenyezi Mungu, sijui atakachotufanyia Mwenyezi Mungu",

Um al-'ala akaongezea, "Naapa kwa Mwenyezi Mungu, sitothibitisha unyoofu wa yeyote baada ya hapo." (Bukhari, ta'bir, 27)

Kwa hiyo, hatujui tutakufa katika hali gani. Wale wanaompoteza mtu wanayemjua wanatakiwa kutotoa hukumu kumhusu; bali wamtolee sadaka na kufanya mambo mema kwa niaba yake, na kumuombea maghfira.

Mtume ﷺ ameashiria katika hadith yake kuwa:

"Wanadamu hufariki kutokana na wanavyoishi na watafufuliwa kutokana na walivyokufa." (Munawi, Fayd al-Qadir, V, 663)

Hili kwa kawaida linaweza kushuhudiwa kwa watu walio karibu nasi. Tofauti na Mitume na watu waliopewa habari njema kuhusu hali zao huko Akhera, hakuna mtu mwenye dhamana ya utakavyokuwa mwisho wake. Kwa maneno mengine, watu hawapaswi kuzitegemea sadaka zao na matendo yao mema. Kila mtu anatakiwa kujua kwamba Mwenyezi Mungu pekee ndiye anayefaa kutegemewa na kukimbiliwa; na ajaribu kutenda matendo yanayoendana na radhi za Mwenyezi Mungu.

Hatupaswi kusahau kuwa ibada na matendo yetu pia yanahitaji kukubaliwa kama ilivyo kwa dua zetu. Katika maneno mengine ya Mtume ﷺ, pumzi ya mwisho imeelezwa kama ifuatavyo:

"Hakika, kuna mtu ambaye hufanya matendo kwa muda mrefu kama amali za watu wa peponi, kisha matendo yake yakageuka kuwa kama ya watu wa motoni na, kwa hakika, kuna mtu ambaye hufanya matendo ya watu wa motoni kwa muda mrefu, na kisha matendo yake yakamalizikia kuwa matendo ya watu wa peponi." (Muslim, kitab al-Qadr, 11).

Mtu mmoja katika marafiki wa Mwenyezi Mungu, Ali al-Bakka (q.s) anaelezea kwanini alipewa jina la Bakka (yaani anayelia sana):

Alikuwa na rafiki yake mwema ambaye alionyesha karama na akawa na hali ya juu ya kiroho. Siku moja wakapanga kusafiri. Kwa miguu ilikuwa ni safari ya muda wa mwaka mmoja; lakini wakafanya makarama na kufika huko walikokuwa wakienda kwa muda wa saa moja. Rafiki yake akamwambia Al al-Bakka kuwa:

"Nitakufa sehemu fulani na wakati fulani. Njoo mahali hapo uwe karibu yangu." Lakini rafiki yake alikufa na ukafiri. Baada ya kuona tukio hili, Ali al-Bakka alianza kulia sana kwa sababu ya wasiwasi wa kupoteza imani yake katika nyakati za mwisho za uhai wake.

Kwa hiyo moyo wa muumini unatakiwa kuwa katikati baina ya matarajio na hofu.

Ahmad bin Antaki (q.s) aliwaambia wale waliomtaka ushauri:

"Hofu yenye manufaa ni ile inayomzuia mtu kufanya dhambi na mambo yasiyopendwa na Mwenyezi Mungu; humfanya awe na huzuni ya kupoteza mambo yanayohusu Akhera, na ikamfanya afikirie hali ya pumzi yake ya mwisho na maisha yake yaliyobaki."

Muhammad Masum Faruki (q.s) anasema kwamba:

"Hofu kwa ajili ya pumzi ya mwisho ni baraka kubwa ambayo marafiki wote wa Mwenyezi Mungu wanapenda kukutana nayo."

Ni ahadi ya Mwenyezi Mungu kuwa wale wanaoishi katika ulimwengu huu kwa unyoofu wa imani, utulivu wa ibada, na

tabia njema pamoja na hofu na wasiwasi wa pumzi yao ya mwisho wataokolewa kutokana na hofu na maumivu ya siku ya kiyama. Hilo limeashiriwa katika aya ifuatayo:

“ Hakika waliosema: Mola wetu Mlezi ni Mwenyezi Mungu! Kisha wakanyooka sawa, hao huwateremkia Malaika wakawaambia: Msiogope, wala msihuzunike; nanyi furahini kwa Pepo mliyokuwa mkiahidiwa.” (41: 30)

NINI ITAKUWA HATIMA YAKO?

Sheikh Ahmad Harb alikuwa na jirani yake wa zamani aitwaye Bahram ambaye alikuwa anaabudu moto. Siku moja Ahmad Harb akamlingania Bahram kwenye Uislamu. Bahram akamwambia:

“Ewe mwenye busara miongoni mwa Waislamu! Nitakuuliza maswali matatu. Ukiyajibu nitaikubali dini yako.” Ahmad Harb alipokubali, Bahram akaanza kuuliza:

“Kwa nini Mwenyezi Mungu aliumba viumbe? Na pamoja na kuwapa baraka zake, kwa nini anayachukua maisha yao? Na kama anachukua maisha yao, kwa nini awafufue?”

Sheikh akajibu kama ifuatavyo:

“Aliwaumba viumbe wake ili kuwafanya wajue umoja wake, uwepo wake, na ukuu wake. Amewapa baraka ili wajue rehema zake na kwamba yeye ndiye anayewapa mahitaji yao yote. Anayachukua maisha yao ili wapate kujua uwezo wake usiokuwa na kikomo. Anawafufua ili wapate kujua kwamba yeye ni wa milele. Kwa muhtasari, katika kila hatua ya maisha yao wanaweza kuona kwamba yeye ndiye Mwenyezi Mungu Mtukufu.”

Bahram aliposikia majibu haya, akasilimu. Sheikh Ahmad Harb akapatwa na woga na kunyong'onyea. Aliporudi katika hali yake ya kawaida, aliulizwa:

"Ewe Sheikh! Nini kimetokea?" Akasema:"Wakati huo nilisikia kwamba: Bahram alikuwa kafiri kwa muda wa miaka sabini na sasa amekuwa Muislamu. Wewe umekuwa Muislamu kwa miaka sabini; je wajua kitakachotokea wakati wa pumzi yako ya mwisho?" (Tadhkirat al-awliya, uk. 97)

Kwa hiyo tunatakiwa kufanya kila jitihada kuishi maisha yetu katika wema ili kwamba tupumue pumzi yetu ya mwisho tukiwa katika imani. Mbali na hayo, tunapaswa pia kukimbilia katika rehema na msamaha wa Mwenyezi Mungu.

Junaid al- Baghdadi alimuona mbwa mwindaji, alipokuwa akizunguka katika majangwa ya Yemen. Akamuona mbwa yule kuwa hana meno, mzee, na dhaifu tofauti na umri wa miaka yake ya mwanzo. Hapo mwanzo alikuwa na uwezo na kushambulia na kukamata paa, lakini sasa hakuwa na nguvu za kumshinda hata kondoo dhaifu.

Junaid alisikitishwa sana na mbwa huyo na kumpa kipande cha mkate wake na kumwambia mbwa:

"Ewe Mbwa! Sijua nani kati yetu atakayekuwa katika hali nzuri kesho. Ukiangalia muenekano, leo mimi naonekana kuwa katika hali nzuri kuliko wewe. Lakini sijui hatima ina mpango gani na mimi. Nikiweza kuilinda imani yangu, nitaliweka taji la rehema ya Mwenyezi Mungu juu ya kichwa changu. Nikinyang'anywa maarifa yangu ya kiroho, nitakuwa dhalili kuliko wewe; kwa sababu bila kuangalia tabia mbaya ya mbwa, hatoingizwa motoni."

Muumini mwenye hisia kama hizo zilizotajwa hapo juu huishi katika hii dunia kana kwamba anatembea katika sehemu

iliyotapakazwa mabomu ya kutega. Ili aifkie pepo, hujifunza kutokana na makaburi. Anajua vyema kwamba kujitayarisha kwa ajili ya wakati wa kufa haina maana ya kujiandalia kaburi bali kujiandaa yeye kwenda kaburini.

Baada ya kifo Bahauddin Naqshiband, mmoja wa wanafunzi wake alimuona katika ndoto na kumuuliza:

“Niambie amali gani ambayo natakiwa kuifanya ili nipate wokovu wa milele?” Akasema:

“Fanya amali yoyote ambayo ni muhimu kwa ajili ya pumzi ya mwisho.”

Mauti yanapokuja, hata mikono yenye nguvu na ustadi wa hali ya juu hukosa kufanya kazi. Baada ya muda huo, hakuna kuvuja jasho, kuchoka, kuhisi baridi, au uvivu. Kwa maneno mengine, nyudhuru zote za kibinadamu zinazotuzuia kufanya ibada na kutekeleza wajibu wetu kwa Mola wetu hufikia tamati kwa pumzi ya mwisho. Wakati huo siyo wakati wa kufanya ibada na juhudi, bali ni wakati wa kuulizwa maswali. Fursa ya kufanya matendo ya kumridhisha Mwenyezi Mungu imeshatolewa duniani. Fursa hiyo inapoondoka hakuna njia ya kuirudisha.

Junaid al-Baghdadi anasema kuwa:

““Siku moja katika dunia hii ina thamani sana kuliko miaka elfu moja katika Akhera. Kwa sababu ukiwa duniani una nafasi ya kupata radhi za Mwenyezi Mungu, hali yakuwa huko Akhera hutopata fursa ya kutenda matendo mema. Katika Akhera tutaulizwa kuhusu matendo yetu.”

Kwa hali hii, waumini wema huichukulia dunia hii kama uwanja wa Akhera. Wanajua kwamba chochote wanachokipanda hapa duniani watakivuna huko Akhera. Hivyo huyatumia maisha yao kwa kufanya matendo mema.

Kwa mujibu wa simulizi moja, Nabii Iliya عليه السلام alipokutana na malaika wa mauti alishikwa na hofu kidogo. Malaika akamuuliza:

"Ewe Iliya! Wewe ni nabii. Unaogopa kifo?" Iliya akajibu:

"Hapana, siogopi kifo. Ninahuzunika kwamba huu ni mwisho wa kipindi cha uhai wangu; kwa sababu nilikuwa nikiutumia muda wangu katika kufanya ibada na kufikisha ujumbe wa Mwenyezi Mungu kwa watu. Nilikuwa nikifurahia utiifu wangu. Lakini kuanzia sasa nitakuwa mfungwa katika kaburi mpaka siku ya Kiyama. Ndiyo maana nina huzuni."

Kwa hiyo, jambo muhimu ni kuwa na uwezo wa kutenda matendo mema, kutoa sadaka, na kuondoka katika hali nzuri hapa duniani kabla ya kufungwa kwa kitabu cha matendo yetu. Kufika mbele ya Mwenyezi Mungu tukiwa na moyo wa amani na salama ni furaha kubwa mno kwa mja.

Katika lugha ya Kituruki tuna msemo wa ajabu usemao: "Yule achekaye mwisho, hucheka vizuri."

Tafsiri ya maneno haya ni kwamba hakuna tabasamu zuri kama tabasamu la wakati wa kuvuta pumzi ya mwisho pindi muumini anapoonyeshwa mafikio yake huko Akhera.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu atujaalie kuwa miongoni mwa wale watakaotabasamu wakati wa kuvuta pumzi ya mwisho. Atubariki hekima na uwezo wa kuziuliza maswali nafsi zetu na kuyasahihisha makosa yetu. Atubariki amani na utulivu wa muungano wa milele katika Akhera.

Amin...

KUIPENDELEA AK HERA ZAIDI YA DUNIA

Muumini ana wajibu wa kumshukuru Mola wake kwa baraka zake zote, hususan baraka ya imani. Kwa sababu kudai kuwa unamiliki kitu ambacho hujakilipia ni kazi bure.

Hali ya wale wanaosahau jukumu la kutoa gharama ya baraka ya imani na wanaodanganywa na raha za muda mfupi za dunia hii ni kama hali ya samaki anayekamatwa na ndoana. Samaki yeye huona chambo tu na anashindwa kuona ndoana iliyojificha ndani yake. Wale wanaosahau kuwa maisha ya kweli ni yale ya Akhera hawawezi kukwepa kuangukia kwenye mitego ya dunia hii.

KUIPENDELEA AKHERA ZAIDI YA DUNIA

Kila muumini huwa na shukrani kwa mtu anayemtendea wema; humshukuru na kumuombea mtu huyo. Anapopata nafasi, hutaka kumlipa wema wake kwa kitu kizuri zaidi. Hata kama kitu kilichotolewa ni glasi ya maji, inahitaji kutolewa shukrani. Qur'an Tukufu ina sema:

"Na mkizihisabu neema za Mwenyezi Mungu, hamwezi kuzidhibiti. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye maghfira, Mwenye kurehemu." (16: 18)

Katika neema zote za Mwenyezi Mungu, imani ndiyo neema kubwa zaidi kuliko zote. Kama ilivyo kwa neema nyinginezo, thamani ya neema ya imani ni shukrani, kumkumbuka Mwenyezi Mungu, Ikhlasi na uchamungu.

Muumini anawajibika kushukuru neema zote anazopewa na Mola wake, hususan neema na baraka ya imani. Kwa sababu kudai kuwa unamiliki kitu ambacho hujakilipia ni madai ya uongo.

Imani ndiyo neema kubwa zaidi kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Mitihani na majaribu mbalimbali katika hii dunia ni vipimo vya kuangalia ni kwa kiwango gani tunatambua thamani ya neema hii. Kinachotarajiwa kutoka kwa muumini ni kuilinda imani yake kwa subira na kunyenyekea katika hali na

mazingira yoyote yale. Wakati huo huo jambo hili humuweka mtu katika nafasi ya kupata neema hii. Qur'an Tukufu inasema kuwa:

"Hakika Mwenyezi Mungu amenunua kwa Waumini nafsi zao na mali zao kwa kuwa wao watapata Pepo…" (9:111)

Muda unaotumika katika dunia hii haulingani hata na sekunde moja ikilinganishwa na maisha ya kudumu ya Akhera, lakini kutokana na mitihani mbalimbali inayopatikana katika dunia hii, makazi ya mtu katika Akhera ama pepo ambayo ni mahali penye furaha zisizokuwa na kikomo, au moto ambao ni mahali pa mateso na adhabu ya milele. Chaguo la mja baina ya ulimwengu huu na Akhera ndiyo linaloamua mwelekeo wa safari yake. Hakuna kudanganyika kukubwa katika haya maisha kuliko kutoichagua Akhera.

Marafiki wa Mwenyezi Mungu, ambao huongazwa na hekima ya Mungu, husoma kila herufi moja inayopatikana katika kitabu cha ulimwengu kwa kutumia macho ya nyoyo zao. Wanaelewa kwamba ulimwengu haukuumbwa kwa mchezo, una lengo maalumu, na kila siku unapochukua ukurasa mmoja kutoka katika kalenda ya maisha na mtu naye hupiga hatua moja kulikaribia kaburi. Wanatafakari majibu ya maswali mbalimbali kama vile: " Nini maana na hekima ya maisha? Kwa nini ardhi imewekwa ili kumtumikia mwanadamu? Tunatoka wapi na tunakwenda wapi?" Hivyo tuishi na nyoyo zenye usikivu, hisia na tafakuri.

ALAMA YA MOYO SAFI

Katika aya zifuatazo, Mola wetu Mtukufu anaashiria mambo tunayoyahitaji zaidi siku ya Hukumu:

"Siku ambayo kwamba mali hayatofaa kitu wala wana. Isipokuwa mwenye kumjia Mwenyezi Mungu na moyo safi." (26: 88-89)

Kupata moyo safi kunategemea kufanya maandalizi kwa ajili ya Akhera kabla ya wito kutoka kaburini. Ili kufikia lengo hili, tunahitaji kuzitakasa nyoyo zetu dhidi ya kila kitu kinachotoweka mbali na Mwenyezi Mungu. Na pia tunahitaji kuzibadilisha neema zote tulizopewa na Mwenyezi Mungu kuwa nyenzo zitakazotusaidia kupata furaha huko Akhera.

Masufi huielezea sifa muhimu sana ya moyo safi kama ifuatavyo:

1. Kutomuumiza yeyote na kutoumizwa na yeyote; kwa sababu moyo ni mahali panapotazamwa na Mwenyezi Mungu.

2. Daima kuichagua Akhera, pindi linapokuja suala la kuchagua baina ya dunia na Akhera.

Muumini anayefika kwenye ukamilifu wa maadili kwa moyo safi hujua kwamba daima Mwenyezi Mungu yuko pamoja naye. Huhisi kwamba muda wote anatazamwa na Mwenyezi Mungu na kuifikiria maana ya aya zifuatazo:

وَهُوَ مَعَكُمْ اَيْنَ مَا كُنْتُمْ

"…naye yu pamoja nanyi popote mlipo. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuyaona mnayoyatenda." (57:4)

وَنَحْنُ أَقْرَبُ اِلَيْهِ مِنْ حَبْلِ الْوَرِيدِ

"Na hakika tumemuumba mtu, nasi tunayajua yanayompitikia katika nafsi yake. Na Sisi tuko karibu naye kuliko mshipa wa shingoni mwake." (50:16)

Marafiki wa Mwenyezi Mungu, ambao wapo katika kilele cha uchamungu, mara zote hukumbuka ukweli wa Akhera na kufuata njia iliyonyooka katika maisha yao. Wanaweza kuacha neema zote za ulimwengu huu kama wakitakiwa kuchagua baina ya ulimwengu huu na Akhera.

HATUBADILI MEMA YA AKHERA KWA THAMANI YA DUNIA NZIMA

Nabii Musa ﷺ alipogundua kuwa Fir'aun alikuwa anamtafuta amuue, akafunga safari haraka sana kwenda Madiyana bila kuchukua chakula chochote. Kwa muda wa siku nane, alitembea bila chakula wala maji na alipofika katika ngome ya mji wa Madiyana alikuwa amechoka. Hapo aliwasaidia mabinti wa Shuaib (Jethro) ﷺ kuwanywesha kondoo wao. Kisha Musa ﷺ akapumzika. Alikuwa mnyonge sana kiasi kwamba alikuwa akimuomba Mwenyezi Mungu akisema:

"…Mola wangu Mlezi! Hakika mimi ni mhitaji wa kheri utakayo niteremshia." (28: 24)

Shuaib ﷺ aliposikia kwamba mtu mmoja mwema aliwasaidia mabinti zake, alimualika nyumbani kwake na kumpa chakula. Japokuwa Musa ﷺ hakuwa na chakula chochote, hakutaka kula chakula alichokuwa amepewa Shuaib ﷺ akasema:

"Sisi ni familia ambayo tungepewa dunia nzima tusiingeibadilisha na amali moja ya Akhera. Sikukusaidia kwa ajili ya kulipwa chakula, bali kwa ajili ya Mwenyezi Mungu."

Shuaib ﷺ alifurahi kusikia maneno haya na kumwambia Mussa ﷺ:

"Chakula hiki siyo kwa ajili ya msaada ulioutoa; bali ni kwa sababu wewe ni mgeni wetu." Hapo Mussa عليه السلام akaikubali zawadi.

Huu ni mfano wa wenye kukumbukwa unaoonyesha imani katika Akhera. Ni uwezo wa kutobadilisha amali ya Akhera kwa thamani ya manufaa ya kidunia hata kwa kukabiliwa na mauti kwa sababu ya njaa.

Mfano mwingine wa uelewa huu umesimuliwa na Wasilah bin Aska. Ilikuwa katika kipindi ambacho tulikuwa tukienda katika vita vya Tabuk. Kwa sababu sikuwa na mali wala kipandwa ili kuungana na jeshi, hivyo nikawatangazia watu wa Madina:

"Nani atakayenichukua kwenye kipandwa chake kwa kubadilishana na fungu la ngawira zangu za vita?"

Mzee mmoja wa Kiansari akakubali pendekezo langu kama tutafanya zamu katika kipandwa. Tulifunga safari. Mwenyezi Mungu akatujaalia ngawira kadhaa na nikapata fungu langu. Niliipeleka kwa mzee wa kiansari; lakini akaniambia:

"Chukua ngamia wako na uondoke." Pamoja na hivyo nikamwambia: "Lakini haya ndiyo makubaliano yetu na hawa ngamia ni wako."

Akasema: "Rafiki yangu! Chukua ngawira zako. Sikutaka mali zako za kidunia, nilitaka kukusaidia tu ili kupata thawabu kwa ajili ya Mwenyezi Mungu." (Abu Dawud, Jihad, 113/2676)

Hivyo, mzee yule wa Kiansari alipendelea kupata malipo huko Akhera kuliko kuwa na ngamia kadhaa, ambao ni miongoni mwa vitu vilivyokuwa na thamani sana wakati huo. Alionyesha mfano wa kutenda kwa ajili ya Mwenyezi Mungu badala ya kuchagua mali nyingi za kidunia.

Rafiki mmoja wa Mwenyezi Mungu alipoulizwa iwapo alikutana na tukio lililomuathiri sana, alisimulia tukio lifuatalo:

"Siku moja nilipoteza begi langu la pesa mjini Makkah. Nilikuwa nahitaji msaada. Nilikuwa nasubiri pesa kutoka Basra; lakini zilichelewa.

Nilihitaji kunyoa nywele hivyo nikaenda kwa kinyozi na kumwambia:

"Sina pesa. Je waweza kuninyoa nywele kwa ajili ya Mwenyezi Mungu?"

Wakati huo kinyozi alikuwa akimhudumia mteja mwingine. Alinionyesha kiti kilichokuwa tupu pembeni ya mteja na kuniambia: "Tafadhali kaa hapa." Alimuacha mteja wake akisubiri na kuanza kuninyoa. Yule mteja mwingine alipoonyesha upinzani, alimwambia:

"Samahani, ninanyoa nywele zako kwa pesa; lakini nitamnyoa mtu huyu kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Kwangu mimi, radhi za Mwenyezi Mungu daima huja mwanzo. Na mja hawezi kutoa kitu chochote kinacholingana na radhi za Mwenyezi Mungu." Na baada ya kuninyoa, alinipa pesa kidogo na kuniambia:

"Ninasikitika kuwa ninaweza kukupa kiasi hiki kidogo. Chukua pesa hizi kwa mahitaji yako ya dharura."

Siku chache baadaye nilipokea pesa nilizokuwa nikizisubiri kutoka Basra. Nilichukua mkoba wa dhahabu na kumpelekea kinyozi, lakini alikataa huku akisema:

"Siwezi kuzichukua. Nilikusaidia kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na hakuna kinachoweza kulipa thamani ya amali iliyofanywa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu."

Niliomba ruhusa na kuondoka, lakini sikuweza kumsahau, kumuombea kinyozi yule kwa siku arobaini nilizopita."

Hii ni mifano bora ya kuitanguliza Akhera juu ya dunia. Huu ni mwenendo bora ambao akili fupi, ambazo hazioni tofauti yoyote kati ya halali na haramu, haziwezi kuuelewa. Huu ndiyo werevu wa kweli ukiangaliwa katika kona ya urafiki na Mwenyezi Mungu.

NI NANI MWENYE AKILI YA KWELI?

Mantiki na akili inahitaji kubadilisha faida ndogo, rahisi na ya muda kwa faida kubwa na za milele. Mwenyezi Mungu anasema:

"Na maisha ya dunia si chochte ila ni mchezo na pumbao tu. Na hakika nyumba ya Akhera ni bora zaidi kwa wanaomcha Mungu. Basi, je, hamtii akilini?" (6: 32)

Katika hadith moja ya Mtume ﷺ watu wenye akili wameelezewa kama ifuatavyo:

"Mtu mwenye akili ni yule anayeihoji nafsi yake na kujiandaa kwa maisha ya Akhera; wakati mpumbavu ni yule anayefuata matamanio ya nafsi yake na bado anatarajia kupata mema kutoka kwa Mwenyezi Mungu." (Tirmidhi, Qiyamah, 25/2459)

Kwa hiyo, werevu wa mtu hupimwa kwa viwango vilivyotajwa hapo juu. Akili salama inatanguliza mambo ya milele mbele ya mambo ya muda mfupi.

Mtume wa Mwenyezi Mungu anasema:

"Hali ya dunia mbele ya Akhera ni kama kuchovya kidole cha mtu katika bahari na kukitoa. Dunia ikilinganishwa na

Akhera ni sawa na kile kile kinachochotwa na kidole kutoka katika bahari.” (Hakim, Mustadrak, 4/319)

Maswahaba wa Mtume ﷺ walijisemea wenyewe pindi washirikina walipokuwa wakiwatesa zama walipokuwa Makkah:

“Tunapata mateso yote haya ili kuwa waja wa Mola wetu; ilhali makafiri wanaomuasi Mwenyezi Mungu wanaishi katika raha. Wanafurahia manufaa yote ya dunia hii.” Mwenyezi Mungu Mtukufu akawaamrisha kuchagua lililo bora au Akhera:

“Kabisa kusikudanganye kubakia kutangatanga kwa waliokufuru katika nchi. Hiyo ni starehe ndogo. Kisha makazi yao yatakuwa Jahannamu. Na ni mahali pabaya mno pa kupumzikia. Lakini walio mcha Mola wao Mlezi watapata Mabustani yanayopita mito kati yake. Watadumu humo. Hayo ni makaribisho yao yatokayo kwa Mwenyezi Mungu. Na vilivyoko kwa Mwenyezi Mungu ni bora kwa watu wema.” (3: 196-198)

Hivyo basi, tunapoziangalia raha na furaha zote za dunia hii kwa mtazamo wa Akhera, tunaona jinsi gani zilivyo ndogo. Kama dunia hii ingekuwa na thamani hata kidogo mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, angewafanya mitume na marafiki zake waishi kwa raha katika makasri; lakini aliwaonyesha waja wake wema uso wa kweli wa dunia hii na kuzielekeza nyoyo zao kwenye Akhera. Mtume wa Mwenyezi Mungu anaeleza yafuatayo:

“Sina uhusiano wowote na hii dunia. Mfano wangu katika hii dunia ni kama msafiri ambaye baada ya kutembea hupumzika chini ya kivuli cha mti kwa muda na baada ya muda huendelea na safari yake.” (Tirmidhi, Zuhd, 44)

Mtindo wa maisha ya maswahaba ambao walilelewa chini ya uangalizi wa Mtume ﷺ ni mifano isiyomithilika kwetu sisi.

Kuitafuta kwao Akhera na tamaa yao ya kufa kishahidi ni mifano adhimu kwetu.

Nyoyo za maswahaba vijana ambao walibeba ujumbe wa Mtume ﷺ zilikuwa zimejaa imani na mapenzi ya kumpenda Mtume ﷺ; waliachana na kila kitu kinachohusiana na dunia hii. Walikuwa watiifu mno kwa Mtume (s.a.w) kiasi kwamba katika mazingira ya hatari mno walitamka kwa ujasiri:

"Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Fanya utakavyo na upendavyo. Tuamrishe. Tupo pamoja nawe. Tunaapa kwa Mwenyezi Mungu, hata kama utaingia katika hii bahari, tutaingia pamoja nawe na hakuna hata mmoja wetu atakayebaki nyuma…" (Ibn Hisham, II, 253-254)

Siku moja katika zama za Ukhalifa wake, Umar ﷺ alikutana na Habbab bin Arat ﷺ, ambaye alikuwa miongoni mwa Waislamu wa mwanzo na kumwambia:

"Waweza kuniambia mateso uliyokumbana nayo?"

Habbab akamwambia:

"Ewe kiongozi wa waumini! Tazama mgongo wangu." Umar ﷺ alipotazama mgongoni mwake, alishituka sana kuona jinsi alivyoumizwa na kujeruhiwa vibaya. Habbab akaendelea kusema:

"Makafiri walikuwa wakiwasha moto na kutulazimisha kulala juu yake. Moto ulikuwa ukizimika kwa sababu ya mafuta ya miili yetu." (Ibn Athir, Usud al-Ghabah, II, 115)

Katika siku za mwanzo za Uislamu, washirikina walitumia kila aina ya adhabu dhidi ya waumini lakini daima waliilinda imani yao; kwa sababu nguvu ya imani yao ilikuwa ikiyaondosha maumivu.

Tofauti na wasiwasi na tamaa ya watu wa leo ya kuishi muda mrefu, tamaa kuu ya kizazi cha maswahaba ni kufa kwa heshima na kwenda Akhera wakiwa na nyoyo safi.

Siku moja Ibn Mas'ud ﷺ aliwaambia wenzake wa kizazi cha *tabi'in*:

"Mnajaribu kufunga, kuswali, na kufanya matendo mema zaidi kuliko maswahaba wa Mtume ﷺ; lakini wao walikuwa bora kuliko nyinyi."

Walipouliza inawezekanaje iwe hivyo, Ibn Mas'ud ﷺ akajibu:

"Waliipa nyongo hii dunia na kujitoa moja kwa moja kwa ajili ya Akhera." (Hakim, Mustadrak, 4/135)

Katika mojawapo ya maneno yake, Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ

anasema kuwa:

"Ewe Mwenyezi Mungu! hakuna maisha bora yenye thamani isipokuwa maisha ya Akhera…" (Bukhari, Riqaq, 1)

Tunapaswa kupandikiza kanuni hii ndani ya nyoyo zetu kama wafuasi wa Mtume ﷺ. Tunapopata neema ya kidunia, tunapaswa kusema, *Hakuna maisha bora yenye thamani isipokuwa maisha ya Akhera* na kumshukuru mmiliki wa kweli wa neema hizi. Tunapaswa kujitenga na hali ya kughafilika, ukigeugeu na uharibifu. Wale wasioonyesha hisia hiyo wanaonywa na ujumbe ufuatao kutoka kwa Mwenyezi Mungu:

"Mwenyezi Mungu humkunjulia riziki amtakaye, na humkunjia kwa kipimo. Na wamefurahia maisha ya dunia. Na uhai wa dunia kwa kulingana na Akhera si kitu ila ni starehe ndogo." (13: 26)

Kama waumini, tunapaswa pia kuwa na subira, tusipoteze azma yetu na mizania yetu ya kisaikolojia na tuseme "*Mola wetu! Hakuna maisha yenye thamani isipokuwa maisha ya Akhera"* pale tunapokumbana na tatizo na shida katika huu ulimwengu. Daima tunapaswa kukimbilia kwa Mwenyezi Mungu na kuishi maisha ya amani kwa kuelewa maana ya aya ifuatayo:

" …starehe ya dunia ni ndogo, na Akhera ni bora zaidi kwa mwenye kuchamungu…" (4: 77)

Ufupi wa maisha ya dunia, yanayofikiriwa kuwa ni ya kudumu, umeelezwa katika aya kama ifuatavyo:

"Ni kama kwamba wao siku watapoiona (hiyo Saa) hawakukaa ila jioni moja tu, au mchana wake." (79: 46)

Ndiyo maana jambo la busara kulifanya katika dunia hii ni kuonyesha maisha ya utiifu kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Hata hivyo, kama ilivyo kwa neema nyingine zote, thamani ya neema ya uhai huwa haijulikani mpaka iondoke.

Ili kuonyesha ukweli huu, watangulizi wetu walikuwa wakipanda miti ya mivinje katika maeneo ya makaburi, ambayo yanatukumbusha kwamba dunia hii si ya kudumu. Kwa kuwa miti ya mivinje haipukutiki majani, inaonyesha umilele wa Akhera.

Wosia ufuatao wa Luqman al-Hakim kuhusu kuitambua Akhera ni wa muhimu sana:

"Mwanangu! Itoe muhanga dunia yako ili upate Akhera, ukifanya hivyo utapata vyote viwili. Lakini usiiache Akhera yako kwa ajili ya dunia hii, ukifanya hivyo utakosa vyote."

Kwa hakika dunia na Akhera ni kama pande mbili za mizani. Ukiweka uzito mwingi kwenye upande mmoja, upande

wa pili utainuka. Kila muumini mwenye akili safi na salama anatakiwa kuelekea upande wa Akhera; kwa sababu wale wanaodanganywa na raha za muda mfupi za ulimwengu huu hupoteza mapenzi na mawazo ya kuifikiria Akhera. Kinyume chake, pindi mapenzi ya kuipenda Akhera yanapokaa katika moyo, mapenzi ya kuipenda hii dunia hutoweka.

TIBA YA UGUMU WA MOYO

Msingi wa matatizo mengi ya kiroho, ukosefu wa utulivu, na ugumu wa moyo upo katika kuisahau Akhera na kuangukia katika kushughulishwa na ulimwengu huu. Masikini wengi hujitesa na kwa kutamani kuwa matajiri; na matajiri wengi hujitesa kwa tamaa ya kupata zaidi. Watu wana tamaa ya raha za muda za ulimwengu huu bila kutafakari kuhusu chanzo cha yote hayo. Isisahaulike kuwa kuridhika ndiyo utajiri wa kweli.

Mtume ﷺ anasema kwamba:

"Mwenyezi Mungu huuweka utajiri ndani ya nyoyo za wale wanaotamani Akhera na kuziweka shughuli zao katika mpangilio. Dunia hujisalimisha na kuwafuata. Mwenyezi Mungu huweka umasikini ndani ya nyoyo za wale ambao malengo yao ni kuipata hii dunia na kuharibu utaratibu wa shughuli zao. Mwishowe, hawawezi kupata zaidi ya fungu lao katika hii dunia." (Tirmidhi, Qiyamah, 30/2465)

Ifuatayo ni tiba iliyotolewa na Mtume ﷺ kwa ajili ya faraja ya moyo na amani ya akili…

Alipoulizwa Mtume ﷺ maana ya neno **"kufungua"** katika aya isemayo: **"Basi yule ambaye Mwenyezi Mungu anataka kumhidi humfungulia kifua chake kwa Uislamu…"** (6: 125), akasema:

"Nuru inapoingia moyoni, kifua hufunguka na kupanuka kwa ajili yake." Mtume ﷺ alipoulizwa kama kuna alama yoyote ya upanukaji huu, akajibu:

"Ndiyo, ipo. Ni mtu kuugeuza uso wake kutoka katika hii dunia, ambayo ni mahali pa udanganyifu, na kuuelekeza Akhera, au kwenye maisha ya milele, na kujiandaa kuwa tayari kwa ajili ya kifo kabla hakijamjia." (Ghazali, Ihya, IV, 406 -7)

Katika hadith nyingine, Mtume wa Mwenyezi Mungu anasema:

"Yule anayeitanguliza hii dunia juu ya Akhera, Mwenyezi Mungu humpatiliza kwa mateso ya aina tatu: wasiwasi usiokoma katika moyo wake; umasikini asioweza kuondokana nao; na ulafi usiokidhika." (Ghazali, Ihya, IV, 411)

KOSA SIYO LA DUNIA BALI NI LA WALE WANAODANGANYIKA NAYO

Mwenyezi Mungu Mtukufu ameweka manufaa ya kidunia mbele yetu kama mtihani katika hii dunia. Wale wanaodanganyika na raha za muda za ulimwengu huu ni kama samaki aliyekamatwa na ndoana. Samaki anadanganyika na chambo, lakini haioni ndoana iliyo nyuma yake. Wale wanaosahau kuwa maisha ya kweli ni maisha ya Akhera hawawezi kukwepa kuangukia katika mitego ya dunia hii.

Kufaulu mitihani hii ya Mwenyezi Mungu kwa mafanikio kunategemea kuuangalia ukweli wa manufaa ya kidunia na kuielewa **"siri ya majaribu na mitihani."** Ili kufikia hatua hii ya werevu, inatakiwa kuijua mitego ya dunia na kuitanguliza Akhera juu ya tamaa za kidunia kama vile mali, tamaa za kihayawani, na umaarufu.

Katika suala hili, Mola wetu anatuonya ndani ya aya zifuatazo:

"Lakini nyinyi mnakhiari maisha ya dunia! Na Akhera ni bora na yenye kudumu zaidi." (87: 16-17)

"…mnataka vitu vya dunia, na Mwenyezi Mungu anataka Akhera. Na Mwenyezi Mungu ni Mtukufu Mwenye nguvu Mwenye hikima." (8: 67)

Mali iliyochumwa hapa duniani humsindikiza mwenye nayo mpaka anapozikwa. Mali pekee ya dhahiri ambayo mtu anaweza kwenda nayo kaburini ni sanda yake ingawaje sanda haiiachi roho. Hata hivyo, imani na matendo yake yatakwenda naye mpaka ndani ya kaburi na kukaa pamoja na roho yake. Ndiyo maana waumini hawapaswi kudanganywa na matamanio ya muda ya ulimwengu huu.

Dhul Qarnain عليه السلام, ambaye, kwa mujibu wa hadith, aliitawala dunia, alitoa wosia wake wa mwisho kabla ya kufa kama ifuatavyo:

"Niosheni na mnivike sanda. Kisha niwekeni ndani ya jeneza; lakini iacheni mikono yangu nje ya jeneza. Waacheni watu wangu waje nyuma ya jeneza langu. Pakieni hazina zangu juu ya nyumbu, ili watu wajue kwamba japokuwa nilikuwa na utajiri mkubwa, ninaondoka katika dunia hii bila hata mali moja; mali zangu zote na watumishi wangu watabaki hapa duniani na hawatafuatana nami. Hivyo ili watu wasidanganywe na dunia hii yenye kupita."

Wanazuoni wanaufafanua wosia huu wa mwisho kama ifuatavyo:

"…niliitawala dunia yote. Nilikuwa na hazina kubwa; lakini neema za kidunia siyo za kudumu milele. Kama mnavyoona, ninaondoka hapa duniani mikono mitupu. Mali za kidunia zi-

mebaki hapa duniani. Kwa hiyo jishughulisheni na matendo ambayo yatakuwa na manufaa huko Akhera."

Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ anatupa wosia ufuatao wenye hekima:

"… ninakuusieni mambo matano ambayo kwayo Mwenyezi Mungu atazikamilisha sifa zenu nzuri:

Msikusanye vitu msivyoweza kula;

Msijenge majengo ambayo hamtoishi;

Msipiganie vitu ambavyo kesho mtaviacha;

Muogopeni Mwenyezi Mungu, ambaye kwake mtarejea na ambaye mbele yake mtakusanywa;

Jiandae kwa ajili ya sehemu ambayo utaenda na kukaa milele." (Ali al-Muttaqi, Kanz al-Ummal, na: 1363).

Kwa kifupi, haina maana kuilaumu dunia wakati wa kuvuta pumzi ya mwisho. Mtu anatumia vibaya uhai wake kwa kuzikimbilia neema za muda mfupi za dunia hii na kutofuata maisha ya watu wema. Hali ya kusikitisha ni kusahau mustakbali wa milele na kudanganyika na tamaa za muda mfupi! Tunapaswa kutafakari juu ya ukweli kwamba hakuna muda au mahali pa kukimbia kifo; haiwezekani kurejea duniani baada ya kufa; na hakuna kimbilio la kuikimbia adhabu ya Siku ya Hukumu.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu atufanye kuwa kama wale wanailinda ikhlasi yao, miongoni mwa wale wnye kipawa na uelewa, na miongoni mwa watu wema! Atupe uwezo wa kuuona ukweli wa dunia hii na Akhera! Na atubariki nguvu ya kuitanguliza Akhera juu ya dunia!

Amin...